# Njia ya Haki

## Habari Njema kwa Waislamu

Habari na mafundisho ya manabii wa Mungu ndani ya Tora, Zaburi na Habari Njema (Injil)

Everyday Publications Inc
@ 2010

**Kitabu 3**

**par P.D. Bramsen**

**Everyday Publications Inc.**
310 Killaly Street W.
Port Colborne, ON
Canada L3K 6A6

# Njia ya Haki

## Kitabu cha Tatu

Copyright © 1998
P.D. Bramsen
The Way of Righteousness (Le Chemin de la Justice)

Traduit en Swahili par permission
par G.I. Harlow

ISBN 0-88873-148-5

Everyday Publications Inc
@ 2010

*Cette série est aussi disponible dans d'autres langues.*

Pour permission de traduire Le Chemin de la Justice dans d'autres langues veuillez contracter:
TWOR@iname.com / www.twor.com

*Imprimé au Canada*

# Njia ya Haki

*Habari na mafundisho ya manabii wa Mungu ndani ya Tora, Zaburi na Habari Njema (Injil)*

## Utangulizi

***"Hata logo ikilala mia za miaka ndani ya maji halitageuka mamba kamwe"*** (mezali ya Wawolof wa Senegal) . . . ***vivyo hivyo kushikamana na dini hakuwezi kugeuza mtu kuwa haki.*** Desturi za dini na matendo mema yanasaidia watu kufikili wao ni *watu wa haki* na kuwafanyiza kuonekana kama wenye *haki mbele ya watu,* lakini hayawafanyizi *haki* ***mbele ya Mungu***.

Everyday Publications Inc
@ 2010

***Njia ya Haki*** ni tafsiri kwa Swahili-Congo ya **"Yoonu Njub"** — programmes 100 za radio kwa kiwolof kwa Waislamu wa Senegal ya Afrique de l'Ouest. Kuanza na Tora ya Musa programmes hizi zinapeleka wasikiaji kwa safari ya Maandiko ya manabii kuona kusudi lisilobadiliki kamwe la Mungu kwa watu wa dunia na kusikia jibu la furaha kubwa la Mungu kwa neno ambalo nabii Yobu aliuliza miaka elfu ine mbele, ***"Mtu anaweza kuwa na haki mbele ya Mungu namna gani?"*** (Yobu 9:2)

Sasa programmes hizi zimechapwa kwa Swahili ndani ya vitabu vitatu kusaidia Waislamu na watu wengine vilevile kufahamu habari hizi za *manabii ya Mungu* vizuri zaidi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kitabu 1 — | Masomo | 1-28 | *Njia ya Haki ndani ya TORA* |
| Kitabu 2 — | Masomo | 29-45 | *Njia ya Haki ndani ya TORA* |
| | Masomo | 46-59 | *Njia ya Haki ndani ya ZABURI na MANABII* |
| Kitabu 3 — | Masomo | 60-88 | *Njia ya Haki ndani ya HABARI NJEMA* |
| | Masomo | 89-100 | *Njia ya Haki — MUHTASARI* |

Waislamu wanaamini ya kwamba Mungu amefunua mapenzi yake kwa njia ya vitabu vitakatifu vine (Tora, Zaburi, Habari Njema, Qur'an). Lakini Waislamu wachache tu wamekuwa na njia kusoma Habari Njema ya Mungu ndani ya Tora, Zaburi, na Maandiko ya Habari Njema. **Masomo haya 100 yanawapatia njia kufanya hivi.**

Watu wengi wanashangaa wakati wanaposikia ya kwamba Qur'an kinaagiza Waislamu kuamini Tora (Taurat), Zaburi na Habari Njema (Injil), sehemu za Maandiko Matakatifu kwa Kiebrania na Kiyunani yanayoita *Biblia.* (Biblia ni kilatin kwa *Kitabu).*

Waislamu wengi wanasema ya kwamba maandiko ndani ya vitabu vya Tora, Zaburi na Habari Njema yamegeuzwa na haifai kuyaamini. Lakini masemo haya si kweli. Kuna karatasi elfu za maandiko ya vitabu hivi vinavyochungwa kwa pahali mbalimbali pa dunia. Karatasi hizi ziliandikwa mia za miaka mbele ya Qur'an. Kuna mafundisho mengine juu ya neno hili ndani ya Somo 90. Lakini hatuhitaji kusimamia Neno la Mungu kwani linasimama imara, Neno takatifu la Mwenyezi Mungu. Neno ambalo inatupasa kufanya si kulisimamia lakini ***kuisoma***.

Everyday Publications Inc
@ 2010

> *"Maana Neno la Mungu ni hai, lenye nguvu na ukali kupita ukali wa upanga unaokata ngambo mbili, likitoboa hata kutenga nafsi na roho, na viungo na mafuta ndani ya mifupa; nalo ni jepesi kufahamu mawazo na makusudi ya moyo. Hakuna kiumbe kinachofichwa mbele yake, lakini vitu vyote ni utupu na kufunuliwa mbele ya macho yake yeye aliye na maneno yetu."*
>
> (Wabrania 4:12,13)

Ndiyo, uwezo wa kuchoma roho ya **Kweli ya Mungu** na utamu wa milele wa **njia ya haki ya Mungu** zinastahili kwa watu kuwa tayari kupata mateso na hata mauti kwa sbababu yake. Nabii Solomono aliandika, *"**Katika njia ya haki** ni uzima; na katika mapito yake hakuna mauti"* (Mezali 12:28) Allahu Akbar! Mungu ni mkubwa, na kwa wote wanaonyenyekea njia yake ya haki anatoa ahadi kuwapa bila bei neno ambalo dini na matendo mema hayawezi kutupatia: wokovu toka azabu na uwezo wa zambi, kuhesbiwa haki na kujua ya kwamba zambi zetu zimesamehewa, zamiri safi, salama kubwa moyoni, furaha rohoni ambayo hakuna neno linaweza kuharibu, tabia mpya, upatano wa karibu na Mungu, na kao pamoja naye katika Paradiso kwa milele!

Tunaweka kwa Mungu watu wote wanaosoma masomo haya mia moja, kwa Mungu yule mwenye huruma na rehema, **mwenye haki**—anayetaka kutolea ahadi hii ya kuleta uzima na kugeuza maisha kwa mtu ye yote anayekubali kuipokea.

> ***"Mutanitafuta, na kuniona wakati mutakaponitafuta kwa moyo wenu wote."*** (Yeremia 29:13)

Everyday Publications Inc
@ 2010

# Fahirisi

## *Kitabu 1*

Habari na Mafundisho ya Manabii wa Mungu kupatana na Tora


| | | *ukurasa* |
|---|---|---|
| | *Utangulizi* | 3 |
| *Somo* | | |
| 1 | Mungu amesema (Mwanzo) | 11 |
| 2 | Mungu ni namna gani? (Mwanzo 1) | 17 |
| 3 | Shetani na Malaika (Mwanzo 1:1; Isaya 14; Ezekieli 28 | 22 |
| 4 | Namna Mungu alivyoumba dunia (Mwanzo 1:1-26) | 27 |
| 5 | Kwa sababu gani Mungu aliumba mtu (Mwanzo 1:26,27; 2:7) | 32 |
| 6 | Adamu na Hawa (Mwanzo 2) | 37 |
| 7 | Namna gani zambi ilivyoingia duniani (Mwanzo 3:1-6) | 43 |
| 8 | Tunda la zambi ya Adamu (Mwanzo 3:7-19) | 48 |
| 9 | Ahadi ya ajabu (Mwanzo 3:15,21-24) | 53 |
| 10 | Njia ya sadaka (Mwanzo 4:1-5) | 59 |
| 11 | Kutotubu kwa Kaina (Mwanzo 4:1-16) | 65 |
| 12 | Nabii Enoka (Mwanzo 4, 5) | 70 |
| 13 | Nabii Noa : Saburi na gazabu (Mwanzo 6) | 76 |
| 14 | Noa na garika kubwa (Mwanzo 7) | 81 |
| 15 | Noa na uaminifu wa Mungu (Mwanzo 8, 9) | 86 |
| 16 | Babeli! (Mwanzo 10, 11) | 91 |
| 17 | Ukumbusho #1 (Mwanzo 1-11) | 97 |
| 18 | Abrahamu: Kwa sababu gani Mungu alimwita (Mwanzo 11,12) | 102 |
| 19 | Imani ya Abrahamu: (Mwanzo 13-15) | 108 |
| 20 | Abrahamu na Isimaeli (Mwanzo 16,17) | 113 |
| 21 | Abrahamu: Uharibifu wa Sodomo na kuzaliwa kwa Isaka (Mwanzo 18-21) | 119 |


Everyday Publications Inc
@ 2010

| *Somo* | | *ukurasa* |
|---|---|---|
| 22 | Sadaka ya Abrahamu (Mwanzo 22) | 125 |
| 23 | Esau na Yakobo (Mwanzo 25) | 131 |
| 24 | Yakobo anageuka Israeli (Mwanzo 28-32) | 137 |
| 25 | Aibu ya Yosefu (Mwanzo 37-39) | 143 |
| 26 | Kutukuzwa kwa Yosefu (Mwanzo 40-42) | 149 |
| 27 | Baki la habari za Yosefu (Mwanzo 42-50) | 155 |
| 28 | Ukumbusho wa kitabu cha kwanza cha Tora (Mwanzo 1-50; Kutoka 1) | 161 |

## *Kitabu 2*

**Masomo 29 – 59**

| | | |
|---|---|---|
| | *Utangulizi* | 3 |
| 29 | Musa (Kutoka 1,2) | 11 |
| 30 | Musa anakutana na Mungu (Kutoka 3,4) | 17 |
| 31 | Ulizo la Farao: Bwana ni nani? (Kutoka 4-7) | 23 |
| 32 | Hukumu kumi (Kutoka 7-10) | 29 |
| 33 | Mwana-Kondoo ya Pasaka (Kutoka 11,12) | 35 |
| 34 | Njia katikati ya Bahari (Kutoka 13-15) | 41 |
| 35 | Chakula jangwani (Kutoka 16,17) | 47 |
| 36 | Mlima Sinai (Kutoka 19, 20) | 53 |
| 37 | Amri Kumi (Kutoka 20) | 59 |
| 38 | Kusudi la Amri Kumi (Kutoka 20) | 65 |
| 39 | Amri zinazovunjwa (Kutoka 32) | 71 |
| 40 | Hema ya Kusanyiko (Kutoka 24-40, Walawi 16) | 77 |
| 41 | Kutokuamini kwa Waisraeli (Hesabu 13,14) | 83 |
| 42 | Nyoka ya shaba (Hesabu 20,21) | 89 |
| 43 | Maneno ya mwisho ya Musa (Torati) | 95 |
| 44 | Yosua na inchi ya Kanana (Yosua) | 101 |
| 45 | Waamuzi na Ruta (Waamuzi na Ruta) | 107 |
| 46 | Samweli, Saulo na Daudi (1 Samueli 1-16; Zaburi 8,23) | 113 |
| 47 | Daudi na Goliata (1 Samweli 17; Zaburi 27) | 121 |
| 48 | Mfalme Daudi na ahadi ya Mungu (1 Samweli 18 - 2 Samweli 7) | 127 |
| 49 | Mfalme Daudi na Bati-Seba (2 Samweli 11,12; Zaburi 51,32) | 133 |
| 50 | Nabii Daudi na Masiya (Zaburi 1, 2) | 139 |

Everyday Publications Inc
© 2010

| *Somo* | | *ukurasa* |
|---|---|---|
| 51 | Mafundisho mengine toka Zaburi (Zaburi 22) | 145 |
| 52 | Nabii Solomono (1 Wafalme 2-10; Zaburi 72) | 151 |
| 53 | Nabii Elia (1 Wafalme 6-18) | 157 |
| 54 | Nabii Yona (Yona) | 163 |
| 55 | Nabii Isaya (Isaya) | 169 |
| 56 | Nabii Yeremia (Yeremia) | 175 |
| 57 | Nabii Danieli (Danieli 1,6) | 181 |
| 58 | Nabii Zekaria (Zekaria) | 187 |
| 59 | Jumlisho la unabii wa manabii (Malaki) | 193 |

## *Kitabu 3*

### Masomo 60 –100

| | | |
|---|---|---|
| | *Utangulizi* | 3 |
| 60 | Nabii Yoane (Luka 1) | 11 |
| 61 | Tangazo (Luka 1; Matayo 1) | 17 |
| 62 | Masiya anazaliwa (Luka 2; Matayo 2) | 23 |
| 63 | Mwana mtakatifu (Luka 2; Matayo 3,4) | 29 |
| 64 | Mwana-Kondoo wa Mungu (Yoane 1,3) | 35 |
| 65 | Mganga mkubwa (Marko 1,2) | 41 |
| 66 | Mwalimu mkubwa (Matayo 5-7) | 47 |
| 67 | Sharti muzaliwe mara ya pili (Yoane 3) | 53 |
| 68 | Mwokozi wa dunia (Yoane 4; Luka 4) | 59 |
| 69 | Amri ya Yesu (Matayo 12; Yoane 5) | 65 |
| 70 | Uwezo wa Yesu (Matayo 12; Yoane 5) | 71 |
| 71 | Mifano mikubwa miwili (Luka 8; Matayo 13) | 77 |
| 72 | Mkate wa Uzima (Marko 6; Yoane 6) | 83 |
| 73 | Yesu analeta matengo (Matayo 15,16; Yoane 7) | 89 |
| 74 | Nuru ya Ulimwengu (Yoane 8,9) | 95 |
| 75 | Bwana wa utukufu (Matayo 16,17) | 101 |
| 76 | Mchungaji Mwema (Yoane 10) | 107 |
| 77 | Moyo wa Mungu (Luka 18,15) | 113 |
| 78 | Ufufuko na Uzima (Yoane 11,12) | 119 |
| 79 | Yesu anaingia Yerusalema (Luka 18-20) | 125 |
| 80 | Masemo magumu na ya kweli (Matayo 22-25) | 131 |
| 81 | Chakula cha mwisho (Matayo 26) | 137 |
| 82 | Yesu anakamatwa (Yoane 14; Matayo 26) | 143 |
| 83 | Yesu anahukumiwa (Matayo 26,27; Yoane 18,19) | 149 |

Everyday Publications Inc
@ 2010

| *Somo* | | *ukurasa* |
|---|---|---|
| 84 | Yesu anasulibishwa (Matayo 27; Marko 15; Luka 23; Yoane 19) | 155 |
| 85 | Yesu amefufuka! (Matayo 28; Luka 24; Yoane 20 | 161 |
| 86 | Yesu anapanda mbinguni (Matayo 28; Luka 24; Matendo 1) | 167 |
| 87 | Roho Mtakatifu amekuja! (Matendo 1,2) | 173 |
| 88 | Yesu atarudi tena! (Ufunuo 19-22) | 179 |
| 89 | Habari Njema | 185 |
| 90 | Maulizo ya watu na majibu ya Mungu (#1) | 193 |
| 91 | Maulizo ya watu na majibu ya Mungu (#2) | 199 |
| 92 | Inapasa mwanafunzi wa Kristo kuishi namna gani? | 206 |
| 93 | Ukumbusho #1 Adamu - Neno gumu la zambi (Mwanzo 1-4) | 212 |
| 94 | Ukumbusho #2 Abrahamu - Haki kwa njia ya imani (Mwanzo 6-22) | 218 |
| 95 | Ukumbusho #3: Musa: Sheria takatifu ya Mungu Kutoka 1-20) | 224 |
| 96 | Ukumbusho #4: Yesu Kristo: "Imekwisha!" (Yoane 19, Waebrania 10) | 230 |
| 97 | Hadeze! (Luka 16) | 236 |
| 98 | Paradiso! (Ufunuo 21,22) | 243 |
| 99 | Unafikili nini juu ya Yesu? (#1) | 249 |
| 100 | Unafikili nini juu ya Yesu? (#2) | 255 |

Everyday Publications Inc
@ 2010

Everyday Publications Inc
@ 2010

Somo 60

# Nabii Yoane

Luka 1

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuanza leo kitabu cha tatu cha mfulizo wetu *Njia ya Haki*.

Mara ya *mbele* tulimaliza safari yetu hata mwisho wa sehemu ya kwanza ya Maandiko Matakatifu, ndani yake ni Tora {Taurat}, Zaburi (Zabur) na Maandiko ya Manabii. Sehemu ile ya kwanza inaitwa ***Agano la Kwanza***, linaloitwa vilevile *Agano la Kale*. Leo tutaanza kujifunza ndani ya sehemu ya pili ya Neno la Mungu, inayoitwa vilevile ***Agano Jipya.***

Everyday Publications Inc
© 2010

**Kwa sababu gani Mungu aligawa Kitabu chake kitakatifu kwa sehemu mbili**, Agano la Kwanza (Agano la Kale) na Agano Jipya? Mungu alifanya hivi kwa sababu nyingi. Labda neno la kwanza ambalo inatupasa kufahamu ni ya kwamba maneno yote ya **Agano la Kwanza** yaliandikwa ***mbele* ya kuzaliwa kwa Masiya**, lakini maneno yote ya **Agano Jipya** yaliandikwa ***nyuma* ya kuzaliwa kwa Masiya**. Hivi, habari kubwa za manabii wa Mungu ndani ya Agano la Kwanza zilikuwa: "Mungu **a*ta*tuma** Masiya!" Lakini habari za Agano Jipya ni: "Mungu **a*me*tuma** Masiya," kama alivyoahidi kwa njia ya manabii wake katika Agano la Kwanza!

Sharti ufahamu vizuri tofauti hii kubwa katikati ya Agano la Kwanza na Agano Jipya. Watu wengine wanachambua Maandiko Matakatifu kwa sababu yana *Agano la **Kale** na Agano **Jipya***. Wanafikili maana ya *Agano Jipya* ni ya kwamba mtu mmoja ame-jaribu kubatili Maandiko ya Manabii na kuyakomboa na kitabu kingine! Lakini neno hili si kweli. Agano Jipya **halibatili** maneno ambayo manabii waliandika ndani ya Agano la Kwanza—lina-**yakinisha** maneno ambayo manabii waliandika! Agano Jipya linaonyesha namna gani Mungu alitimiza ahadi na unabii na mifano

ya Agano la Kwanza. Ndani ya Agano la Kwanza, manabii wote walitangaza: **"Masiya atakuja! Atakuja! Atakuja!**" Lakini habari za kitabu cha Agano Jipya ni: "Masiya **amekuja! Masiya, ambaye manabii wote walisema na kuandika habari zake, amekuja! Amekuja!"**

Ndiyo, ingetupasa **kushukuru** Mungu na moyo unaojaa furaha kwa sababu kuna Agano la Kwanza **na** Agano Jipya ndani ya Maandiko Matakatifu. Kwa sababu ndani ya sehemu hizi mbili tunaweza kuona ya kwamba maneno Mungu aliyoahidi zamani sana — ameyatimiza! Mungu alituma Mwokozi kwetu, **namna alivyoahidi kwa babu zetu ndani ya Tora, Zaburi na vitabu vingine vya manabii**. Kama mbegu ya mbuyu inavyoota kuwa mti mkubwa sana, vivyo hivyo Agano la kwanza linakomea ndani ya Agano Jipya.

Labda umejua ya kwamba sehemu ya pili ya Maandiko, **Agano Jipya**, ina jina lingine. Jina hili ni ***"Injil".*** *Injil* ni neno la Kiarabe na maana yake ni ***Habari Njema.*** Na kweli habari zake ni habari nzuri kabisa, kwa sababu inatupasha namna Masiya alivyotimiza maneno manabii waliyotabiri, na kufungua kwa njia hii mlango wa salamu kwa wana wa Adamu kwa milele!

Everyday Publications Inc
© 2010

Sharti ufahamu vilevile ya kwamba Masiya hakuandika kitabu cha Habari Njema yeye mwenyewe. Kama Mungu alivyotumia watu wengi kuandika kitabu cha Agano la Kwanza, vivyo hivyo alitumia watu wengi kuandika kitabu cha Agano Jipya. Mungu alitumia **wanaume wane** kuandika habari za Masiya na kuja kwake duniani. Wanaume hawa walikuwa *Matayo, Marko, Luka* na *Yoane*. **Kwa nini Mungu aliongoza watu *wane* kuandika habari za Masiya?** Kwa nini hakuchagua mtu mmoja tu kuandika kitabu cha Habari Njema? Kwa sababu Mungu alitaka kutujulisha habari zinazostahili kuaminiwa bila shaka hata kidogo. Alitumia waandishi wane **kuthibitisha na kuyakinisha neno lake**. Kama meza yenye miguu mine inasimama imara kupita meza yenye mguu mmoja tu, vivyo hivyo tunaamini ushuhuda wa washuhuda wane kupita ushuhuda wa mshuhuda mmoja tu. Mungu alitumia washuhuda wane, ili tuweze kujua ya kwamba mambo yote ambayo yanaandikwa ndani ya kitabu cha Habari Njema juu ya Masiya ni kweli kabisa! Kama Mungu alivyoweka maneno yake ndani ya nia za manabii, vivyo hivyo Mungu aliongoza watu wane walioishi kwa muda wa Masiya kuandika maneno waliyoona na kusikia juu ya Mwokozi wa dunia. {Kabisa kabisa Mungu aliongoza *watu wanane* kuandika juu ya Masiya. Barua za mitume Paulo, Petro, Yakobo na Yuda ni sehemu ya Injil—

Maandiko ya Habari Njema—vilevile, na maneno yote waliyoandika ni makamilifu na yanapatana kabisa!}

Unajua kama Matayo, Marko, Luka na Yoane waliandika kitabu kitakatifu cha Habari Njema kwa lugha gani? Waliandika kwa Kiyunani. Lakini sisi tutakisoma kwa Kiswahili kwani watu wengi hawafahamu Kiyunani. Tunashukuru Mungu kwa watu wale waliotafsiri Habari Njema kwa Kiswahili. Hivi kitabu cha Habari Njema tunachoshika ndani ya mikono yetu inapatana kabisa na habari ambazo Mungu alitia ndani ya nia za Matayo, Marko, Luka, na Yoane.

Mara nyingine tunasikia watu wanaojaribu kushindana na kitabu cha Habari Njema, wakisema, "Huwezi kukitegemea! Kimegeuzwa! Kuna makosa ndani yake na maneno fulani yasiyopatana na maneno mengine!" Rafiki, mtu anayeshindana na Habari Njema takatifu anashindana na Mungu mwenyewe. Maandiko Matakatifu yanastahili kabisa matumaini na utii wetu. Kama Neno la Mungu katika Tora na Zaburi ni kamilifu, ni kamilifu katika Habari Njema vivyo hivyo! Haiwezekani kuvunja Maandiko Matakatifu. Mungu ni mkuwa na anaweza kulinda Neno lake la milele. Amelinda Kweli yake kwa watu wote ambayo wanaitafuta na roho yao yote. Hakuna mtu anayeweza kugeuza Neno la Mungu lililo hai na linalodumu milele! Hili ndilo neno Bwana mwenyewe anatangaza ndani ya Habari Njema wakati anaposema: ***"Mbingu na dunia zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kabisa!"*** (Matayo 24:35)

Basi saa imefika kwa sisi **kuanza safari yetu kupita ndani ya kitabu cha Habari Njema, Agano Jipya.** Ndani ya somo la mbele tulijifunza juu ya nabii Malaki aliyeishi miaka mia ine mbele ya Masiya. Kwa muda wa miaka ile mia ine nyuma ya wakati wa Malaki, Mungu hakutuma manabii wengine karibu na Wayuda kuandika Neno la Mungu. Kwa nini Mungu hakutuma manabii wengine? Hakutuma manabii wengine kwa sababu kuandika kwa kitabu cha Agano la Kwanza kulikwisha. **Mungu alikuwa amesema maneno yote aliyotaka kusema kwa njia ya manabii.** Sasa Mungu alingoja kwa saa aliyochagua mbele ya kuleta Masiya duniani ili aweze kusimamisha Agano Jipya.

Tumeona mbele maneno manabii Isaya na Malaki waliyotabiri juu ya shauri la Mungu kutuma nabii mbele ya Masiya kutayarisha njia mbele yake. Unajua kama alikuwa nabii gani? Ndiyo, alikuwa, nabii Yoane {jina lake kwa Qur'an ni *Yahya*}. Baba ya Yoane alikuwa Zakaria. Zakaria alikuwa nabii aliyetumikia Mungu na watu kwa njia ya kutoa sadaka za nyama hekaluni katika Yerusalema.

Everyday Publications Inc @ 2010

Tufungule sasa Habari Njema takatifu *{Injil}* and kusikia maneno Luka aliyoandika juu ya kuzaliwa kwa nabii Yoane. Tusome ndani ya sura 1, kuanza na shairi 5:

> (Luka 1) *5 Zamani katika siku za Herode, mfalme wa Yudea, palikuwa na kuhani mmoja, jina lake **Zakaria**, wa zamu ya Abiya; na mke wake alikuwa mmoja wa binti za Haruni, jina lake **Elisabeti**. 6*
> *Nao wote wawili walikuwa wenye haki mbele ya Mungu, wakitembea pasipo ushitaki katika amri zote na maagizo ya Bwana. 7 Nao*
> *walikuwa hawana mtoto, maana Elisabeti alikuwa tasa, nao wote wawili ni wazee sana.*
>
> *8 Alipokuwa akifanya kazi ya ukuhani katika taratibu ya zamu yake mbele ya Mungu, . . . 10 Na makutano yote ya watu walikuwa*
> *wakiomba inje saa ya kuchoma uvumba. 11 **Na malaika ya Bwana alionekana kwake, akisimama upande wa kuume wa mazabahu ya kuchoma uvumba**. 12 Zakaria akafazaika wakati alipomwona, woga ukamshika. 13 Malaika akamwambia: Usiogope, Zakaria, kwa sababu maombi yako yamesikiwa; na mke wako Elisabeti atakuzalia mwanamume, na utaita jina lake Yoane. 14 Nawe*
> *utakuwa na furaha na shangwe; tena wengi watafurahi kwa kuzaliwa kwake. 15 Maana atakuwa mkubwa mbele ya Bwana, na hatakunywa mvinyo wala malofu; naye atajazwa Roho Mtakatifu, hata toka tumbo la mama yake. 16 Na wengi wa wana wa Israeli atawageuza kwa*
> *Bwana Mungu wao. 17 Naye atatangulia mbele yake mwenye roho na nguvu za Elia, kugeuza mioyo ya baba kwa watoto wao, na kugeuza waasi kwa akili za wenye haki; kufanya tayari watu waliotengenezwa*
> *kwa Bwana. 18 Zakaria akamwambia malaika: Mimi nitajua neno hili namna gani? Kwani mimi mzee na siku za mke wangu zimekuwa*
> *nyingi. 19 Malaika akamjibu, akamwambia: Mimi ndimi **Gabrieli** ninayesimama mbele ya Mungu; nami nilitumwa nikuambie na*
> *kukupasha habari hizi njema. 20 **Na tazama, utakuwa bubu, usiweze kusema, hata siku ile maneno haya yatakapofanyizwa, kwa sababu hukusadiki maneno yangu; nayo yatatimizwa kwa wakati wake.***
>
> *21 Na wale watu walikuwa wakingojea Zakaria, wakashangaa kwa*
> *kukawa kwake katika hekalu. 22 Hata alipotoka hakuweza kusema nao; wakatambua ya kuwa ameona maono katika hekalu; naye aliwapungukia mkono, akakaa bubu. 23 Siku zake za kazi zilipotimia, akakwenda zake*
> *kwa nyumba yake. 24 Halafu nyuma ya siku zile, Elisabeti, mke wake*
> *alipata mimba . . . 25 (alisema) "Bwana amenitendea katika siku zile aliponiangalia kuondosha haya yangu mbele ya watu.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

Tunaona ya kwamba Mungu alituma malaika Gabrieli karibu na Zakaria kumpasha ya kwamba mke wake Elisabeti atakuwa na mwana. Mwana huyu atakuwa nabii mkubwa atakayetayarisha njia mbele ya Masiya. Hivi kwa mwisho wa sura hii, Maandiko yanasema:

> (Luka 1) *57 Hata Elisabeti, wakati wake wa kuzaa ulipotimizwa, akazaa mwanamume. 58 Jirani na jamaa zake wakasikia namna Bwana alimwongezea rehema yake; wakafurahi pamoja naye. 59 Siku ya nane wakakuja kutahiri mtoto; wakamwita Zakaria sawa na jina la baba yake. 60 Mama yake akajibu, akasema: Sivyo; lakini ataitwa* ***Yoane****. 61 Wakamwambia: Hakuna mtu katika jamaa yako anayeitwa jina hili. 62 Wakashiria baba yake kumwuliza jina gani alilotaka kuita mtoto. 63 Akaomba wamletee kibao cha kuandikia, akaandika, akisema: Jina lake ni Yoane. Wakashangaa wote. 64 Mara moja kinywa chake kilifunguliwa na ulimi wake pia, akasema, akisifu Mungu. 65 Woga ukawaingia wote waliokaa karibu nao; na maneno haya yote yalipashwa katika inchi yote ya vilima vya Yudea. 66 Na wote waliosikia wakayaweka katika mioyo yao wakisema: Huyu atakuwa mtoto wa namna gani? Kwa sababu mkono wa Bwana ulikuwa pamoja naye.*
>
> *67 Zakaria, baba yake, akajazwa Roho Mtakatifu, akatabiri akisema: 68 "Atukuzwe Bwana, Mungu wa Israeli; kwani* ***amekuja kwa watu wake, na kuwakomboa. 69 Ametunyanyulia pembe ya wokovu, katika nyumba ya mtumishi wake Daudi;*** *70* ***kama alivyosema kwa vinywa vya manabii wake watakatifu, waliokuwa tangu mwanzo****. 71 Tuokolewe toka adui zetu, na katika mikono ya wote ambao wanatuchukia; 72 kuwatendea rehema baba zetu; na* ***kukumbuka agano lake takatifu****; 73* ***kiapo ambacho alimwapia Abrahamu baba yetu****, 74 ya kwamba atatupa sisi, tukiokolewa toka mikono ya adui zetu, tumwabudu pasipo woga, 75 katika utakatifu na katika haki mbele yake, siku zote za maisha yetu."*
>
> Nyuma ya kusema maneno haya, aligeuka kwa Yoane, mtoto mchanga, akasema, *76 "Nawe, Mtoto, utaitwa nabii wake Mungu aliye juu;* ***kwa maana utatangulia mbele ya uso wake Bwana, kutengeneza njia zake;*** *77 kujulisha watu wake wokovu katika kusamehewa zambi zao, 78 kwa sababu ya upole wa rehema zake Mungu wetu,* ***katika mwanga uliotoka juu kutufikia,*** *79 kuwaangazia wanaokaa katika giza, na katika uvuli wa mauti, na kuongoza miguu yetu katika njia ya salama."*

Everyday Publications Inc @ 2010

Hii ilikuwa sifa ya Zakaria kwa Mungu nyuma ya kuzaliwa kwa Yoane kwa sababu alijua **wakati kwa Masiya kuzaliwa ulikuwa umefika!** Yoane, mwana wa Zakaria, hakuwa Masiya, lakini yule atakayetangulia Masiya, kwa **kutangaza kufika kwa Masiya** na kutengeneza njia mbele yake.

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Asante kwa kujifunza pamoja nasi. Usikose kufika mara ya nyuma wakati tutakaposoma habari za namna Mungu alivyotuma malaika yake Gabrieli kwa bikira jina lake Maria kumjulisha habari kubwa sana. Kuna kweli nyingi za faida ndani ya somo la nyuma!

Mungu akubariki wakati unapofikili juu ya maneno haya ya Zakaria:

> ***"Atukuzwe Bwana! . . . Ametunyanyulia [Mwokozi mwenye uwezo] katika nyumba ya mtumishi wake Daudi, kama alivyosema kwa vinywa vya manabii yake watakatifu, walio-kuwa tangu mwanzo."*** (Luka 1:68-70)

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Somo 61

# Tangazo

Luka 1; Matayo 1

Salama iwe kwako, rafiki. Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tuendelee sasa na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Ndani ya masomo makumi sita ya kwanza tumejifunza katika Maandiko ya Agano la Kwanza, ndiyo Agano la Kale, maana Tora {*Taurat*} ya Musa, Zaburi {*Zabur*] ya Daudi, na Maandiko ya manabii mengine. Ndani ya somo la mbele tulianza kusoma Maandiko ya **Agano Jipya**, ndiyo *"Injil."* Maana ya ***Injil*** kwa Kiarabe ni ***Habari Njema***. Kweli, maneno ya Habari Njema {*Injil*} ni habari nzuri kabisa kwa wote ambao wanaziamini, kwa sababu zinatupasha ya kwamba **Mungu ametuma Mwokozi mwenye uwezo mkubwa duniani, kama alivyoahidi zamani kwa njia ya manabii yake**.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Mbele ya kuanza mafundisho yetu ndani ya Habari Njema, ni vizuri kwa sisi kukumbuka **kwa sababu gani Mungu alikusudi kutuma Mwokozi** kwa wazao wa Adamu. Unakumbuka nini ilitokea siku Adamu na Hawa walipoasi Mungu? Ndani ya Tora, tuliona namna kuasi kwa Adamu kulivyoongoza watu wote wa dunia kwenda mbali na ufalme wa Mungu na kuwaingiza ndani ya ufalme wa Shetani. Kwa sababu ya zambi ya Adamu sisi sote mmoja mmoja tunazaliwa ndani ya zambi. Adamu na wazao wake wanaweza kuzaa watoto wenye kutenda zambi tu. Wenye zambi wanazaa wenye zambi. Zambi yetu inatuhukumu ili hatuna njia kujifanyiza haki mbele ya Mungu ambaye atalazimishwa kutuhukumu!

Lakini, tusifu Mungu kwa sababu Maandiko ya Manabii hayakwishi na habari za zambi ya Adamu! Kama tulivyoona mbele, siku ile ile Adamu na Hawa walipofanya zambi, Mungu alianza kufunua **shauri lake la ajabu sana kutuma Mkombozi duniani** atakayeokoa wazao wa Adamu toka utawala wa Shetani na zambi. Siku ile ya matata wakati zambi ilipoingia dunia, Mungu alitangaza ya kwamba

Mkombozi huyu mtakatifu atazaliwa na *"mwanamke"* tu (Mwanzo 3:15; Wagalatia 4:4). Masiya, atakayemwanga damu yake kama sadaka kamilifu kwa wenye zambi, hatakuwa mzao wa baba ya dunia mwenye zambi. Ilikuwa lazima kwake kuwa mkamilifu na mtakatifu kama Mungu alivyo mkamilifu na mtakatifu. Kwa sababu hii nabii Isaya (aliyeishi miaka mia saba mbele ya kuja kwa Masiya) aliandika: ***"Bikira atapata mimba naye atazaa mtoto mwanamume**, na ataita jina lake Emanueli – maana yake 'Mungu pamoja nasi'!"* (Isaya 7:14; Matayo 1:23)

Sasa turudi kwa kitabu cha Habari Njema ili tuweze kuona **namna Mungu alivyotimiza ahadi yake juu ya Mkombozi huyu mkamilifu na mtakatifu atakayezaliwa na bikira**—ndiye mwanamke kijana asiyelala na mwanamume. Ndani ya somo letu la mbele, tuliona namna malaika ya Mungu, Gabrieli, alivyotokea kwa Myuda mmoja jina lake Zakaria. Gabrieli alimwambia Zakaria ya kwamba yeye na mke wake watazaa mwana, jina lake Yoane, na ya kwamba mwana huyu atatayarisha njia mbele ya Mkombozi.

Sasa tuendelee kusoma ndani ya Habari Njema {*Injil*} ya Luka, sura 1, na kuona namna Mungu alivyotuma malaika yake kwa bikira, jina lake Maria. Maandiko yanasema:

Everyday Publications Inc
@ 2010

> (Luka 1) *26 Mwezi wa sita [wa Elisabeti, mama ya Yoane] malaika Gabrieli alitumwa na Mungu kwa mji wa Galilaya, ulioitwa Nazareti, 27 kwa **bikira** aliyepatana kuwa mke wa mtu aliyeitwa Yosefu, **wa nyumba ya Daudi;** na jina la yule bikira lilikuwa **Maria**. 28 Malaika alikuja kwake akasema: Salama, uliyepewa neema, Bwana yuko pamoja nawe; wewe umebarikiwa katikati ya wanawake. 29 Naye alifazaika sana kwa sababu ya neno hili, alifikili katika moyo wake: Salamu gani hii? 30 Malaika akamwambia: Usiogope, Maria, kwani umepata neema kwa Mungu. 31 Tazama, utapata mimba, utazaa mwana, utaita jina lake **Yesu**. 32 Huyu atakuwa mkubwa, ataitwa **Mwana wake Mungu aliye juu**; na Bwana atampa kiti cha baba yake Daudi; 33 atamiliki nyumba ya Yakobo hata milele; na ufalme wake hautakuwa na mwisho. 34 Maria akamwambia malaika: Neno hili litakuwa namna gani, kwani sijui mume? 35 Malaika akamjibu akamwambia: Roho Mtakatifu atakuja juu yako, na nguvu zake Mungu aliye juu zitakutulia kivuli; kwani kile kitu ambacho kitazaliwa nawe kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu. 36 Na tazama, Elisabeti wa jamaa yako, ana mimba ya mtoto mume katika uzee wake; na huu ni mwezi wa sita kwake yeye aliyeitwa tasa. 37 Kwani hapana neno lisilowezekana kwa Mungu. 38 Maria akasema: Tazama,*

*mimi mjakazi wa Bwana; iwe kwangu sawa na neno lako. Malaika akaondoka kwake.*

Tuache kusoma hapa na tusemezane kidogo juu ya maneno yaliyotokea wakati malaika ya Mungu, Gabrieli, alipoonekana kwa Maria. Maria alikuwa msichana aliyeheshimu Neno la Mungu. Mtu mmoja, jina lake Yosefu alipewa ahadi ya kwamba Maria atakuwa mke wake, lakini hawajaanza kukaa pamoja. Wao wawili walikuwa wazao wa Mfalme Daudi. Unakumbuka ya kwamba pamoja na kutabiri ya kuwa Masiya **atazaliwa na bikira**, manabii wa Mungu walitabiri vilevile ya kwamba **atakuwa wa jamaa ya Mfalme Daudi.**

Kwa kufahamu vizuri, inakupasa kufahamu neno lingine juu ya Maria, ndilo hili: Maria alikuwa mzao wa Adamu, naye alizaliwa na tabia ya zambi kama sisi sote. Sharti tuonyeshe neno hili kwa sababu watu wengi wanampa Maria pahali pa heshima pa Mungu na kumwabudu na kuomba kwake. Kufanya hivi ni **kuabudu sanamu!** Ndiyo, Maria **anastahili kupewa heshima** kwa sababu Mungu alichagua kuleta Masiya duniani kwa njia yake. Lakini baraka hii ambayo Mungu alimpa **haimstahilishi kupokea kuabudu**, kwa sababu Maandiko yanasema: *"Uabudu Bwana Mungu wako, umtumikie yeye **peke yake!"*** (Matayo 4:10)

Everyday Publications Inc
@ 2010

Basi ndani ya mashairi tuliyosoma sasa tu tunaona namna Gabrieli alivyofikia Maria kumjulisha ya kwamba yeye ndiye bikira kwa njia yake Mungu alikusudi kuleta Mwokozi wa wenye zambi duniani. Gabrieli alimwambia Maria jina la Mtoto ambaye atamzaa vilevile. Alisema naye, "*Utaita jina lake **Yesu***." Maana ya jina hili Yesu ni ***Bwana anaokoa***. {Ndani ya Qur'an Yesu anaitwa *Isa*. Agano Jipya kwa lugha ya Kiarabe linamwita *Yasu*, kupatana na jina lake la haki. *Yesu* kwa Kiyunani na *Yosua* kwa Kiebrania ni jina moja, maana yake *Bwana anaokoa*.} Lakini Gabrieli alikuwa na jina lingine kwa Masiya vilevile. Ulilisikia? Alimwita, ***"Mwana wake aliye juu."*** Ndiyo, hili ndilo neno Gabrieli alilosema. Tulisoma mbele ndani ya Zaburi za Daudi ya kwamba Mungu aliita Masiya *Mwana wake*. Sasa tunaona ya kwamba Gabrieli, malaika ya Mungu, aliita Masiya *"Mwana wa Mungu"* vilevile.

Tunajua ya kwamba watu wengi wanaosikia jina hili **"Mwana wa Mungu"** wanajibu, "Neno hili haliwezekani! *Astaghferullah!* {Maana yake kwa Islam: *Mungu akusamehe kwa kusema matukano namna hii!*} Lakini kama watu wa kabila moja wanavyosema: "Mbele ya kupiga mchungaji kwa kinywa inapasa kujua kama anapiga

msonyo kwa sababu gani." Vivyo hivyo, mbele ya kuzarau jina hili "Mwana wa Mungu," sharti ujaribu kufahamu maana ya maneno haya *"Mwana wa Mungu"*! Ndani ya Maandiko Matakatifu, Masiya anaitwa ***Mwana wa Mungu*** kupita mara mia moja na makumi mbili. Hivi, sisi tunaoamini Maandiko ya Manabii hatuwezi kusubutu kukana ya kwamba Mungu anaita Masiya **Mwana wake.** Lakini tunataka kujua **kwa nini** Mungu anaita Yesu **Mwana wake**.

Kwanza inatupasa kufahamu ya kwamba maana ya jina hili *Mwana wa Mungu* **si kusema Mungu alioa mke na kuzaa mwana!** Mtu ye yote anayefikili maneno namna hii anatukana Mungu. Mungu ndiye Mjuu sana na hazai watoto kama mtu. Sivyo! Sharti tufahamu neno hili kabisa. Hatuna saa leo kueleza maana ya jina hili *Mwana wa Mungu,* lakini lazima ufahamu ya kwamba maana yake **haiko** kusema Mungu alikamata mke na kuzaa mwana kwa njia yake! Neno hili si nguvu kufahamu kwa sababu hapa katika Congo tunaita mtu ye yote aliyeishi muda mrefu ndani ya inchi hii "mwana wa Congo", hata kama ni wazi ya kwamba haiwezekani kwa Congo kuwa na mke na kuzaa mwana. Vilevile, wakati unaposafiri inje ya inchi, labda watu wanakuita "mwana wa Congo," lakini maana yake haiko kusema Congo ni baba yako! Ni kusema umetoka kwa Congo, ndiyo inchi yako.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Ni vivyo hivyo na Yesu Masiya. Mungu alimwita Mwana wake **kwa sababu alitoka kwa Mungu.** Masiya alitoka kwa Mungu. Mbele ya kuzaliwa kwake alikuwa pamoja na Mungu; alikuwa ndani ya Mungu. Yeye ni ***"Ruh Allah"***; *Roho ya Mungu*. {"*Ruh Allah*" ni Kiarabe kwa Roho/Nafsi ya Mungu; kama "*Ruah*" kwa Kiebrania. Hili ni jina moja kwa Yesu ndani ya Qur'an, lakini halikani ya kwamba Masiya ni *Roho* Mwana wa milele wa Mungu: *Roho* ya pili ndani ya Mungu aliye Tatu ndani ya Moja.} Masiya ni "***Kalimat***" vilevile; *Neno* aliyekuwa pamoja na Mungu katika mwanzo. {"*Kalimat Allah*" ni Kiarabe kwa *Neno la Mungu*: ni jina kwa Masiya tu ndani ya Biblia na ndani ya Qur'an vilevile.} Hili ndilo neno Maandiko yanalotangaza wakati yanaposema:

> "*Katika mwanzo alikuwa* ***Neno****, na* ***Neno alikuwa pamoja na Mungu****, na* ***Neno alikuwa Mungu****. Huyu kwa mwanzo alikuwa pamoja na Mungu. Vitu vyote vilifanywa kwa huyu; na pasipo yeye hakikufanyika hata kitu kimoja kilichofanyika.* ***Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.***" (Yoane 1:1-3,14)

Ndiyo, Masiya ni **Neno la Mungu** aliyetoka mbinguni, na

kuzaliwa kama mtu. Sisi sote tunajua ya kwamba Masiya hakuwa na baba ya dunia. Basi, kama hakuwa na baba ya dunia, alitoka wapi? Yeye ni Mwana wa nani? Sikiliza tena neno ambalo Gabrieli alimwambia Maria. Alisema naye: *"**Roho Mtakatifu atakuja juu yako, na nguvu zake Mungu aliye juu zitakutulia kivuli; kwani kile kitu ambacho kitazaliwa nawe kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu.**"* (Luka 1:35)

Labda umesikia watu wengine wakisema: "Ndiyo, tunajua ya kwamba Yesu hakuwa na baba ya dunia, lakini kuzaliwa kwa Yesu na bikira si neno kubwa. Mungu alitaka kuonyesha uwezo wake tu. Aliumba Adamu bila baba au mama. Nyuma yake aliumba Hawa na baba tu, maana alimfanya toka ubavu wa mwili wa Adamu. Halafu, kwa kuonyesha uwezo wake hata kupita, Mungu aliumba mtu akitumia mwanamke tu. Hii ndiyo sababu ya pekee Yesu alizaliwa bila baba ya dunia."

Rafiki, ni kweli ya kwamba Mungu ni Mwenye uwezo wote na ya kwamba hakuna neno lisilowezekana kwake! Lakini juu ya kuzaliwa kwa Yesu na bikira, inakupasa kufahamu ya kwamba kusudi lake lilikuwa kubwa kupita sana kuonyesha uwezo wa Mungu tu! Usiache mtu ye yote kukudanganya! Yesu alizaliwa na bikira elfu za miaka nyuma ya kuumbwa kwa Adamu na Hawa kwa sababu ya kusudi kubwa sana. Unajua kwa kusudi gani? Maandiko Matakatifu yanatupasha kusudi hili katika 1 Timoteo 1:15: *[Yesu Masiya] alikuja kwa dunia **kuokoa wenye zambi**."* **Yesu alizaliwa duniani kukomboa wazao wa Adamu wenye zambi, wapotevu chini ya hukumu ya Mungu—hivi hakuweza kutoka Yeye mwenyewe kwa mtu anayechafuwa na zambi!** Tuliona mbele, ya kwamba kwa kusudi la Mungu ilikuwa lazima kwa Masiya kumwanga damu yake kama zabihu kulipa kwa zambi. Kwa kuwa **Zabihu Kamilifu** ilipasa Mkombozi kuwa bila zambi au kosa hata moja, kama kondoo mwenye afya asiye na hatia aliyetolewa kila mwaka kwa Karama ya Sadaka {*Id al-Adha*}.

Fikili kwanza! Mtu mwenye deni kubwa anaweza kulipa deni za watu wengine? Sivyo! Yule tu asiye na deni anaweza kulipa deni za watu wengine. Vivyo hivyo, ilipasa Masiya kuwa mtu asiyekuwa na deni ya zambi ili aweze kulipa deni ya zambi ya wana wa Adamu. Mungu anataka tujue ya kwamba Masiya na wana wa Adamu ni namna mbalimbali kabisa. Sisi ni **wana wa Adamu**, lakini Yesu ni Mwana wa Mungu. Sisi, kama wana wa Adamu, ni wachafu **kama uchafu wa udongo** kwa sababu ya

Everyday Publications Inc
@ 2010

zambi zetu. Lakini, Yesu ni **kama mvua inayotoka mbinguni.** Yeye ni safi na mtakatifu, kama Mungu ni safi na mtakatifu. Kwa sababu hii Mungu haoni haya kumwita ***Mwana wake!*** Hivi rafiki, tunataraji ya kwamba nyuma ya kusikiliza mafundisho ya leo, unafahamu vizuri kupita kwa sababu gani ilipasa Yesu Masiya kuzaliwa na bikira, na **maana ya kweli ya jina hili *"Mwana wa Mungu"*.**

Kwa kumaliza tunataka kusoma ndani ya Habari Njema juu ya kuzaliwa kwa Masiya. Miezi michache nyuma ya wakati Maria alipopata mimba kwa uwezo wa Roho ya Mungu, Mungu alituma malaika yake kwa Yosefu atakayekuwa mume wake. Maandiko yanasema:

> (Matayo 1) *18 Kuzaliwa kwa Yesu Kristo kulikuwa hivi: Maria mama yake alipoposwa na Yosefu, mbele ya kukaribiana, alionekana na mimba kwa Roho Mtakatifu. 19 Yosefu mume wake, akiwa mtu wa haki, wala hakutaka kumpa haya wazi, alikusudi kumwacha kwa siri. 20 Lakini wakati alipokuwa akifikili maneno haya, tazama, malaika ya Bwana alimtokea katika ndoto, akisema: Yosefu, mwana wa Daudi, usiogope kuchukua Maria mke wako, maana mimba yake ni* ***kwa uwezo wa Roho Mtakatifu****. 21 Naye atazaa mwana; nawe utamwita jina lake* ***Yesu****, kwa sababu* ***ndiye atakayeokoa watu wake toka zambi zao****. 22* ***Maneno haya yote yamekuwa ili litimie neno lililosemwa na Bwana kwa nabii,*** *akisema: 23 Tazama, bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana, nao watamwita jina lake Emanueli; maana yake* ***Mungu pamoja nasi.*** *24 Na wakati Yosefu alipoamka toka usingizi, alifanya kama malaika ya Bwana alivyomwagiza; akachukua mke wake; 25 lakini hakumjua hata alipozaa mwana wake wa kwanza; aliita jina lake* ***Yesu****.*

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Inatupasa kuacha hapa kwa leo. Mungu akitaka, tutaendelea mara ya nyuma ndani ya Habari Njema na kusoma habari za kushangaza za kuzaliwa kwa Yesu, Masiya . . .

Mungu akubariki wakati unapokaa kukumbuka maneno malaika aliyosema juu ya Masiya:

> ***"Utamwita jina lake Yesu, kwa sababu ndiye atakayeokoa watu wake toka zambi zao!"*** (Matayo 1:21)

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 62

# Masiya Anazaliwa

### Luka 2; Matayo 2

Salamu kwako, rafiki, kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea leo na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo la mbele katika Habari Njema takatifu {*Injil*}, tuliona namna Mungu alivyotuma malaika yake, Gabrieli, kwa inchi ya Wayuda, kwa mji wa Nazareti, kwa bikira jina lake Maria. Malaika huyu alitokea kwa bikira kumwambia ya kwamba atapata mimba kwa uwezo wa Roho ya Mungu, na kuzaa mwana na kumpa jina, ndilo ***Yesu***. Maana ya jina hili ni ***Bwana anaokoa***. Hivi tuliona ya kwamba wakati ule watu wa Mungu waliongojea kwa miaka mingi ulikuwa umefika! **Mkombozi** ambaye Mungu aliahidi siku Adamu na Hawa walipofanya zambi, **alikuwa ndani ya tumbo la uzazi la bikira**, karibu kufika duniani!

Everyday Publications Inc @ 2010

Jina la somo letu leo ni **"Masiya anazaliwa!"** Mbele ya kurudi kusoma katika Habari Njema kuona kama Yesu Masiya alizaliwa namna gani, tuseme kidogo juu ya dunia kwa **wakati** alipozaliwa. Mfalme mkubwa katika Roma, Kaisari Augusto, alitawala inchi nyingi kupita inchi ya Wayuda. Lakini ufalme wa Roma haukuzuiza shauri la Mungu kutuma Mkombozi duniani. Ndiyo, Mungu alikusudi kutumika na Waroma kutimiza maneno manabii waliyosema mbele.

Unakumbuka masemo ya nabii Mika aliyeishi miaka 700 mbele ya kuja kwa Masiya? Mika alitangaza ya kwamba Masiya atazaliwa katika **Betelehemu**, mji wa jamaa ya Daudi. Lakini Maria, atakayezaa Yesu hakupanga katika Betelehemu, lakini katika **Nazareti**, ndio mji karibu kilomètres 150 toka Betelehemu kwa upande wa kaskazini. Basi namna gani Masiya atazaliwa katika Betelehemu?

Eh rafiki, hakuna neno linaloweza kushinda Bwana Mungu! Yeye ni Mungu, naye ni juu ya maneno yote yanayotokea hapa duniani. Anajua kila neno litakalotokea. Leo tutasoma ya kwamba, wakati saa ilipokaribia kwa kuzaa mtoto wake, mfalme mkubwa wa Roma alitoa amri kusema sharti kila mwanamume na mwanamke aendee mji wa wazazi wake aandikwe na kulipa kodi. Hivi ilipasa Maria na Yosefu kwenda Betelehemu, mji wa Mfalme Daudi, kwa sababu walikuwa wazao wa Daudi. Sasa tufungue Habari Njema ya Luka, sura 2, na kusikia namna Yesu Masiya alivyozaliwa katika **Betelehemu**, kama Mungu alivyoahidi miaka mingi mbele.

Maandiko yanasema:

> (Luka 2) *1 Katika siku zile amri ilitoka kwa **Kaisari Augusto** ili majina ya watu wote katika dunia yaandikwe. . . 3 Na watu wote walikwenda kuandikwa, kila mtu kwa mji wake. 4 Na Yosefu vilevile aliondoka Galilaya toka mji wa **Nazareti,** akapanda kwenda Yuda hata mji wa Daudi ulioitwa **Betelehemu**, (kwa sababu alikuwa wa jamaa ya Daudi,) 5 aandikwe pamoja na Maria aliyepatana kuwa mke wake, naye ana mimba. 6 Walipokuwa pale, siku zake za kuzaa zilitimia. 7 **Akazaa mwanamume wake wa kwanza**, akamfunga nguo za kitoto, akamlalisha katika sanduku ya kulisha nyama, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

Sharti tuache kwanza hapa. Uliona pahali gani Masiya alipozaliwa? Lilikuwa kao la namna gani? Masiya alizaliwa kama **mkulima**, si kama mtajiri. Alizaliwa ndani ya zizi la nyama kwa sababu nafasi ilikosa nyumbani mwa wageni. Yule atakayekuwa Mwokozi na Mwamuzi wa dunia alizaliwa ndani ya zizi la kunuka la nyama! Labda unafikili: "Ni nguvu kuamini neno hili. Kama Yesu ni Mwokozi wa dunia na Bwana wa utukufu atakayehukumu wana wa Adamu, kwa sababu gani hakuzaliwa ndani ya nyumba ya mtawala, na utukufu mkubwa, ili watu wote waweze kujua ya kwamba yeye ni Mfalme wa wafalme na Bwana wa wabwana?"

Inatupasa kukumbuka, rafiki, ya kwamba **mawazo ya Mungu ni mbali na mawazo ya watu,** na utukufu wa Mungu ni mbali na utukufu wa dunia. Yesu alizaliwa pamoja na utukufu mkubwa kweli, lakini zaidi ya wana wa Adamu hawakutambua neno hili, kwa sababu **utukufu wa Mungu** na **utukufu wa dunia** ni mbalimbali kabisa.

Kama mfano, labda umeona watajiri wanaopanga ndani ya nyumba kubwa na za mapambo, wakivaa mavazi mazuri sana na

kukaa bila masumbuko kwa sababu wana watumishi kuwasaidia na kila kitu wanachotaka. Huu ndio utukufu wa dunia. Lakini, **utukufu wa Mungu** ni mbali na **utukufu wa dunia**. Kwa sababu hii Masiya, aliyekuja toka mbele ya Mungu, hakuzaliwa katika raha na wingi wa mali. Hakuwa kama watajiri wingi wasiofahamu taabu na masumbuko ya watu masikini. Sivyo. Yule aliyetumwa na Mungu kuokoa wana wa Adamu toka uwezo wa Shetani na zambi alizaliwa katika umasikini, hata ndani ya zizi la nyama! Hivi hakuna mtu anayeweza kusema Masiya alikuja kuokoa watajiri tu, au ya kwamba hafahamu mahitaji ya watu masikini. Mungu anataka kila mtu kujua ya kwamba Mkombozi ambaye alimtuma duniani alikuja kuokoa **kila mtu** ambaye anamwamini—wazee na vijana, wanaume na wanawake, watajiri na wamasikini, walio huru na watumwa. Hivi Maandiko yanasema: *"Kwa maana munajua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, namna alivyokuwa tajiri, lakini kwa* ***ajili yenu alikuwa masikini,*** *hata ninyi mupate kuwa* ***matajiri*** *kwa* ***umasikini wake****."* (2 Wakorinto 8:9) {Labda sababu nyingine kwa kuzaliwa kwa Yesu ndani ya zizi la nyama ni kutukumbusha ya kwamba yeye ni "Mwana-kondoo ya Mungu." Wana-kondoo wanazaliwa ndani ya mazizi. Tutajifunza zaidi juu ya Yesu kama "Mwana-kondoo ya Mungu" ndani ya somo #64.}

Everyday Publications Inc
@ 2010

Sasa tuendelee na habari za kuzaliwa kwa Masiya na kusoma sehemu yake ya kushangaza zaidi. Usiku Yesu alipozaliwa ndani ya nyumba ya nyama, Mungu alituma malaika zake karibu na wachungaji kondoo wengine waliokuwa wakichunga kundi lao shambani karibu na Betelehemu. Sikiliza habari nzuri ambazo Mungu aliwajulisha juu ya kuzaliwa kwa Masiya.

Maandiko yanasema:

> (Luka 2) *8 Katika inchi ile wachungaji walikuwa wakikaa katika shamba, wakilinda kundi lao usiku, kwa zamu. 9 Na tazama,* ***malaika ya Bwana*** *aliwatokea, utukufu wa Bwana ukawaangazia, wakaogopa sana. 10 Malaika akawaambia: Musiogope, kwani tazama, ninawaletea ninyi Habari Njema ya furaha kubwa itakayokuwa kwa watu wote. 11 Kwa sababu* ***leo amezaliwa kwenu katika mji wa Daudi, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana.*** {*Kristo* ni neno kwa Kiyunani kwa *Masiya*, ndilo neno kwa Kiebrania, maana yake *Mpakaliwa*} *12 Na hii ni alama kwenu, mutakuta mtoto amefungwa nguo za kitoto, amelala katika sanduku ya kulisha nyama.*
>
> *13 Gafula walikuwa pamoja na malaika,* ***makutano ya jeshi la***

> ***mbingu**, wakisifu Mungu, wakisema: 14 **Utukufu kwa Mungu aliye juu, na salama duniani, katika watu ambao wanampendeza.***
>
> *15 Walipoondoka malaika kwenda mbingu, wachungaji walisemezana: Twende zetu hata Betelehemu, tuone neno hili lililofanyikana, kama Bwana alivyotujulisha. 16 Wakakwenda kwa haraka, wakakuta Maria na Yosefu, na mtoto amelala katika sanduku ya kulisha nyama. 17 Na wakati walipoona walipasha habari za neno hili lililosemwa nao juu ya huyu mtoto. 18 Na wote waliosikia walishangaa kwa maneno waliyoambiwa na wachungaji. 19 Lakini Maria akashika maneno haya yote, akayafikili kwa moyo wake. 20 **Na wachungaji walirudi wakitukuza Mungu na kumsifu kwa maneno yote ambayo walisikia na kuyaona kama walivyoambiwa.**"* Amina.

Mungu alijulisha nani kwanza habari njema juu ya kuzaliwa kwa Masiya? Mfalme wa Roma? Au watajiri, au viongozi wa watu kwa maneno ya dini? Hapana. Mungu alitangaza habari za kuzaliwa kwa Masiya kwanza kwa wakulima, kwa wachungaji wanyenyekevu waliongojea kuja kwake! Bila shaka wachungaji waliona furaha kubwa wakati walipoona mtoto Yesu! Na kweli walipendelewa sana! **Walikuwa wamemwona yule ambaye manabii wote waliandika habari zake: Masiya, Mwokozi wa dunia, Neno la Milele la Mungu ndani ya mwili kidogo wa mtoto mchanga!**

Everyday Publications Inc. © 2010

Tuendelee sasa na kuona nini ilitokea karibu mwaka mmoja nyuma ya kuzaliwa kwa Yesu. Tuliona ya kwamba Mungu alitangaza kuzaliwa kwa Yesu kwa **wakulima** kwa njia ya **malaika** zake waliotokea mbinguni. Sasa tutasikia ya kwamba Mungu alitangaza kuzaliwa kwa Masiya kwa **waakili** kwa njia ya **nyota** nzuri sana iliyoonekana mbinguni. Sikia maneno yanayoandikwa ndani ya Habari Njema ya Matayo, sura 2.

Maandiko yanasema:

> (Matayo 2) *1 Wakati Yesu alipozaliwa katika Betelehemu ya Yudea siku za mfalme Herode, tazama, waakili wa mashariki walifika Yerusalema, 2 wakisema: Yuko wapi yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayuda? Kwa sababu **tuliona nyota yake katika mashariki, nasi tumekuja kumwabudu.** 3 Wakati mfalme Herode aliposikia maneno haya, alifazaika, na Yerusalema pia pamoja naye. 4 Alikusanya wakubwa wa makuhani wote na waandishi wa watu, akawauliza pahali Kristo atakapozaliwa. 5 Nao wakamwambia: Katika Betelehemu ya*

*Yudea; kwa maana* **ndivyo ilivyoandikwa na nabii:** *6 Nawe Betelehemu, inchi ya Yuda, wewe ni mdogo sana katikati ya wakubwa wa Yuda: kwa sababu kwako atatoka mtawala, atakayechunga watu wangu Israeli. 7 Kisha Herode akaita waakili kwa siri, akapata hakika kwao wakati nyota ilipoonekana. 8 Akawatuma Betelehemu, akasema: Shikeni njia, mutafute sana maneno ya mtoto; mukikwisha kumwona, muniletee habari, ili mimi niende kumwabudu vilevile.* (Lakini rohoni mwake Mfalme Herode alikusudi kuua mtoto, kwa sababu hakutaka mtu ye yote kuwa mfalme ila yeye mwenyewe!)

*9 Nao (waakili) wakati waliposikia maneno ya mfalme wakashika njia; na tazama, ile nyota waliyoona katika mashariki iliwatangulia, hata ikafika na kusimama juu ya pahali mtoto alipokuwa. 10 Nao walipoona nyota walifurahi na furaha kubwa sana. 11 Wakaingia nyumbani, wakaona mtoto pamoja na Maria mama yake, wakaanguka, wakamwabudu; nao walipokwisha kufungua hazina zao, walimtolea zawadi, zahabu, na uvumba na manemane. 12 Nao wakikwisha kuonywa na Mungu katika ndoto wasirudi kwa Herode, wakakwenda kwao kwa njia nyingine.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

Hili ndilo jumlisho fupi la habari za kuzaliwa kwa Masiya. Tunaweza kusema nini juu ya maneno yote ambayo tumesikia leo? Neno moja tunaloweza kusema, neno lililo hakika kabisa ni ya kwamba kuzaliwa kwa Yesu, Masiya kulikuwa **namna nyingine** na kuzaliwa kwa watoto wote duniani! Katikati ya manabii na wafalme na watu wote wa dunia hakuna mwingine aliyezaliwa namna Yesu alivyozaliwa.

* Tumeona leo ya kwamba Masiya alizaliwa na **bikira, kwa uwezo wa Mungu, namna manabii wa Mungu walivyotabiri.**

* Tumesikia ya kwamba Yesu alizaliwa katika mji wa **Betelehemu**, kama nabii Mika alivyotabiri miaka 700 mbele.

* Tuliona vilevile ya kwamba **Mungu alituma malaika yake na nuru ya utukufu toka mbinguni** kwa wachungaji wengine kuwajulisha habari njema, wakisema: *"Ninawaletea ninyi Habari Njema ya furaha kubwa itakayokuwa kwa watu wote. Kwa sababu leo amezaliwa kwenu katika mji wa Daudi Mwokozi, ndiye Kristo Bwana!"*

* Halafu tuliona ya kwamba **makutano ya malaika walionekana pamoja na malaika ya kwanza, wakisifu Mungu** na kusema, *"Utukufu kwa Mungu aliye juu, na salama duniani, katika watu ambao wanampendeza!"*

***** Tuliona vilevile ya kwamba **Mungu aliweka nyota kubwa kwa mbingu** kutangaza kwa waakili waliokaa katika inchi ya mbali, ya kwamba Masiya, Mfalme wa wafalme, Mwokozi wa wenye zambi amezaliwa!

Rafiki, tuseme nini juu ya maneno haya yote? Tunaweza kusema ya kwamba: Hakuna mtu aliyezaliwa kama Mtu huyu. **Kuzaliwa kwa Yesu kulikuwa ya namna peke yake.** Haiwezekani kusawanisha Yesu na mtu ye yote kwa maneno ya kuzaliwa kwake. Yesu ni mkubwa kupita nabii. **Ni yeye ambaye manabii wote walisema juu yake. Yeye ni Masiya toka mbingu!**

Rafiki, kama Yesu angalikuwa nabii tu sawasawa na manabii wengine, basi **kwa nini** manabii wote wa Mungu walitangaza kuja kwake mbele ya kuzaliwa kwake? **Kwa nini** malaika walishuka toka mbingu kutukuza kuzaliwa kwake? Kama Yesu angalikuwa nabii tu kama manabii wengi wengine, **kwa sababu gani** Mungu aliweka nyota kubwa mbinguni kutangaza kuzaliwa kwake? Na kwa **sababu gani** alizaliwa na bikira? **Waza sana juu ya maulizo haya makubwa ambayo Mungu anataka ujibu.**

Everyday Publications Inc © 2010

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutaona namna gani Yesu Masiya alianza kazi yake duniani . . .

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya habari za malaika kwa wachungaji:

> ***"Musiogope, kwani tazama, ninawaletea ninyi Habari Njema ya furaha kubwa itakayokuwa kwa watu wote. Kwa sababu leo amezaliwa kwenu katika mji wa Daudi, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana!"*** (Luka 2:10,11)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 63

# Mwana Mtakatifu

### Luka 2; Matayo 3,4

Asante kwa kufika kusoma tena pamoja nasi ndani ya mfulizo *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo la mbele katika kitabu cha Habari Njema takatifu {*Injil*}, tulisoma habari nzuri kabisa za kuzaliwa kwa Masiya. **Hakuna mtu aliyezaliwa namna Yesu alivyozaliwa.** Alizaliwa na bikira, kwa uwezo wa Mungu, katika mji wa Betelehemu, kama manabii walivyotabiri mbele. Usiku Yesu alipozaliwa, Mungu alituma jeshi la malaika za kungaa karibu na wachungaji walioshinda usiku mashambani yaliyozunguka Betelehemu. Mmoja wa malaika alisema na wachungaji: *"Ninawaletea ninyi Habari Njema ya furaha kubwa itakayokuwa kwa **watu wote**. Kwa sababu leo amezaliwa kwenu katika mji wa Daudi, **Mwokozi,** ndiye Kristo Bwana!"* (Luka 2:10,11)

Leo tunakusudi kujifunza kama **Yesu alikuwa namna gani wakati alipokuwa mtoto na kama mtu wa kukomea.** Kitabu cha Habari kinaonyesha ya kwamba nyuma ya kuzaliwa kwa Yesu, Yosefu na Maria walikuwa na wana wane na binti vilevile. Mtoto Yesu alipata nguvu pamoja na wadogo wake ndani ya nyumba iliyojaa kabisa kwa upande wa kaskazini wa Palestina, kwa Nazareti. Kama munavyojua, Yosefu hakuzaa Yesu, lakini kwa macho ya watu, Yesu alikuwa mwana wa Yosefu. Yosefu alikuwa seremala, na Yesu alishiriki ndani ya kazi hii vilevile wakati alipokaa nyumbani mwa Yosefu na Maria mama yake. Hivi Yesu alijuana na kazi ya nguvu. Maandiko Matakatifu yanasema: *"Yesu alizidi kuendelea katika akili na kimo, na katika neema mbele ya Mungu na watu."* (Luka 2:52)

Kama watoto wote, Yesu alikula na kulala, alicheza na kujifunza chuoni. Lakini kwa njia moja alikuwa namna nyingine ya watoto wengine. Unajua kama ilikuwa nini? Ni neno hili: **Yesu hakufanya zambi kamwe!** Masemo yasiyokuwa haki hayakutoka kinywani mwake hata mara moja. (1 Petro 2:22) Hakusema na mtu kamwe, "Unisamehe", kwa sababu hakutendea mtu ye yote mabaya

Everyday Publications Inc. @ 2010

kamwe. Hakuweza kufanya zambi, kwa sababu **shina la zambi halikuwa ndani yake**. Alikuwa na tabia takatifu. Uovu haukuwa ndani yake. Alifanya tu yaliyopendeza Mungu. **Alikuwa na mwili namna ya miili yetu lakini hakuwa na tabia ya zambi kama sisi.** Haya ndiyo maneno Maandiko yanayosema: *"Hatuna kuhani mkubwa asiyeweza kuchukua maneno yetu ya uzaifu; lakini yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, lakini **pasipo kufanya zambi**."* (Waebrania 4:14,15)

Wakati Yesu alipokuwa na miaka makumi tatu, **saa imefika kwa yeye kuanza kazi yake** kama Mwokozi wa dunia. Siku moja aliagana na watu wa jamaa yake, akatoka mji wa Nazareti na kwenda kwa mto Yorodani pahali nabii Yoane {Yahya} alipokuwa akihubiri na kubatiza watu ndani ya maji.

Unakumbuka Yoane aliyezaliwa miezi sita mbele ya Yesu? Yoane ndiye nabii aliyetumwa na Mungu kutayarisha mioyo ya watu ili waweze kutubu zambi zao na kukaribisha Masiya ambaye Mungu alikuwa ametuma. Sikiliza maneno yanayoandikwa ndani ya Habari Njema juu ya nabii Yoane na namna gani alitayarisha njia kwa Masiya.

Everyday Publications Inc @ 2010

Ndani ya Habari Njema ya Matayo, sura 3, Maandiko yanasema:

> (Matayo 3) *1 Siku zile Yoane Mbatizaji alikuja, akihubiri katika jangwa la Yudea, 2 akisema: **Tubuni, sababu ufalme wa mbinguni umekaribia**. 3 Kwa sababu huyu ndiye aliyesemwa na nabii Isaya, akisema: Sauti ya mtu akilia katika jangwa, **Tengenezeni njia ya Bwana, nyosheni mapito yake.** 4 Naye Yoane mwenyewe alikuwa na vazi lake la singa za ngamia, na mkaba wa ngozi kwa kiuno chake; na chakula chake kilikuwa nzige na asali ya poli. 5 Halafu walimkwendea Yerusalema na Yudea wote, na inchi zote karibu na Yorodani, wakabatizwa naye katika mto wa Yorodani, wakikiri zambi zao.*

Tuache kwanza kusoma na tufikili juu ya maneno tunayosoma. Ulisikia habari za Yoane? Tunaweza kuzijumlisha hivi: "Tubuni zambi zenu! Mwache kutenda matendo yenu maovu, na mujitayarishe kukutana na Masiya mtakatifu aliyefika kwenu toka mbinguni!" Wale waliotubu zambi zao mbele ya Mungu walibatizwa na Yoane ndani ya mto. Hivi nabii Yoane alianza kuitwa *Yoane Mbatizaji*. Kubatizwa ndani ya maji hakukuweza kusukula watu toka zambi zao. Kulikuwa alama tu kuonyesha ya kwamba walikuwa wametubu zambi zao na walikuwa tayari kupokea Masiya kama Mwokozi wao.

Wengine wa wale waliokubali kwa Yoane kuwabatiza walikuwa watu wa mbili za jamii za kujulikana zaidi za Wayuda. Jamii hizi walikuwa *Wasadukayo* na *Wafarisayo*. **Wasadukayo** walikuwa Wayuda wenye mali nyingi zaidi na walikuwa na ushawishi ndani ya serikali ya Waroma. Lakini mioyoni mwao waliona bule Maandiko ya Manabii. **Wafarisayo** walikuwa wafundi kwa maneno ya dini waliokuwa na bidii sana kwa maneno ya kuomba, kufunga chakula, kutoa zaka na kulipa sehemu moja ya kumi. Lakini ibada yao ilikuwa bule, kwa sababu walijaribu kuwa na haki mbele ya Mungu kwa njia ya kazi zao wenyewe. Vilevile Wafarisayo walichanganya mazoeo yao na Neno la kweli la Mungu. Hivi, ibada yao ya Mungu ilikuwa neno la kuonekana tu na walizarau watu wale wasioshirikiana nao. Kwa ufupi tunaona ya kwamba Wafarisayo na Wasadukayo waliheshimu Mungu na **midomo** yao lakini **mioyo** yao ilikuwa mbali naye.

Sasa tuendelee kusoma ndani ya Habari Njema na kusikia namna Yoane alivyohamakia wafundi hawa wa dini kwa sababu ya unafiki wao. Maandiko yanasema ndani ya Matayo 3, kuanza na shairi 7:

Everyday Publications Inc @ 2010

> (Matayo 3) *7 Lakini akiona wengi wa Wafarisayo na Wasadukayo wakikuja kwa ubatizo wake, aliwaambia: Uzao wa nyoka, ni nani ambaye aliwaonya ninyi kukimbia hasira itakayokuja? 8 Basi zaeni matunda yanayofaa na toba: 9 musifikili kusema ndani yenu, Tuna Abrahamu, ndiye baba yetu; kwani ninawaambia ninyi, Mungu anaweza katika mawe haya kunyanyulia Abrahamu watoto. 10 Na shoka limekwisha kuwekwa katika shina la miti; basi kila mti usiozaa matunda mazuri unakatwa, na unatupwa katika moto. 11 Kweli mimi ninawabatiza ninyi kwa maji hata toba;* ***lakini yeye anayekuja nyuma yangu ana nguvu kuliko mimi, na sistahili hata kuchukua viatu vyake; yeye atawabatiza ninyi kwa Roho Mtakatifu na kwa moto.*** *12 Pepeto lake ni katika mkono wake, naye atasafisha sana kiwanja chake; na atakusanya ngano yake katika gala, lakini makanda atayateketeza kwa moto usiozimika!*
>
> *13 Wakati ule* ***Yesu*** *akatoka Galilaya hata kufika Yorodani kwa Yoane abatizwe naye. 14 Lakini Yoane alitaka kumzuiza, akisema: Mimi ninahitaji kubatizwa nawe, nawe unakuja kwangu? 15 Yesu akajibu akamwambia: Kubali hivi sasa: sababu hivi imetupasa* ***kutimiza haki yote****. Basi Yoane akakubali.*

Hivi Yoane alibatiza Bwana Yesu ndani ya mto Yorodani. Labda

watu wengine wanauliza, "Kwa sababu gani Yesu, asiyekuwa na zambi, aliomba Yoane kumbatiza?" Ndiyo, Bwana Yesu hakuhitaji kutubu kwa sababu hakufanya zambi hata moja. Halafu kwa nini Yesu alifikia Yoane ili Yoane aweze kumbatiza namna alivyobatiza wenye zambi? Yesu alisema nini juu ya neno hili? Yesu alisema na Yoane, "*Kubali hivi sasa: sababu hivi imetupasa kutimiza haki yote.*" Kwa njia ya kubatizwa, Yesu alikuwa mfano kwetu tuweze kubatizwa vilevile, lakini zaidi ya ile alionyesha ya kwamba alikuja kuishi kama sisi na kufa kwa ajili yetu.

Kwa mwisho wa sura hii (Matayo 3) Maandiko yanasema:

> (Matayo 3) *16 Wakati **Yesu** alipobatizwa mara moja alitoka katika maji; na tazama, mbingu zikamfunguliwa, akaona **Roho ya Mungu** akishuka kama hua, akikuja juu yake; 17 na tazama, **sauti kutoka mbinguni** ikisema: "Huyu ni Mwana wangu, mpendwa wangu, ninapendezwa naye."* Amina.

Rafiki, ilikuwa sauti ya nani iliyosikiwa toka mbingu? Ilikuwa sauti ya Bwana Mungu! Mungu alisema nini? Mungu alisema na Yesu, ***"Huyu ni Mwana wangu, mpendwa wangu, ninapendezwa naye."*** Tumesoma mbele ndani ya Maandiko Matakatifu ya kwamba nabii Daudi na malaika Gabrieli waliita Masiya *"Mwana wa Mungu."* Sasa tunasikia Mungu yeye mwenyewe akiita Yesu *"Mwana wangu, mpendwa wangu!"* Kwa sababu gani Mungu aliita Yesu Mwana wake? Kama tulivyoona mbele, Yesu anaitwa *Mwana wa Mungu* kwa sababu alitoka mbinguni. Yesu hakuwa na baba ya dunia. Mungu aliweka Mwana wake ndani ya tumbo la uzazi la bikira. Hapa tunaona sababu nyingine. **Mungu aliita Yesu Mwana wake kumweka mbali na wote wengine.**

Everyday Publications Inc @ 2010

Kwa njia gani Yesu alikuwa namna nyingine na wana wa Adamu? Kwa njia ile yeye ni namna nyingine nasi vilevile. Kila mzao wa Adamu ana tabia inayochafuwa na zambi, lakini **tabia ya Yesu haikuchafuwa na zambi**. Hakuwa na zambi hata moja kwa sababu alizaliwa kwa njia ya Roho Mtakatifu. Masiya alikamata **mwili wa mtu** kama sisi, lakini hakukamata **tabia yetu ya zambi.** Alikuwa na tabia takatifu na kamilifu! Kwa sababu hii Mungu, Mtakatifu aliweza kufurahia Yesu, namna baba anavyofurahia mwana mwaminifu, mwenye utii. Watu wanasema ya kwamba mwana ni kivuli cha baba yake. Kila mtu anayeona mwana anajua kama baba yake ni mtu wa namna gani. Vivyo hivyo, kila mtu anayejua Yesu anajua kama Mungu ni namna gani, kwa sababu Yesu ndiye aliyetoka kwa

Mungu **kuonyesha tabia ya Mungu**. Hakuna mtu aliyeona Mungu, lakini Masiya amemfunua! Yesu tu ana tabia ya mtu iliyo takatifu, kwa sababu yeye ndiye wa pekee aliyetoka kwa Roho Mtakatifu wa Mungu! Kwa sababu hii Mungu hakuwa na haya kufanyiza sauti yake kusikiwa toka mbinguni ikisema, *"Huyu ni Mwana wangu, mpendwa wangu,* ***ninapendezwa naye."***

Ndani ya saa nusu inayobaki leo, tutaanza kusoma ndani ya sura 4 kusikia nini ilitokea wakati Yoane alipokwisha kubatiza Yesu. Maandiko yanasema:

> (Matayo 4) *1 Kisha Yesu aliongozwa na Roho jangwani ajaribiwe na Shetani. 2* ***Akafunga siku makumi ine mchana na usiku, nyuma akaona njaa.*** *3 Mjaribu akakuja kwake, akamwambia:* ***Kama ukiwa Mwana wa Mungu,*** *amuru mawe haya yawe mikate. 4 Naye akijibu akasema:* ***Imeandikwa,*** *Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno linalotoka katika kinywa cha Mungu. 5 Kisha Shetani akampeleka hata mji mtakatifu, akamweka juu ya mnara wa hekalu, 6 akamwambia:* ***Kama ukiwa Mwana wa Mungu****, ujitupe mwenyewe chini; kwa sababu imeandikwa, Atakuagizia malaika zake, na mikononi mwao watakuchukua, usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe. 7 Yesu akamwambia:* ***Tena imeandikwa****, Usijaribu Bwana Mungu wako. 8 Tena, Shetani akamchukua hata mlima mrefu sana, akamwonyesha falme zote za ulimwengu, na utukufu wao, 9 akamwambia: Haya yote nitakupa kama ukianguka kuniabudu. 10 Ndipo Yesu alimwambia: Kwenda zako, Shetani; kwa sababu* ***imeandikwa,*** *Uabudu Bwana Mungu wako, umtumikie yeye peke yake. 11 Kisha Shetani akamwacha; na tazama, malaika wakakuja wakamtumikia.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

Mara tatu Shetani alijaribu kuvuta Yesu kumwasi yeye na kufanya zambi. Mara tatu zote Yesu alijibu Shetani kwa njia ya kutumia mashairi toka Neno la Mungu. Namna Shetani alivyojaribu Adamu na Hawa katika Shamba la Paradiso {Edeni}, vivyo hivyo alijaribu Bwana Yesu kufanya zambi katika jangwa. **Lakini Yesu hakufanya zambi.**

Kwa nini Shetani alijaribu Yesu? Kwa sababu alijua Yesu ni Mkombozi mtakatifu aliyekuja duniani toka mbingu kuokoa wana wa Adamu toka utawala wake. Shetani alijua ya kwamba Yesu akifanya hata zambi moja, hataweza kuokoa wana wa Adamu toka utawala wa zambi. Kwa sababu hii Shetani alichokoza Yesu na kujaribu kumdanganya. Lakini Yesu hakuanguka ndani ya mtego wa Shetani.

Ndiyo, Shetani alishinda na kuchafua wazazi wetu, Adamu na Hawa, lakini hakuweza kushinda Mwana wa Mungu. **Bwana Yesu hakuweza kufanya zambi kwa sababu Mungu hawezi kufanya zambi.** Mwana ni kama Baba. Yesu alikuwa Neno la Mungu lililo hai na lenye uwezo kwa mwili wa mtu. Mungu alimtuma duniani kuokoa wana wa Adamu toka uwezo wa Shetani na zambi, kwa sababu Yeye tu alishinda Shetani na zambi. Kwa sababu hii Maandiko yanasema juu ya Masiya:

> *"**Kuhani mkubwa wa namna hii alitufaa sisi sana, aliye mtakatifu, pasipo uovu, wala alama ya uchafu,** aliyetengwa na wenye zambi, aliyekuwa juu kuliko mbingu; **asiye na uhitaji siku zote kama wale makuhani wakubwa wengine,** kwanza kutoa zabihu kwa ajili ya zambi zake mwenyewe, kisha kwa ajili ya watu; maana yeye alifanya hivi mara moja wakati alipojitoa mwenyewe."* (Waebrania 7:26,27)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Rafiki, asante kwa kusoma pamoja nasi. Jaribu sana kukutana nasi kwa mafundisho yetu mara ya nyuma kusikia kwa sababu gani wanafunzi wa nabii Yoane walimwacha kusudi wafuate Yesu . . .

Everyday Publications Inc
@ 2010

Mungu akusaidie kufahamu vizuri maneno yote tuliyosoma leo. Tunakuacha na shairi hili toka Maandiko Matakatifu:

> ***"[Yesu] alionekana kusudi aondoshe zambi zetu; na zambi si ndani yake."*** (1 Yoane 3:5)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## SOMO 64

# MWANA-KONDOO YA MUNGU

### YOANE 1,3

Salama iwe kwako, rafiki, kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha tuweze kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Ni furaha kuweza kuendelea tena na mfulizo wetu *Njia ya Haki*.

Ndani ya masomo mawili ya mbele, tuliona kwamba Masiya alikuwa namna nyingine kwa maneno ya kuzaliwa kwake na tabia yake.

* Kwa maneno ya **kuzaliwa kwake**, tuliona ya kwamba hakuna mtu aliyezaliwa kama Yesu, kwa sababu hakuwa na baba ya dunia. Alizaliwa na bikira, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu ya Mungu.

Everyday Publications Inc
© 2010

* Kwa maneno ya **tabia yake** Yesu alikuwa namna nyingine vilevile. Hakuna mtu mwingine aliyezaliwa na tabia takatifu kama yeye. Alikuwa na mwili kama sisi, lakini hakuwa na tabia yetu ya zambi. Yesu hakuchafuwa na zambi, kwa sababu alikuwa Mwokozi ambaye alitumwa duniani na Mungu kubeba azabu kwa zambi yetu kwa ajili yetu.

Leo tunakusudi kuendelea ndani ya Habari Njema *{Injil}* na kusikia **ushuhuda wa nabii Yoane** *{Yahya}* **juu ya Yesu**. Yoane alikuwa nabii ambaye Mungu alituma kutayarisha njia mbele ya Masiya.

Mbele ya kuendelea na kusoma, vizuri tukumbuke ya kwamba kuna watu wawili walioitwa *Yoane*: nabii Yoane (Mbatizaji), na mtume Yoane. Tusome sasa ndani ya Habari Njema ya Yoane, sura 1, kuanza na shairi 19:

> (Yoane 1) *19 Na huu ni **ushuhuda wake Yoane,** wakati Wayuda walipotuma kwake makuhani na Walawi kutoka Yerusalema wamwulize: Wewe nani? Na alikiri, hakukana lakini alikiri: Mimi siye Kristo (Masiya) . . . 22 Basi wakamwambia: Wewe nani? Tuweze kuwajibu ambao walitutuma. Unasema nini juu yako mwenyewe? 23*

*Akasema: Mimi ni sauti ya mtu anayepaza sauti jangwani, Nyosheni njia ya Bwana . . . 26 Yoane akawajibu, akasema: Mimi ninabatiza kwa maji, lakini mmoja anasimama katikati yenu ambaye hamjui. 27* ***Ndiye anayekuja nyuma yangu,*** *aliyekuwa mbele yangu,* ***wala mimi sistahili kufungua kamba ya kiatu chake.*** *28 Maneno haya yalifanyika kwa Betania ngambo ya Yorodani, pahali alipokuwa Yoane, akibatiza.*

*29 Kesho yake Yoane aliona* ***Yesu*** *anakuja kwake, akasema:* ***Tazama Mwana-kondoo wa Mungu anayechukua zambi ya ulimwengu.*** *30* ***Huyu ndiye ambaye nilisema juu yake, Nyuma yangu anakuja mtu aliyekuwa mbele yangu kwa sababu alikuwa mbele yangu.***

Tuache kwanza hapa na tufikili juu ya ushuhuda wa nabii Yoane. Ulisikia kama alisema juu ya Masiya namna gani? Tusikilize Maandiko tena. Yanasema: *"Yoane aliona Yesu anakuja kwake, akasema: Tazama* ***Mwana-kondoo wa Mungu*** *anayechukua zambi ya ulimwengu!"* Tuliona mbele ya kwamba manabii wa Mungu waliita Masiya na majina mbalimbali kama Mkombozi, Mfalme, Bwana, Neno la Mungu na Mwana wa Mungu. Sasa tunasikia ya kwamba aliitwa ***"Mwana-kondoo wa Mungu."*** Hili ni jina lenye maana zaidi na sharti tuieleze wazi.

Everyday Publications Inc @ 2010

Kwa sababu gani Yoane aliita Yesu Mwana-kondoo wa Mungu? Yesu alikuwa mwana-kondoo? Sivyo, Yesu hakuwa mwana-kondoo. Sisi sote tunajua ya kwamba ni usemi tu. Basi kwa nini nabii Yoane aliita Yesu **Mwana-kondoo wa Mungu**? Kwa nini mtu ye yote angetaka kuwa sawasawa na mwana-kondoo? Kwa nini Yoane alionyesha Yesu na kusema na wanafunzi wake, "*Tazama Mwana-kondoo wa Mungu anayechukua zambi ya ulimwengu!"*?

Kwa kufahamu maana ya jina hili *"Mwana-kondoo wa Mungu"* inatupasa kukumbuka neno Mungu aliloamuru wakati Adamu na Hawa walipokwisha kufanya zambi. Mungu aliamuru ya kwamba malipo kwa zambi ni mauti na hadeze na ya kwamba zambi haziwezi kusamehewa bila kumwangwa kwa damu ya sadaka isiyokuwa na kipaku. Hivi tulisoma ya kwamba mwana wa pili wa Adamu na Hawa, ndiye Abeli, aliamini Mungu, alichinja **mwana-kondoo** na kumtoa kwa Mungu juu ya mzabadu kuondoa (au *kufunika*) zambi yake. Wakati Mungu alipoona damu ya mwana-kondoo, alizima azabu kwa zambi ya Abeli, akamhesabu kuwa mwenye haki, kwa sababu **mwana-kondoo bila hatia alikufa kwa pahali pake**. Hata

hivi Mungu alisema vilevile ya kwamba damu ya mwana-kondoo haitatosha kama malipo kwa zambi kwa milele, kwa sababu bei ya nyama na ile ya mtu si sawasawa. **Mwana-kondoo alikuwa kivuli tu, mfano wa Mkombozi mtakatifu atakayekuja duniani na kumwanga damu yake kuponyesha wenye zambi toka hukumu ya haki ya Mungu.**

Miaka mia saba mbele ya kuzaliwa kwa Yesu, nabii aliandika ya kwamba Masiya atakuwa *"kama* ***mwana-kondoo*** *anayepelekwa kuchinjwa"* kama sadaka kuondoa zambi zetu (Isaya 53:7). Hivi, tangu wakati wa Abeli na kufika wakati wa Masiya, wote walioamini Mungu walitoa sadaka za wana-kondoo. Noa, Abrahamu, Musa, Daudi, Solomono na manabii wote, na wote walioamini Neno la Mungu, walitolea Mungu sadaka za wana-kondoo bila kipaku. Kwa njia hii wao wote walitazamia siku wakati Mungu atakapotuma sadaka ya mwisho, ndiye Mkombozi mtakatifu, atakayemwanga damu yake kama sadaka inayoondoa zambi kwa milele.

Kwa sababu hii, rafiki, wakati nabii Yoane alipoona Yesu akimkaribia, alimwonyesha na mkono na kusema na wanafunzi wake: ***"Tazama Mwana-kondoo wa Mungu anayechukua zambi ya ulimwengu!"*** Kwa njia hii Yoane alijulisha wanafunzi wake ya kwamba Yesu aliyesimama mbele yao alikuwa Masiya, *"Mwana-kondoo"* ambaye Mungu alituma toka mbingu, Sadaka Kamilifu ambaye manabii wote walikuwa wametabiri habari zake. Yesu ni sadaka kamilifu aliyekuja duniani kufa kwa pahali pa wana wa Adamu ili Mungu aweze kutusamehe zambi zetu kwa milele!

Everyday Publications Inc. @ 2010

Kisha Maandiko yanasema:

> (Yoane 1) *35 Tena kesho yake Yoane alikuwa akisimama na wawili katika wanafunzi wake. 36 Akatazama Yesu akitembea, akasema:* ***Tazama Mwana-kondoo wa Mungu.*** *37 Wale wanafunzi wawili wakamsikia akisema, wakafuata Yesu. 38 Yesu akageuka, akawaona wakimfuata, akawaambia: Munatafuta nini? Wakamwambia: Rabi (maana yake, Mwalimu), unakaa wapi? 39 Akawaambia: Kujeni na mutaona. Walikuja na waliona pahali alipokaa; wakakaa kwake siku ile; ilikuwa karibu na saa kumi. 40 Mmoja wa wale wawili waliosikia Yoane, na kumfuata, alikuwa Anderea, ndugu ya Simoni Petro. 41 Huyu akakuta kwanza Simoni, ndugu yake mwenyewe, akamwambia:* ***Tumeona Masiya!*** *. . . 42 Akampeleka kwa Yesu, Yesu akamtazama, akasema: Wewe Simoni, mwana wa Yona, utaitwa Kefa (maana yake jiwe).*

> *43 Kesho yake Yesu alitaka kuondoka kwenda Galilaya, akaona Filipo, akamwambia: Unifuate. 44 Naye Filipo alikuwa mtu wa Betesaida, mji wa Anderea na Petro. 45 Filipo akaona Natanaeli, akamwambia:* ***Tumeona Yeye aliyeandikiwa na Musa katika torati, na manabii waliandika juu yake, Yesu, mtu wa Nazareti, mwana wa Yosefu.*** *46 Natanaeli akamwambia: Kitu kizuri kinaweza kutoka Nazareti? 47 Filipo akamwambia: Kuja uone.*

Hivi tunaona wanafunzi wa Yoane wakianza kufuata Yesu. Kwa nini wanafunzi wa nabii Yoane walimwacha kwa kufuata Bwana Yesu? Walianza kufuata Yesu kwa sababu waliamini maneno ambayo Yoane aliwaambia wakati aliposema Yesu ni Masiya na **Mwana-kondoo wa Mungu, yule ambaye manabii wote wa Mungu walitabiri habari zake!** Hivi, wakati mmoja wa wanafunzi wa Yoane, ndiye Anderea, alipotambua kwamba Yesu alikuwa Masiya, alikwenda kutafuta ndugu yake Simoni Petro, akamwambia: "***Tumeona Masiya!"*** Na wakati mwanafunzi mwingine jina lake Filipo alipotambua kama Yesu alikuwa nani, alifurahi sana sana, akamwambia rafiki yake Natanaeli, ***"Tumeona Yeye aliyeandikiwa na Musa katika torati, na manabii waliandika juu yake, Yesu, mtu wa Nazareti!"***

Everyday Publications Inc
@ 2010

Ndiyo, Anderea na Petro, Filipo na Natanaeli walifurahi sana wakati walipoona Yesu, kwa sababu walijua ya kwamba kwa **elfu za miaka manabii walikuwa wametabiri ya kwamba Masiya atakuja! Sasa waliona Masiya na macho yao wenyewe!** Mungu asifiwe! Mkombozi mwenye uwezo juu yake manabii wote walikuwa wakitabiri alikuwa pale katikati yao! Mungu asifiwe kwa sababu nyuma ya miaka ile mingi sana Masiya alikuwa amefika! Hivi, wanafunzi hawa wane wa Yoane walianza kufuata Yesu, wanafunzi wake wane wa kwanza.

Nyuma ya maneno haya, Maandiko yanasema

> (Matayo 4): *21 Akaendelea mbele, akaona ndugu wengine wawili, Yakobo mwana wa Zebedayo, na Yoane ndugu yake, waliokuwa katika chombo pamoja na Zebedayo baba yao; akawaita: [19* ***Munifuate, nami nitawafanya ninyi kuwa wavuvi wa watu.****] 22 Mara moja wakaacha chombo na baba yao, wakamfuata. 23 Yesu akazunguka katika Galilaya yote, akifundisha katika masunagogi yao, na kuhubiri Habari Njema ya ufalme, na kuponyesha ugonjwa na uzaifu wa kila namna katikati ya watu. 24 Na habari zake zikaenea katika Suria yote: wakamletea wote waliokuwa hawawezi, walioshikwa na*

*magonjwa mbalimbali, nao wenye pepo wachafu, na wenye kifafa, na wenye kupooza; akawaponyesha. 25 Na makutano makubwa wakamfuata, wakitoka Galilaya, na Dekapoli na Yerusalema, na Yudea, na ngambo ya Yorodani.*

Mungu akitaka, ndani ya somo la nyuma, tutaendelea kusoma juu ya namna Bwana Yesu alivyofundisha makutano na kufanya maajabu makubwa. Tutaona ya kwamba masemo yake na kazi zake zilihakikisha ya kwamba **Yesu alikuwa kweli Masiya** juu yake manabii wote walikuwa wameandika! Lakini kwa saa inayobaki leo, tutasoma juu ya maneno yaliyopata **nabii Yoane**. Kama tulivyoona, wakati Yoane alipotangaza ya kwamba Yesu alikuwa Masiya, wanafunzi wake walianza kumwacha kusudi waweze kufuata **Bwana Yesu**. Neno hili lilifurahisha Yoane? **Alipendezwa kwa sababu wanafunzi wake walikuwa wamemwacha na kwenda kufuata Yesu?** Unafikili nini?

Sikiliza maneno yanayoandikwa ndani ya Habari Njema ya Yoane, sura 3.

Everyday Publications Inc
@ 2010

(Yoane 3) *26 Wakakuja kwa Yoane, wakamwambia: Rabi, yeye aliyekuwa pamoja nawe ngambo ya Yorodani, ambaye ulimshuhudia, tazama yeye anabatizwa, na watu wote wanakwenda kwake. 27 Yoane akajibu, akasema: Mtu hawezi kupokea kitu isipokuwa amepewa toka mbinguni. 28 Ninyi wenyewe munanishuhudia ya kwamba nilisema, Mimi si Kristo, lakini nimetumwa mbele yake. 29 Mwenye bibi arusi ndiye bwana arusi; lakini rafiki yake bwana arusi anayesimama na kumsikia, anafurahi sana kwa sababu ya sauti ya bwana arusi; basi* ***hii furaha yangu imetimia****. 30* ***Sharti yeye azidi, lakini sharti mimi nipunguke****.*

Unafikili nini juu ya maneno haya? Yoane alionyesha **furaha kubwa** wakati wanafunzi wake walipomwacha kusudi wafuate Masiya! Furaha yake ilitimia kwa sababu **alikuwa ametimiza kazi yake**; alikuwa ametayarisha njia mbele ya Masiya. **Kama nabii wa kweli wa Mungu**, neno Yoane alilotaka kupita maneno yote mengine lilikuwa kuongoza watu karibu na **Masiya**. Yoane alikuwa namna nyingine na viongozi wengi wa dini kwa wakati wa sasa! **Kiongozi mzuri kwa maneno ya roho atakuonyeshea kila mara njia kufika karibu na Bwana Yesu, kwa sababu Yesu ndiye wa pekee anayeweza kukufikisha kwa Mungu mtakatifu mbinguni.** Yoane alijua ya kwamba kulikuwa na **manabii wengi wa Mungu**, lakini **Mwokozi mmoja** tu! Kwa sababu hii alisema: *"Anayeamini Mwana*

*ana uzima wa milele; na asiyetii Mwana hataona uzima, lakini gazabu ya Mungu inakaa juu yake." (*Yoane 3:36)

Juu ya mwisho wa maisha ya Yoane, Maandiko yanasema:

> *"Kwa maneno mengi mengine aliwahubiria watu [juu ya Masiya]. Lakini Herode mtawala akihamakiwa naye, kwa neno la Herodia [ambaye alimwoa], mke wa Filipo, ndugu yake, na kwa maovu yote ambayo aliyafanya Herode, akaongeza neno hili juu ya maneno haya yote, akafunga Yoane katika kifungo."* (Luka 3:18-20)

Mwishoni Herode aliagiza Yoane akatiwe kichwa kwa kupendeza mke wake (ona Marko 6:17,27). Hivi, Yoane alifikia utukufu wa Mungu mbinguni.

Maandiko yanatupasha ya kwamba Yoane alikuwa nabii mkubwa, hata mkubwa kupita manabii ambao walimtangulia. Kwa njia gani Yoane alikuwa mkubwa kupita manabii wengine? Hili ndilo jibu: **Manabii wote wengine** walitangaza: "**Masiya atakuja!** Atakuja! Atakuja!" Lakini nabii Yoane alitangaza: "**Masiya amefika**! **Yeye ni hapa!** Jina lake ni Yesu! Tazameni! Mwana-kondoo wa Mungu atakayeuawa kuondoa zambi amekuja! Mumfuate Yeye!" Hivi Yoane alitimiza kazi yake kama nabii mwenye sifa aliyetayarisha njia mbele ya Masiya.

Everyday Publications Inc
@ 2010

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ikipendeza Mungu, ndani ya somo la nyuma, tutaendelea ndani ya Habari Njema takatifu na kuona kwa sababu gani Yesu aliitwa Mganga Mkubwa.

Mungu akupe ufahamu kwa maneno yote tuliyojifunza leo. Hakuna neno lililo kubwa kuliko tangazo la nabii Yoane juu ya Masiya, wakati aliposema,

> ***"Tazama Mwana-kondoo wa Mungu anayechukua zambi ya ulimwengu!"*** (Yoane 1:29)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 65

# Mganga Mkubwa

### Marko 1,2

Salama iwe kwako, rafiki. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea tena leo na mfulizo wetu *Njia ya Haki*.

Zaidi ya wasomaji wetu wanajua ya kwamba kwa safari yetu ndani ya Maandiko Matakatifu, tumefika kwa kitabu cha Habari Njema {*Injil*}. Hiki ndicho kitabu kitakatifu ambacho kinaonyesha Habari Njema juu ya Masiya aliyekuja duniani kufungua wana wa Adamu toka utawala wa Shetani na zambi. Ndani ya somo la mbele, tuliona ya kwamba Yesu Masiya alianza kufikia vijiji, aki**fundisha** makutano ya watu na aki**ponyesha** kila namna ya ugonjwa katikati ya watu. Kwa njia hii jina lake lilianza kujulikana katika inchi nzima.

Leo tunaendelea kusoma juu ya Yesu Masiya na kuona kwa njia gani **mafundisho na kazi zake** zilikuwa namna nyingine kabisa na watu wote ambao walimtangulia. Yesu hakuwa na mke, nyumba, au mali ya dunia. Alikuwa namna nyingine na watu wote. Aliweka roho juu ya neno moja tu, ndilo kufanya mapenzi yake ambaye alimtuma, na kutimiza kazi ambayo Mungu alimpa kufanya.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Ndani ya Habari Njema ya Marko, sura ya kwanza, Maandiko yanasema:

> (Marko 1) *21 [Yesu na wanafunzi wake] walikwenda kwa mji wa Kapernaumu, na siku ya sabato aliingia katika sunagogi, akafundisha. 22 Na walishangaa kwa mafundisho yake sababu* ***aliwafundisha kama mtu mwenye mamlaka, wala si kama waandishi.*** *23 Ndani ya sunagogi alikuwa mtu mmoja mwenye pepo mchafu. Mara moja akapaza sauti, 24 akasema: Ee, Yesu wa Nazareti, tuna nini nawe? Umekuja hapa kutuangamiza sisi? Ninatambua wewe ni nani, ndiwe Mtakatifu wa Mungu. 25 Yesu alimhamakia, akasema: Nyamaza umtoke! 26 Pepo mchafu alipasua mtu, akalia kwa sauti kubwa,* ***akatoka kwake****. 27 Na wote walishangaa sana, wakaulizana, wakasema: Neno gani hili: Ndiyo mafundisho mapya yenye uwezo; anaamuru pepo wachafu na wanamtii! 28 Na sasa hivi habari zake zikatangazwa pahali po pote katika inchi yote iliyozunguka Galilaya.*

Mafundisho ya Yesu yalikuwa namna nyingine kabisa na mafundisho ya walimu wa sheria, ndio waandishi. Watu wote waliosikiliza Yesu ndani ya sunagogi {nyumba iliyosimamishwa kwa kuabudu na kufundisha Maandiko} walishangaa kwa masemo yake kwa sababu aliwafundisha na amri ambayo walimu wao wa sheria walikosa.

Munajua habari za **walimu wa sheria**. Ilikuwa kazi yao kueleza Tora {Taurat}, Zaburi {Zabur} na vitabu vingine vya manabii. Lakini zaidi yao hawakuweza kueleza Maandiko ya Manabii vizuri, kwa sababu hawakuyafahamu wao wenyewe. Walijua maneno yote juu ya kazi ya dini yao na mafundisho ya wazazi wao, lakini hawakujua Neno la Bwana. "Wafundi" hawa wa dini waliheshimu Mungu na midomo yao, lakini hawakupenda Neno lake. Hivi, wakati Yesu, asiyejifunza ndani ya vyuo vyao vya dini, alipoingia sunagogi lao, na kuanza kueleza Maandiko waziwazi na amri, walimu hawa walipata haya kabisa. Haya yao iliongezeka wakati watu waliposhangaa kabisa juu ya masemo na kazi za Yesu na walipoulizana, "Huyu ni nani? Alipata mafundisho haya wapi? Namna gani anaweza kufundisha na amri hivi? Anaagiza hata pepo wachafu nao wanamtii! Hatujaona neno namna hii mbele! Hakuna mtu aliyefundisha kama huyu. Hakuna mtu aliyefanya maneno kama yeye!"

Everyday Publications Inc
@ 2010

Kweli, tangu siku Adamu alipofanya zambi kufika siku Yesu alipoanza kufanya maajabu watu hawakuona kamwe mtu mwenye uwezo mkubwa namna hii. Lakini sasa waliona Mmoja aliyeweza kusema neno moja tu na Shetani na pepo zake wachafu walikimbia! Masiya aliyetoka mbinguni tu aliweza kufanya hivi! Ulisikia neno pepo mchafu alilosema na Yesu? Alilalamika akisema, "Yesu wa Nazareti, tuna nini nawe? Umekuja hapa kutuangamiza sisi? **Ninatambua wewe ni nani, ndiwe Mtakatifu wa Mungu!" Pepo wachafu** walijua pahali Yesu alipotoka na kama alikuwa nani, lakini zaidi ya **watu** hawakujua kabisa kama Yesu alikuwa nani. Shetani na malaika zake waovu waliogopa Bwana Yesu sana, kwa sababu walijua kabisa kwamba yeye ndiye Neno na kwa yeye Mungu alikuwa ameumba mbingu na dunia katika mwanzo. Walijua Yesu alikuwa Mtakatifu wa Mungu aliyekuwa na amri kuwatupa ndani ya moto wa milele! Kwa sababu hii jina hili Yesu liliwatetemesha kwa woga.

Sasa tuendelee kusoma ndani ya sura 1 ya Marko, kuanza na shairi 29:

> (Marko 1) *29 [Wakati Yesu na wanafunzi wake] walipotoka sunagogi, walikwenda ndani ya nyumba ya Simoni na Anderea pamoja na*

*Yakobo na Yoane. 30 Na mama ya mke wa Simoni alilala na homa, wakamwambia habari zake. 31 Alikwenda kwake, akamshika mkono, akamsimamisha,* ***homa ikamwacha*** *mara moja, akawatumikia.*

*32 Wakati wa mangaribi, wakati jua lilipokuwa limekwisha kushuka, watu walileta mbele yake wote wenye ugonjwa na pepo. 33 Na wote wa mji walikusanyika kwa mlango. 34 Na aliponyesha wengi wenye ugonjwa namna nyingi na alifukuza pepo wachafu wengi. Lakini hakuruhusu pepo wachafu waseme maneno kwa sababu walimtambua.*

*35 Na wakati wa asubui mapema sana, mbele ya mchana, akatoka, akakwenda kwa pahali pa jangwa akaomba kule. 36 Simoni na wenzake walimfuata. 37 Wakimwona, walimwambia: Watu wote wanakutafuta wewe. 38 Akawaambia: Twende kwa miji mingine karibu nihubiri kule, maana nimekuja sababu ya maneno yale. 39 Akakwenda, akihubiri katika masunagogi yao katika inchi yote ya Galilaya na alifukuza pepo wachafu.*

*40 Mtu mmoja, mwenye ukoma, alikuja kwake akamwomba, akapiga magoti mbele yake, akamwambia: Kama ukitaka, unaweza kunisafisha. 41 Akimhurumia, akanyosha mkono wake, akamgusa, akamwambia: Ninataka, safishwa! 42 Mara moja* ***ukoma ulimwacha,*** *akasafishwa!*

Everyday Publications Inc @ 2010

Hivi Yesu aliponyesha watu toka gonjwa namna namna, akionyesha **huruma** kwa wazao wa Adam, kwa sababu walilegea na walikosa msaidizi, kama kondoo bila mchungaji. Lakini kulikuwa na sababu nyingine kwa maajabu makubwa mengi Yesu aliyofanya. Yesu aliponyesha kila namna ya ugonjwa na kufukuza pepo wachafu ku**hakikisha** kwa wana wa Adamu ya kwamba alikuwa Masiya ambaye Mungu aliahidi zamani sana kwa njia ya manabii wake. Kwa mfano, tumesoma ya kwamba nabii Isaya, mia za miaka mbele ya kuzaliwa kwa Yesu, aliandika ya kwamba wakati Masiya atakapokuja, *"macho ya vipofu yatafunguliwa, na masikio ya viziwi yatafunguliwa. Ndipo kiwete atarukaruka kama ayala, na ulimi wa bubu utaimba!"* (Isaya 35:5,6) Na masemo haya nabii Isaya alitangaza ya kuwa Masiya atafanya maajabu yasiyofanywa mbele kamwe. Tumesoma mbele ya kwamba Mungu aliwapa Musa na Elia uwezo kufanya maajabu makuwa. Lakini manabii hawa wawili walifanya maajabu machache tu wakati yanaposawanishwa na yale yaliyofanywa na Masiya. Vilevile Musa na Elia hawakuwa na uwezo wao wenyewe kufanya maajabu. Lakini,

Yesu Masiya alifurika kwa uwezo wa Mungu kwa sababu yeye mwenyewe ndiye uwezo wa Mungu!

Tukiendelea ndani ya Habari Njema ya Marko, sura 2, Maandiko yanasema:

> (Marko 2) *1 Aliingia Kapernaumu tena, na nyuma ya siku chache watu walisikia ya kama yuko katika nyumba. 2 Wakakusanyika wengi hata hawakupata tena nafasi mbele ya mlango, akahubiri neno kwao. 3 Wakaleta kwake mmoja mwenye kupooza aliyebebwa na watu wane. 4 Hawakuweza kumkaribia kwa sababu ya makutano; lakini walipanda juu, wakatoboa dari juu ya pahali pake, wakashusha kitanda cha mtu mwenye kupooza. 5 Yesu akiona imani yao alisema kwa mtu mwenye kupooza:* ***Mwana, zambi zako zimesamehewa****. 6 Lakini, waandishi fulani walioketi kule wakabishana katika mioyo yao, wakasema: 7 Mtu huyu anasema maneno gani? Anatukana Mungu! Nani anayeweza kusamehe zambi ila mmoja tu, ndiye Mungu? 8 Mara moja Yesu alifahamu kwa roho yake ya kuwa wanafikili hivi, akawaambia: Kwa sababu gani munabishana vile katika mioyo yenu? 9 Nini inapita nyepesi? Au kusema kwa mtu mwenye kupooza: Zambi zako zimesamehewa, au kusema: Simama, ukamate kitanda chako, utembee? 10 Basi, ili mufahamu Mwana wa watu [ndiye Masiya] ana amri kusamehe zambi katika dunia, pale alimwambia mtu mwenye kupooza, 11* ***ninakuambia: Simama, ukamate kitada chako, uende kwa nyumba yako.*** *12 Alisimama mara moja, akakamata kitanda chake, akatoka mbele yao wote; hata wote wakashangaa, wakasifu Mungu, wakisema: Hatujaona maneno namna hii!*

Everyday Publications Inc
@ 2010

Ndani ya habari hizi, tunaona uwezo wa Yesu haukutosha kuponyesha **mwili** tu wa mgonjwa, lakini alikuwa na uwezo vilevile kuponyesha **moyo wake** wenye zambi! Yesu, aliye Mganga Mkubwa, alijua ya kwamba neno gumu zaidi ya mwenye kupooza halikuwa uzaifu wa miguu yake, lakini **zambi** iliyokuwa ndani ya moyo wake. Kwa sababu hii Yesu alisema naye kwanza: *"Mwana, zambi zako zimesamehewa."*

Waandishi (walimu wa sheria) walifikili nini wakati Yesu aliposema maneno haya? Walisema rohoni mwao: "Yesu anatukana! Nani anayeweza kusamehe zambi ila mmoja, ndiye Mungu?" Maneno waliyofikili yalikuwa **kweli** kwa sehemu na kwa sehemu **hayakuwa kweli.** Ndiyo, hakuna anayeweza kusamehe zambi ila Mungu peke yake. Lakini wakati waandishi walipofikili Yesu

alikuwa akitukana, walianguka kwa sababu hawakufahamu ya kwamba **Yesu alikuwa Mpatanishi ambaye Mungu alituma duniani kutengeneza maneno ya watu na Mungu.** Yesu alikuwa Neno la Mungu; hivi wakati Yesu aliposema "Zambi zako zimesamehewa," alikuwa Mungu Mwenyewe akisema, ***"Zambi zako zimesamehewa!"*** Bwana Yesu alikuwa sauti ya Mungu duniani! Na zaidi ya ile, Yesu ni Yule aliyezaliwa kutoa uzima wake kama **Zabihu kamilifu** inayoondoa zambi kwa milele. Kama baba wa dunia akimpa mwana wake amri kumtumikia na kusema kwa ajili yake, vivyo hivyo Mungu alimpa Yesu amri kusamehe zambi. Usamehe wa zambi unapatikana ndani ya Bwana Yesu tu. Lakini waandishi hawakuamini maneno haya.

Saa yetu inabaki nusu tu, lakini mbele ya kuagana, tuendelee kusoma mashairi yanayofuata. Maandiko yanasema:

> *"Wakati Yesu alipokuwa akipita toka pale [toka nyumba alipoponyesha mwenye kupooza], aliona mtu aliyeitwa Matayo, akiketi kwa pahali pa kupokea kodi; akamwambia:* ***Unifuate****. Akaondoka na kumfuata." (Matayo 9:9) "Alipokuwa akikula chakula katika nyumba yake [ya Matayo] wengi wa watu wa kulipiza kodi, na wenye zambi wakakusanyika kwa Yesu na wanafunzi wake kwani walikuwa wengi wakimfuata. Wakati waandishi na Wafarisayo walipoona amekula pamoja na watoza kodi, waliwaambia wanafunzi wake: Kwa sababu gani anakula pamoja na watoza kodi na wenye zambi? Yesu aliposikia vile, alisema kwao:* ***Watu wenye afya njema hawahitaji mganga ila wenye ugonjwa tu. Sikuja kuita wenye haki ila wenye zambi kwa toba."*** (Marko 2:15-17)

Everyday Publications Inc
@ 2010

Na masemo haya Yesu, Mganga Mkubwa, alitaka kuonyeshea waandishi ya kwamba walikuwa **wagonjwa** kwa macho ya Mungu kwa sababu ya zambi yao. Lakini walimu hawa wa dini hawakutambua zambi yao. Ndiyo, walikuwa wakishitaki Yesu kwa sababu alikuwa akikula pamoja na wenye kulipiza kodi na wale walioitwa "wenye zambi." Lakini Yesu alizaliwa kwa kusudi hili tu, ndilo kuwa pamoja na **wenye zambi** na kuwaponyesha toka ***zambi*** yao!

Basi wewe, unafahamu kwamba ulizaliwa na ugonjwa mbaya sana unaoitwa **zambi**? Kwa sababu ya zambi hii ndani yako inakupasa kufa na kuhukumiwa na Mungu Mtakatifu. Lakini Mungu asifiwe, **kuna Mmoja anayeweza kukuponyesha toka zambi iliyo moyoni mwako!** Unajua ni Nani? Ndiyo, ni **Yesu Masiya**—Yule asiyekuwa na zambi na aliyefika duniani kuokoa wanadamu toka

zambi zao. Lakini, kwa Yesu kuweza kuponyesha moyo wako toka zambi, sharti ufahamu kwanza ya kwamba unashikwa na ugonjwa wa zambi. Wale tu wanaojua wao ni wagonjwa wanakwenda kuona mganga. Vivyo, wale tu wanaojua wao ni wenye zambi, wanafika karibu na Yesu, Mwokozi wa wenye zambi. **Yesu hakuja kwa sababu ya wale wanaozania wao ni wenye haki, lakini kwa wale wanaojua wao ni wenye zambi.** Kwa sababu hii alisema na walimu wa sheria, *"Watu wenye afya njema hawahitaji mganga ila **wenye ugonjwa** tu. Sikuja kuita wenye haki ila **wenye zambi** kwa toba."*

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Sharti tuache hapa leo. Ndani ya somo la nyuma, ikipendeza Mungu, tutaendelea ndani ya Habari Njema na kusikia masemo ya ajabu sana yaliyotoka kwa kinywa cha Yesu, Mganga wa wenye zambi ...

Mungu akubariki wakati unapokaa kufikili juu ya maneno Bwana Yesu aliyosema kwa waandishi (walimu wa sheria):

> ***"Watu wenye afya njema hawahitaji mganga ila wenye ugonjwa tu. Sikuja kuita wenye haki ila wenye zambi kwa toba."*** (Marko 2:17)

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 66

# Mwalimu Mkubwa

### Matayo 5-7

Salama kwako, rafiki. Tunakusalimu ninyi kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea leo na mfulizo *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo la mbele tuliona ya kwamba Yesu Masiya alikuwa akifikia vijiji inchini mwa Wayuda, akifundisha makutano, akiponyesha wagonjwa na akitoa pepo wachafu. Watu walishangaa juu ya maneno haya, wakaulizana, *"**Neno gani hili?** Ndiyo mafundisho mapya yenye uwezo; anaamuru pepo wachafu na wanamtii!"* (Marko 1:27)

Leo tunakusudi kuendelea ndani ya Habari Njema {*Injil*} na kusikia **maneno ya ajabu yaliyotoka kwa kinywa cha Bwana Yesu** siku alipokuwa mlimani pamoja na wanafunzi wake. Hatuwezi kusoma kila kitu Yesu alichofundisha wanafunzi wake siku ile; lakini, kila mtu anayetaka, anaweza kusoma habari zenyewe nzima ndani ya Habari Njema ya Matayo, sura 5 kufika sura 7.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Maandiko yanasema:

> (Matayo 5) *1 Naye [Yesu] akiona makutano, alipanda mlimani; na*
> *wakati alipokwisha kuketi, wanafunzi wake walikuja kwake, 2 aka-*
> *fungua kinywa chake, akawafundisha, akisema:*
>
> *3 **Heri** walio masikini wa roho: maana ufalme wa mbinguni ni wao.*
>
> *4 **Heri** wenye huzuni: maana watafarijiwa.*
>
> *5 **Heri** wenye upole: maana wao watariti inchi.*
>
> *6 **Heri** wenye njaa na kiu kwa haki; maana wao watashibishwa.*
>
> *7 **Heri** wenye rehema: maana wao watapata rehema.*
>
> *8 **Heri** wenye moyo safi: maana wao wataona Mungu.*
>
> *9 **Heri** wenye kufanya salama: maana wataitwa wana wa Mungu.*

*10 **Heri** walioteswa kwa sababu ya haki; maana ufalme wa mbinguni ni wao.*

*11 **Heri** ninyi, wakati wanapowatukana ninyi na kuwatesa ninyi na kuwasemea ninyi kila neno baya kwa uwongo, kwa sababu yangu. 12 Furahini, shangilieni; kwa sababu zawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyotesa manabii waliokuwa mbele yenu.*

*17 Musizanie nilikuja kuharibu torati au manabii; sikuja **kuharibu**, lakini **kutimiliza.** 18 Kwa maana kweli ninawaambia ninyi, Hata mbingu na inchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja haitaondoka, **hata yote yatimie**. 19 Basi mtu ye yote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kufundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; lakini mtu ambaye atazitenda na kuzifundisha, huyu ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni. 20 **Kwa sababu ninawaambia ninyi, haki yenu isipopita haki ya waandishi na Wafarisayo, hamutaingia hata kidogo katika ufalme wa mbinguni.***

Everyday Publications Inc
@ 2010

*21 **Mumesikia** kwamba watu wa zamani waliambiwa: Usiue, na mtu akiua, itampasa hukumu. 22 **Lakini mimi ninawaambia ninyi**: Kila mtu anayekasirikia ndugu yake itampasa hukumu ... 27 **Mumesikia** watu wa zamani walivyoambiwa: Usisikie watu wa zamani walivyoambiwa: Usizini; 28 **lakini mimi ninawaambia ninyi**: Kila mtu anayetazama mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake. ... 33 Tena **mumesikia** watu wa zamani walivyoambiwa: Usiape kwa uwongo, lakini mutimizie Bwana viapo vyako: 34 **lakini ninawaambia ninyi**: Usiape kabisa; wala kwa mbingu, kwa maana ni kiti cha ufalme cha Mungu; 35 wala kwa dunia, kwa maana ni kiti cha kuwekea miguu yake ... 37 Lakini maneno yenu yawe, ndiyo, ndiyo; siyo, siyo, kwa maana neno zaidi ya haya linatoka kwa yule mwovu.*

*38 **Mumesikia** ya kama imesemwa: Jicho kwa jicho, na jino kwa jino; 39 **Lakini mimi ninawaambia ninyi:** Musishindane na mtu mwovu. Lakini kama mtu akikupiga shavu la kuume, umgeuzie la pili vilevile. 40 Na kama mtu akitaka kukushitaki na kutwaa kanzu yako, umwachie joho yako vilevile. 41 Na mtu ambaye atakusukuma kwenda kilomètre moja, kwenda naye mbili. . . .*

*43 **Mumesikia** ya kama imesemwa: Upende jirani yako, na, Uchukie adui yako. 44 **Lakini mimi ninawaambia ninyi**: Pendeni adui zenu, muwabariki wenye kuwalaani ninyi, muwatendee mema*

*wenye kuwachukia ninyi, muwaombee wenye kuwazarau, na kuwatesa ninyi: 45 mupate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni, sababu yeye anaangazia jua lake waovu na wema, naye ananyeshea mvua wenye haki na wasio haki. 46 Maana kama mukiwapenda wenye kuwapenda ninyi, munapata zawabu gani? Hata watoza kodi hawafanyi sawasawa? 47 Tena kama mukisalimu ndugu zenu tu, munatenda tendo gani la kupita wengine? Hata Mataifa, hawafanyi sawasawa? 48* ***Basi muwe wakamilifu, kama Baba yenu ya mbinguni alivyo mkamilifu.***

(Matayo 6) *1* ***Angalieni musifanye wema wenu mbele ya watu kusudi mwonekane nao****: kwa maana mukifanya hivi hamupati zawabu kwa Baba yenu aliye mbinguni. 2 Basi* ***wakati unapotoa sadaka****, usipige baragumu mbele yako kama* ***wadanganyifu*** *wanavyofanya ndani ya masunagogi na njiani, waonekane na watu. Kweli ninawaambia ninyi, Wao wamekwisha kupata zawabu yao. 3 Lakini wakati wewe unapotoa sadaka, mkono wako wa kushoto usijue mkono wako wa kuume unalofanya, 4 hata sadaka zako ziwe kwa siri, na Baba yako anayeona kwa siri atakupa zawabu.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

*5 Na* ***wakati munapoomba, musiwe kama wadanganyifu****, kwani wanapenda kusimama na kuomba ndani ya masunagogi na njiani, waonekane na watu. Kweli ninawaambia ninyi, wao wamekwisha kupata zawabu yao. 6 Lakini wewe, wakati unapoomba, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukikwisha kufunga mlango wako, omba kwa Baba yako aliye kwa siri, na Baba yako anayeona kwa siri, atakupa zawabu. 7 Na mukiomba musiseme maneno bule mara na mara kama Mataifa wanavyofanya: kwa sababu wao wanafikili watasikiwa kwa sababu ya masemo mengi. 8 Basi musifanane nao; maana Baba yenu anajua vitu munavyohitaji nanyi hamujamwomba bado.*

*9 Basi ombeni hivi:*

*'****Baba yetu*** *uliye mbinguni, jina lako litukuzwe.*

*10 Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni.*

*11 Utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku.*

*12 Utusamehe deni zetu, kama sisi vilevile tunavyosamehe wadeni wetu.*

*13 Na usitulete katika majaribu, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa maana ufalme na uwezo na utukufu ni wako, kwa milele. Amina.*

16 Tena **wakati munapofunga chakula**, musiwe **kama wadanganyifu** na uso wa kukunjamana; kwa maana wao wanageuza nyuso zao ili waonekane na watu ya kama wanafunga. Kweli ninawaambia ninyi, Wao wamekwisha kupata zawabu yao. 17 Lakini wewe, wakati unapofunga chakula, pakaa kichwa chako na mafuta, na nawa uso wako: 18 hata usionekane na watu ya kama unafunga, lakini na Baba yako aliye kwa siri: na Baba yako anayeona kwa siri atakupa zawabu.

19 **Musijiwekee hazina** duniani pahali nondo na kutu zinapoharibu, na wizi wanavunja na kuiba; 20 lakini mujiwekee hazina mbinguni, pahali nondo wala kutu haziharibu, wala wizi hawavunji na kuiba; 21 kwa maana pahali hazina yako iko, pahali moyo wako utakapokuwa vilevile.

22 Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utajaa nuru. 23 Lakini jicho lako likiwa baya, mwili wako wote utajaa giza. Basi nuru iliyo ndani yako ikiwa giza, ni giza kubwa sana! 24 **Hakuna mtu anayeweza kutumikia bwana wawili;** kwa maana atachukia mmoja, na kupenda mwingine; au atashikamana na mmoja, na kuzarau mwingine. Hamuwezi kutumikia Mungu na mali.

Everyday Publications Inc
@ 2010

25 Kwa hivi ninawaambia ninyi, **Musisumbukie maisha yenu**, nini mutakayokula, au nini mutakayokunywa, wala miili yenu, nini mutakayovaa. Maisha si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi? 26 Angalieni ndege za anga, ya kwamba wao hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi galani; na Baba yenu ya mbinguni anawakulisha. Basi ninyi si damani kuliko wao? 27 Na nani katikati yenu akisumbuka anaweza kuongeza kimo cha mwili wake mkono mmoja?

28 Na kwa nini munasumbukia mavazi? Fikilieni maua ya shamba namna yanavyoota, hayafanyi kazi, wala hayasokoti; 29 lakini ninawaambia ninyi ya kwamba hata Solomono katika utukufu wake wote hakuvikwa mavazi mazuri kama moja yao. 30 Basi ikiwa Mungu anavika hivi majani shambani yaliyo leo tu, na kesho, yanatupwa katika tanuru, hatawavika ninyi, Ee ninyi wenye imani ndogo? 31 Basi musisumbuke mukisema: Tutakula nini? au: Tutakunywa nini? au: Tutavikwa nini? 32 Kwa maana Mataifa wanatafuta maneno haya yote; kwa sababu Baba yenu ya mbinguni anajua ya kama munahitaji vitu hivi vyote. 33 **Lakini ninyi tafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki yake; na vitu hivi vyote vitaongezwa kwenu.**

(Matayo 7) *1* ***Musihukumu ili musihukumiwe.*** *2 Kwa kuwa hukumu ambayo munahukumu ndiyo mutahukumiwa; na kipimo ambacho munapimia mutapimiwa. 3 Kwa nini unaona kitakataka ndani ya jicho la ndugu yako, lakini hufikili boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe? 4 Au namna gani utamwambia ndugu yako: Unipe ruhusa nitoe kitakataka ndani ya jicho lako; na tazama, boriti ni ndani ya jicho lako mwenyewe? 5 Mdanganyifu, uondoe kwanza boriti ndani ya jicho lako mwenyewe; kisha utaona wazi kutoa kitakataka ndani ya jicho la ndugu yako. (12 Basi* ***yo yote munayotaka watu wawatendee ninyi, muwatendee vivyo hivyo;*** *maana hii ni torati na manabii.)*

*7 Ombeni nanyi mutapewa;* ***tafuteni, nanyi mutaona****; pigeni mlango, nanyi mutafunguliwa; 8 kwa maana kila mtu anayeomba anapokea; naye anayetafuta anapata; naye anayepiga mlango atafunguliwa.*

*13* ***Ingieni kwa mlango ulio mwembamba****; kwani mlango ni mpana na njia ni pana inayokwenda hata upotevu, nao ni wengi wanaoingia kwa mlango huu. 14 Lakini mlango ni mwembamba, na njia imesonga inayokwenda hata uzima, nao ni wachache ambao wanaiona.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

*15* ***Angalieni kwa manabii wa uwongo*** *wanaokuja kwenu wakivaa mavazi ya kondoo, lakini kwa ndani wao ni imbwa wakali za mwitu. 16 Mutawatambua kwa njia ya matunda yao. Watu wanakusanya zabibu katika miiba au tini katika mibaruti? 17 Vivyo hivyo kila mti mzuri unazaa matunda mazuri, lakini kila mti mwovu unazaa matunda mabaya. 18 Mti mzuri hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu hauwezi kuzaa matunda mazuri. 19 Kila mti usiozaa matunda mazuri unakatwa na unatupwa katika moto. 20* ***Kwa hivi mutawatambua kwa njia ya matunda yao.***

*21* ***Si kila mtu ambaye ananiambia: Bwana, Bwana, atakayeingia ufalme wa mbinguni****; lakini yeye anayefanya mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. 22 Wengi wataniambia siku ile: Bwana, Bwana, hatukutabiri kwa jina lako, na kwa jina lako tulitoa pepo wachafu, na kwa jina lako tulifanya matendo mengi ya uwezo? 23 Halafu nitawaambia: Sikuwajua ninyi wakati wo wote; ondokeni kwangu, ninyi munaotenda maovu.*

*24 Na* ***kila mtu anayesikia maneno yangu haya na kuyafanya****, atafananishwa na* ***mtu mwenye akili*** *aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba; 25 na mvua ilinyesha, na maji yalikuja, na*

> *pepo zilivuma, zikapiga nyumba ile, nayo haikuanguka kwa sababu misingi yake imewekwa juu ya mwamba. 26* ***Kila mtu anayesikia maneno yangu haya, naye hayafanyi,*** *atafananishwa na* ***mtu mpumbavu*** *aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga; 27 na mvua ilinyesha, na maji yalikuja, na pepo zilivuma, zikapiga nyumba ile, nayo ikaanguka; na anguko lake lilikuwa kubwa.*
>
> *28 Wakati Yesu alipomaliza maneno haya,* ***makutano walishangaa kwa mafundisho yake,*** *29 kwa maana* ***aliwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi wao.***

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Kwa somo la nyuma, tutawaza pamoja juu ya maneno ya ajabu na yenye maana kubwa tuliyosoma leo, masemo ya Yesu, Mwalimu Mkubwa toka mbingu. Mungu akubariki wakati unapokaa kuwaza juu ya neno hili zuri sana Bwana Yesu alilosema juu ya mlima:

> ***"Tafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki yake; na vitu hivi vyote vitaongezwa kwenu."*** (Matayo 6:33)

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 67

# Sharti Muzaliwe Mara ya Pili!

## Yoane 3

Salamu kwako, rafiki. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea na somo lingine leo la mfulizo *Njia ya Haki.*

Ndani ya majifunzo yetu ndani ya Habari Njema {*Injil*}, tumeona ya kwamba Yesu Masiya alikuwa namna nyingine na watu kwa **namna alivyozaliwa**, ndani ya **wema** wake na **matendo** yake. Na ndani ya programme ya mbele tulifahamu ya kwamba hata **mafundisho** yake yalikuwa namna nyingine vilevile. Tangu zamani hakuna mtu aliyesema wazi maneno ya ndani ndani kama yeye. Wale ambao walimsikia walishangaa, kwa sababu aliwafundisha na amri ambayo makuhani {*marabouts*} na walimu wa sheria {*imans*} hawakuwa nayo. Masemo machache toka kinywa cha Yesu yalikuwa na faida kupita masemo mengi mengi ya viongozi vyao kwa maneno ya dini. Kwa sababu ya neno hili zaidi ya viongozi vya Wayuda hawakufurahia Yesu. Mafundisho yake **yalibisha desturi zao** na vilevile **alifunua udanganyifu wao** mbele ya watu wote!

Everyday Publications Inc
@ 2010

Ndani ya somo letu la mbele tulisikia hotuba Yesu aliyofundisha kwa wanafunzi wake wakati alipokuwa juu ya mlima pamoja nao. Hotuba yake inaweza kujumlishwa na maneno matatu: ***"Musiwe kama wadanganyifu!"*** Udanganyifu ni chukizo kwa Mungu na unaharibu watu. Kwa sababu hii Yesu alisema na makutano: *"Musiwe kama wadanganyifu!"* Unajua maana ya kuwa mdanganyifu. Mtu akijaribu kujionyesha kuwa mtu mzuri naye ni namna nyingine ndani ya roho yake, yeye ni mdanganyifu. Yesu alisema mdanganyifu ni kama kaburi linalopakaliwa pembe; linaonekana kama kitu cha mapambo inje, lakini ndani linajaa mifupa ya wafu na uchafu wote (Matayo 23:27).

Hakuna mtu anayeweza kudanganya Mungu. Neno la Mungu linasema: *"Vitu vyote ni utupu na kufunuliwa mbele ya macho yake yeye aliye na maneno yetu."* (Waebrania 4:13) Yesu anayejua moyo wa mtu, aliona udanganyifu ndani ya mioyo ya viongozi hawa vya dini,

Wafarisayo na waandishi. Walionekana kama wenye bidii waki-omba, kufunga chakula na kutoa zaka, lakini mioyoni mwao hawakupenda Mungu na Neno lake kweli kweli. Kwa sababu hii, matendo yao ya "haki" na desturi zao za ibada zilikuwa bule. Hivi, **Yesu alifundisha wanafunzi wake, akisema**:

> *"Na wakati munapo**omba,** musiwe kama wadanganyifu, kwani wanapenda kusimama na kuomba ndani ya masunagogi na njiani waonekane na watu. Kweli ninawaambia ninyi, Wao wamekwisha kupata zawabu yao."* (Matayo 6:5) *"Wakati unapo**toa** sadaka, usi-pige baragumu mbele yako kama **wadanganyifu** wanavyofanya ndani ya masunagogi na njiani, waonekane na watu. Kweli ninawaambia ninyi, Wao wamekwisha kupata zawabu yao."* (Matayo 6:2) *"Wakati **munapofunga chakula**, musiwe kama **wadanganyifu** na uso wa kukunjamana; kwa maana wao wanageuza nyuso zao ili waonekane na watu ya kama wanafunga. Kweli ninawaambia ninyi, Wao wamekwisha kupata zawabu yao."* (Matayo 6:16)
>
> *"**Musiwe kama wadanganyifu**. Kwa sababu ninawaambia ninyi, Haki yenu isipopita haki ya waandishi na Wafarisayo, hamu-taingia hata kidogo katika ufalme wa mbinguni."* (Matayo 6:5; 5:20) *"Heri walio **masikini wa roho**: maana ufalme wa mbinguni ni wao. Heri **wenye njaa na kiu kwa haki:** maana watashibishwa. Heri **wenye moyo safi**: maana wao wataona Mungu. Basi muwe **wakamilifu**, kama Baba yenu ya mbinguni alivyo mkamilifu."* (Matayo 5:3,6,48) *"Ingieni kwa mlango ulio mwembamba; kwani mlango ni mpana na njia ni pana inayokwenda hata upotevu, nao ni **wengi** wanaoingia kwa mlango huu. Lakini mlango ni mwembamba, na njia imesonga inayokwenda hata uzima, nao ni **wachache** ambao wanaiona."* (Matayo 7:13,14)

Everyday Publications Inc
@ 2010

Hivi Bwana Yesu alionya watu kuchagua njia inayosonga na inayokwenda hata uzima wa milele. Ulifahamu maneno Yesu aliyosema juu ya njia ya wokovu? Ni neno kubwa sana! Kwa mtu kuweza kuona Mungu na kukaa mbele yake mbinguni kwa milele inampasa kuwa mtu wa namna gani? Yesu alisema nini juu ya neno hili? Kwa ufupi, alisema: **"Lazima uwe na moyo safi na mkamilifu!"**

Lakini namna gani mwana wa Adamu aliyezaliwa na zambi anaweza kuwa na moyo safi na mkamilifu? Kuna kitu anachoweza kufanya kugeuza moyo wake mwovu kuwa moyo safi unaoweza kukubaliwa na Mungu? Hapana! Mtu yeye mwenyewe hana njia

kusafisha moyo wake. "Mti ukilala muda mrefu sana ndani ya maji hautageuka kamwe kuwa mwamba." {Mezali ya kabila moja la Afrika} Vivyo hivyo sisi wenye zambi hatuwezi **kufanya** kitu cho chote **kujigeuza** kuwa safi mbele ya Mungu. Lakini, ndani ya saa inayobaki kwa programme yetu leo, tutaona ya kwamba **neno lisilowezekana kwa mtu linawezekana kwa Mungu!**

Sasa tukae kusoma ndani ya Habari Njema kuona namna gani mkubwa mmoja kwa maneno ya dini toka Yerusalema, jina lake **Nikodemo**, alikuja kusemezana na Yesu usiku. Yesu alimwonyesha namna gani mwenye zambi anaweza kupokea moyo mpya, moyo safi na zawadi ya Mungu, ndiyo uzima wa milele. Tunasoma ndani ya Habari Njema ya Yoane, sura 3. Maandiko yanasema:

> (Yoane 3) *1 Palikuwa mtu mmoja wa Wafarisayo, jina lake Nikodemo, mkubwa wa Wayuda. 2 Huyu alikuja kwa Yesu usiku, akamwambia: Rabi, tunajua wewe ni mwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa sababu hakuna mtu anayeweza kufanya alama hizi unazofanya ila Mungu awe pamoja naye. 3 Yesu akajibu, akamwambia:* ***Kweli, kweli ninakuambia, Ila mtu azaliwe mara ya pili hawezi kuona ufalme wa Mungu.***
>
> *4 Nikodemo akamwambia: Namna gani mtu anaweza kuzaliwa akiwa mzee? Anaweza kuingia tumboni mwa mama yake mara ya pili na kuzaliwa? 5 Yesu akajibu: Kweli, kweli ninakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu. 6* ***Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho. 7 Usishangae kwa sababu nilikuambia, Sharti muzaliwe mara ya pili****. 8 Upepo unavuma pahali unapotaka, na sauti yake unaisikia, lakini hujui pahali unapotoka wala unapokwenda; ndivyo kila mtu aliyezaliwa kwa Roho.*
>
> *9 Nikodemo akajibu, akamwambia: Maneno haya yanawezekana namna gani? 10 Yesu akajibu, akamwambia: Wewe mwalimu katika Israeli, na hufahamu maneno haya? 11 Kweli, kweli, ninakuambia, Tunasema tunayojua, tunashuhudu tunayoona, na hamukupokea ushuhuda wetu. 12 Kama nimewaambia ninyi maneno ya dunia na hamuyaamini, mutaamini namna gani kama nikiwaambia ninyi maneno ya mbingu? 13 Na hapana mtu aliyepanda mbinguni ila yeye aliyeshuka toka mbinguni, ndiye Mwana wa watu aliye mbinguni. 14* ***Na kama Musa alivyonyanyua nyoka jangwani, vivyo hivyo sharti Mwana wa watu anyanyuliwe, 15 ili kila mtu akimwamini asipotee, lakini awe na uzima wa milele. 16***

Everyday Publications Inc
@ 2010

> ***Kwa maana Mungu alivyopenda ulimwengu, hata kutoa Mwana wake wa pekee, ili kila mtu akimwamini asipotee lakini apate uzima wa milele.*** Amina.

Tuwaze kidogo juu ya maneno ambayo Yesu alimwambia mwalimu wa dini yule, ndiye Nikodemo. **Yesu alisema na Nikodemo sharti neno gani litokee kwanza mbele ya Nikodemo kuweza kupata uzima wa milele na ruhusa ya kuishi pamoja na Mungu kwa milele?** Alisema, *Kweli, kweli ninakuambia, Ila mtu azaliwe mara ya pili hawezi kuona ufalme wa Mungu.* ***Sharti muzaliwe mara ya pili.*** (Yoane 3:4,7) Nikodemo alifahamu maana ya kuzaliwa tena? Hapana! Kwa sababu hii Yesu akamwambia: *Wewe mwalimu katika Israeli, na hufahamu maneno haya? Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho. Usishangae kwa sababu nilikuambia,* ***Sharti muzaliwe mara ya pili.*** (Yoane 3:10,6,7)

Kwa ufupi, Yesu alikuwa akimwambia ya kwamba ni sharti kwa mtu ye yote anayetaka kuona Mungu na kuishi katika utakatifu kwake **kuzaliwa mara mbili!** Si kusema ya kwamba inakupasa kuingia ndani ya tumbo la uzazi la mama yako mara ya pili na kuzaliwa tena (kwa mwili). Kwawe kuzaliwa tena inapasa **Roho ya Mungu kukufanya tena**, akisafisha moyo wako na kukufanya mpya kwa uwezo wake (Tito 3:5). Sharti uzaliwe kwa **uwezo unaotoka mbinguni**, ulio **namna nyingine kabisa na dini ya kuonekana** tu. Ni lazima kwawe kugeuzwa **ndani – moyoni** mwako! Mtu ye yote anayezaliwa kwa njia ya Adamu anachafuwa na zambi na hawezi kushiriki ndani ya ufalme wa Mungu. Wana wa Adamu hawana uwezo kuondosha shina la zambi linaloota ndani ya mioyo yao. Hata mti ukilala muda mrefu ndani ya maji neno hili halimgeuzi kuwa mamba. Vivyo hivyo hata kama mtu akishinda saa nyingi kwa matendo ya ibada na kazi njema, neno hili haliwezi kamwe kufanyiza moyo wake mwovu kuwa safi. Inapasa Mungu mwenyewe kutenda ajabu ndani ya moyo wake na kuufanya mpya, kwa sababu anayeharibika hawezi kuriti yasiyoharibika (ona 1 Wakorinto 15:50). Kwa ufupi, "*Sharti muzaliwe mara ya pili!*"

Hili ndilo neno ambalo Yesu alifundisha mkubwa wa dini, ndiye Nikodemo. Lakini ilikuwa nguvu kwa Nikodemo kufahamu mafundisho haya. Hivi aliuliza Yesu: Neno hili linawezekana namna gani? **Namna gani** ninaweza kuzaliwa tena na kupokea moyo mpya na safi?

Yesu alimjibu,

Everyday Publications Inc @ 2010

> *"Kama Musa alivyonyanyua nyoka jangwani, vivyo hivyo sharti Mwana wa watu anyanyuliwe, ili **kila mtu akimwamini** asipotee, lakini awe na uzima wa milele. Kwa maana Mungu alivyopenda ulimwengu, hata kutoa Mwana wake wa pekee, ili **kila mtu akimwamini** asipotee, lakini apate uzima wa milele."* (Yoane 3:14-16)

Kuonyesha Nikodemo namna alivyoweza kuepuka hukumu ya milele na kupata uzima wa milele, Yesu alimkumbusha maneno yaliyopata wazazi wake jangwani kwa wakati wa nabii Musa. Kama tulivyoona ndani ya Tora, siku moja wakati Waisraeli waliponungunikia Mungu na Musa, Mungu alituma nyoka za sumu katikati yao kuwauma ili wengi wao walikufa. Lakini wakati wana wa Israeli walipotubu, Mungu aliagiza Musa kufanya **nyoka ya shaba na kuinyanyua juu ya mti, ili kila mtu ambaye aliitazama asife lakini aponyeshwe**.

Everyday Publications Inc @ 2010

Hivi, Yesu alikuwa akimwambia Nikodemo kwamba namna ilivyopasa wana wa Israeli kutazama na imani nyoka ya shaba juu ya mti kwa kuponyeshwa toka mauti, vivyo hivyo wana wa Adamu wanahitaji **kuamini** tu njia Mungu aliyotayarisha kuwaokoa toka azabu ya milele. **Sisi** ni kama wana wa Israeli walioumwa kwa nyoka. **Shetani** ni kama nyoka ya shaba, na **zambi** ni kama sumu inayofanyiza mtu kufa. Shetani ameuma wana wote wa Adamu, na kwa sababu ya sumu ya zambi sisi sote tutapotea kwa milele isipokuwa Mungu anatupatia njia ya wokovu! Sisi wenyewe hatuna njia yo yote kujiponyesha toka hukumu ya Mungu, kwa sababu mshahara wa zambi ni mauti. Lakini Bwana Mungu asifiwe—kwani kama alitayarisha njia kuponyesha wana wa Israeli toka sumu ya nyoka, vivyo hivyo ametayarisha **njia** kuokoa wana wa Adamu toka "sumu" ya zambi.

Unajua njia Mungu aliyotayarisha kufanya mpya mioyo ya wana wa Adamu inayojazwa zambi? Bwana Yesu alisema nini juu ya neno hili? Alisema sharti Mkombozi mtakatifu anyanyuliwe juu ya mti (msalaba) kuvumilia azabu ya zambi kwa ajili ya wenye zambi—*"ili kila mtu akimwamini asipotee, lakini apate uzima wa milele."*

Hivi nani anaweza kuokolewa? Maandiko yanasema nini? Yanasema: ***"Kila mtu akimwamini** . . . asipotee!"* Inatupasa kuamini nani? Sharti tuamini Mkombozi ambaye Mungu alituma. Unamwamini? Unaamini ndani ya roho yako ya kwamba Mungu, asiyetaka mtu ye yote kupotea, alituma Yesu Mwokozi duniani **kwa wewe**, kubeba deni yako ya zambi **kwa wewe**? Njia ya haki ambayo

Mungu alitayarisha kutengeneza maneno yetu ya zambi ni kufa kwa Yesu juu ya msalaba. Maandiko yanasema: ***"Mungu alimfanyiza yeye [Yesu Masiya] asiyejua zambi, kuwa zambi kwa ajili yetu ili sisi tuwe haki ya Mungu katika yeye."*** (2 Wakorinto 5:21)

Rafiki, Mungu hakubadilika. Neno Bwana Yesu alilosema na Nikodemo karibu miaka elfu mbili mbele, analisema kwa wewe leo vilevile: ***"Sharti muzaliwe mara ya pili!"*** Mungu anataka kusafisha na kufanya mpya moyo wako kwa uwezo wake. Lakini, sharti uamini Habari Njema yake. Lazima uamini Masiya ambaye alituma. Inakupasa kuamini ya kwamba Yesu, asiyefanya zambi kamwe, alilipa deni yako ya zambi, ili uweze kukaa karibu na Mungu kwa milele. ***"Sharti muzaliwe mara ya pili!" . . . Hakuna mtu anayeweza kuona ufalme wa Mungu isipokuwa amezaliwa mara ya pili!"*** Amina.

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Asante kwa kujifunza pamoja nasi. Ndani ya somo la nyuma, tutaendelea ndani ya Habari Njema na kusikia mazungumzo ya Bwana Yesu na mwanamke aliyekuwa na waume watano . . .

Everyday Publications Inc
@ 2010

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya maneno Yesu Masiya aliyosema:

> ***"Usishangae kwa sababu ninakuambia, Sharti muzaliwe mara ya pili."*** (Yoane 3:7) ***"Heri wenye moyo safi: maana wao wataona Mungu."*** (Matayo 5:8)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Somo 68

# Mwokozi wa dunia

Yoane 4, Luka 4

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea na mfulizo *Njia ya Haki*.

Kufika sasa ndani ya majifunzo yetu ndani ya Habari Njema, tumeona ya kwamba Yesu Masiya alikuwa namna nyingine na watu kwa **namna alivyozaliwa**, ndani ya **wema** wake, kwa **matendo** yake na ndani ya **mafundisho** yake.

Everyday Publications Inc @ 2010

* Juu ya **kuzaliwa** kwake tuliona ya kwamba hakuna mtu aliyezaliwa namna Yesu alivyozaliwa kwani hakuna mtu aliyezaliwa na bikira, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu wa Mungu.

* Tuliona vilevile ya kwamba kwa **tabia yake** alikuwa namna nyingine, kwani hakuna mwingine aliyezaliwa na tabia takatifu kama yeye.

* Hakuna mwingine kama yeye kwa **matendo yake** kwani hakuna mwingine aliyefanya kamwe maajabu kama yeye. Aliweza kusema neno tu kwa wagonjwa kuponyeshwa, kwa kufukuza Shetani na pepo zake wachafu, na kwa kuondoshwa kwa zambi.

* Kwa njia ya **mafundisho yake** Yesu alikuwa namna nyingine vilevile. Tuliona neno hili katika somo la mbele ndani ya mazungumzo yake na Nikodemo, mtawala wa Wayuda kwa maneno ya dini. Alionyeshea Nikodemo ya kwamba hataweza kamwe kufikia Mungu isipokuwa Roho ya Mungu alisafisha moyo wake na kuufanya mpya. Kwa sababu hii Bwana Yesu alisema naye, ***"Sharti muzaliwe mara ya pili!"***

Leo tutasikia Yesu Masiya akisema na mtu aliyekuwa **namna nyingine kabisa** na Nikodemo. Nikodemo alikuwa Myuda; lakini mtu ambaye tutamwona ndani ya somo letu leo **hakuwa Myuda**.

Nikodemo alikuwa mwanamume; leo tutaona Yesu akisema na **mwanamke**. Nikodemo alikuwa mtu wa dini kabisa, lakini mwanamke huyu alikuwa **mwenye zambi mkubwa** aliyekuwa na waume watano. Kwa macho ya watu, mtawala mwenye kushika dini, ndiye Nikodemo alikuwa mtu mzuri kupita mwanamke huyu wa zambi. Lakini sivyo kwa macho ya Mungu, kwa sababu wazao wote wa Adamu—wenye kushika dini na wenye kuzama ndani ya zambi vilevile ni chini ya utawala wa zambi. Kwa sababu hii ni lazima kwa wana wote wa Adamu kuzaliwa mara ya pili kwa uwezo unaotoka juu.

Sasa tugeuke kwa Habari Njema tena na kusikiliza **mazungumzo ya Yesu na mwanamke huyu wa zambi toka Samaria.** Samaria ilikuwa inchi katikati ya Yudea na Galilaya inchini mwa Wayuda. Wengi wa Wasamaria walitoka inchi nyingine; kwa macho ya Wayuda walikuwa wapagano na kwa sababu hii hawakupatana nao. Lakini Yesu Masiya hakuwa na upendeleo kwa sababu Mungu hana upendeleo. **Yesu alifika duniani kutafuta na kuokoa kila mwenye zambi anayetaka kupokea moyo mpya na safi.** Kwa sababu hii Yesu hakuwa na haya kusemezana na mwanamke wa Samaria aliyekuwa na waume watano.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Tusikilize maneno yanayoandikwa ndani ya sura 4 ya Habari Njema ya Yoane. Maandiko yanasema:

> (Yoane 4) *4 Imepasa [Yesu] apite katikati ya Samaria. 5 Basi akafika mji wa Samaria, ulioitwa Sukari, karibu na shamba ambalo Yakobo alimpa mwana wake Yosefu. 6 Na palikuwa kule kisima cha Yakobo. Basi Yesu, kwa sababu amechoka kwa safari yake, alikaa hivi kwa kisima, ilikuwa karibu na saa sita azuhuri. 7 Mwanamke wa Samaria anakuja kuteka maji. Yesu akamwambia: Unipe maji ya kunywa. 8 Maana wanafunzi wake wamekwenda mjini wanunue chakula. 9 Basi yule mwanamke wa Samaria akamwambia: Namna gani wewe* ***Myuda*** *unaomba maji kwangu, nami ni mwanamke wa Samaria? (kwa sababu Wayuda hawapatani na Wasamaria). 10 Yesu akajibu akamwambia: Kama ungalijua zawadi ya Mungu, naye ni nani ambaye anakuambia, Unipe maji ya kunywa, ungalimwomba yeye, naye angalikupa* ***maji yaliyo hai.*** *11 Mwanamke akamwambia: Bwana, huna kitu cha kutekea, na kisima kinakwenda chini sana, basi umepata wapi maji yaliyo hai? 12 Wewe mkubwa kuliko baba yetu Yakobo, ambaye alitupa sisi kisima hiki, naye mwenyewe alikunywa maji yake, na watoto wake, na nyama zake? 13 Yesu akajibu, akamwambia: Kila mtu anayekunywa maji haya ataona kiu tena: 14* ***lakini ye yote anayekunywa maji yale ambaye ninampa mimi,***

**hataona kiu hata milele**; lakini maji ambayo ninampa yatakuwa
ndani yake kisima cha maji yanayochemuka hata uzima wa milele. 15
Mwanamke akamwambia: Bwana, unipe maji haya nisione kiu, nisi-
hitaji kuja tena hapa kuteka. 16 Yesu akamwambia: Kwenda kuita
mume wako urudi naye hapa. 17 Yule mwanamke akajibu, akasema:
Sina mume. Yesu akamwambia: Umesema vema, Sina mume, 18 kwa
sababu umekuwa na waume watano, na yeye uliye naye sasa si mume
wako; hivi umesema kweli. 19 Yule mwanamke akamwambia: Bwana,
ninaona ya kwamba wewe ni **nabii**. 20 Baba zetu waliabudu katika
kilima hiki, na ninyi munasema ya kama imepasa watu kuabudu kati-
ka Yerusalema. 21 Yesu akamwambia: Mwanamke, unisadiki, saa
inakuja wakati hamutaabudu Baba katika kilima hiki wala katika
Yerusalema. 22 Ninyi munaabudu ambacho hamukijui; sisi
tunaabudu tunachojua, kwa sababu wokovu unatoka kwa Wayuda. 23
Lakini saa inakuja, imekuwa hata sasa, wakati waabudu wa kweli
watakapoabudu Baba katika roho na kweli: kwa sababu Baba anatafu-
ta watu kama hawa wamwabudu. 24 **Mungu ni Roho; nao wenye
kumwabudu sharti wamwabudu katika roho na kweli.** 25 Yule
mwanamke akamwambia: Ninajua Masiya anakuja (anayeitwa
Kristo); kama yeye atakapokuja, atatuambia maneno yote. 26 Yesu
akamwambia: **Mimi ninayesema nawe, ndiye."**

Everyday Publications Inc
@ 2010

27 Palepale wanafunzi wake walikuja; na walishangaa kwa sababu
alikuwa akisema na mwanamke, lakini hapana mtu aliyesema:
Unatafuta nini: au: Kwa nini unasema naye? 28 Basi yule mwana-
mke akaacha chungu chake, akakwenda zake mjini, akawaambia
waume: 29 **Kujeni mutazame mtu ambaye aliniambia maneno
yote ambayo niliyatenda. Huyu si Kristo [Masiya]?** 30 Basi
wakatoka mjini, wakakwenda kwake.

39 Na katika mji ule Wasamaria wengi walimwamini kwa sababu
ya neno la mwanamke aliyeshuhudia, ya kwamba: Aliniambia mambo
yote ambayo niliyatenda. 40 Basi wale Wasamaria walipokwenda
kwake walimsihi akae kwao na alikaa kule siku mbili. 41 Na watu
wengi waliamini kwa sababu ya neno lake. 42 Wakamwambia yule
mwanamke: Sasa tunaamini, si kwa sababu ulituambia, lakini kwa
sababu **sisi wenyewe tumesikia, na tunajua kweli huyu ni
Kristo, Mwokozi wa ulimwengu.**

Habari za mwanamke wa Samaria zinakwisha hapa. Ni habari kubwa sana kwa sababu zinaonyesha namna mwanamke wa zambi alivyovumbua ya kwamba Yesu ni Mwokozi ambaye Mungu alituma duniani. Kuvumbua neno hili kuligeuza maisha yake kabisa.

Kwa mwanzo wa mazungumzo yao mwanamke hakujua ni nani aliyesema naye. Alifikili alikuwa Yesu alikuwa Myuda **namna ya Wayuda wote wengine**. Lakini wakati walipokuwa wakisemezana, Yesu alimwambia maneno mengine ambayo mtu tu hakuweza kujua, hivi sasa mwanamke alifikili kwamba Yesu alikuwa **nabii**. Lakini mwishoni alianza kufahamu ya kwamba Yesu huyu ambaye alisema naye alikuwa **mkubwa kupita nabii**. Alikuwa **Masiya—yule ambaye manabii wote walikuwa wametabiri habari zake, Mwokozi wa dunia!**

Basi wakati mwanamke alipotambua ya kwamba Mtu huyu aliyeketi kwa kisima na kusema naye alikuwa Masiya, aliweka chungu chake chini, akakimbia mjini na kuwaambia watu, *"Kujeni mutazame mtu ambaye aliniambia maneno yote ambayo niliyatenda. Huyu si Kristo [Masiya]?"*

Halafu watu wa mji walitoka kuona Yesu, wakamwomba kukaa kwao. Yesu alibaki kwa mji wao kwa siku mbili, akiwafundisha namna gani waliweza kuwa na moyo safi na kugeuka waabudaji wa kweli wa Mungu. Hivi, Maandiko yanasema:

Everyday Publications Inc @ 2010

> *"Na watu wengi waliamini kwa sababu ya neno lake. Wakamwambia yule mwanamke:* ***Sasa tunaamini, si kwa sababu ulituambia, lakini kwa sababu sisi wenyewe tumesikia, na tunajua kweli huyu ni Kristo, Mwokozi wa ulimwengu."*** (Yoane 4:41,42)

Basi tuendelee ndani ya Habari Njema na kuona nini ilitokea siku chache nyuma ya maneno haya. Tutaona ya kwamba **si watu wote waliopokea Yesu kama Mwokozi wa ulimwengu.** Ndani ya Habari Njema ya Luka, sura 4, Maandiko yanasema:

> (Luka 4) *14 Yesu akarudi kwa nguvu za Roho hata Galilaya; habari zake zikaenea katika inchi hata kando zote. 15 Naye alifundisha katika masunagogi yao, akitukuzwa na watu wote. 16 Akafika* ***Nazareti, pahali alipokuwa tangu utoto wake****; akaingia katika sunagogi siku ya sabato kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama kusoma. 17 Akapewa kitabu cha nabii Isaya. Na alipofungua kitabu akaona pahali palipoandikwa, 18 Roho ya Bwana ni juu yangu kwa sababu amenitia mafuta kuhubiri Habari Njema kwa masikini; kuhubiri wokovu kwa wafungwa, na vipofu kupata kuona tena, kufungua waliochubuka, 19 kuhubiri mwaka wa Bwana uliokubaliwa. 20 Akafunga kitabu, akampa mlinzi, akaketi. Na watu wote waliokuwa ndani ya sunagogi walimkazia macho. 21 Akaanza kuwaambia:* ***Leo andiko hili limetimia kwa masikio yenu."***

Na masemo haya Yesu alijitaja kuwa Masiya na Mwokozi ambaye nabii Isaya aliandika habari zake miaka mia saba mbele. Lakini, ilishinda Wayuda walioishi kwa Nazareti kuamini ya kwamba Yesu huyu aliyepata nguvu katikati yao alikuwa Mwokozi wa ulimwengu aliyetumwa toka mbingu. Kwa sababu hii walimzarau wakisema, *"Huyu siye mwana wa Yosefu?"* (Luka 4:22)

Maandiko yanaendelea kusema ya kwamba Yesu alionya watu wa Nazareti wasizarau Masiya ambaye Mungu alituma kwao. Lakini neno hili liliwakasirisha hata kupita. Hivi, Maandiko yanasema:

> (Luka 4) *28 Na wale wote waliokuwa katika sunagogi walijazwa kasirani wakisikia maneno haya. 29 Wakaondoka wakamtoa inje ya mji, wakampeleka hata ukingo wa kilima palipojengwa mji wao, wapate kumtupa chini, 30 lakini yeye akipita katikati yao alikwenda zake.*

Hivi tunaona ya kwamba watu wa Nazareti walijaribu kuua Yesu! Kwa nini walitaka kumwua? Walijaribu kumwua kwa sababu Yesu alijitaja kuwa **Masiya** ambaye manabii wote wa Mungu walikuwa wameandika juu yake. Kama watu wa kabila moja wanavyosema, "Kweli ni kama pilipili inayochoma sana." Masemo ya Yesu, masemo ya kweli yalikasirisha watu wa Nazareti sana sana hata walijaribu kumtupa toka ukingo wa kilima. Lakini hawakuweza kwa sababu saa iliyowekwa na Mungu kwa kufa kwake ilikuwa haijafika bado. Ni upumbavu kabisa kwa watu waovu kutaka kuharibu Yule aliyewekwa na Mungu kuwa Mwokozi na Mwamuzi wa dunia! Kwa wakati wa nyuma watu watamwua kweli—lakini Mungu akamfufua toka wafu nyuma ya siku tatu. Tutajifunza zaidi juu ya neno hili ndani ya somo lingine.

Everyday Publications Inc @ 2010

Halafu tunaweza kujumlisha somo letu la leo namna gani? Tulisikia habari za **mafungu mawili ya watu**. Watu wa kila fungu walisikia ya kwamba Yesu alijitaja kuwa Masiya, lakini mawazo yao juu ya neno hili yalikuwa mbalimbali kabisa.

1) Kwanza tulisikia juu ya mwanamke wa zambi aliyekutana na Yesu kwa kisima na juu ya watu wa Samaria. Walipokea maneno ya Yesu na furaha kubwa na **waliamini** ya kwamba Yesu ni Masiya, Mwokozi wa dunia.

2) Halafu tulisoma juu ya watu wa dini wa Nazareti. Walizarau masemo ya Yesu. **Hawakuamini** ya kwamba Yesu, aliyepata nguvu ndani ya mji wao wenyewe, alikuwa Masiya.

Hivi tunaona ya kwamba wenye zambi walioishi ndani ya mji wa Samaria walipokea Yesu kama Mwokozi aliyetumwa toka mbinguni, lakini watu wa dini katika Nazareti hawakumpokea.

Basi wewe? Unafanana na watu wa fungu gani? Wewe ni kama watu wa Samaria **waliokubali Yesu kama Bwana na Mwokozi wao?** Au wewe ni kama watu wa Nazareti, **waliokataa kuamini ya kwamba Yesu alikuwa Masiya aliyetumwa toka mbinguni kuokoa wenye zambi?** Unafahamu ya kwamba Yesu ni Mkombozi ndiye manabii wote waliandika juu yake? Umempokea kuwa Mwokozi wako?

Sikiliza maneno Maandiko Matakatifu yanayosema juu ya Yesu Masiya. Yanasema:

> *"Nuru ilingaa katika giza na giza halikuishinda. . . . Alikuwa ulimwenguni, na ulimwengu ulifanywa naye na ulimwengu haukumtambua. Alikuja kwake, nao walio wake hawakumpokea.* ***Lakini wote ambao walimpokea aliwapa uwezo wa kuwa watoto wa Mungu . . .*** *waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili; wala si kwa mapenzi ya mtu, lakini kwa Mungu!"* (Yoane 1:5,10-13)

Everyday Publications Inc @ 2010

Rafiki, Umezaliwa na Mungu? Unaamini Yesu kweli kweli? Umempokea kuwa Bwana na Mwokozi wako?

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Tumefika kwa mwisho wa somo hili. Ndani ya somo 69 tutasoma habari za maalama Yesu aliyoonyesha ili watu wote waweze kujua ya kwamba yeye ndiye Mwokozi wa pekee wa kweli wa dunia. . . .

Mungu akubariki wakati unapokumbuka ushuhuda wa watu wa Samaria juu ya Yesu, ndio

> ***"Tunajua kweli huyu ni Kristo, Mwokozi wa ulimwengu!"*** (Yoane 4:42)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 69

# AMRI YA YESU

(MATAYO 12; YOANE 5)

Salama iwe kwako, rafiki, kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele.

Tumefikia masomo yetu ndani ya Maandiko Matakatifu sasa kwa kitabu cha Habari Njema ambacho kinatujulisha Habari Njema juu ya Yesu Masiya. Yeye ni Mwokozi aliyefikia dunia kufungua wana wa Adamu toka utawala wa Shetani na hukumu ya milele.

Ndani ya masomo machache ya mbele, tuliona Yesu akisafiri ndani ya inchi ya Wayuda, aki**fundisha** makutano ya watu na ku**ponyesha** wagonjwa wao. Hivi watu wengi sana walimfuata. Lakini zaidi ya **viongozi vyao vya dini walikuwa na wivu** kwa sababu hawakuweza kubisha hekima ya masemo yake, wala maajabu ambayo alitenda.

Everyday Publications Inc @ 2010

Leo tutaendelea ndani ya Habari Njema na kuona ya kwamba **viongozi vya Wayuda kwa maneno ya dini walibishana na Bwana Yesu juu ya kushika siku ya pumziko** (sabato). Sabato ilikuwa siku ya saba ya juma, siku ambayo Mungu aliwapa Wayuda kuwa siku ya pumziko, nyuma ya kutumika kazi siku sita. Lakini, viongozi vya dini kwa wakati ule, Wafarisayo, walishitaki Yesu kusema alivunja sabato kwa sababu alitenda mema siku ile. Kwa njia hii walijaribu kupunguza sifa ya Yesu, kwa sababu iliwashinda kuona neno baya ndani ya maisha yake ambalo waliweza kumshitaki juu yake.

Tusome Habari Njema ya Matayo, sura 12. Maandiko yanasema, kuanza na shairi 1:

> (Matayo 12) *1 Kwa wakati ule Yesu alipita* ***siku ya sabato*** *katika mashamba ya nafaka; wanafunzi wakaona njaa, wakaanza kuvunja masuke; wakakula. 2 Lakini Wafarisayo, wakati walipoona, walimwambia: Tazama, wanafunzi wako wanafanya neno lisilo halali kufanya siku ya sabato. 3 Lakini aliwaambia: Hamukusoma neno Daudi alilofanya wakati alipoona njaa, nao waliokuwa pamoja naye;*

> *4 namna alivyoingia nyumbani mwa Mungu, akakula mikate ya onyesho isiyo halali kwake kula, wala kwa wale waliokuwa pamoja naye, lakini kwa makuhani tu? 5 Au hamukusoma katika sheria namna kwa siku ya sabato makuhani katika hekalu wanavyokufuru siku ya sabato, nao hawana kosa? 6 Lakini ninawaambia ninyi, **mmoja aliye mkubwa kupita hekalu ni hapa.** 7 Lakini kama mungalijua maana ya neno hili: **Ninataka rehema wala si sadaka**, musingalilaumu wasio na kosa. 8 Kwani **Mwana wa watu ni Bwana ya sabato.***

Yesu ana mia za majina ya heshima ndani ya Maandiko Matakatifu. Alijiita mara nyingi na moja la majina haya, ndilo ***"Mwana wa watu."*** Jina hili, Mwana wa watu, linatukumbusha ya kwamba Masiya alijinyenyekeza na kuwa na mfano wa mwana wa Adamu. Linaonyesha utukufu wake vilevile, kwa sababu Huyu ambaye alijinyenyekeza kuwa mtu, ndiye aliye na amri na hukumu juu ya wana wa Adamu. Fikili kwanza! Neno na Roho na uwezo na utukufu wa Mungu—zilikuja duniani na kukamata mwili wa mtu! Ndiyo, Yesu Kristo ni Mwana wa watu, Bwana wa sabato na Bwana juu ya wote. Lakini Wafarisayo hawakukubali maneno haya na kupokea Yesu kama Mwana wa watu na Bwana wa sabato.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Tusikie nini ilitokea nyuma ya maneno haya. Maandiko yanasema:

> (Matayo 12): *9 Akaondoka pale, akaingia katika sunagogi lao; 10 na tazama mtu **mwenye mkono uliokauka.** Wakamwuliza [Yesu] wakisema: Ni halali kuponyesha siku ya sabato? wapate kumshitaki. 11 Akawaambia: Ni nani katikati yenu aliye na kondoo mmoja, na kama akianguka katika shimo siku ya sabato, hatamshika na kumwondosha? 12 Basi mtu ni ya damani kuliko kondoo mara ngapi! **Kwa hivi ni halali kufanya mema siku ya sabato**. 13 Halafu akamwambia mtu yule: Nyosha mkono wako. Akaunyosha; ukapona kabisa kama mkono wake mwingine. 14 Lakini Wafarisayo wakatoka, wakafanya shauri juu yake, namna wanavyoweza kumwua. 15 Na Yesu akifahamu maneno haya, akaondoka kule; wengi wakamfuata; akawaponyesha wote.*

Tunaona namna Wafarisayo walivyoshitaki Yesu juu ya kutenda mabaya kwa sababu hakunyenyekea desturi zao. Udanganyifu kabisa! Watawala hawa hawakuwa na huruma hata kidogo kwa wagonjwa au wenye njaa, lakini hata hivi walijaribu kuaminisha watu ya kwamba desturi zao zilizokataza watu kutenda mema siku ya sabato zilitoka kwa Mungu! Lakini Yesu aliyejua uovu wa moyo

yao, aliwakumbusha maneno Mungu aliyotangaza ndani ya Maandiko, ya kwamba *"Kama mungalijua maana ya neno hili: Ninataka rehema wala si sadaka, musingalilaumu wasio na kosa. Kwani Mwana wa watu ni Bwana wa sabato."* (Matayo 12:7,8)

Tuendelee kusoma Maandiko kuanza na shairi 22:

> (Matayo 12) *22 Halafu wakaleta kwake* ***mmoja mwenye pepo mchafu****, kipofu na bubu; naye alimponyesha, hata yule bubu alisema na kuona. 23 Makutano yote wakashangaa, wakasema: Huyu ni mwana wa Daudi? 24 Lakini wakati Wafarisayo waliposikia, wakasema: Mtu huyu hatoi pepo wachafu, ila kwa Belzebuli, mkubwa wa pepo wachafu. 25 Naye akijua mafikili yao, akawaambia: Kila ufalme unaotengwa juu yake wenyewe utapata kuangamia; na kila mji au nyumba inayotengwa juu yake yenyewe, haitasimama. 26 Na kama Shetani akifukuza Shetani, ametengwa juu yake mwenyewe; basi ufalme wake utasimama namna gani? 27 Na kama mimi nikitoa pepo wachafu kwa Belzebuli, wana wenu wanawatoa kwa nani? Basi wao watakuwa waamuzi wenu. 28 Lakini kama mimi kwa Roho ya Mungu nikitoa pepo wachafu, ufalme wa Mungu umekwisha kuwafikia ninyi.*
>
> (Yoane 5) *1 Nyuma ya maneno haya kulikuwa karamu ya Wayuda. Yesu akapanda kwenda Yerusalema. 2 Katika Yerusalema, karibu na mlango wa kondoo ni birika, linaloitwa kwa Kiebrania Betesaida, lililo na baraza tano. 3 Makutano makubwa ya wagonjwa walilala barazani, vipofu, viwete, na wenye kupooza, wakingoja maji yachemuke. 4 Kwa sababu wakati fulani malaika alishuka, akaingia ile birika, akichemusha maji: basi yeye aliyeingia wa kwanza nyuma ya kuchemuka kwa maji, akaponyeshwa ugonjwa wote aliopata.*
>
> *5 Kulikuwa na* ***mtu mmoja aliyekuwa na ugonjwa*** *wake miaka makumi tatu na minane. 6 Yesu alipomwona huyu amelala, naye akijua amekuwa hivi muda wa siku nyingi, akamwambia: Unataka kuwa mzima? 7 Yule mgonjwa akamjibu: Bwana, sina mtu wa kunitia birikani wakati maji yanapochemuka, lakini wakati ninapokuja, mtu mwingine anashuka mbele yangu. 8 Yesu akamwambia: Simama, uchukue kitanda chako, utembee. 9 Na mara moja yule mtu alipata kuwa mzima, akachukua kitanda chake, akatembea.*
>
> *Siku ile ilikuwa sabato. 10 Basi Wayuda wakamwambia yeye aliyeponyeshwa: Leo ni sabato, haifai kwako kuchukua kitanda chako. 11 Akawajibu: Yeye ambaye alinifanya kuwa mzima ndiye ambaye aliniambia: Uchukue kitanda chako uende. 12 Lakini wakamwuliza: Mtu gani aliyekuambia, Uchukue kitanda chako uende? 13 Lakini yeye aliyeponyeshwa hakujua ni nani; kwani Yesu amejitenga, kwa sababu*

Everyday Publications Inc
@ 2010

*makutano yalikuwa kule.*

*14 Nyuma ya maneno haya Yesu akamkuta ndani ya hekalu, akamwambia: Angalia umekuwa mzima; usifanye zambi tena, neno baya zaidi lisikushike. 15 Yule mtu akakwenda zake, akapasha Wayuda habari ya kwamba Yesu ndiye ambaye alimfanya kuwa mzima. 16 Kwa sababu ile Wayuda wakaanza kutesa Yesu, wakitaka kumwua, 17 akawajibu: Baba yangu anatumika kazi hata sasa, nami ninatumika. 18* ***Basi kwa sababu hii Wayuda wakazidi kutaka kumwua, si kwa sababu alivunja sabato tu, lakini tena kwa sababu aliita Mungu Baba yake, akijifanya sawa na Mungu.***

Tuache kusoma kwa muda mfupi. Kwa sababu gani viongozi vya dini walichokoza Yesu na kujaribu kumwua? Kwa sababu Yesu aliponyesha mgonjwa siku ya sabato? Sivyo. Walijaribu kumwua kwa sababu a**lisema Mungu alikuwa Baba yake**. Iliwashinda kukubali ya kwamba Yesu alikuwa Masiya, aliyetoka kwa Mungu. Hivi walimshitaki kusema alitukana Mungu na walitafuta njia kumharibu.

Lakini Maandiko yanasema:

Everyday Publications Inc
@ 2010

(Yoane 5) *19 Yesu akajibu, akawaambia: Kweli ninawaambia ninyi,* ***Mwana*** *hawezi kufanya neno kwa yeye mwenyewe tu, lakini anafanya kama anavyoona Baba kufanya, kwa sababu yote anayofanya Baba, yule Mwana anafanya vilevile. 20 Maana Baba anapenda Mwana, na anamwonyesha yote anayofanya yeye mwenyewe, na kazi kubwa zaidi kuliko hizi atamwonyesha, ili ninyi mushangae. 21 Kwa sababu kama Baba anavyofufua wafu na kuwaweka hai, hivi Mwana anawaweka hai wale ambao anawataka. 22 Maana Baba hamhukumu hata mtu mmoja, lakini amempa Mwana hukumu yote; 23 ili watu wote waheshimu Mwana kama wanavyoheshimu Baba. Mtu yule asiyeheshimu Mwana haheshimu Baba ambaye alimtuma. 24* ***Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Yeye anayesikia neno langu na kumwamini yeye ambaye alinituma ana uzima wa milele; hafiki kwa hukumu, lakini amepita kutoka mauti kuingia uzima****.*

*31 Kama* ***nikijishuhudia*** *mimi mwenyewe, ushuhuda wangu si kweli. 32 Mwingine ananishuhudia, nami ninajua ya kuwa ushuhuda wake ambao ananishuhudia ni kweli. 33 Ninyi mulituma watu kwa* ***Yoane****, na ameshuhudia kweli. 34 Lakini mimi sipokei ushuhuda kwa watu; lakini ninasema maneno haya ili ninyi mupate kuokolewa. 35 Yeye alikuwa taa inayowaka na kuangaza, na ninyi mulipenda*

*kufurahi kwa nuru yake kwa wakati. 36 Lakini ushuhuda nilio nao unapita ule wa Yoane, kwa sababu **kazi** ambazo Baba alinipa nizimalize, na sasa ninazitenda, zinanishuhudia kama Baba alinituma. 37 Na **Baba** ambaye alinituma alinishuhudia. Sauti yake hamukusikia wakati wo wote, wala hamukuona sura yake. 38 Na hamukulinda neno lake ndani yenu, kwa sababu ninyi hamwamini yeye aliyetumwa naye.*

*39 Munatafuta katika maandiko, kwa sababu munazania ya kuwa ndani yao muna uzima wa milele; na **maandiko** haya ndiyo yananishuhudia; 40 wala hamutaki kuja kwangu mupate uzima. 41 Mimi sipokei utukufu kwa watu. 42 Lakini nimewajua ninyi ya kuwa hamuna mapendo ya Mungu ndani yenu. 43 Mimi nimekuja kwa jina la Baba yangu, nanyi hamunipokei; kama mwingine anakuja kwa jina lake mwenyewe, huyu mutapokea. 44 Munaweza namna gani kuamini, ninyi munaopokezana utukufu ninyi kwa ninyi, na hamutafuti utukufu ule unaotoka kwa Mungu aliye wa pekee.*

*45 Musizanie ya kama nitawashitaki ninyi kwa Baba; yuko mmoja ambaye atawashitaki ninyi, hata Musa, taraja lenu. 46 Kwa sababu kama mungaliamini **Musa**, mungaliniamini mimi; kwa sababu yeye aliandika habari zangu. 47 Lakini kama hamwamini maandiko yake, mutaamini maneno yangu namna gani?*

Everyday Publications Inc
@ 2010

Umesikia namna gani Bwana Yesu alihamakia Wafarisayo waliotaka kumwua? Aliwaambia ya kwamba **mtu ye yote anayekataa** Masiya aliyetumwa na Mungu toka mbingu anakataa ushuhuda wa **masemo** na **kazi** bora sana za Masiya; anakataa ushuhuda wa nabii **Yoane**, ushuhuda wa nabii **Musa** na ushuhuda wa **Maandiko**. Kwa ufupi, yeye anayekataa Masiya anakataa **Mungu mwenyewe**. Yeye anayezarau Mwana anazarau Baba ambaye alimtuma. Kukataa neno na amri ya Yesu ni kukataa neno na amri ya Mungu—kwani Yesu ndiye Neno la Mungu, Yule ambaye Mungu aliwekea hukumu na amri yote.

Mtu ye yote anayeamini Mungu na manabii yake ataamini vilevile ya kwamba Yesu ni Masiya aliyekuja toka mbinguni, kwa sababu manabii wote wa Mungu walimshuhudia. Wale wanaojua na kuamini Maandiko ya manabii wanajua na kuamini vilevile ya kwamba Yesu, Mwana wa Maria, ndiye aliyechaguliwa na Mungu kuwa Mwokozi wa ulimwengu. Haya ndiyo maneno ambayo Yesu aliwaambia viongozi vya dini wakati aliposema,

(Yoane 5) *39 Munatafuta katika maandiko, kwa sababu munazania*

> *ya kuwa ndani yao muna uzima wa milele; na* ***maandiko haya ndiyo yananishuhudia****. . . . 45 Musizanie ya kwamba nitawashitaki ninyi kwa Baba; yuko mmoja ambaye anawashitaki ninyi, hata Musa, taraja lenu. 46 Kwa sababu kama mungaliamini Musa, mungaliniamini mimi; kwa sababu yeye aliandika habari zangu. 47* ***Lakini kama hamwamini maandiko yake, mutaamini maneno yangu namna gani?***

Ingekuwa vizuri kama sisi sote mmoja mmoja tungefikili maneno haya sana, kwani Mungu anataka kutufahamisha maana yao ya ndani ndani. Mungu anataka kweli kuwa ndani ya mioyo yetu. **Kama tukisema tunaamini manabii, halafu ni sharti kwa sisi kumwamini Yeye ambaye walimshuhudia**, ndiye **Yesu Masiya**! Rafiki, tunakuacha na ulizo hili: Unaamini manabii **kweli kweli**? Watu wengi wanaamini ushuhuda wa mtu mmoja mbio, lakini watu wachache tu wanaamini **ushuhuda unaohakikishwa wa manabii wengi wa Mungu** walioandika Maandiko Matakatifu. Basi wewe? *"Unaamini manabii?"* (Matendo 26:27)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Everyday Publications Inc @ 2010

Rafiki, tumefikia mwisho wa somo hili, lakini ndani ya somo la nyuma tutaendelea na habari hizi za ajabu za Yesu Masiya . . .

Mungu akubariki na kusema na roho yako wakati unapowaza juu ya maneno ambayo Yesu aliwaambia Wafarisayo:

> ***"Lakini kama hamwamini maandiko yake [ndiye nabii Musa], mutaamini maneno yangu namna gani?"*** (Yoane 5:47)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 70

# UWEZO WA YESU

MARKO 4-6; MATAYO 9,10

Tunakusalimu tena kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. kama tunavyoona ndani ya mfulizo *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo letu la mbele tuliona ya kwamba **viongozi vya Wayuda kwa maneno ya dini walitafuta njia kuharibu Yesu kwa sababu alisema Mungu ni Baba yake, akijitaja kuwa mamoja na Mungu.** Makutano makubwa walifuata Bwana Yesu pahali po pote alipokwenda. Watu wengine ndani ya makutano haya waliamini masemo ya Yesu na wengine hawakuamini. Yesu alichagua mitume kumi na wawili katikati ya wale ambao walimwamini, ili aweze kuwa pamoja nao, kuwafundisha na kuwatuma kutangaza Habari Njema ya wokovu.

Everyday Publications Inc. @ 2010

**Mitume kumi na wawili** ambao Yesu alichagua walikuwa Simoni aliyeitwa *Petro* vilevile, na *Anderea*, ndugu yake; *Yakobo* mwana wa Zebedayo, na mdogo wake *Yoane*. Watu hawa wane walikuwa wavuvi. Mitume wengine walikuwa *Filipo, Bartolomayo, Tomasi, Matayo* mtoza kodi, *Yakobo mwana wa Alufayo, Tadeo, Simoni Mkanana*, na *Yuda Iskariota,* ambaye atamtoa kwa adui zake. (Ona Matayo 10:2-4.) Hawa ndio wanafunzi kumi na wawili waliofuatana na Yesu. Kulikuwa na **wanawake fulani** waliokwenda pamoja naye vilevile. Walikuwa: *Maria Magdalene* kwake Yesu alikuwa ametoa pepo wachafu saba; *Yoana,* mke wa Kuza mlinzi mali wa Herode; *Susana* na *wanawake wengine.* Wanawake hawa walimtumikia kwa mali zao. (Ona Luka 8:2,3.)

Kama tulivyoona mbele, watu walishangaa juu ya mafundisho ya Bwana Yesu, kwa sababu aliwafundisha na amri ambayo walimu wao wa dini walikosa. Hakuwa na amri kwa njia ya masemo yake tu, lakini aliihakikisha kwa njia ya kazi zake za uwezo. Kwani Maandiko yanasema: *"Ufalme wa Mungu si katika neno, lakini **katika***

***uwezo**."* (1 Wakorinto 4:20) Ndani ya somo la leo tutaona ya kwamba **Bwana Yesu alikuwa na uwezo na amri** juu ya kila kiumbe na mambo yote mengine duniani.

Tunaanza somo letu ndani ya Habari Njema ya Marko, sura 4. Maandiko yanasema:

> (Marko 4) *35 Siku ile, wakati wa mangaribi, [Yesu] aliwaambia: Tuvuke ngambo. 36 Wakaacha makutano, wakamchukua vilevile katika chombo. Na vyombo vingine vilikuwa pamoja naye. 37 **Zoruba kubwa ya upepo ilikuja**, mawimbi yakapiga ndani ya chombo, hata chombo kilijaa maji. 38 Yeye alikuwa kwa upande wa nyuma wa chombo, akalala juu ya mto. Wakamwamsha wakamwambia: Mwalimu, si kitu kwako tunapotea? 39 Akaamka, akahamakia upepo, akasema na bahari: **Nyamaza, utulie**. Upepo ukakoma, ikakuwa **kimya kubwa**. 40 Akawaambia: Maneno gani munaogopa? Hamuna imani? 41 Wakaogopa sana, wakasemezana: Basi **huyu ni nani hata upepo na bahari zinamtii?***
>
> (Marko 5) *1 Wakafika ngambo ya bahari hata inchi ya Wagerase. 2 Na wakati alipotoka chombo, mara moja mtu aliyetoka pahali pa makaburi, **mwenye pepo mchafu**, akakutana naye. 3 Alikuwa na makao yake katikati ya makaburi; hakuna mtu aliyeweza kumfunga hata na minyororo. 4 Kwa sababu alifungwa mara nyingi pingu na minyororo, naye alikata minyororo na alivunja pingu, hakuna mtu aliyeweza kumshinda. 5 Siku zote, usiku na mchana, katika makaburi na vilima, alikuwa akipiga makelele na kujikata kwa mawe. 6 Na wakati alipoona Yesu mbali, alipiga mbio, akamwabudu, 7 akapiga kelele kwa sauti kubwa, akasema: Nina nini nawe, Yesu Mwana wa Mungu aliye juu? Ninakuapisha kwa Mungu usinitese. 8 Kwani alimwambia: Toka kwa mtu huyu, wewe pepo mchafu. 9 Akamwuliza: Jina lako nani? Akamjibu: Legioni (maana: Jeshi), kwa sababu sisi ni wengi. 10 Akamwomba sana asiwaondoshe inje ya inchi ile. 11 Na kundi kubwa la nguruwe lilikuwa kule kwa mlima, wakikula. 12 Wakamwambia, wakisema: Ututume kwa nguruwe tuingie ndani yao. 13 Akawapa ruhusa. Pepo wachafu wakatoka wakaingia kwa nguruwe, kundi lote likatelemuka mbio kilimani hata bahari, wakazama katika bahari, wakakuwa kama elfu mbili, wakakufa baharini. 14 Wachungaji wakakimbia wakapasha habari mjini na katika mashamba. Watu wakatoka waone neno lililotokea. 15 **Watu wakakuja kwa Yesu, wakatazama mwenye pepo mchafu ameketi, amevaa nguo, mwenye akili tena—yeye aliyekuwa na lile jeshi—wakaogopa.** 16 Na wale walioona waliwaelezea maneno*

Everyday Publications Inc © 2010

ambayo yalimpata yule mwenye pepo wachafu, na habari za nguruwe.
17 Wakaanza kumwomba aondoke katika mipaka yao. 18 Naye
alipokuwa akiingia kwa chombo, yule aliyekuwa na pepo mchafu
akamwomba awe pamoja naye. 19 Hakumruhusu, lakini aka-
mwambia, Kwenda kwa nyumba yako kwa watu wako kuwaambia
maneno makubwa gani ambayo Bwana alifanya juu yako na namna
alivyokurehemu. 20 Akakwenda, akaanza kuhubiri katika inchi ya
Dekapoli maneno makubwa ambayo Yesu alimfanyia, na **wote wali-
shangaa.**

21 Na wakati Yesu alipokwisha kuvuka tena kurudi ngambo kati-
ka chombo, makutano makubwa wakakusanyika kwake, naye alikuwa
kando ya bahari. 22 Mtu mmoja wa wakubwa wa sunagogi alikuja
kwake, jina lake Yairo; akimwona, akaanguka kwa miguu yake, 23
akamwomba sana, akasema: Binti yangu mdogo ni karibu kufa, uje
uweke mikono juu yake apate kupona, na kuishi. 24 Akakwenda
pamoja naye, makutano makubwa wakamfuata, wakamsongasonga.
25 **Mwanamke mwenye kutoka damu miaka kumi na miwili,**
26 aliyeteswa sana kwa waganga wengi na kutoa mali zake zote laki-
ni haikufaa kwake hata kidogo, lakini hali yake ikazidi kuwa mbaya,
27 yeye aliposikia habari za Yesu, alipita katika makutano kwa
nyuma, **akagusa vazi lake**. 28 Kwani alisema: Kama nikigusa
mavazi yake tu, nitapona. 29 Mara moja **kisima cha damu yake
kikakauka**, akafahamu katika mwili wake ya kama amepona
ugonjwa ule. 30 Mara moja Yesu akafahamu katika roho yake ya
kuwa nguvu zimetoka kwake, akageuka katika makutano akasema:
Nani aliyegusa mavazi yangu? 31 Wanafunzi wake wakamwambia:
Unaona makutano wanakusongasonga, nawe unasema: Nani aliyeni-
gusa? 32 Akatazama pande zote amwone yule aliyefanya neno hili.
33 Mwanamke, akijua neno ambalo lilimpata, aliogopa, akatetemeka,
akakuja, akaanguka mbele yake, akamwelezea kweli yote. 34 Aka-
mwambia: Binti, imani yako imekuponyesha. Kwenda zako na salama,
uwe mzima, usiwe na mateso yako tena.

35 Hata alipokuwa kusema, watu walitoka kwa nyumba ya mku-
bwa wa sunagogi wakasema: **Binti yako amekwisha kufa**, kwa nini
unasumbusha mwalimu tena? 36 Lakini Yesu hakuangalia neno li-
lilosemwa, akamwambia mkubwa wa sunagogi: Usiogope, amini tu.
37 Hakuruhusu mtu kumfuata, ila Petro, na Yakobo, na Yoane ndugu
yake Yakobo. 38 Wakafikia nyumba ya mkubwa wa sunagogi, akaona
makelele, na watu wakilia, wakifanya maombolezo mengi. 39 Na
wakati alipokwisha kuingia, akasema: Kwa nini munafanya makelele

Everyday Publications Inc @ 2010

*na kulia? Mtoto hakufa, lakini amelala tu. 40 Wakamchekea sana. Naye alipokwisha kufukuza wote, akakamata baba na mama ya mtoto na watu walio pamoja naye, akaingia ndani alipokuwa mtoto. 41 Akashika mkono wa mtoto, akamwambia:* ***Talita kumi, maana yake: Msichana, ninakuambia: Simama.*** *42* ***Mara moja msichana akasimama****, akatembea, kwani alikuwa mwenye miaka kumi na miwili.* ***Wakashangaa sana*** *kwa maajabu makubwa. 43 Akawaagiza sana, mtu asijue habari zile; akaamuru wampe chakula.*

(Matayo 9) *27 Na wakati Yesu alipopita toka kule,* ***vipofu wawili*** *walimfuata wakilalamika na kusema: Uturehemu, wewe Mwana wa Daudi. 28 Na wakati alipokuja nyumbani, vipofu walikuja kwake; Yesu akawaambia: Munaamini ya kama ninaweza kufanya neno hili? Wakamwambia: Ndiyo, Bwana. 29 Halafu akagusa macho yao akisema: Iwe kwenu kadiri ya imani yenu. 30* ***Macho yao yakafunguliwa,*** *Yesu akawaagiza kwa nguvu, akisema: Angalieni hata mtu mmoja asijue. 31 Lakini wao wakatoka, wakaeneza habari zake katika inchi ile yote.*

*32 Na wakati walipokuwa wakitoka, tazama,* ***bubu mmoja, mwenye pepo mchafu*** *aliletwa kwake. 33 Na wakati pepo mchafu alipotolewa,* ***bubu akasema; makutano wakashangaa*** *wakisema: Haikuonekana hivi katika Israeli wakati wo wote. 34 Lakini Wafarisayo walisema: Kwa mkubwa wa pepo wachafu anatoa pepo wachafu.*

Everyday Publications Inc. @ 2010

(Marko 6) *1 Yesu akatoka kule, akafika katika inchi yake mwenyewe; wanafunzi wake wakamfuata. 2 Ilipokuwa sabato, akaanza kufundisha katika sunagogi. Watu wakisikia, wakashangaa, wakasema:* ***Huyu amepata maneno haya wapi? Na akili gani aliyopewa huyu? Na nini matendo ya uwezo yaliyofanywa na mikono yake?*** *3 Huyu si seremala, mwana wa Maria, na ndugu ya Yakobo na Yose na Yuda na Simoni? Ndugu zake wanawake si hapa pamoja nasi? Wakachukizwa naye. 4 Yesu akawaambia: Nabii hapunguki heshima ila katika inchi yake na katika jamaa yake na katika nyumba yake. 5 Hakuweza kufanya matendo ya uwezo kule ila kuweka mikono yake juu ya wagonjwa wachache, akawaponyesha. 6* ***Akashangaa kwa sababu ya kutoamini kwao****.*

*Akazunguka katika vijiji, akifundisha. 7 Aliita watu kumi na wawili, akaanza kuwatuma wawili wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu. 8 Akawaagiza: (Matayo 10) 16 Tazameni, ninawatuma ninyi* ***kama kondoo katikati ya imbwa za mwitu****; muwe basi wenye akili kama nyoka, na wapole kama hua. 17 Lakini angalieni kwa maneno ya watu; kwa maana watawapeleka ninyi mbele ya*

> *mabaraza, na katika masunagogi yao watawapiga ninyi. 28* ***Musi-waogope wale wanaoua mwili lakini hawawezi kuua nafsi; lakini zaidi mwogope yeye anayeweza kuharibu nafsi na mwili vilevile katika Gehena.*** *34 Musifikili ya kama nimekuja kuleta salama duniani; sikuja kuleta salama lakini upanga. 35 Kwani nimekuja kufitini mtu na baba yake, na binti na mama yake na mkwe na mkwe wake; 36 adui za mtu watakuwa wale wa nyumba yake mwenyewe. 37 Yeye anayependa baba au mama kupita mimi hanistahili, naye anayependa mwana au binti kupita mimi hanistahili. . . 39 Naye anayeona uzima wake ataupoteza; naye anaye-poteza uzima wake kwa ajili yangu, atauona.* Amina.

Hivi tumeona leo ya kwamba Bwana Yesu alikuwa na uwezo wa Mungu ndani ya **masemo yake** na ndani ya **kazi zake**. Makutano ambao walimfuata walishangaa kabisa, wakasema: ***"Huyu amepata maneno haya wapi? Na akili gani aliyopewa huyu? Na nini matendo ya uwezo yaliyofanywa na mikono yake!"*** (Marko 6:2)

Basi, Yesu alipata uwezo na hekima yake wapi? Hakuzi***pata*** pahali po pote, kwani Yeye mwenyewe **NI** Uwezo na Hekima ya Mungu. Bwana Yesu alifanya kazi zote za uwezo za Mungu duniani, kuonyeshea watu **pahali gani alipotoka na kama alikuwa nani**. Alikuwa na amri juu ya kila kiumbe na maneno yote mengine kama bahari, tufani, vivi hivi kwani aliitwa ***"Ruh Allah"*** na ***"Kalimat Allah"*** {kwa kiarabe}, maana yake yeye ni **Roho ya Mungu** na **Neno la Mungu**. Kwa sababu hii Yesu aliweza kutuliza tufani kubwa na kuponyesha mtu mkali mwenye pepo wachafu kwa njia ya kusema neno tu. Bwana Yesu alikuwa na uwezo usio na mpaka. Kwa sababu hii aliweza kuponyesha mwanamke aliyeteswa na ugonjwa wa damu kwa miaka kumi na miwili. Mwanamke huyu alikuwa ame-poteza mali yake yote kwa waganga na dawa zao bila kupata kusaidia, lakini mara moja alipogusa vazi la Yesu aliponyeshwa. Vivyo hivyo, wakati Yesu alipogusa macho ya vipofu wawili, mara moja watu hawa waliweza kuona tena. Na Yesu hakuwa na amri juu ya watu walio hai tu, lakini juu ya wafu vilevile! Kwa sababu hii ali-weza kufufua mtoto aliyekwisha kufa. Uwezo wa Yesu ulipita uwezo wa nabii tu kwani Yeye mwenyewe alikuwa **Neno la Mungu ndani ya mwili wa mtu.**

Ndiyo, Neno la Mungu linatujulisha ya kwamba Yesu Masiya amepewa uwezo **wote** na amri **yote.** Kwa sababu hii, ukiamini Yesu kama Mwokozi na Bwana wako, huhitaji kuogopa tena neno lo lote kama: mauti, au uzima, au pepo wachafu, au wachawi, au wakati wa

Everyday Publications Inc. @ 2010

sasa, au wakati wa kuja! **Hutahitaji kuvaa hirizi tena** wala kutoa sadaka kwa roho fulani kukuchunga kwa sababu **Bwana Yesu atakulinda**. Kwa sababu hii Maandiko yanasema: *"Katika yeye [Yesu]* ***unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa mwili.*** *Na ninyi mumetimilika katika yeye* ***aliye kichwa cha falme zote na mamlaka****!"* (Wakolosayi 2:9,10)

Rafiki, unaamini Yule aliye *"juu ya uwezo na amri yote ya dunia"?* Au unakaa kujaribu kutuliza wenye uwezo na amri wa dunia hii?

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutaendelea ndani ya Habari Njema na kusikia namna Yesu alivyofundisha makutano na mifano . . .

Mungu akubariki na kukufundisha maana ya ndani ya maneno aliyotangaza juu ya Masiya:

> ***"Katika yeye [Yesu] unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa mwili."*** (Wakolosayi 2:9,10)

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 71

# Mifano Mikubwa Miwili

### Luka 8; Matayo 13

Salama iwe kwako, rafiki. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea leo na mfulizo huu *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo la mbele tuliona ya kwamba Yesu Masiya alikuwa na amri kubwa kupita amri ya nabii. Yesu alijaa uwezo wa Mungu. **Alikuwa Uwezo mwenyewe wa Mungu ndani ya mwili wa mtu!** Kwa sababu hii aliweza kutuliza tufani, kutoa pepo wachafu, kuponyesha wagonjwa na vipofu, na hata kufufua wafu!

Leo tutaendelea ndani ya Habari Njema {*Injil*} na kusikia namna gani Bwana Yesu alifundisha makutano akitumika na **mifano**. Yesu alifundisha kweli mara nyingi akitumia mifano kwa sababu zaidi ya watu ambao walimfuata njiani hawakutaka kujua Neno la Mungu kweli kweli. Neno walilotaka lilikuwa kwa Yesu kuponyesha miili yao toka **ugonjwa**, lakini hawakutaka aponyeshe nafsi zao toka zambi. Fungu lingine la watu ambao walimfuata, kama kundi la vingugwa, walikuwa viongozi wa Wayuda kwa maneno ya dini waliosikiliza masemo ya Yesu karibu karibu waweze kupata njia kumshitaki. Wakati watu hawa walipokuwa karibu Yesu alitumika na mifano wakati aliposema na makutano. Alingoja wakati yeye na wanafunzi wake wa kweli walipokuwa peke yao mbele ya kueleza maana ya mifano.

Mungu anataka kila mtu kujua kweli na kuokolewa, lakini kama tukiwa wakaidi rohoni Mungu hatatufunulia kweli yake. Mungu anataka sisi kutafuta kweli na roho moja, namna zaidi ya watu wanavyotafuta mali! Nabii Solomono aliandika, ***"Kama ukiutafuta (ufahamu) kama feza, na kuutafutatafuta kama hazina zilizofichwa; halafu utafahamu woga wa Bwana, na kupata maarifa kwa Mungu."*** (Mezali 2:4,5) Basi wewe? Unahesabu **kweli ya Mungu** kuwa na faida kupita mali au vitu vyo vyote vingine? Neno la Mungu ni kwa pahali pa kwanza ndani ya nia na roho yako? Labda hujui hali ya kweli ya moyo wako mbele ya Mungu. Basi sikiliza

Everyday Publications Inc
@ 2010

vizuri '**Mfano wa Mpandaji Mbegu**' ambao Bwana Yesu alitangaza kwa watu.

Tunasoma ndani ya Habari Njema ya Luka, sura 8. Maandiko yanasema:

> (Luka 8) *4 Makusanyiko makubwa walikusanyika kwake, na watu wa kila mji wakikuja mbele yake, alisema kwa mfano: 5* ***Mpandaji mbegu alitoka kupanda mbegu zake****: wakati alipopanda nyingine zilianguka karibu na njia, zikakanyagwa, ndege za hewa wakazikula. 6 Nyingine zikaanguka juu ya mwamba, zikamea, zikakauka kwa kukosa maji. 7 Nyingine zikaanguka kati ya miiba, na miiba ikamea pamoja nazo, ikazisonga. 8 Nyingine zikaanguka juu ya udongo mzuri, zikamea, zikazaa matunda hata mia moja. Alipokwisha kusema maneno haya, alipaza sauti, akisema:* ***Mwenye masikio ya kusikia, asikie.***
>
> *9 Wanafunzi wakamwuliza, wakisema: Mfano huu ni nini? 10 Akasema: . . . 11 maana ya mfano ni hii:* ***Mbegu*** *ni Neno la Mungu. 12 Na wale* ***karibu na njia*** *ndio wanaosikia, kisha Shetani anakuja kuondosha neno katika mioyo yao wasipate kuamini na kuokolewa. 13 Na wale* ***juu ya mwamba*** *ndio wale wakati wanaposikia neno, wanalipokea kwa furaha, na hawa hawana mizizi, wanasadiki kwa saa kidogo, lakini wakati wa majaribu, wanajitenga wenyewe. 14 Nazo zilizoanguka* ***katika miiba****, hawa ni wale wanaosikia, na wanakwenda zao, wanasongwa na masumbuko, na utajiri, na anasa za maisha haya, nao hawazai matunda kwa utimilifu. 15 Lakini zile juu ya* ***udongo mzuri****, ndio hawa walio watu wenye mioyo ya kweli na mema, wanasikia neno, na kulishika, kisha wanazaa matunda kwa uvumilivu.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

Unafahamu maana ya mfano wa mpandaji mbegu? Ndani ya mfano huu tunaona mbegu na udongo. Mbegu ni mfano wa nini? Bwana Yesu alisema nini? Alisema: Mbegu ni **Neno la kweli la Mungu**. Basi udongo? Udongo ni mfano wa nini? **Udongo ni mfano wa moyo wa mtu.**

Ndiyo, Neno la Mungu ni sawasawa na mbegu njema, kwa sababu ni hai na lina uwezo kuzaa uzima wa milele na baraka ya kweli ndani ya moyo na maisha yako. Lakini moyo wa mtu ni kama udongo ulio nguvu sana na kukauka mara nyingine. Tufikili juu ya neno hili. Tunaona udongo namna ngapi ndani ya mfano huu? Tuliona mbegu ilianguka juu ya udongo namna ine.

1) Nyingine zilianguka juu ya **njia iliyokuwa ngumu**.

2) Nyingine zilianguka katikati ya **miamba mingi.**

3) Nyingine zilianguka katikati ya **miiba**.

4) Nyingine zilianguka juu ya **udongo mzuri**.

**Kwanza**, Yesu alifundisha ya kwamba watu wengi duniani wana moyo unaofanana na **njia ngumu** ambayo watu wanatembea juu yake. Mioyo ya watu wengine ni migumu kama sakafu. Mbegu zikianguka juu ya njia ngumu—nini itatokea? Zitaota na kuzaa matunda? Sivyo, hata kidogo. Haziwezi hata kuingiza mashina ndani ya udongo namna hii. Watu wanatembea juu yao na kuzikanyaga, na ndege watazikula. Mioyo ya watu wengi ni namna hii. Watu wenye mioyo kama udongo mgumu ndio wale **wasioweka roho juu ya Maandiko ya Manabii** na hivi hawaamini ya kwamba Yesu ni Mwokozi wa ulimwengu. Wanaweka roho juu ya mawazo yao wenyewe tu au juu ya desturi za babu zao. Neno la kweli la Mungu haliwezi kuzaa uzima ndani ya mioyo yao, kama vile mbegu zinazoanguka juu ya njia iliyo ngumu haziwezi kuzaa uzima.

Everyday Publications Inc @ 2010

Udongo namna ya **pili** ambao Yesu alisema juu yake ulikuwa na **miamba mingi na udongo nusu.** Udongo wenye miamba mingi ni mfano wa moyo wa mtu anayesikiliza Neno la Mungu na kulipokea mara moja na furaha, lakini **hadumu**, kwa sababu Neno la Mungu halikupata njia kuingia kabisa ndani ya moyo wa mtu ule. Anasema anaamini, lakini wakati anapopata taabu au akiteswa kwa sababu ya Neno la Kweli, anaacha kweli. Kuna watu wengi namna hii. Neno la Mungu haliingii kabisa ndani ya mioyo yao, kwa sababu wanapenda sifa ya watu kupita sifa ya Mungu. Hivi, Neno la Mungu halina faida kwao, kama vile mbegu zilizoanguka juu ya mwamba zisizokuwa na faida.

Udongo namna ya **tatu** una **miiba mingi**. Nini inatokea wakati mbegu zinapoanguka katikati ya miiba? Zitazaa matunda? Sivyo, hata kidogo! Miiba itazisonga wakati zisipozaa matunda bado. Udongo wenye miiba ni mfano wa moyo wa mtu anayesikiliza Neno la Mungu, lakini masumbuko ya dunia, na **udanganyifu wa mali na choyo unamshinda**, na kushinda Neno hata haliwezi kuzaa matunda. Wana wengi wa Adamu wana mioyo kama udongo wenye miiba. Wanafikili: "Ndiyo, siku nyingine nitaanza kusoma Maandiko ya Manabii. Wakati ninapopata saa, nitasikiliza Neno la Mungu, *'insha'a Allah!"* {Kiarabe*: Mungu akitaka hivi}.* Lakini Shetani anajua vizuri ya kwamba watu namna hii hawataweka saa kamwe kufahamu Neno la Mungu. Kila siku masumbuko na mahitaji yatatawala

mioyo na nia zao. Ni lazima kwao kutumika kazi, kupata mali, kwenda kwa soko, kununua na kuuza, kujifunza, kulala usingizi, vivyo hivyo.

Ni hivi ndani ya maisha yako? Yanajaa masumbuko na mafikili mengi sana nawe hujaweka saa hata mara moja kutafuta Kweli ya Mungu na moyo wako wote? Kumbuka ya kwamba siku moja mauti yatakupata gafula na maisha yako yatakwisha kwa milele. Siku ile utajua maneno gani yalikuwa kweli na maneno gani yalikuwa wongo, lakini kujua kweli ambayo hukutafuta wala kutii wakati ulipokuwa hai hakutakuwa na faida kwako, kwa sababu saa kwa toba itakuwa imepita nawe utapotea kwa milele!

Namna ya **ine** ya udongo ulikuwa **udongo mzuri**. Mbegu ambayo mlimaji alipanda ndani ya shamba lake ambalo alilitayarisha vizuri mbele ziliingiza mashina ndani ya udongo na kuzaa matunda mengi hata mlimaji alivuna mara mia ine kupita mbegu alizopanda. Udongo mzuri uliopokea mbegu ni mfano wa mtu anayesikia Neno la Mungu na **kulichunga moyoni** mwake, na kuzaa haki na uzima wa milele. Neno la Mungu ni hai na lenye uwezo na litazaa uzima wa milele na mwenendo wa haki ndani ya watu wote ambao wanalipokea na unyenyekevu na roho ya kweli.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Haya ndiyo maneno Yesu aliyofundisha kwa njia ya mfano wa mpandaji. Neno la Mungu ni kama **mbegu nzuri,** na mioyo yetu ni kama **udongu mgumu**. Inapasa nini kutokea mbele ya kupanda mbegu ndani ya udongo mgumu? Inapasa kutayarisha udongo kwa njia ya kuulima na jembe. Vivyo hivyo moyo unaopendeza Mungu ni moyo wa kuvunjika na wa toba, uliotayarishwa kupokea Mbegu Njema ya Neno la Mungu. Moyo unaopendeza Mungu ndio moyo unaopokea Neno lake na unyenyekevu na imani. Hii ndiyo maana ya Maandiko wakati yanaposema: *"Kila mtu awe mwepesi wa kusikia, lakini si mwepesi kusema; . . Basi wekeni mbali uchafu wote na ubaya unaozidi, na kupokea* ***kwa upole neno lililopandwa ndani, linaloweza kuokoa roho zenu.****"* (Yakobo 1:19,21)

Hali ya moyo wako ni namna gani? Una moyo wa unyenyekevu, ulio tayari kupokea maneno Mungu anayosema ndani ya Maandiko Matakatifu kwa njia ya manabii wake? Neno la Mungu linapata nguvu ndani ya moyo wako? Au moyo wako ni kama udongo mgumu, wenye mawe na miiba? Neno la Mungu ni Mbegu Njema, lakini linazaa uzima na baraka ndani ya mioyo ya wale tu ambao wanaliamini na roho ya kweli na kulitii.

Sasa tusikie mfano mwingine Yesu aliopasha kwa makutano. Ni **Mfano wa Magugu**. Maandiko yanasema:

> (Matayo 13) *24 [Yesu] akawatolea mfano mwingine akisema: **Ufalme wa mbinguni umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema shambani mwake;** 25 **lakini wakati watu walipolala usingizi, adui yake alikuja, akapanda magugu katikati ya ngano, akakwenda zake.** 26 Lakini wakati majani ya ngano yalipoota na kuzaa matunda, magugu yakaonekana vilevile. 27 Watumishi wa mwenye nyumba wakakuja, wakamwambia: Bwana, hukupanda mbegu njema shambani mwako? Basi limepata magugu wapi? 28 Akawaambia: Adui amefanya hivi. Watumishi wanamwambia: Unataka basi twende kuyaokota? 29 Lakini alisema: Hapana, isiwe mukiokota magugu, munaondosha ngano vilevile pamoja nayo. 30 Yote yakue pamoja hata mavuno; na kwa wakati wa mavuno nitawaambia wavunaji: Okoteni kwanza magugu na kuyafunga matita mukayachome; lakini kusanyeni ngano galani mwangu.*
>
> *36 Halafu akaacha makutano, akakwenda nyumbani, wanafunzi wake wakakuja kwake wakisema: Utuelezee mfano wa magugu ya shamba. 37 Akajibu, akasema: Yeye anayepanda mbegu njema ni **Mwana wa watu**; 38 na shamba ni **dunia**; mbegu njema ni hawa **wana wa ufalme**; na magugu ni **wana wa yule mwovu**; 39 adui ambaye aliwapanda ni **Shetani**; na mavuno ni **mwisho wa dunia**; na wavunaji ni **malaika**. 40 Basi sawasawa magugu yanavyookotwa na kuchomwa kwa moto, ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia. 41 Mwana wa watu atatuma malaika zake, nao wataokota toka ufalme wake vitu vyote vinavyokwaza, nao wanaotenda uovu, 42 na kuwatupa katika tanuru ya moto; kule kutakuwa kulia na kusaga meno. 43 Halafu wenye haki watangaa kama jua katika ufalme wa Baba yao. **Mwenye masikio ya kusikia, asikie."*** Amina.

Everyday Publications Inc @ 2010

Ndani ya mfano wa magugu, Bwana Yesu alisawanisha dunia na shamba la ngano. **Mpandaji** ni mfano wa **Yesu Masiya. Ngano** iliyoota shambani ni mfano wa wale walio **watoto wa Mungu** kwa sababu waliamini Habari Njema ya Masiya. **Adui** aliyepanda magugu katikati ya ngano ni **Shetani**. **Magugu** ndio wale **wasio wa Mungu** kwa sababu hawakupokea Habari Njema ya Masiya. Mavuno ndiyo **Siku ya Hukumu**. **Ngano inayowekwa ndani ya gala** ni mfano wa **wale walio na ruhusa kuishi mbele ya Mungu kwa milele.** Lakini, m**agugu yanayokokotwa na kuchomwa** ni mfano wa **wale watakaotupwa ndani ya moto wa milele.**

Rafiki, wewe ni kama **ngano**? Au **magugu**? Tafuta roho yako! Siku ya Hukumu inakaribia! Mwamuzi anasimama kwa mlango! Una tumaini kwa siku utakaposimama mbele ya Mwamuzi? Huhitaji kuogopa siku ile kama ukiamini moyoni mwako Habari Njema ya Yule aliyekuja kukuokoa toka jehanum na uharibifu wa milele. Sikiliza maneno Yesu Masiya aliyotangaza juu ya Siku ya Hukumu: *"Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Yeye **anayesikia** neno langu na **kumwamini** yeye ambaye alinituma ana uzima wa milele; **hafiki kwa hukumu**, lakini amepita **kutoka mauti kuingia uzima**."* (Yoane 5:24) Amina!

~~~~~~~~~~~~~~~~

Mara ya nyuma, Mungu akitaka, tutaendelea ndani ya Habari Njema na kuona namna Yesu alifanya ajabu kubwa, ndilo kulisha watu zaidi ya elfu tano na mikate mitano na samaki wawili tu ...

Mungu akupe ufahamu kwa maneno yote uliyojifunza leo, wakati unapokumbuka masemo ya Bwana Yesu:

***"Mwenye masikio ya kusikia, asikie!"*** (Matayo 13:43)

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 72

# Mkate wa Uzima

### Marko 6; Yoane 6

Salama iwe kwako, rafiki. Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea leo na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo letu la mbele tuliona Bwana Yesu akisema na makutano. Aliwafundisha kwa njia ya mifano iliyojaa na kweli za ndani ndani, za milele. **Lakini zaidi ya watu hawakufahamu vizuri maana ya mifano ile kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao.** Hawakutambua mema ya mambo ya mbingu lakini waliweka roho juu ya maneno ya dunia tu. Zaidi yao hawakufuata Yesu kwa sababu alikuwa Mwokozi wa wenye zambi; walitembea pamoja naye kwa sababu ya faida waliyopata kwake kwa mahitaji yao ya mwili.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Leo tutasoma maneno mengine Yesu aliyosema. Tutaona vilevile ya kwamba alihakikisha masemo yake kwa njia ya ajabu. Somo letu la leo linaitwa "**Mkate wa Uzima."** Tungeweza kuliita vilevile "Chakula kinacholeta Uzima wa Milele."

Sasa tuendelee kusoma ndani ya kitabu kitakatifu, Habari Njema ya Marko, sura 6. Maandiko yanasema:

> (Marko 6) *30 Na mitume walikusanyika kwake Yesu . . . 31*
> *Akawaambia: Kujeni ninyi peke yenu katika pahali pasipo watu, muka-*
> *pumzike kidogo, sababu watu waliokuja na waliokwenda walikuwa*
> *wengi, wala hawakuwa na nafasi ya kula. 32 Wakakwenda katika cho-*
> *mbo hata pahali pasipo watu. 33 Watu wengi waliwaona wakikwenda*
> *zao, wakawatambua na walikwenda huko na miguu toka miji yote,*
> *wakatangulia kufika. 34 Na wakati alipotoka chombo, aliona makutano*
> *makubwa, akawahurumia, kwa sababu walikuwa kama kondoo wasio*
> *na mchungaji; akaanza kuwafundisha maneno mengi.*
>
> *35 Hata saa nyingi zilipopita, wanafunzi wake wakamkwendea,*
> *wakasema: Pahali ni tupu na mchana unapita. 36 Uage watu hawa*

*waende katika mashamba na miji kandokando, wajinunulie chakula. 37 Akawajibu, akasema: Ninyi muwape chakula. Wakamwambia: Twende tukanunue mikate ya dinari mia mbili, tuwape kula? 38 Akawaambia: Muna mikate mingapi? Kwendeni mutazame. Walipokwisha kujua wakasema: Mitano na samaki mawili. 39 Akawaamuru wawaketishe wote, kundi kundi katika majani mabichi. 40 Wakakaa safu safu, hapa mia, hapa makumi tano. 41 Akatwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama mbinguni, akazibariki, akavunja mikate, akawapa wanafunzi waiweke mbele yao, na wale samaki wawili akawagawia wote. 42* ***Wote wakakula, wakashiba.*** *43 Wakaokota vipande vilivyovunjika vitunga kumi na viwili, na vya vipande vya samaki. 44 Waliokula mikate walikuwa wanaume* ***elfu tano****.*

*45 Mara moja [Yesu] alishurutisha wanafunzi waingie chomboni, watangulie kwenda ngambo hata Betesaida, wakati yeye alipokuwa akiaga makutano. 46 Hata alipokwisha kuagana nao, alikwenda kilimani kuomba. 47 Na wakati mangaribi ilipofika chombo kilikuwa katikati ya bahari, na yeye alikuwa pekee katika inchi kavu. 48 Akawaona wakitaabika kwa kuvuta makasia, kwa sababu upepo ulikuwa kushindana nao; hata ilipopita kama zamu ya ine ya usiku akakuja kwao, akitembea juu ya bahari; akataka kuwapita. 49 Na wakati walipomwona akitembea juu ya bahari, walizani ya kama ni kivuli, wakapiga kelele, 50 kwa sababu wote walimwona, wakafazaika. Mara moja akasema nao, akawaambia: Tieni moyo; ni mimi, musiogope. 51 Akapanda kwao katika chombo; upepo ukakoma; wakashangaa sana mioyoni mwao; 52 kwa sababu hawakufahamu habari za mikate, lakini mioyo yao ilikuwa migumu. 53 Na wakati walipokwisha kuvuka, wakafikia inchi ya Genesareti, wakatia nanga.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

(Yoane 6) *22 Siku ya pili makutano waliosimama ngambo ya bahari wakaona ya kama hakuna chombo kingine kule, ila kimoja, walipoingia wanafunzi wake; tena ya kama Yesu hakuingia katika chombo kile pamoja na wanafunzi wake, lakini wanafunzi wake walikwenda peke yao. . . . 24 Basi wakati makutano walipoona ya kama Yesu hakuwa kule, wala wanafunzi wake, wao wenyewe wakaingia vyombo, wakakwenda . . . wakitafuta Yesu. 25 Wakati walipomwona ngambo ya bahari, walimwambia: Rabi, ulikuja hapa saa gani? 26 Yesu akawajibu, akasema, Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Munanitafuta, si kwa sababu muliona alama, lakini kwa sababu mulikula mikate mukashiba, 27* ***Musifanye kazi kwa chakula chenye kuharibika, lakini kwa chakula kinachodumu***

> ***hata uzima wa milele****, ambacho Mwana wa watu atawapa ninyi, kwani huyu ndiye aliyetiwa mhuri na Baba, ndiye Mungu."*

Tuache kwanza kusoma. Kwa nini Yesu alisema na makutano, ***"Musifanye kazi kwa chakula chenye kuharibika"***? Ni kusema haifai kwetu kutumika kazi kujipatia chakula? Sivyo, hii si maana yake, kwa sababu Neno la Mungu linasema vilevile: *"Kama mtu hataki kufanya kazi, basi asile chakula hata kidogo."* (2 Watesalonika 3:10). Kama ni hivi, kwa nini Yesu alisema: *"Musifanye kazi kwa chakula chenye kuharibika"*? Maana ya neno Yesu alilosema ndiyo hii: Kama ukitumika kwa kushibisha tumbo lako tu, na kutafuta vitu vya dunia tu, utapoteza vyote kwa mwisho wa maisha yako, kwa sababu mwili wako utakufa na kugeuka mavumbi tena. Lakini kuna kitu kimoja ndani ya mwili wako kisichokufa kamwe, ndicho **roho yako**. Roho ya mtu itakaa milele—au ndani ya pahali pa utukufu panapoitwa **Mbingu** (Paradiso) au ndani ya pahali pa kuogofya panapoitwa **Jehanum**. Kwa sababu hii Yesu alisema, *Musifanye kazi kwa chakula chenye kuharibika, lakini kwa chakula kinachodumu hata uzima wa milele!"* Kwa njia hii Yesu alionya makutano, wasitafute vyakula vya kuharibika tu, lakini watafute Neno la Mungu lisilopita milele. Kwa sababu *"Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno linalotoka katika kinywa cha Mungu."* (Matayo 4:4) Haya ndiyo masemo ya Bwana Yesu.

Everyday Publications Inc. @ 2010

Ni huzuni kwa sababu zaidi ya watu waliozunguka Yesu hawakuweka roho juu ya Neno la Mungu, wala kuamini ndani ya Yule ambaye Mungu alituma! Kujaza matumbo yao kulikuwa na faida kwao kupita kujaza mioyo yao na kweli zilizoweza kuwaokoa toka hukumu ya Mungu. Kwa sababu hii Yesu alisema nao, (Yoane 6) *27 Musifanye kazi kwa chakula chenye kuharibika, lakini kwa chakula kinachodumu hata uzima wa milele . . . 28 Halafu walimwambia: Tufanye nini, tupate kufanya kazi za Mungu? 29 Yesu akajibu, akawaambia: Hii ni kazi ya Mungu,* ***mumwamini yeye aliyetumwa naye****.*

Ulisikia jibu la Yesu? Namna gani mtoto wa Adamu anayezaliwa mwenye zambi anaweza kupendeza Mungu? Sisi tunaweza kutumika kazi na kufanya maneno yanayopendeza Mungu? Sisi wenyewe tunaweza kujiokoa toka uwezo wa Shetani na zambi na jehanum? Tunaweza kujipatia moyo mkamilifu na mtakatifu ambao Mungu anaamrisha? Sivyo! Kama watu wa kabila moja wanavyosema, "Hata mti ukilala ndani ya maji muda mrefu sana, hautageuka mamba kamwe." Basi namna gani mzao wa Adamu anaweza kupendeza Mungu? Bwana Yesu alisema nini juu ya neno hili? Alisema, *"Hii ni*

*kazi ya Mungu,* ***mumwamini yeye aliyetumwa naye.*** *"* Hakuna mtu anayeweza hata kuanza kupendeza Mungu kufika wakati anapoamini ndani ya Mkombozi mtakatifu ambaye Mungu alituma.

Ni huzuni kwa sababu zaidi ya watu hawakuamini ya kwamba Yesu alikuwa Mwokozi aliyetumwa na Mungu. Kwa sababu hii walisema naye,

> (Yoane 6) *30 Unafanya alama gani basi, tuone na tukuamini? Unafanya kazi gani? 31 Baba zetu walikula mana katika jangwa, kama ilivyoandikwa: Aliwapa mkate toka mbinguni. 32 Yesu akawaambia: Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Siye Musa aliyewapa ninyi mkate ule toka mbinguni, lakini Baba yangu anawapa ninyi mkate wa kweli toka mbinguni. 33 Sababu mkate wa Mungu ni ule unaoshuka toka mbinguni, na kupa dunia uzima. 34 Basi wakamwambia: Bwana, siku zote utupe mkate huu. 35 Yesu akawaambia:* ***Mimi ni mkate wa uzima, yeye anayekuja kwangu hatasikia njaa kabisa, naye mwenye kuniamini hataona kiu kabisa!"***

Everyday Publications Inc @ 2010

Maana ya masemo haya ya Yesu ndiyo hii: Kama Mungu alivyotuma vyakula toka mbinguni kulisha wana wa Israeli kwa miaka makumi ine kusudi wasife katika jangwa, vivyo hivyo Mungu alituma kwa wana wote wa Adamu "Chakula" kinacholeta uzima ili tusife ndani ya zambi zetu!

"Chakula" hiki ni wapi? Kuna chakula fulani duniani ambacho unaweza kula kukuwezesha kukaa karibu na Mungu milele? Sivyo, hakuna chakula namna hii. Basi, "Chakula" hiki kinacholeta uzima wa milele ni nini? Bwana Yesu alisema nini? Alisema,

> (Yoane 6) *35* ***Mimi ni mkate wa uzima****, yeye anayekuja kwangu hatasikia njaa kabisa, naye mwenye kuniamini hataona kiu kabisa. 36 Lakini niliwaambia ninyi ya kama muliniona vile, lakini hamuniamini. 37 Wote ambao [Mungu] Baba ananipa watakuja kwangu, naye anayekuja kwangu sitamtupa inje kabisa . . . 40 Na haya mapenzi yake Baba ambaye alinituma, kila mtu anayetazama Mwana na kumwamini apate uzima wa milele, nami nitamfufua siku ya mwisho.*
>
> *41 Basi Wayuda wakamnungunikia kwa sababu alisema: Mimi ni mkate ulioshuka toka mbinguni. 42 Wakasema: Huyu si Yesu, mwana wa Yosefu, baba yake na mama yake tunaowajua? Basi, kwa sababu gani anasema: Nimeshuka toka mbinguni?*
>
> *43 Basi Yesu akajibu, akawaambia: Musinungunike katikati yenu . . . 45 Kila mtu aliyesikia Baba na aliyefundishwa, anakuja kwangu.*

*46 Si kwamba mtu aliona Baba ila yeye aliyetoka kwa Mungu, yeye ndiye aliyeona Baba. 47 Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Yeye mwenye kuniamini mimi ana uzima wa milele. 48 Mimi ni mkate wa uzima. 49 Baba zenu walikula mana katika jangwa, wakakufa. 50 Huu ni mkate unaoshuka toka mbinguni, ili mtu apate kuukula, asife. 51* ***Mimi ni mkate wa uzima ulioshuka toka mbinguni****; kama mtu akikula mkate huu, atakaa milele . . ."*

*60 Basi wanafunzi wake wengi waliposikia haya, wakasema: Neno hili ni gumu, nani anayeweza kulisikia? 61 Lakini Yesu alijua yeye mwenyewe ya kama wanafunzi wake walimnungunikia neno hili, akawaambia: Neno hili linawachukiza ninyi? 62 Basi nini, kama mutaona Mwana wa watu akipanda pahali alipokaa mbele? 63 Roho ndiye anayepatiza uzima; mwili haufai kitu; maneno ambayo niliyasema kwenu ni roho, nayo ni uzima. 64 Lakini kuna wengine katikati yenu wasioamini. Kwa sababu Yesu alijua tangu mwanzo ni nani wasioamini na ni nani ambaye atamtoa. . .*

*66 Kwa sababu ya maneno haya, wengi katika wanafunzi wake wakarudi nyuma, wala hawakutembea tena pamoja naye. 67 Basi Yesu akawaambia kumi na wawili: Ninyi munataka kuondoka vile? 68 Simoni Petro akamjibu:* ***Bwana, tutakwenda kwa nani? Wewe una maneno ya uzima wa milele. 69 Na tumeamini na tunajua wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu wa uzima.***

Everyday Publications Inc. @ 2010

Hivi wanafunzi wengi wakageuka na hawakutembea pamoja na Yesu tena kwa sababu ya mafundisho yake magumu. Lakini, katikati ya wale waliofuata Yesu kulikuwa na wengine wasiotaka kumwacha kwa sababu waliamini kabisa ya kwamba Yesu alikuwa Masiya, Mtakatifu toka Mungu—**Mkate wa Uzima—"Chakula cha Kweli" kinacholeta uzima wa milele!**

Ni vivyo hivyo sasa. Wakati unapokwisha kujua kama Yesu ni nani na kama yeye ni namna gani na kazi kubwa ambayo alikufanyia—hutaweza kukubali bwana ye yote mwingine tena! Uzima wa milele unatoka kwa Yesu tu. Yeye peke yake anaweza kushibisha hamu ya moyo wa mtu anayetaka sana kujua kabisa kwamba ameokolewa kweli na kuwa na ushirika wa karibu na Mungu.

Basi wewe? Una njaa na kiu kwa uzima wa milele? Unataka sana kuwa na ushirika na Mungu hapa duniani na kwa wakati wa kuja? Kama ni hivi, waza sana juu ya mwito wa Bwana Yesu anayesema, ***"Kujeni kwangu, ninyi wote munaosumbuka na wenye mzigo mzito, nami nitawapumzisha ninyi . . . Mimi ni mkate wa uzima, yeye***

***anayekuja kwangu hatasikia njaa kabisa, naye mwenye kuniamini hataona kiu kabisa."*** (Matayo 11:28; John 6:35) Amina.

~~~~~~~~~~~~~~~~

Rafiki, asante kwa kujifunza pamoja nasi. Mara ya nyuma, Mungu akitaka, tutaendelea ndani ya Habari Njema na kusikia namna gani makutano walitengana kwa sababu ya Yesu. . .

Mungu akubariki wakati unapokumbuka maneno haya ya Bwana Yesu:

> ***"Mimi ni mkate wa uzima, yeye anayekuja kwangu hatasikia njaa kabisa, naye mwenye kuniamini hataona kiu kabisa."*** (Yoane 6:35)

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 73

# Yesu Analeta Mtengo

### Matayo 15,16; Yoane 7

Salama iwe kwako, rafiki kwa jina la Mungu, Bwana wa salama. Ndani ya somo letu la mbele tuliona Bwana Yesu aliongeza mikate mitano na samaki mbili kutosha kulisha makutano ya kupita watu elfu tano. Kesho yake makutano makubwa walizunguka Yesu, lakini Yesu, aliyejua mawazo ya mioyo yao, alisema nao,

> *"Munanitafuta, si kwa sababu muliona alama, lakini kwa sababu mulikula mikate mukashiba. Musifanye kazi kwa chakula chenye kuharibika, lakini kwa chakula kinachodumu hata uzima wa milele.* ***Mimi ni mkate wa uzima****, yeye anayekuja kwangu hatasikia njaa kabisa, naye mwenye kuniamini hataona kiu kabisa!"* (Yoane 6:26,27,35)

Everyday Publications Inc @ 2010

Na huzuni watu wengi waligeuka wakaacha kufuata Yesu kwa sababu waliweka roho juu ya vyakula vya kulisha miili yao kupita juu ya chakula kilichoweza kulisha roho zao. Lakini wengine walikaa kufuata Yesu kwa sababu waliamini ndani ya mioyo yao ya kwamba Yesu ndiye Yule Mtakatifu toka Mungu na chimbuko cha uzima wa milele.

Leo tunakusudi kuendelea ndani ya Habari Njema takatifu na kuona namna Yesu alivyo**kabilishwa na watawala wa Wayuda kwa maneno ya dini**, na ya kwamba Wayuda **walitengana kwa sababu ya Yesu**. Mbele ya kuanza, itatusaidia kujua ya kwamba mafundi ya dini walioitwa Wafarisayo na zaidi ya Wayuda walishika desturi fulani ambazo wao wenyewe na wazazi wao walisimamisha. Kwa mfano, wakati waliporudi kwao toka kutembea katikati ya watu, hawakuweza kula chakula kufika walipokwisha kunawa mikono. Walikuwa na desturi nyingi nyingine, kama kunawa vikombe, vyungo vya maji, na mabirika ili waweze kuwa "safi".

Sikia maneno yanayoandikwa ndani ya Habari Njema ya Matayo sura 15. Maandiko yanasema:

> (Matayo 15) *1 Halafu Wafarisayo na waandishi walikwendea Yesu toka Yerusalema wakisema: 2 Kwa nini wanafunzi wako wanavunja desturi za wazee? Kwa sababu hawanawi mikono yao wakati wanapokula chakula. 3 Akajibu, akawaambia:* ***Kwa nini ninyi vilevile munavunja amri ya Mungu kwa sababu ya desturi yenu?*** *4 Kwa sababu Mungu alisema: Heshimu baba yako na mama yako; na, Yeye anayetukana baba yake au mama yake, afe kufa. 5 Lakini ninyi munasema: Kila mtu anayemwambia baba yake au mama yake: Yote uliyopaswa kusaidiwa na mimi yameletwa kwa Mungu; 6 yeye haheshimu baba yake.* ***Mumefanya Neno la Mungu kuwa bule kwa sababu ya desturi zenu****. 7 Ninyi wadanganyifu, Isaya alitabiri vema juu yenu akisema: 8* ***Watu hawa wananikaribia na vinywa vyao, na wananiheshimu na midomo yao; lakini moyo wao ni mbali nami****. 9* ***Lakini wananiabudu bule, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya watu.***

Uliona namna Yesu alivyofunua udanganyifu wa Wafarisayo na walimu wa sheria mbele ya watu wote? Viongozi kwa maneno ya dini walijaribu kuonekana kama wenye haki mbele ya watu, lakini Bwana Yesu alijua yaliyokuwa mioyoni mwao. Labda **mikono, miguu na nyuso** zao zilikuwa safi, lakini **mioyo** yao **ilichafuwa** na zambi! **Moyo safi ni neno kubwa kupita kuwa na mikono safi**. Kunawa kwa kawaida ya dini hakuwezi kusafisha moyo wako. Ukiwa na chungu kilicho kichafu kwa upande wa ndani, kitasafishwa kama ukisukula upande wake wa inje tu? Sivyo, hata kidogo! Vivyo hivyo, desturi za dini ambazo Wayuda walishikamana nazo hazikuweza kuondosha zambi iliyokuwa ndani ya mioyo yao. Kwa sababu hii Yesu alisema nao:

Everyday Publications Inc @ 2010

> (Matayo 15) *7* ***Ninyi wadanganyifu,*** *Isaya alitabiri vema juu yenu akisema: 8 Watu hawa wananikaribia na* ***vinywa*** *vyao, na wananiheshimu na midomo yao****; l****akini* ***moyo*** *wao ni mbali nami****.*** *9 Lakini wananiabudu bule, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya watu."*
>
> *10 [Yesu] akaita makutano kwake, akawaambia: Sikieni na kufahamu: 11 Si kitu kinachoingia kinywani kinachofanyiza mtu mchafu; lakini kitu kinachotoka kinywani, ni hiki kinachofanyiza mtu mchafu. 12 Halafu wanafunzi wakakuja, wakamwambia: Unajua ya kama Wafarisayo walichukizwa wakati waliposikia neno hili? 13 Lakini akajibu, akasema: Kila mbegu Baba yangu ya mbinguni asiyopanda, itaondoshwa. 14 Muwaache; wao ni viongozi vipofu. Na* ***vipofu wakiongoza vipofu, wote wataanguka ndani ya shimo****.*

*15 Petro akajibu, akamwambia: Utuelezee mfano huu. 16 Akasema: Ninyi vilevile hamuyafahamu bado? 17 Hamutambui ya kama kitu kinachoingia kinywani kinapita hata tumbo na kinatupwa kwa choo? 18 Lakini vitu vinayotoka kinywani mwa mtu vinatoka moyoni; navyo vinafanyiza mtu mchafu. 19 Kwani kwa moyo yanatoka mawazo mabaya, uuaji, uasherati, uzini, wizi, ushuhuda wa uwongo, matukano; 20* ***ni vitu hivi vinavyofanya mtu mchafu;*** *lakini kula pasipo kunawa mikono hakufanyizi mtu mchafu.*

*29 Yesu akaondoka kule, akafika kando ya bahari ya Galilaya; akapanda mlimani, akaketi pale. 30 Makutano makubwa wakamfikia wakiwa na viwete, vipofu, mabubu, vilema na wengine wengi pamoja nao, wakawaweka kwa miguu yake; akawaponyesha; 31 hata makutano wakashangaa wakati walipoona mabubu wanasema, vilema wanakuwa wazima, viwete wanatembea, na vipofu wanaona; wakatukuza Mungu wa Israeli.*

(Matayo 16) *1 Wafarisayo na Wasadukayuo wakakuja na kumjaribu wakimwomba awaonyeshe alama toka mbingu. 2 Lakini alijibu, akawaambia: Wakati wa mangaribi munasema, Itakuwa nzuri, kwa maana mbingu ni nyekundu. 3 Na asubui, Itakuwa mbaya leo, kwani mbingu ni nyekundu na zimetandwa. Ee ninyi wadanganyifu, munajua kutambua uso wa mbingu; lakini hamuwezi kutambua alama za nyakati. 4 Kizazi kibaya cha uzini kinatafuta alama; lakini hakitapewa alama ila alama ya Yona.*

Everyday Publications Inc @ 2010

(Matayo 12) *40 Kwani kama Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la samaki mkubwa, vivyo hivyo Mwana wa watu atakuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa inchi. 41 Watu wa Ninawe watasimama siku ya hukumu pamoja na kizazi hiki nao watakihukumu; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na tazama,* ***yeye aliye mkubwa kupita Yona ni hapa!***

Hivi Yesu alitabiri ya kwamba kama nabii Yona alivyokuwa tumboni mwa samaki mkubwa kwa siku tatu, vivyo hivyo Yesu atashinda siku tatu kaburini. Na kama Yona alivyotoka samaki siku ya tatu, vivyo hivyo Yesu atafufuka toka wafu siku ya tatu. Neno hili litahakikisha kabisa (na hakuna mtu atakayeweza kukana) ya kwamba yeye ni Masiya toka mbinguni, Yule aliyekuja kutuokoa toka uwezo wa zambi na mauti na jehanum!

Ndani ya saa nusu inayobaki tuendelee ndani ya Habari Njema na kuona namna mafundi ya dini walivyodumu ndani ya

kutoamini kwao. Ndani ya Habari Njema ya Yoane, sura 7 Maandiko yanasema:

> (Yoane 7) *1 Na nyuma ya maneno haya, Yesu akatembea katika Galilaya; hakutaka kutembea katika Yudea, kwa sababu Wayuda walikuwa wakitafuta kumwua. 2 Na karamu ya Wayuda, siku kubwa ya vibanda, ilikuwa karibu. 3 Basi ndugu zake wakamwambia: Ondoka hapa, kwenda katika Yudea, vile wanafunzi wako wapate kuona kazi unazofanya. 4 Kwa sababu hakuna mtu anayefanya neno kwa siri, na yeye mwenyewe anataka kujulikana. Kama ukifanya maneno haya, ujionyeshe mwenyewe kwa dunia. 5 Kwa sababu **hata ndugu zake hawakumwamini.***
>
> *6 Basi Yesu akawaambia: Wakati wangu haujafika bado; lakini wakati wenu siku zote ni tayari. 7 Dunia haiwezi kuwachukia ninyi, lakini inanichukia mimi, kwa sababu mimi ninashuhudia ya kama kazi zao ni mbovu. 8 Pandeni ninyi kwa karamu, sijapanda bado kwa karamu hii, kwani wakati wangu haujatimia bado. 9 Alipokwisha kuwaambia maneno haya, alikaa katika Galilaya. 10 Lakini wakati ndugu zake walipokwisha kupanda, basi yeye akapanda kwenda kwa karamu vile, si kwa wazi, lakini kama kwa siri. 11 Basi Wayuda wakamtafuta katika karamu, wakasema: Yeye ni wapi? 12 Kulikuwa manunguniko mengi katikati ya makutano juu yake, wengine wakisema: Yeye mtu mwema, wengine wakasema: Hapana, lakini anadanganya makutano. 13 Lakini hapana mtu ambaye alimtaja kwa wazi, kwa sababu waliogopa Wayuda.*
>
> *14 Hata ilikuwa katika karamu, Yesu akapanda, akaingia katika hekalu, akafundisha. 15 Wayuda wakashangaa, wakasema: Mtu huyu amepata kujua kusoma namna gani, naye hakufundishwa? 16 Yesu akawajibu, akasema: Mafundisho yangu si yangu, ila yake ambaye alinituma. 17 Kila mtu akipenda kufanya mapenzi yake, atajua habari za yale mafundisho, kama yanatoka kwa Mungu au kama mimi ninasema kwa amri yangu. . . 19 Musa hakuwapa ninyi torati? lakini hapana mmoja wenu anayechunga torati. Kwa sababu gani munatafuta kuniua?*
>
> *20 Makutano wakajibu, wakasema: Wewe mwenye pepo! 21 Yesu akajibu, akawaambia: Nilifanya kazi moja, na ninyi wote munashangaa. 22 Kwa sababu hii Musa aliwapa ninyi tohara (si kwamba ya kutoka kwa Musa, lakini kwa baba zenu); na ninyi siku ya sabato munatahiri mtu. 23 Kama mtu anatahiriwa siku ya sabato, torati ya Musa isivunjike, munanikasirikia mimi kwa sababu nilifanyiza mtu*

Everyday Publications Inc
@ 2010

*kuwa mzima kabisa siku ya sabato? 24* ***Musihukumu hukumu ya macho, lakini muhukumu hukumu ya haki****. . . 30 Basi wakatafuta kumkamata, lakini hapana mtu aliyemtia mikono kwake, kwa sababu saa yake haijafika bado. 31 Lakini* ***katikati ya makutano, wengi walimwamini****,* ***wakasema: Wakati Kristo atakapokuja, atafanya alama zaidi kupita alizofanya mtu huyu?*** *32 Wafarisayo wakasikia makutano wakinungunika maneno yale juu yake, na Wafarisayo na wakubwa wa makuhani walituma watumishi wamkamate.*

*37 Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya karamu, Yesu akasimama, akapaza sauti yake, akisema:* ***Mtu akiona kiu aje kwangu, anywe. 38 Yeye anayeamini mimi, kama maandiko yalivyosema, mito ya maji ya uzima itatoka tumbo lake.*** *. . 40 Basi watu wengine katika makutano wakati waliposikia neno hili walisema: Kweli huyu ni nabii. 41 Wengine walisema: Huyu ni Kristo. Lakini wengine walisema: Nini, Kristo anatoka Galilaya? 42 Maandiko hayakusema ya kama Kristo anatoka katika uzao wa Daudi, na kutoka Betelehemu, pahali Daudi alipokaa? 43 Basi yakaingia magawanyiko katikati ya makutano kwa sababu yake. 44 Na wengine wao wakataka kumkamata, lakini hapana mtu ambaye alimtia mkono.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

*45 Basi watumishi wakakwendea wakubwa wa makuhani na Wafarisayo, ambao waliwaambia: Kwa nini hamukumleta? 46 Watumishi wakajibu:* ***Mtu hajasema bado kama mtu huyu anavyosema.*** *47 Basi Wafarisayo wakawajibu: Nanyi vile mulidanganyika? 48 Nani katika wakubwa au Wafarisayo ambaye alimwamini? 49 Lakini makutano hawa wasiofahamu torati wamelaaniwa. 50* ***Nikodemo*** *akawaambia (yule aliyekuja kwake kwanza usiku akiwa mmoja wao): 51 Torati yetu inahukumu mtu mbele ya kumsikia kwanza na kujua maneno ambayo anafanya? 52 Wakajibu, wakamwambia: Wewe umetoka vile Galilaya? Tafuta, ukaone ya kama kutoka Galilaya hakutokea nabii. 53 Wakakwenda kila mtu kwa nyumba yake.*

Tutaacha hapa leo. Tumeona namna makuhani, waandishi (walimu wa sheria) na Wafarisayo walivyochokoza Yesu. Walitaka kumfunga na kumwua, lakini hawakuweza kumtendea neno, kwa sababu siku ambayo Mungu alikusudi kwa Yesu kufa kama sadaka kwa zambi ilikuwa haijafika bado.

Ni huzuni kuona ya kwamba zaidi ya viongozi wa Wayuda walikuwa na **mioyo migumu**. Walizarau Yesu na walionya watu ya

kwamba wataondosha katika sunagogi mtu ye yote ambaye alikiri kwamba Yesu alikuwa Masiya. Hivi kulikuwa na magawanyiko katikati ya makutano kwa sababu ya Yesu. Hakuna mtu aliyesema wazi neno juu yake kwa sababu waliogopa viongozi vya dini na makuhani. Kwa siri, katikati yao wenyewe walisema, " Huyu ni mtu mwema." Wengine walijibu, "Sivyo, anadanganya watu!" Wengine waliuliza, "Wakati Masiya atakapofika atafanya maajabu makubwa kupita mtu huyu?"

Rafiki, **wewe** unasema nini juu ya Yesu? Unafikili nini juu yake? Unaamini ya kwamba Yesu ni Masiya juu yake manabii wote waliandika? Au unafikili Yesu alikuwa mmoja wa manabii tu? Usiache mtu ye yote kukuongoza vibaya ndani ya neno hili. Kwa namna gani utajibu ulizo hili unachagua kao lako kwa wakati wa kuja! **Unajua kama Yesu ni nani?** Unajua kwa sababu gani alifika duniani? Sikiliza maneno Yesu aliyosema juu yake mwenyewe:

> *"Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima: mtu hakuji kwa Baba, i**la kwa mimi.** . . Kwa ajili ya maneno haya nilizaliwa, na kwa ajili ya maneno haya nilikuja katika dunia, ili nishuhudie kweli. **Kila mtu wa kweli anasikia sauti yangu.**"* (Yoane 14:6; 18:37)

Everyday Publications Inc @ 2010

Rafiki, wewe ni kwa upande wa nani? Wewe ni tayari kufungana na Kweli—hata kama ukikataliwa na jamaa yako mwenyewe? Watu wa kabila moja wanasema: "Sharti mtu anayetaka asali awe na uhodari kushindana na nyuki." Bwana Yesu alisema,

> *"Musifikili ya kama nimekuja kuleta salama duniani; . . . Nimekuja kufitini mtu na baba yake, na binti na mama yake, na mkwe na mkwe wake; adui za mtu watakuwa wale wa nyumba yake mwenyewe. **Yeye anayependa baba au mama kupita mimi hanistahili!**"* (Matayo 10:34-37)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ushiriki tena nasi mara ya nyuma wakati tutakapoendelea ndani ya Habari Njema kuona namna Yesu alivyoponyesha mtu aliyezaliwa kipofu. Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya maneno haya ya Yesu Masiya:

***"Kila mtu wa kweli anasikia sauti yangu."*** (Yoane 18:37)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Somo 74

# Nuru ya Ulimwengu

Yoane 8,9

Salama iwe kwako leo, rafiki. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea pamoja na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo la mbele tuliona namna makuhani, walimu wa sheria na Wafarisayo **walivyosumbusha Yesu** na kujaribu kumfunga ili waweze kumwua. Lakini hakuna mtu aliyeweza kukamata Yesu, kwa sababu saa Mungu aliyoweka mbele kwa yeye kufa kama sadaka ilikuwa haijafika bado. Leo tutaendelea ndani ya kitabu cha Habari Njema na kusikia namna Yesu alivyohamakia wale walioshindana naye, na namna gani aliponyesha mtu aliyekuwa kipofu tangu kuzaliwa kwake. Somo letu la leo linaitwa **"Nuru ya Ulimwengu."**

Everyday Publications Inc
@ 2010

Ndani ya Habari Njema ya Yoane, sura 8, tunasoma:

> (Yoane 8) *2 Asubui mapema [Yesu] akaingia tena hekaluni, watu wote wakamkaribia; akakaa kuwafundisha ... 12 Yesu akasema nao tena, akisema:* ***Mimi ni nuru ya dunia; yeye ambaye ananifuata hatakwenda kwa giza kabisa, lakini atakuwa na nuru ya uzima.*** *13 Basi Wafarisayo wakamwambia: Wewe unajishuhudia mwenyewe tu, ushuhuda wako si kweli. 14 Yesu akajibu, akawaambia: Hata nikijishuhudia mwenyewe, ushuhuda wangu ni kweli; kwa sababu ninajua pahali ninapotoka na pahali ninapokwenda, lakini ninyi hamujui pahali ninapotoka wala pahali ninapokwenda. . . 23 Munatoka chini, ninatoka juu; ninyi ni wa dunia hii, mimi si wa dunia hii. 24 Basi niliwaambia ninyi: Mutakufa katika zambi zenu;* ***kwa sababu hamwamini ya kama mimi ndiye, mutakufa katika zambi zenu.*** *25 Halafu wakamwambia: Wewe nani? Yesu akawaambia: Sawasawa nilivyowaambia ninyi tangu mwanzo. . . 28 Wakati mutakaponyanyua Mwana wa watu, mutafahamu ya kuwa mimi ndiye, na sifanyi neno kwa mimi mwenyewe; lakini sawasawa Baba yangu alivyonifundisha, ninavyosema. . . 32 nanyi mutajua kweli, na* ***kweli itawaweka ninyi huru.***

33 Walijibu: Tu uzao wa Abrahamu, wala hatukuwa katika
utumwa wa mtu wakati wo wote; namna gani unasema: Mutawekwa
huru? 34 Yesu akawajibu: Kweli, kweli ninawaambia ninyi, **Kila
mtu anayefanya zambi ni mtumwa wa zambi.** 35 Na mtumwa
hakai ndani ya nyumba siku zote; lakini Mwana anakaa siku zote. 36
Kama Mwana basi anawaweka ninyi huru, mutakuwa huru kweli. 37
Ninajua ya kama ninyi ni uzao wa Abrahamu, lakini munatafuta
kuniua kwa sababu neno langu halina nafasi ndani yenu. 38
Ninasema maneno niliyoona kwa Baba yangu, nanyi munafanya
maneno muliyosikia kwa baba yenu. 39 Wakajibu, wakamwambia:
Abrahamu ni baba yetu. Yesu akawaambia: Kama mungekuwa wato-
to wa Abrahamu, mungefanya kazi za Abrahamu. 40 Lakini sasa
munatafuta kuniua, mtu ambaye aliwaambia ninyi kweli, niliyosikia
kwa Mungu. Abrahamu hakufanya hivi; 41 ninyi munafanya kazi za
baba yenu.

Wakamwambia: Sisi hatukuzaliwa katika uzini, tuna Baba mmoja,
ndiye Mungu. 42 Yesu akawaambia: **Kama Mungu angekuwa
Baba yenu, mungenipenda;** kwa sababu nilitoka kwa Mungu, nami
nimekuja; wala sikuja kwa roho yangu, lakini yeye ambaye alinituma.
43 Maneno gani hamuwezi kufahamu usemi wangu? Ni kwa sababu
hamuwezi kusikia neno langu. 44 Ninyi wa baba yenu Shetani na
tamaa za baba yenu munataka kufanya. Yeye alikuwa mwuaji tangu
mwanzo, na hakukaa katika kweli; kwa sababu hakuna kweli ndani
yake. Wakati anaposema uwongo, anasema yaliyo yake mwenyewe,
kwa sababu yeye ni mwongo, na baba ya wongo. 45 Nami, kwa
sababu ninasema kweli, hamuniamini. 46 Nani katikati yenu ambaye
ananishitaki juu ya zambi? Kama nikisema kweli, maneno gani
hamuniamini? 47 Yeye aliye wa Mungu, anasikia maneno ya
Mungu; basi ninyi hamusikii, kwa sababu ninyi si wa Mungu.

Everyday Publications Inc
@ 2010

48 Basi Wayuda walimjibu, wakamwambia: Hatusemi vizuri ya
kama wewe mtu wa Samaria, na una pepo? 49 Yesu akajibu: Sina
pepo, lakini ninaheshimu Baba yangu: nanyi hamuniheshimu. 50
Nami sitafuti utukufu wangu mwenyewe; yuko mmoja anayetafuta
na kuhukumu. 51 Kweli, kweli, ninawaambia ninyi, Kama mtu
akishika neno langu, hataona kufa hata milele. 52 Halafu Wayuda
wakamwambia: Sasa tunajua ya kuwa wewe mwenye pepo.
Abrahamu amekufa, na manabii; nawe unasema: Kama mtu akishika
neno langu hataona kufa hata milele. 53 Wewe mkubwa kupita baba
yetu Abrahamu, naye amekufa? Na manabii wamekufa; unajifanya
wewe mwenyewe nani? 54 Yesu akajibu: Kama nikijitukuza

*mwenyewe, utukufu wangu si kitu, ndiye Baba yangu ambaye ananitukuza; nanyi munasema ya kama yeye ndiye Mungu wenu. 55 Nanyi hamukumjua, lakini mimi ninamjua; kama nikisema: Simjui, nitakuwa mwenye wongo kama ninyi, lakini ninamjua na ninashika neno lake. 56 Baba yenu Abrahamu alifurahi kuona siku yangu; akaiona, akafurahi. 57 Halafu Wayuda wakamwambia: Wewe hujafika bado miaka makumi tano, nawe umeona Abrahamu? 58 Yesu akawaambia: Kweli, kweli ninawaambia ninyi,* ***Mbele Abrahamu hajazaliwa, mimi niko.*** *59 Basi* ***wakatwaa mawe, wamtupie****, lakini Yesu akajificha, akatoka hekalu, akipita katikati yao, akakwenda zake.*

(Yoane 9) *1 Na angali Yesu alipokuwa akipita akaona* ***mtu, kipofu tangu kuzaliwa****. 2 Wanafunzi wake wakamwuliza wakisema: Rabi, nani alifanya zambi, mtu huyu au wazazi wake, hata akazaliwa kipofu? 3 Yesu akajibu: Huyu hakufanya zambi, wala wazazi wake; lakini hata kazi za Mungu zionekane kwake. 4 Imetupasa kufanya kazi zake ambaye alinituma ungali mchana; usiku unakuja asipoweza mtu kufanya kazi. 5 Nikingali katika dunia, mimi ni nuru ya dunia.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

*6 Wakati alipokwisha kusema maneno haya, akatema mate kwa udongo, akafanya matope kwa yale mate, akapakaa macho ya kipofu kwa matope. 7 Akamwambia: Kwenda zako, unawe katika birika ya Siloamu (maana yake, Kutumwa). Basi akakwenda zake, akanawa, akarudi* ***anaona****. 8 Basi jirani zake, na wale ambao walimjua zamani kuwa kipofu, wakasema: Huyu siye aliyekaa na kuomba zawadi? 9 Wengine wakasema: Ndiye; wengine wakasema: Anafanana naye; lakini yeye mwenyewe alisema: Mimi ndiye. 10 Basi wakamwambia: Macho yako yalifunguliwa namna gani? 11 Yeye akajibu, akasema: Mtu anayeitwa Yesu alifanya matope na alipakaa macho yangu, akaniambia: Kwenda zako hata birika la Siloamu, unawe; basi nikakwenda, nikanawa, nikapata kuona. 12 Wakamwambia: Yuko wapi? Akasema: Sijui.*

*13 Wakapeleka yule aliyekuwa zamani kipofu kwa Wafarisayo. 14 Siku Yesu alipofanya matope na kufungua macho yake ilikuwa siku ya sabato. 15 Basi tena Wafarisayo walimwuliza vilevile namna gani alivyopata kuona. Akawaambia: Aliweka matope juu ya macho yangu, nikanawa, na sasa ninaona. 16 Basi wengine wa Wafarisayo wakasema: Mtu huyu hakutoka kwa Mungu kwa sababu hashiki siku ya sabato. Wengine wakasema: Mtu mwenye zambi anaweza kufanya alama kama hizi? Na matengano yalikuwa katikati yao. 17 Basi waka-*

*mwambia kipofu tena: Wewe unasema nini katika habari zake, kwa sababu amefungua macho yako? Akasema: Yeye nabii.*

*18 Basi Wayuda hawakusadiki habari zake ya kama alikuwa kipofu na alipata kuona, hata waliita wazazi wake yule aliyepata kuona.*
*19 Wakawauliza, wakasema: Huyu ndiye mwana wenu munayesema alizaliwa kipofu? Basi sasa akaona namna gani? 20 Wazazi wake wakawajibu, wakasema: Tunajua ya kuwa huyu ni mwana wetu, na alizaliwa kipofu; 21 lakini namna anavyoona sasa, hatujui, na yeye nani aliyefungua macho yake hatujui; yeye ni mtu mzima, mumwulize, atajisemea mwenyewe. 22 Wazazi wake walisema maneno haya kwa sababu* ***waliogopa Wayuda****, kwa sababu Wayuda wamekwisha kupatana ya kama mtu akikiri Yesu kuwa Kristo, watamtokeza katika sunagogi. 23 Hivi basi wazazi wake walisema: Yeye ni mtu mzima, mumwulize.*

*24 Basi mara ya pili waliita yule mtu aliyekuwa kipofu, wakamwambia: Umpe Mungu utukufu. Sisi tunajua ya kwamba mtu huyu ni mwenye zambi. 25 Basi, akajibu, akasema: Kama yeye ni mwenye zambi, sijui;* ***ninajua neno moja, mimi nilikuwa kipofu, na sasa ninaona.*** *26 Wakamwambia tena: Alikufanyia nini? Alikufungua macho namna gani? 27 Akawajibu: Nimekwisha kuwaambia ninyi sasahivi na hamukusikia; sababu gani munataka kusikia tena? Munataka kuwa wanafunzi wake vile? 28 Basi wakamtukana, wakasema: Wewe mwanafunzi wake; lakini sisi wanafunzi wa Musa.*
*29 Tunajua Mungu alisema na Musa, lakini maneno ya mtu huyu hatujui pahali anapotoka.*

Everyday Publications Inc. @ 2010

*30 Mtu yule akajibu, akawaambia:* ***Hili ni neno la kushangaa; hamujui pahali anapotoka, naye alifungua macho yangu.*** *31*
*Tunajua Mungu hasikii wenye zambi; lakini kama mtu akiabudu Mungu, na kufanya mapenzi yake, huyu anamsikia. 32 Tangu mwanzo wa dunia, halikusikiwa ya kama mtu alifungua macho ya mtu aliyezaliwa kipofu. 33 Kama mtu huyu hakutoka kwa Mungu, hawezi kufanya neno moja. 34 Wakamjibu, wakasema: Wewe ulizaliwa katika zambi, nawe unatufundisha? Wakamtokeza inje.*

*35 Yesu alisikia ya kama walimtokeza inje; akamvumbua, akamwambia: Unaamini Mwana wa Mungu? 36 Akajibu, akasema: Yeye nani, Bwana, niweze kumwamini? 37 Yesu akamwambia: Umemwona, ndiye yeye anayesema nawe. 38* ***Akasema: Bwana, ninaamini. Akamwabudu.*** *39 Yesu akasema: Mimi nimekuja katika dunia hii kwa kuhukumu, ili wasioona, waone, na wanaoona wawe vipofu. 40 Na wengine wa Wafarisayo waliokuwa pamoja naye,*

*wakasikia maneno haya, wakamwambia: Sisi ni vipofu vilevile?* 41
*Yesu akawaambia: Kama mungekuwa vipofu, musingekuwa na zambi; lakini sasa munasema: Tunaona; basi zambi yenu inakaa.*

Hivi Bwana Yesu aliponyesha mtu aliyezaliwa kipofu na alihamakia Wafarisayo kwa sababu ya nia zao pofu. Wafundi hawa wa dini walikuwa na upofu uliokuwa mbaya kupita upofu wa mwili. Waliweza kuona, lakini **hawakutaka kuona**, na kwa sababu hii walikamata mawe waweze kutupia Yesu. **Hawakutaka kuamini** ya kwamba yeye ni Masiya na Nuru ya ulimwengu. Hawakutaka kuamini ya kwamba Yesu alikuwa mbele ya kuzaliwa kwa Abrahamu; ya kama alikuwa Neno aliyekuwa pamoja na Mungu katika mwanzo. **Hawakutaka kuona kweli.**

Ndani ya habari za leo tuliona **wapofu namna mbili**: Wale walio wapofu kwa maneno ya **macho**; na wale walio wapofu kwa maneno ya **nia**. Giza la nia pofu ni baya kupita giza la macho yasiyoweza kuona. Macho yako yakiwa mapofu, huwezi kuona vitu vya dunia hii, lakini moyo na nia zako zikiwa pofu, huwezi kuona wala kufahamu maneno ya milele!

Everyday Publications Inc @ 2010

Neno la Mungu linatufundisha ya kwamba wana wote wa Adamu ni **wapofu tangu kuzaliwa kwao**—wapofu katika nia zao na mioyo yao. Kwa sababu ya zambi ya Adamu, sisi sote tumezaliwa katika giza la zambi na ujinga. Hatujui Mungu na hatuna hamu kwa kweli yake. Kama mende zinazokimbia huko na kule wakati tunapowasha taa, sisi tunaepuka nuru ya Neno la Mungu na tunafurahi kukaa katika giza maisha yetu mazima. Ni huzuni kwa sababu zaidi ya wazao wa Adamu wanakufa katika giza la zambi na ujinga. Nabii Hosea aliandika: *"Sikieni neno la Bwana . . . Watu wangu **wameharibika kwa kukosa kujua;** kwa kuwa umekataa kujua, nitakukataa wewe vilevile . . .!"* (Hosea 4:1,6)

**Habari njema** ndizo ya kwamba Mungu hataki hata mmoja wetu kupotea katika giza la zambi na ujinga. Kwa sababu hii alifika dunian kwa njia ya kutuma kwetu Bwana Yesu Kristo. Nabii Zakaria alisema juu ya Bwana Yesu kama ***"Mwanga"*** ambaye Mungu atatuma toka juu *"**kuwaangazia** wanaokaa katika giza, na katika kivuli cha mauti, na **kuongoza** miguu yetu katika njia ya salama."* (Luka 1:79) Manabii walikuwa kama nyota zinazoleta nuru usiku, lakini Yesu Kristo ni kama mwanga, anayeleta nuru na uzima kwa wote ambao wanamwamini. Mungu aliumba jua ngapi kuangaza dunia yetu? Moja tu. Mungu alituma Waokozi wengapi toka mbingu kuokoa

wenye zambi toka giza la zambi na jehanum ya milele? Mmoja tu. Lakini zaidi ya wana wa Adamu hawafahamu neno hili, hivi wanajikwaa katika giza la zambi. Kwa sababu hii Maandiko yanatangaza juu ya Bwana Yesu Kristo, yakisema: *"Nuru ilingaa katika giza na **giza halikuishinda** . . . Alikuwa ulimwenguni na ulimwengu ulifanywa naye na **ulimwengu haukumtambua**."* (Yoane 1:5,10)

Rafiki msikiaji, Bwana Yesu amefungua "macho" ya nia na moyo wako? Au unakaa kukwaa katika giza la zambi na ujinga?

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Asante kwa kushiriki nasi ndani ya masomo haya. Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutaendelea ndani ya Habari Njema na kuona namna utukufu wa Mungu ulingaa toka Yesu kama jua.

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya tangazo hili la Bwana Yesu:

> ***"Mimi ni nuru ya dunia; yeye ambaye ananifuata hatakwenda kwa giza, lakini atakuwa na nuru ya uzima."*** (Yoane 8:12).

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 75

# Bwana wa Utukufu

## Matayo 16,17

Ni furaha kukusalimu tena, rafiki, kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tuendelee sasa na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo la mbele, ndani ya mafundisho ya kitabu cha Habari Njema, tulisikia namna Yesu Masiya alivyofungua macho ya mtu aliyezaliwa kipofu. Hakuna neno lisilowezekana kwa Yesu kwa sababu Yeye ni Neno la Mungu aliyeonekana duniani kama mtu. Kwa sababu hii Yesu aliweza kutawala maneno yote duniani, maneno kama upepo, bahari, pepo wachafu, gonjwa na mauti. Kila pahali Yesu alipokwenda makutano walimsonga, lakini **wachache tu walitambua kama alikuwa nani**. Walifikili yeye ni nabii, lakini hawakufahamu ya kwamba utimilifu wote wa Mungu ulikaa ndani yake. Hawakufahamu ya kama Yesu ni Bwana wa Utukufu, aliyetoka mbinguni. Ndani ya somo letu la leo, Mungu akitaka, tutaona namna gani **Bwana Yesu alijaa nuru ya utukufu wa Mungu** na namna gani alionyesha utukufu ule kwa muda mfupi sana siku moja wakati alipokuwa juu ya mlima pamoja na watatu wa wanafunzi wake.

Everyday Publications Inc @ 2010

Lakini sasa turudi kwa Habari Njema. Maandiko yanasema:

> (Luka 9) *18 Ilikuwa angali alipoomba peke yake, wanafunzi wake walikuwa pamoja naye; akawauliza, akisema: Watu wanasema ya kama mimi ni nani? 19 Wakajibu wakasema; Yoane Mbatizaji; lakini wengine Elia, na wengine ya kwamba mmoja wa manabii wa zamani amefufuka tena.* (Matayo 16) *15 Lakini* ***ninyi munasema mimi ni nani?*** *16 Simoni Petro akajibu na kusema: Wewe ni Kristo* (Masiya), *Mwana wa Mungu aliye hai. 17 Yesu akajibu, akamwambia: Heri wewe Simoni wa Yona; kwa kuwa mwili na damu hazikukufunulia neno hili, lakini Baba yangu aliye mbinguni.*

Tuache kwanza hapa na kufikili juu ya neno Yesu alilouliza wanafunzi wake siku moja wakati walipokuwa peke yao. Yesu aliwauliza, "**Watu** wanasema mimi ni nani?" Wanafunzi walijibu Yesu ya kwamba zaidi ya watu walisema yeye ni mmoja wa manabii. Halafu Yesu aliwauliza tena akisema, "Lakini **ninyi** munasema mimi ni nani?" Mmoja wa wanafunzi, Simoni Petro, alijibu Yesu, ***"Wewe ni Masiya, Mwana wa Mungu aliye hai."***

Kweli, ulizo la Yesu kwa wanafunzi wake ni ulizo kubwa, ulizo ambalo inatupasa sisi sote kujibu. Wewe unayesikiliza leo, unafikili Yesu ni nani? Unafikili nini juu yake? Unafikili yeye ni mmoja wa manabii? Au unakubali masemo ya Petro ya kwamba yeye ni "Masiya, Mwana wa Mungu aliye hai"? **Unafikili Yesu ni nani?** Unaamini ya kwamba Yesu ni Masiya—Mkombozi ambaye Mungu aliahidi zamani siku ile wakati wazazi wetu, Adamu na Hawa, walipofanya zambi? Unaamini ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu aliye hai"—Neno la Mungu aliyeshuka toka mbinguni?

Kama unavyojua, kufika leo, kuna **watu wengi wanaokana ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu,** kwa sababu wanafikili maana ya jina hili ni ya kwamba Mungu alikamata mke na alizaa mtoto na mke huyu! Lakini hii si maana yake hata kidogo! Utukufu wa Mungu ni mkubwa kupita ile! Mungu ni Roho na hazai watoto namna watu wanavyozaa. **Lakini neno hili halizuizi Mungu asiite Yesu Mwana wake!** Tulijaribu kueleza mbele neno hili na mfano huu: Nikitoka inchi yangu, ndiyo Congo, na watu wananiita "mwana wa Congo", si kusema ya kwamba Congo ilikamata mke na kuzaa mwana! Sivyo, ninaitwa "mwana wa Congo" kwa sababu mimi ni mtu wa Congo.

Everyday Publications Inc @ 2010

Ilikuwa vivyo hivyo na Yesu, Masiya, aliyezaliwa na bikira. Hata mbele ya kuzaliwa kwake, alikuwa mbinguni. Yeye ni *"Kalimat Allah"* na *"Ruh Allah"*—Neno na Nafsi ya Mungu. {Ona somo 61 kwa elezo la maana ya maneno haya kwa Kiarabe.} Yesu tu alistahili kuitwa Mwana wake Aliye Juu, kwa sababu Yeye peke yake alikuwa pamoja na Mungu katika mwanzo. Hii ni **siri kubwa**, lakini zaidi ya ile, ni **kweli kubwa!** Mungu hakutuma Mwana wake ulimwenguni kwa kutuokoa toka zambi zetu tu, lakini kutuonyeshea vilevile ya kwamba Yeye ni namna gani. Yesu alionyesha namna ya Mungu duniani. Mtu ye yote anayeona Mwana anajua kama Baba ni namna gani. Mtu ye yote anayeona Yesu anajua kama Mungu ni namna gani. Yesu anaitwa Mwana wa Mungu, kwa sababu **alitoka kwa Mungu,** kwa sababu **yeye ni sawasawa na Mungu**, na kwa sababu Yeye ndiye **Neno la Mungu na Nafsi ya Mungu**. Rafiki, si neno

kama sisi tukiamini au kama tukikataa kuamini, kweli hii haiwezi kubadilika: **Yesu ni Mwana wa Mungu aliye hai!**

Tuendelee ndani ya Habari Njema ya Matayo na kusikia nini ilitokea nyuma ya tangazo la Petro ya kwamba Yesu ni Masiya, Mwana wa Mungu aliye hai. Maandiko yanasema:

> (Matayo 16) *21 Toka wakati ule* ***Yesu akaanza kuonyesha wanafunzi wake ya kwamba imempasa kwenda Yerusalema na kupata mateso mengi*** *kwa wazee na wakubwa wa makuhani na waandishi na* ***kuuawa****, na* ***kufufuliwa*** *siku ya tatu. 22 Petro akamchukua, akaanza kumkemea akisema: Iwe mbali nawe, Bwana; neno hili halitatokea juu yako kamwe. 23 Lakini akageuka, akamwambia Petro: Kwenda nyuma yangu, Shetani; kwani wewe ni jiwe la kukwaza kwangu, kwani* ***huwazi maneno yaliyo ya Mungu, lakini maneno yaliyo ya watu.***

Ulisikia maneno Yesu aliyosema kwa wanafunzi wake? Alisema nao ya kwamba itampasa kwenda Yerusalema na kupata mateso mengi kwa mikono ya wazee, wakubwa wa makuhani na waandishi, na ya kwamba ilikuwa lazima auawe na kufufuliwa tena siku ya tatu. Kwa njia hii Yesu alitangaza ya kuwa atamwanga damu yake kulipa deni ya zambi zetu.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Lakini **Petro hakuweza kukubali** ya kwamba Bwana Yesu, mwenye uwezo na amri yote, ataacha watawala waovu wa Wayuda kumfunga, kumtesa na kumwua. Kwa sababu hii Petro alisema na Yesu, "*Iwe mbali nawe, Bwana; neno hili halitatokea juu yako kamwe.*" Lakini Yesu alijua ya kwamba alikuja duniani ili kumwanga damu yake kama sadaka inayoondoa zambi. Kwa sababu hii alisema na Petro: "*Kwenda nyuma yangu, Shetani; kwani wewe ni jiwe la kukwaza kwangu, kwani huwazi maneno yaliyo ya Mungu, lakini maneno yaliyo ya watu.*"

**Yesu alijua kwa sababu gani** alikuwa amefika duniani. Alikuja kutoa damu yake takatifu kwa wenye zambi, kama manabii wa Mungu walivyotabiri zamani. Yesu alikuja kutimiza mfano wa mwana-kondoo wa sadaka. Eh, msikiaji, kama tukikumbuka neno moja tu la somo letu la leo, tukumbuke hili: **Yesu Masiya alikuja duniani kufa kama sadaka kulipa kwa zambi—zambi zangu na zako!** Mungu akitaka, nyuma ya masomo machache mengine, tutaona namna gani unabii wa Yesu juu ya kufa kwake mwenyewe ulitimizwa katika Yerusalema. Hivi rafiki, hata kama watu wengine wanatangaza habari nyingine zisizopatana na zile Bwana Yesu na

manabii walizotabiri zamani, kweli juu ya mauti ya Yesu na ufufuko wake haibadiliki. **Mungu Yeye mwenyewe aliamuru mauti ya Masiya juu ya msalaba,** na hakuna mtu anayeweza kugeuza amri za Mungu! **Yesu alichagua kufa kama Sadaka kubwa zaidi.** Alikufa kwa sababu anatupenda wewe na mimi na hataki tupotee.

Tuone nini ilitokea juma moja nyuma ya wakati Yesu alipojulisha wanafunzi wake ya kwamba atatoa uzima wake kwa Yerusalema. Maandiko yanasema:

> (Matayo 17) *1 Na nyuma ya siku sita Yesu akatwaa Petro, na Yakobo, na Yoane ndugu yake pamoja naye, na kuwaleta juu ya mlima mrefu peke yao; 2* ***akageuzwa sura*** *mbele yao;* ***sura yake ikangaa kama jua, na mavazi yake yalikuwa meupe kama nuru.***
>
> (Luka 9) *30 Na tazama, watu wawili walisemezana naye, nao ni Musa na Elia, 31 walioonekana katika utukufu, wakasema habari za kufa kwake atakapotimiza katika Yerusalema.* (Matayo 17) *3 Petro ... akamwambia Yesu: Bwana, ni vizuri kwetu kukaa hapa; ukitaka nitafanya hema tatu hapa; moja kwa wewe, moja kwa Musa, na moja kwa Elia. 5 Wakati alipokuwa akisema, tazama wingu la kungaa likawafunga kwa kivuli; na tazama, sauti toka wingu ikisema:* ***Huyu ni Mwana wangu, mpendwa wangu, ambaye ninapendezwa naye; sikieni yeye.*** *6 Na wakati wanafunzi waliposikia wakaanguka kifudifudi, wakaogopa sana. 7 Na Yesu akakuja, akawagusa na kusema: Simameni, musiogope. 8 Na wakinyanyua macho yao hawakuona mtu ila Yesu peke yake. 9 Na wakati walipokuwa wakishuka mlima, Yesu akawaamuru akisema: Musimwambie mtu habari za maono haya hata Mwana wa watu atakapofufuka toka wafu.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

Ulifahamu neno lililotokea juu ya mlima ule? Lilikuwa tokeo la ajabu, la kushangaza sana. Tulisoma ya kwamba kuonekana kwa Yesu kuligeuzwa—uso wake ulingaa kama jua na mawazi yake yalikuwa meupe kama nuru. Nuru ileile ya kuogofya na ya kushangaza inayotoka kwa Mungu na kuzunguka kiti ya kifalme cha Mungu mbinguni ilikuwa ikingaa toka Yesu! Nuru ya utukufu iliyojaza pahali patakatiu pa patakatifu ndani ya Hema ya Kusanyiko kwa wakati Musa na Waisraeli walipokuwa jangwani—utukufu ule ule ulikuwa ndani ya Yesu, hata kama watu hawakuweza kuuona. Lakini kwa dakika chache, mbele ya macho ya wanafunzi watatu, Mungu alifunua utukufu wake wa kuogofya uliofichama ndani ya mwili wa Yesu! Na kwa dakika ile Mungu alituma toka mbinguni

manabii wawili, Musa na Elia, kusemezana na Yesu juu ya mauti yake kwa Yerusalema. Tulisoma vilevile ya kwamba wingu la kungaa lilifunika mlima, na sauti toka Mwenyezi ilisikiwa toka wingu, likisema, ***"Huyu ni Mwana wangu, mpendwa wangu, ambaye ninapendezwa naye; sikieni yeye."***

Sababu kwa maneno haya yote ilikuwa nini? Kwa nini Mungu alifanya maneno haya ya utukufu mbele ya Petro, Yoane na Yakobo? Sababu yenyewe ndiyo hii: Mungu alitaka kuhakikisha kabisa mbele ya washuhuda hawa watatu ya kwamba kweli Yesu ni Mwana wa milele wa Mungu toka mbingu, na ni lazima kwa watu wote kumsikiliza. Kwa sababu hii Maandiko yanatangaza kwa Yoane 5:23:

> *Mtu yule asiyeheshimu **Mwana** haheshimu **Baba ambaye alimtuma.*** Na kwa Waebrania 1:1-3: *Mungu aliyesema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, katika siku hizi za mwisho amesema nasi katika Mwana, ambaye alimweka kuwa mriti wa vitu vyote, kwa yeye aliyefanya ulimwengu. **Yeye akiwa kungaa kwa utukufu wake, na chapa ya nafsi yake mwenyewe,** akikwisha kufanya katika yeye utakaso wa zambi zetu, aliketi mkono wa kuume wa Mwenye Ukuu.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

Wewe unayesikiliza leo, unafikili nini juu ya Yesu? Unasema nini juu yake? Unaamini ya kama Yesu ni Bwana wa Utukufu, aliyetoka mbinguni? Au unafikili pamoja na zaidi ya watu ya kwamba yeye ni mmoja wa manabii tu? Mbele ya kulagana leo, tusikilize mengine ya masemo ya mitume, Petro na Yoane walioandika sehemu ya Maandiko Matakatifu nyuma ya kuona kungaa kwa utukufu wa Mungu kwa njia ya Yesu juu ya mlima.

Mtume Petro aliandika:

> *"Hatukufuata hadizi zilizotengenezwa kwa hila, wakati tulipowajulisha ninyi uwezo na kuja kwa Bwana wetu Yesu Kristo, lakini s**isi wenyewe tuliona ukubwa wake.** Maana alipata kwa Mungu Baba heshima na utukufu, wakati sauti ilipokuja kwake toka utukufu mkubwa: "Huyu ni Mwana wangu mpendwa, ambaye ninapendezwa naye. Basi **tulisikia sauti hii** ikitoka mbinguni, wakati tulipokuwa pamoja naye katika mlima mtakatifu."* (2 Petro 1:16-18)

Mtume Yoane aliandika:

> *"Neno lililokuwa tangu mwanzo, ambalo **tulisikia**, ambalo **tuliona** kwa macho yetu, ambalo **tulitazama** na kulipapasa kwa mikono yetu,*

> *kwa habari za Neno la uzima; na uzima ulifunulia, nasi tumeona . . . tukatazama utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee akitoka kwa Baba, amejaa neema na kweli.* (1 Yoane 1:1,2; Yoane 1:14)

Na kwa mwisho wa Habari Njema yake Yoane aliandika,

> *"Alama nyingi nyingine Yesu alifanya mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki;* ***lakini hizi zimeandikwa mupate kuamini ya kwamba Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu: na kwa kuamini mupate uzima kwa jina lake."*** (Yoane 20:30,31)

Ni nguvu kwa wewe kufahamu maneno haya? Mungu anataka kukuaminisha kweli hizi za ajabu. Maandiko yanasema:

> *"Mwenye kufuata tabia ya asili* ***hapokei*** *maneno ya Roho ya Mungu: kwa sababu maneno haya ni upumbavu kwake; wala hawezi kuyafahamu kwa sababu yanatambulikana na Roho . . . Lakini tunasema akili katikati yao walio watimilifu; lakini si akili ya dunia hii, wala ya watawala wa dunia hii, wanaogeuka kuwa bule; lakini tunasema* ***akili ya Mungu katika siri****, akili inayofichwa, Mungu aliyoamuru mbele ya dunia kwa utukufu wetu. Hata mmoja wa watawala wa dunia hii hakuijua: kwa sababu kama wangalijua wasingalisulibisha Bwana wa utukufu."* (1 Wakorinto 2:14,6-8)

Everyday Publications Inc
@ 2010

Mungu akufahamishe maneno tuliyosoma leo.

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Kufika saa tutakapofika pamoja tena kwa kusoma, Bwana akubariki wakati unapowaza juu ya maneno Mungu Mwenyezi aliyotangaza toka mlimani juu ya Bwana Yesu wakati aliposema:

> ***"Huyu ni Mwana wangu, mpendwa wangu, ambaye ninapendezwa naye; sikieni yeye!"*** (Matayo 17:5)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Somo 76

# Mchungaji Mwema

Yoane 10

Tunakusalimu tena leo kwa jina la Mungu, Bwana wa salama. Ni furaha kuweza kuendelea tena pamoja na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo letu la mbele, tulisikia Bwana Yesu akiwaambia wanafunzi wake ya kwamba ni **lazima kwake kufa katika Yerusalema na kufufuliwa toka wafu siku ya tatu.** Yesu alijua ya kwamba alizaliwa duniani kumwanga damu yake kama sadaka inayoondoa zambi. Mara ya mbele tuliona vilevile Bwana Yesu akionyesha utukufu wake mkubwa wakati alipokuwa juu ya mlima pamoja na wanafunzi wake watatu. Uso wa Yesu ulingaa kama jua, na mavazi yake yalikuwa meupe kama nuru. Hivi utukufu wa Mungu ulionekana ndani ya Yesu.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Leo tunataka kuendelea ndani ya Habari Njema takatifu na kusikia namna Bwana Yesu alivyosawanisha wale ambao walimfuata na **kondoo wenye kutulia**. Tumeona tena na tena ndani ya Maandiko ya Manabii ya kwamba Mungu alisawanisha wana wa Adamu na **kondoo wapotevu bila mchungaji.** Lakini, Mungu hataki wana wa Adamu kupotea kama kondoo bila mchungaji. Kwa sababu hii alituma toka mbingu Mchungaji mwenye uwezo kutuongoza ndani ya njia ya salama na kutuokoa toka adui zetu wabaya zaidi: Shetani, zambi, mauti na jehanum. **Unajua Mchungaji Mwema**, ambaye Mungu alituma kwa wana wa Adamu? Kama sivyo, tunakuomba kusikiliza karibu karibu mafundisho ya leo.

Tunasoma ndani ya Habari Njema, sura 10. Siku moja, Yesu alisema na Wayuda:

> (Yoane 10) *1 Kweli, kweli ninawaambia ninyi, mtu asiyeingia kwa mlango wa zizi la kondoo, lakini anapanda kuingia pahali pengine, huyu ni **mwizi** na **mnyanganyi**. 2 Lakini mtu anayeingia kwa mlango ni mchungaji wa kondoo. . . 6 **Mfano huyu** Yesu aliwa-*

*ambia; lakini hawakufahamu maana ya maneno aliyosema nao. 7 Basi Yesu aliwaambia tena: Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Mimi ni mlango wa kondoo. . . 9 **Mimi ni mlango**; kama mtu ataingia kwa mimi, ataokolewa, na ataingia na kutoka, naye atapata chakula. 10 Mwizi hakuji, ila aibe, achinje, na kuharibu; mimi nimekuja wapate uzima, na waupate tele. 11 **Mimi mchungaji mwema,** mchungaji mwema anatoa uzima wake kwa ajili ya kondoo. 12 Lakini mtu wa mshahara, wala si mchungaji, nao kondoo si mali yake, anaona imbwa ya poli anakuja; na anaacha kondoo na kukimbia, na imbwa ya poli anawanyanganya na kusambaza kondoo. 13 Mtu wa mshahara anakimbia kwa sababu yeye ni mtu wa mshahara, na hasumbukii maneno ya kondoo. 14 Mimi ni mchungaji mwema; na ninajua kondoo zangu na zangu wananijua. 15 Sawasawa Baba anavyonijua, mimi vilevile ninajua Baba; nami ninatoa uzima wangu kwa ajili ya kondoo. . . 17 Hivi Baba ananipenda, kwa sababu ninatoa uzima wangu, ili niutwae tena. 18 Hakuna mtu anayeuondoa kwangu, lakini mimi mwenyewe ninautoa. Nina uwezo kuutoa, na nina uwezo kuutwaa tena. Agizo hili nilipokea kwa Baba yangu.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

*19 Yakaingia tena matengano katikati ya Wayuda kwa sababu ya maneno haya. 20 Wengi wao wakasema: Ana pepo, tena ana wazimu; kwa nini munasikia maneno yake? 21 Wengine wakasema: Maneno haya si maneno ya mwenye pepo. Mwenye pepo anaweza kufungua macho ya vipofu?*

*24 Halafu Wayuda wakamzunguka, wakamwambia: Hata wakati gani utatuhangaisha sisi? Kama wewe ni Kristo, utuambie waziwazi. 25 Yesu akawajibu: Niliwaambia ninyi, na hamwamini; kazi hizi ninazofanya kwa jina la Baba yangu, hizi zinanishuhudia. 26 Lakini hamuamini kwa sababu ninyi si wa kondoo zangu; kama nilivyowaambia ninyi. 27 Kondoo zangu wanasikia sauti yangu, nami ninawajua, nao wananifuata. 28 Nami ninawapa uzima wa milele; nao hawatapotea hata milele, wala hakuna mtu anayeweza kuwanyanganya toka mkono wangu. 29 Baba yangu ambaye alinipa hawa, ni mkubwa kupita wote, na hakuna mtu anayeweza kuwanyanganya toka mkono wangu. 30 **Mimi na Baba yangu ni mmoja**. 31 Basi Wayuda wakatwaa mawe tena, wampige. 32 Yesu akawajibu: Kazi njema nyingi nimewaonyeshea ninyi kutoka kwa Baba yangu; kwa sababu ya kazi gani katika hizi munanipigia mawe?*

*33 Wayuda wakamjibu, wakasema: Kwa kazi njema hatukupigi kwa mawe, ila kwa matukano, na kwa sababu wewe, uliye mtu, **unajifanyiza mwenyewe kuwa Mungu**. 34 Yesu akawajibu: Hai-*

> *kuandikwa katika torati yenu, ya kama: Mimi nilisema, ninyi miungu? 35 Kama aliwaita wale miungu, wao ambao lilifikia Neno la Mungu (na maandiko hayawezi kuvunjika); 36 munasema juu yake ambaye Baba alimtakasa na kumtuma katika dunia: Unatukana, kwa sababu nilisema: Mimi ni Mwana wa Mungu? 37 Kama sitendi kazi za Baba yangu, musiniamini. 38 Lakini kama nikizitenda,* ***hata ikiwa hamuniamini mimi, mwamini zile kazi; mupate kujua na kuamini ya kwamba Baba ni ndani yangu, nami ni ndani ya Baba.*** *39 Wakatafuta tena kumkamata, lakini alitoka mikono yao.*

Ulisikia maneno Yesu aliyosema na Wayuda? Kwa sababu saa haitoshi kwa kueleza wazi masemo yote ya Yesu tutasema zaidi juu ya majina mawili ya Yesu. Yesu alijiita mwenyewe na majina haya: **Mlango wa kondoo** na **Mchungaji Mwema**.

Kwanza tulisikia, ya kwamba nyuma ya kusawanisha wana wa Adamu na kondoo, Yesu alisema na makutano, *"**Mimi ni mlango wa kondoo** . . . mtu akiingia kwa mimi, ataokolewa."* Kwa sababu gani Yesu alijiita "***Mlango wa kondoo***?" Kwa wakati ule mchungaji alitengeneza kiwanja cha matawi yenye miiba au mawe, chenye mlango mmoja tu pahali kundi walipoweza kuingia. Mangaribi wakati kondoo walipokwisha kuingia, mchungaji yeye mwenyewe alilala kwa mlango wa kiwanja kulinda kondoo zake. Hivi mbele ya nyama ya mwitu kuweza kuingia kiwanja na kuua kondoo mmoja, ilimpasa kupita kwa mlango pahali mchungaji alipolala. Halafu mchungaji alifukuza nyama mkali wakati nyama asipoingia bado na kuumiza kondoo. Kwa njia hii mchungaji mwenyewe alikuwa "*mlango wa kondoo*."

Everyday Publications Inc
@ 2010

Bwana Yesu alijiita mwenyewe ***"Mlango wa kondoo."*** Ni kusema Yesu analinda wote walio watu wake. Na maana yake ni vile ya kwamba kwa wewe kuweza kugeuka sehemu ya "kundi" la Mungu, ni **sharti kwako kupita kwa Yesu**. Mtu ye yote anayetaka kuokolewa toka mitego ya Shetani, toka azabu ya zambi, toka uwezo wa mauti na azabu ya jehanum ya milele sharti apite kwa Yesu. Yeye peke yake ni mlango kwa wenye zambi kupata uzima wa milele. Kwa sababu hii Neno la Mungu linasema: *"Wala* ***hakuna wokovu katika mwingine,*** *kwa maana* ***hakuna jina lingine*** *chini ya mbingu walilopewa watu tupate kuokolewa nalo."* (Matendo 4:12) Yesu ni mlango wa peke kwa wokovu.

Unakumbuka maneno tuliyosoma mbele kidogo juu ya nabii Noa na garika? Mungu aliagiza Noa kufanya milango mingapi ndani ya chombo kitakachokuwa kimbilio kwa wote waliotaka kuepuka

hukumu ya garika? **Mlango mmoja tu**. Ilipasa mtu ye yote aliyetaka kuepuka garika kuingia kwa mlango ule mmoja. Mtu ye yote aliyeingia **alipona**. Mtu ye yote asiyeingia mlango **alipotea!** Vivyo hivyo, Maandiko Matakatifu yanaonyesha wazi ya kwamba Siku ya Hukumu Mungu amefungua mlango mmoja tu wa wokovu kwa wana wa Adamu. Masiya yeye mwenyewe ndiye Mlango kwa njia yake watu wanaweza kuingia uzima wa milele. Kwa sababu hii Yesu alisema, *"**Mimi ni mlango; kama mtu ataingia kwa mimi, ataokolewa** . . . lakini mtu asiyeingia kwa mlango wa zizi la kondoo, lakini anapanda kuingia pahali pengine, huyu ni mwizi na mnyanganyi."* (Yoane 10:9,1)

Yesu alijiita na jina lingine vilevile linalofanana na jina la kwanza. Yesu si *"Mlango kwa kondoo"* tu, yeye ni ***"Mchungaji Mwema"*** vilevile. Yesu ni Mchungaji ***Mwema*** kwa sababu ndiye ambaye alitupenda na kutoa uzima wake kwa sisi. Kweli yeye ni Mchungaji wa ajabu! Nabii Daudi aliandika juu yake ndani ya Zaburi 23,

> *"Bwana ni mchungaji wangu; sitapungukiwa na kitu. Ananilalisha katika malisho ya majani mabichi; ananiongoza kando ya maji matulivu; anarudisha nafsi yangu; ananiongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake. Ndiyo, hata nikipita kati ya bonde la kivuli cha mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana wewe ni pamoja nami; gongo lako na fimbo yako zinanifariji. Unanitengenezea meza mbele ya adui zangu; umenipakalia mafuta kichwani; kikombe changu kinafurika. Hakika wema na rehema zitanifuata siku zote za maisha yangu; na nitakaa nyumbani mwa Bwana milele."* (Zaburi 23)

Everyday Publications Inc @ 2010

Neno ambalo inatupasa kufahamu ni ya kwamba Masiya Mwenyewe ni Mchungaji Mwema ambaye Daudi aliandika habari zake. Kwa sababu hii Yesu aliweza kusema, *"Mimi ni mchungaji mwema"* na, *"Mimi na Baba [Mungu] yangu ni **mmoja**"* (Yoane 10:11,30) Lakini wakati Yesu aliposema yeye ni **mmoja na Mungu**, Wayuda walimshitaki juu ya kutukana, wakakamata mawe kumtupia. Iliwashinda kukubali ya kwamba Yesu alikuwa Mungu kwa mwili wa mtu. Kufika leo, zaidi ya wana wa Adamu wanajikwaa juu ya masemo haya ya Yesu. Wengine wanaanguka kwa njia ya kufikili ya kwamba maana ya kusema Yesu ni mmoja na Mungu ni ya kwamba kuna Miungu wawili. Lakini neno hili si kweli, kwani Maandiko ya Manabiii yanatangaza wazi umoja wa Mungu, yakisema, *"Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja!"* (Torati 6:4) **Lakini hata kama *"Mungu ni mmoja"*, neno hili halikuzuiza Mungu asijifunue duniani kama mtu.**

Labda **mfano huu** utatusaidia kufahamu. Fikili juu ya jua linalowaka duniani na kutupa sisi nuru na moto. Tuna jua ngapi namna hii? Moja tu. Jua ni wapi? Ni mbali sana katika hewa, lakini ni hapa duniani vilevile likitusaidia na nuru yake inayoleta uzima. Jua la kuwaka na mwanga wa jua ni moja. Vivyo hivyo, Mungu na Yesu ni mmoja. Yesu alisema, *"Mimi na Baba [Mungu] ni **mmoja**!"* Bwana Yesu alifika hapa duniani kushiriki nasi nuru ya mapendo na wokovu wa Mungu. Sikiliza maneno Maandiko Matakatifu yanayosema juu ya Mungu na Yesu:

> *"**Mungu** wetu ni moto wa kuteketeza . . . akikaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa! . . . Hakuna mtu aliyeona **Mungu** wakati wo wote; **Mwana pekee** aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye alimfunua. . . Yeye [Mwana] akiwa kungaa kwa utukufu wake, na chapa ya nafsi yake mwenyewe, akichukua vitu vyote kwa Neno la uwezo wake, akikwisha kufanya katika yeye utakaso wa zambi zetu, aliketi mkono wa kuume wa Mwenye Ukuu . . . Katika yeye [Yesu Kristo] ilipendeza [Mungu] utimilifu wote ukae . . . **Katika yeye [Kristo] unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa mwili!"*** (Waebrania 12:29; 1 Timoteo 6:16; Yoane 1:18; Waebrania 1:3; Wakolosayi 1:19; 2:9)

Everyday Publications Inc
@ 2010

Ndiyo, hili ndilo Neno la Mungu linatangaza: ***"Katika yeye [Kristo] unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa mwili!"*** (Wakolosayi 2:9) Hivi, Bwana Yesu aliweza kusema, *"Mimi na Baba [Mungu] ni **mmoja**!"* Kristo ni **Mchungaji Mwema** aliyetoka mbinguni, aligeuka mtu, aliishi duniani na alitoa uzima wake mtakatifu kwa kutuokoa toka laana ya zambi yetu. Yeye vilevile alifufuliwa toka wafu na anataka kuwapa wote ambao wanamwamini uzima wa milele. Kwa sababu hii Yesu aliweza kusema:

> *"Mimi ni mchungaji mwema . . . ninatoa uzima wangu kwa ajili ya kondoo . . . ili niutwae tena. Hakuna mtu anayeuondoa kwangu, lakini mimi mwenyewe ninautoa. Nina uwezo kuutoa, na nina uwezo kuutwaa tena. Agizo hili nilipokea kwa Baba yangu."* (Yoane 10:14-18)

Tunajua bila shaka hata kidogo ya kwamba Yesu ni *"Mchungaji Mwema,"* kwa sababu **ndiye ambaye alitupenda ya kutosha hata alitoa uzima wake kwa ajili yetu!**

Mbele ya kulagana leo, tusikilize mara moja tena maneno matamu ya Bwana Yesu katika Yoane 10:

> *9 **Mimi ni mlango**; kama mtu ataingia kwa mimi, ataokolewa . . . 10*

> *Mwizi hakuji, ila aibe, achinje, na kuharibu; . . . 11* ***Mimi mchungaji mwema****, mchungaji mwema anatoa uzima wake kwa ajili ya kondoo. 12 Lakini mtu wa mshahara, wala si mchungaji, nao kondoo si mali yake, anaona imbwa ya poli anakuja; na anaacha kondoo na kukimbia . . . 14 Mimi ni mchungaji mwema . . . 27* ***Kondoo zangu wanasikia sauti yangu, nami ninawajua, nao wananifuata.*** *28* ***Nami ninawapa uzima wa milele; nao hawatapotea hata milele, wala hakuna mtu anayeweza kuwanyanganya toka mkono wangu!****"*

Rafiki unayesikiliza, **unafuata nani**? Unafuata **Mchungaji Mwema**? Au unafuata mwingine?

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Tunakuomba kujifunza somo la nyuma pamoja nasi vilevile wakati tunapotaraji kusikia maneno Yesu aliyofundisha juu ya huruma inayojaza moyo wa Mungu. . .

Mungu akubariki wakati unapokumbuka maneno Yesu Masiya aliyosema juu yake mwenyewe:

Everyday Publications Inc
© 2010

> *"****Mimi ni mlango****;* ***kama mtu ataingia kwa mimi, ataokolewa! . . . Mimi mchungaji mwema, mchungaji mwema anatoa uzima wake kwa ajili ya kondoo!"*** (Yoane 10:9,11)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Somo 77

# Moyo wa Mungu

Luka 18,15

Salama iwe kwako, rafiki, kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea tena leo na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Ndani ya majifunzo yetu katika Maandiko ya manabii tumeona ya kwamba Mungu ni **mtakatifu na mwenye haki** na ya kwamba hawezi kuvumilia zambi. Lakini tuliona vilevile ya kwamba yeye ni **mwenye rehema na huruma**. Hizi ni habari nzuri sana kwa sisi kwa sababu tunahitaji rehema yake sana sana, kwani sisi sote tumechukiza Mungu sana. Makosa na zambi zetu ni machukizo kwa Mungu, na zitatuhukumu kwa milele kama asipoturehemu! Leo tunataka kusoma **mifano miwili** ambayo Bwana Yesu alisema kwa makutano. Kwa njia ya mifano hii tutajifunza juu ya **rehema kubwa inayojaza moyo wa Mungu, na namna gani wenye zambi wanaweza kupokea rehema ile.**

Everyday Publications Inc
@ 2010

Ndani ya **mfano wa kwanza,** tutaona **wanaume wawili**: mmoja hakupokea rehema ya Mungu na mmoja aliipokea. Mmoja alikuwa wa jamii ya Wafarisayo na alikuwa na bidii sana kwa maombi, kufunga chakula, na kutoa zaka. Kwa macho ya watu alionekana kama mwenye kushika dini sana. Mtu wa pili alikuwa mtoza kodi na kwa sababu hii alikuwa mwenye zambi kabisa kwa macho ya watu kwani zaidi ya watoza kodi walikuwa wadanganyi.

Sikiliza habari za Mfarisayo na mtoza kodi. Tunasoma ndani ya Habari Njema ya Luka, sura 18. Maandiko yanasema:

> *9 Akasema [Yesu] mfano huu kwa watu ambao walijihesabu wao wenyewe kuwa wenye haki, wakabeua wengine wote. 10* ***Watu wawili*** *walipanda kwa hekalu kuomba; mmoja Mfarisayo na wa pili mtoza kodi. 11 Yule* ***Mfarisayo*** *akasimama,* ***akaomba hivi ndani ya roho yake****: Mungu, ninakushukuru kwa sababu mimi si sawa-*

> *sawa na watu wengine, wanyanganyi, wasio haki, wazini, au si kama mtoza kodi huyu. 12 Ninafunga mara mbili kila jenga, ninatoa zaka ya mapato yangu yote. 13 Na yule **mtoza kodi** alisimama mbali, hakutaka hata kunyanyua macho yake kwa mbingu, lakini alipiga kifua chake, akisema: **Mungu, unirehemu mimi mwenye zambi.** 14 Ninawaambia ninyi: huyu alishuka nyumbani kwake naye amehesabiwa kuwa na haki kuliko yule mwingine, **kwa maana kila mtu ambaye anajitukuza atanyenyekezwa, naye mwenye kujinyenyekeza atatukuzwa.*** (Luka 18)

Yesu alitaka kutufundisha nini kwa njia ya mfano huu mfupi? Alitufundisha ya kwamba Mungu anaonyesha rehema kwa wote wanao**kubali** uzalimu wao mbele yake na ya kwamba anahukumu wote wanao**zania** wao ni wenye haki mbele yake. Hii ndiyo maana ya shairi ndani ya Maandiko Matakatifu linalosema: *"Mungu **anashindana na wenye kiburi,** lakini **anawapa wanyenyekevu neema**."* (1 Petro 5:5) Neno mtu analoheshimu Mungu anazarau.

Mungu anaweza kukubali wale wanaojisifu wenyewe, wakifikili, "**Mimi** ni mtu wa haki! **Ni**naombaga! **Ni**nafunga chakula! **Ni**natoa zaka! **Ni**nafikiaga msikiti! **Ni**nakwendaga nyumba ya Mungu! **Ni**nafanya maneno fulani na fulani!"? Maneno haya yote tunayosema juu yetu wenyewe yanapendeza Mungu? Sivyo, hata kidogo! Mungu hawezi kufurahia kazi zilizo matunda ya kiburi.

Mungu anachukia moyo wa kiburi. Unakumbuka Kaina, mzaliwa wa kwanza wa Adamu, aliyejaribu kukaribia Mungu kwa njia ya kazi zake mwenyewe? Mungu alikubali zabihu yake? Sivyo, Mungu hakuipokea. Rafiki, Mungu hakubadilika. Hata leo, moyo wa Mungu hauwezi kufurahi juu ya **kazi za mtu** kumkaribia, kwa sababu kazi zetu si kamilifu mbele yake. Neno Mungu analotaka ni kwa sisi **kutambua hali yetu ya zambi,** kama yule mtoza kodi, aliyepiga kifua chake na kusema, *"**Mungu, unirehemu mimi mwenye zambi.**"* Ni roho ya kuvunjika namna hii inayofurahisha Mungu. Lakini anachukizwa sana na watu ambao wanajisawanisha na wenzao, kama Mfarisayo, aliyesema hivi ndani ya roho yake: *Mungu, ninakushukuru kwa sababu mimi si sawasawa na watu wengine, wanyanganyi, wasio haki, wazini, au si kama mtoza kodi huyu."*

Neno Mfarisayo asilotambua ndilo ya kwamba Siku ya Hukumu, Mungu hatatusawanisha na wenzetu wenye zambi. Sivyo, Mungu atatusawanisha na sheria yake mwenyewe, ndiyo sheria takatifu na kamilifu inayosema: *"Mtu anayeshika sheria yote, lakini*

Everyday Publications Inc @ 2010

*akakosa katika neno moja tu, amekosa juu ya yote."* (Yakobo 2:10) Mungu yule aliyesema, "*Usizini*" alisema vilevile, "*Usiseme uwongo*." Kama hukuzini, lakini umesema uwongo, umevunja sheria ya Mungu. Huwezi kuingia Paradiso karibu na Mungu, kwa sababu Maandiko yanasema: *"Ndani yake hakitaingia kabisa kitu cho chote kilicho kichafu, wala yeye anayefanya machukizo na uwongo."* (Ufunuo 21:27) Kwa sababu hii wana wa Adamu wanahitaji **rehema ya Mungu**. Rafiki, wewe, kama mtoza kodi ndani ya mfano, umepokea **rehema ya Mungu**? Au, kama Mfarisayo, unakaa kujaribu kujifanyiza haki kwa njia ya **kazi yako mwenyewe?**

Sasa tusome **mfano wa pili** unaoonyesha ya kwamba moyo wa Mungu unajaa mapendo na rehema, kama ya baba anayependa watoto wake. Ndani ya Habari Njema ya Luka, sura 15, tunasoma

> (Luka 15) *1 Watoza kodi wote, na wenye zambi walikuja kwake kusikia maneno yake [Yesu]. 2 Wafarisayo na waandishi wakanungunika, wakisema: Mtu huyu anakaribisha wenye zambi, anakula pamoja nao. 3 Akawaambia mfano huu . . .*
>
> *11* ***Mtu mmoja alikuwa na wana wawili.*** *12 Na* ***yule mdogo*** *alimwambia baba yake: Baba, unipe sehemu ya mali inayoanguka kwangu. Akagawanya mali zake kwao. 13 Nyuma ya siku chache yule mdogo akakusanya vitu vyake vyote, akasafiri kwenda inchi ya mbali, kule akapoteza mali zake kwa maisha ya uasherati. 14 Alipokwisha kupoteza vyote, njaa kubwa ikaingia inchi ile; akaanza kuhitaji. 15 Akakwenda, akapatana na mtu wa inchi ile; yeye akamtuma katika mashamba yake kulisha nguruwe. 16 Akatamani kushibisha tumbo lake kwa makanda waliyokula nguruwe; lakini hakuna mtu ambaye alimpa kitu.*
>
> *17 Wakati alipopata kujitambua, akasema: Wangapi wa watumishi wa mshahara wa baba yangu wanakula chakula na kushiba, na mimi hapa ninakufa kwa njaa? 18 Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu, nitamwambia: Baba, nimefanya zambi juu ya mbingu na mbele yako, 19 sistahili tena kuitwa mwana wako, unifanye kuwa kama mmoja wa watumishi wako wa mshahara.*
>
> *20 Akaondoka, akakwenda kwa baba yake. Alipokuwa angali mbali,* ***baba yake*** *akamwona, akamhurumia, akapiga mbio, akamwangukia shingo lake, akambusu sana. 21 Yule mwana akamwambia: Baba, nimefanya zambi juu ya mbingu na mbele yako, sistahili tena kuitwa mwana wako. 22 Lakini baba akawaambia watumwa wake: Leteni hapa vazi lililo bora, mukamvalishe, mumpe*

Everyday Publications Inc @ 2010

*pete kwa kidole chake, na viatu kwa miguu. 23 Na leteni kinda la*
*ngombe mwenye kunona, mukalichinje, tupate kula na kufurahi. 24*
*Kwani huyu mwana wangu alikufa, naye ameishi tena, alipotea, naye*
*anaonekana. Wakaanza kufurahi.*

*25 Basi **mwana wake mkubwa** alikuwa katika shamba; na*
*wakati alipokuja na kukaribia nyumba, alisikia sauti ya kuimba na*
*kucheza. 26 Akaita mmoja wa watumishi, akauliza maana ya maneno*
*haya. 27 Akamwambia: Ndugu yako amekuja; na baba yako ame-*
*chinja kinda la ngombe mwenye kunona, kwa sababu amempokea*
*salama na mzima. 28 Akakasirika, akakataa kuingia; naye baba yake*
*alitoka, akamsihi. 29 Lakini akajibu, akamwambia baba yake: Tazama,*
*miaka mingi hii nimekutumikia, wala sikukosea amri yako hata mara*
*moja; lakini hukunipa mimi hata mwana-mbuzi nifurahi pamoja na*
*rafiki zangu. 30 Lakini wakati huyu mwana wako alipokuja, aliyeku-*
*la vitu vyako pamoja na makahaba, umemchinjia kinda la ngombe*
*mwenye kunona. 31 Naye akamwambia: Mwana, wewe ni pamoja*
*nami siku zote, na vitu vyangu vyote ni vyako. 32 Ilitufaa kufurahi*
*na kuchekelea, kwa maana huyu ndugu yako alikufa, naye ameishi*
*tena; alipotea, naye ameonekana.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

Mungu anatufundisha nini kwa njia ya mfano huu wa ajabu? Tuliona watu watatu ndani yake: baba, mwana mdogo na mwana mkubwa.

* **Baba** ndani ya habari hizi ni mfano wa **Mungu**.

* **Mwana mdogo** ni mfano wa **wenye zambi wanaotubu** zambi zao za mbele na wanaogeuka kwa Mungu kupata rehema.

* **Mwana mkubwa** ni mfano wa **watu wa kushika dini ambao wanajidanganya wenyewe** kwa njia ya kufikili wao ni wenye haki mbele ya Mungu.

Tufikili kwanza juu ya **mwana mdogo** aliyeishi kufuatana na tabia yake ya zambi na kutenda zambi katika inchi ya mbali. Nini ilimpata? Tuliona ya kwamba mwishoni alifahamu ya kwamba alikuwa amekosea Mungu na watu. Alihuzunishwa kwa sababu ya zambi zake, akatubu, akisema, "*Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu, nitamwambia: Baba, **nimefanya zambi** juu ya mbingu na mbele yako, sistahili tena kuitwa mwana wako, unifanye kuwa kama mmoja wa watumishi wako wa mshahara.*" Hivi, tuliona ya kwamba mwana mdogo aligeuzia luba la nguruwe mgongo, akashika njia kwendea nyumba ya baba yake.

Basi **baba**—alifanya nini? Alikasirikia mwana wake aliyepoteza mali yake? Alimpokea tena kama mtumwa tu? Sivyo! Yesu alisema,

> *"Alipokuwa [mwana] angali mbali, baba yake akamwona, akamhurumia, akapiga mbio,* ***akamwangukia shingo lake, akambusu sana****.* ***Baba*** *akawaambia watumwa wake: Leteni hapa vazi lililo bora, mukamvalishe, mumpe pete kwa kidole chake, na viatu kwa miguu. Na leteni kinda la ngombe mwenye kunona, mukalichinje, tupate kula na kufurahi. Kwani huyu mwana wangu alikufa, naye ameishi tena, alipotea, naye anaonekana."*

Maneno haya yanatufundisha nini? Tunajifunza ya kwamba Mungu ni sawasawa na baba yule aliyekuwa na rehema nyingi! **Mungu anapenda wenye zambi**, na anataka kuwarehemu, **lakini anangoja** kwa kila mwenye zambi kutubu zambi zake na kushika njia ya haki ambayo ametayarisha.

Halafu **mwana mkubwa** alituonyesha neno la kushangaza. Mwana mkubwa hakuwa na roho ya rehema kama baba yake. Sivyo, lakini alikasirika na alikataa kuingia nyumba, akisema na baba yake, *"Tazama,* ***miaka mingi hii nimekutumikia,*** *wala sikukosea amri yako hata mara moja; lakini hukunipa mimi hata mwana-mbuzi nifurahi pamoja na rafiki zangu!"* Ulisikia masemo ya mwana mkubwa? Alisema, "Tazama, miaka ile yote nimekutumikia, kama mtumwa!" Lakini, mwana mkubwa hakufahamu ya kwamba baba hakutaka mwana ambaye alimtumikia kama **mtumwa**. Alitaka mwana ambaye **atampenda na roho yote** na kufurahi kufanya mapenzi yake.

Everyday Publications Inc @ 2010

Kufika leo, wengi wa wana wa Adamu ni kama mwana mkubwa ndani ya mfano huu. Wanafikili wao ni "**watumwa tu wa Mungu.**" Lakini Mungu hataki sisi kuwa watumwa tu. Anataka tuwe kama **wana na binti** kwake. Kwa sababu hii Maandiko Matakatifu yanasema juu ya wale wanaopokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wao, *"Kwa maana hamukupokea tena roho ya* ***utumwa*** *inayoleta woga, lakini mulipokea roho ya* ***kufanywa wana****, kwa sababu hii tunalia: Aba Baba!"* (Waroma 8:15)

Rafiki, kwa mafikili yako wewe ni **mtumwa wa Mungu** au **mwana wa Mungu**? Unajisawanisha na nani ndani ya mfano tuliosoma? Wewe ni kama mwana mdogo aliyefahamu zambi zake na kupokea rehema ya Mungu? Au wewe ni kama mwana mkubwa aliyetumikia baba yake kama mtumwa? Mungu hataki wewe kuwa kama **mtumwa anayeogopa bwana wake**. Neno Mungu analotaka ni kwa wewe kuwa kama **mwana anayependa baba yake,** na anayefu-

rahi kufanya mapenzi yake. Mungu anakupenda na anataka sana kukutendea kwa rehema, lakini anangoja kwa wewe kutubu na kugeuka kwake. Hili ndilo neno nabii Isaya aliloandika akisema: ***"Na hivi Bwana atangoja ili apate kuwahurumia ninyi, na hivi atatukuzwa apate kuwarehemu ninyi; kwa maana Bwana ni Mungu wa hukumu: heri wote ambao wanamngojea!"*** (Isaya 30:18)

**Mungu, Mwenye huruma, Mwenye rehema, anakungojea wewe kufika kwake**, kama baba ndani ya mfano alivyongoja kwa mwana mdogo wake kurudi kwake. Mungu anataka wewe kutubu na moyo wa unyenyekevu na roho ya kuvunjika. Ukifika kwa Mungu hivi na kumtafuta na roho yako yote, unaweza kujua kabisa ya kwamba utakutana na Mungu mwenye moyo wa baba, unaojaa huruma na rehema. Lakini mwenye kiburi anayezarau rehema kubwa ya Mungu afahamu ya kwamba atahukumiwa tu bila rehema!

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutaendelea ndani ya Habari Njema kuona namna Yesu alivyorudisha uzima kwa mfu aliyekuwa ndani ya kaburi kwa siku ine! . . .

Everyday Publications Inc
@ 2010

Sasa Mungu akupe ufahamu kwa maneno tuliyojifunza leo. Na kumbuka:

> ***"Mungu anashindana na wenye kiburi, lakini anawapa wanyenyekevu neema."*** (1 Petro 5:5)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 78

# Ufufuko na Uzima

### Yoane 11,12

Salama iwe kwako, rafiki, kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuja tena leo na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Ndani ya majifunzo yetu katika Habari Njema {*Injil*}, tumeona ya kwamba Yesu, Masiya, ana **majina mengi**. Maneno haya yanatusaidia kufahamu kama yeye ni nani. Tumesikia ya kwamba Yesu aliitwa: *Neno la Mungu lililokuwa pamoja na Mungu katika mwanzo, Mwana wa Mjuu Sana, Mwana wa Watu, Mwana-Kondoo wa Mungu, Mwokozi, Mkate anayeleta uzima, Nuru ya Ulimwengu, Bwana wa Utukufu, Lango la Zizi la Kondoo, na Mchungaji Mwema.* Leo tutaona majina mawili mengine, ndiyo ***"Ufufuko"*** na ***"Uzima."***

Everyday Publications Inc @ 2010

Tuliona ya kwamba Yesu alisafiri pahali pote katika inchi ya Wayuda, akifundisha, akitenda mema, akiponyesha wagonjwa, viwete, vipofu na wenye pepo wachafu. Makutano makubwa walimfuata. Lakini "wafundi wa dini," waliojulikana kama Wafarisayo, walionea Yesu wivu sana. Hawakuweza kubisha ya kwamba alisema na **hekima**, na **maajabu** aliyofanya.

Leo tunakusudi kuendelea ndani ya Habari Njema. Tutaona **Yesu akitenda ajabu lingine ambalo Mungu tu anaweza kutenda, na lililofunua utukufu wa Mungu ndani yake, ili watu waweze kumwamini.** Tusome ndani ya Habari Njema ya Yoane, sura 11. Maandiko yanasema kuanza na shairi 1:

> *1 Na mtu mmoja alikuwa na ugonjwa, jina lake* ***Lazaro*** *wa Betania,*
> *mji wa* ***Maria*** *na ndugu yake mke* ***Marata.*** *2 Ndiye Maria yule*
> *aliyepakaa Bwana na marasi, na alipangusa miguu yake na nyole*
> *zake, yeye yule ndugu yake Lazaro aliyekuwa na ugonjwa. 3 Basi*
> *ndugu zake wake walituma mjumbe kwake [**Yesu**], wakisema: Bwana,*

*tazama, yeye ambaye unampenda ana ugonjwa. 4 Wakati Yesu aliposikia, alisema: Ugonjwa huu si wa kufa, lakini kwa utukufu wa Mungu, ili Mwana wa Mungu atukuzwe kwa neno hili. 5 Na Yesu alipenda Marata, na ndugu yake mke, na Lazaro. 6 Basi, wakati aliposikia ya kwamba alikuwa na ugonjwa, alikaa kule siku mbili pahali pale.* (Yesu alijua ya kwamba Lazaro atakufa. Lakini Yesu alikusudi kutumika na mauti ya Lazaro kuonyesha uwezo wa Mungu ulio ndani yake mwenyewe, ili watu waweze kujua ya kwamba alitoka mbinguni.)

*7 Halafu nyuma [ya kubaki siku mbili nyingine pahali walipokwa, Yesu] akawaambia wanafunzi wake: Twende katika Yudea. 8 Wanafunzi wake wakamwambia: Rabi, sasahivi tu Wayuda walitafuta kukupiga kwa mawe; nawe unataka kwenda tena kule? 9 Yesu akawajibu: Hapana saa kumi na mbili katika muchana? . . . 11 Rafiki yetu analala usingizi; lakini ninakwenda kumwamsha. 12 Basi wanafunzi wakamwambia: Bwana, kama amelala atapona. 13 Lakini Yesu alisema juu ya kufa kwake, lakini wao walizania ya kama alisema juu ya kupumzika katika usingizi. 14 Halafu Yesu aliwaambia waziwazi ya kwamba:* ***Lazaro amekufa.*** *15 Nami ninafurahi kwa ajili yenu ya kwamba sikuwa kule, mupate kuamini; lakini twende kwake.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

*17 Basi wakati Yesu alipofika, akamkuta amekwisha kuwa katika kaburi* ***siku ine****. 18 Na Betania ulikuwa karibu na Yerusalema, kama kilomètres tatu. 19 Na Wayuda wengi walikuwa wamekuja kwa Marata na Maria, kuwafariji kwa ajili ya ndugu yao. 20 Basi Marata, wakati aliposikia ya kwamba Yesu anakuja, alikwenda kumkuta; lakini Maria alikaa nyumbani. 21 Basi Marata akamwambia Yesu: Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. 22 Lakini ninajua, hata sasa yo yote ambayo utaomba Mungu, Mungu atakupa. 23 Yesu akamwambia:* ***Ndugu yako atafufuka****. 24 Maria akamwambia: Ninajua ya kama atafufuka katika ufufuko wa siku ya mwisho.*

*25 Yesu akamwambia:* ***Mimi ni ufufuko na uzima: yeye ambaye ananiamini, hata anapokufa, ataishi; 26 na kila mtu mwenye uzima na kuniamini mimi hatakufa milele. Unaamini haya?*** *27 Akamwambia: Ndiyo, Bwana, nimeamini ya kwamba wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu, yeye anayekuja duniani. 28 Na wakati alipokwisha kusema maneno haya, akakwenda zake, akaita ndugu yake mke Maria, kwa siri akisema: Mwalimu amekuja, naye anakuita. 29 Naye wakati aliposikia, akaondoka upesi, akakwenda kwake. . . 32 Basi wakati Maria alipofika pahali alipokuwa Yesu, na*

*kumwona, akaanguka kwa miguu yake, akamwambia: Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa.*

*33 Basi wakati Yesu alipomwona akilia, na wale Wayuda waliokuja pamoja naye wakilia, aliugua katika roho, akafazaika, 34 akasema: Mumemweka wapi? Wakamwambia: Bwana, kuja, utazame. 35 Yesu akalia machozi. 36 Basi Wayuda wakasema: Tazama namna alivyompenda! 37 Lakini wengine walisema: Mtu huyu aliyefungulia kipofu macho, hakuweza kufanya hata mtu huyu asife?*

*38 Basi Yesu akiugua tena katika roho yake, akafika kaburi. Nalo lilikuwa pango, na jiwe limewekwa juu yake. 39 Yesu akasema: **Mwondoshe jiwe**. Marata, ndugu mke ya yule mtu aliyekufa, akamwambia: Bwana, ananuka sasa; maana, amekuwa maiti siku ine. 40 Yesu akamwambia: **Sikukuambia, kama ukiamini utaona utukufu wa Mungu**? 41 Basi wakaondosha lile jiwe toka pahali maiti ilipowekwa. Na Yesu alinyanyua macho yake, akasema: Baba, ninakushukuru kwa sababu ulinisikia. 42 Na nilijua ya kwamba unanisikia siku zote; lakini kwa ajili ya watu ambao wananizunguka nilisema, waamini ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma. 43 Wakati alipokwisha kusema maneno haya, akapaza sauti kubwa: **Lazaro, toka inje**. 44 Na yule aliyekufa akatoka inje, akifungwa mikono na miguu kwa sanda, na uso wake umefungwa kwa kitambaa. Yesu akawaambia: **Mumfungue, aende zake.***

Everyday Publications Inc
@ 2010

Mbele ya kumaliza habari hizi za ajabu, ni vizuri kwa sisi kuwaza kidogo juu ya ajabu hili la uwezo Bwana alilofanya. Tangu kuumbwa kwa dunia kufika leo, hakuna mtu aliyesikia habari za mtu aliyeweza kumpa maiti uzima wakati alipokwisha kulala kaburini siku ine; ndiyo maiti inayokwisha kupooza na kunuka. Lakini hili ndilo neno Yesu alilofanya wakati alipofufua Lazaro toka wafu.

Uwezo wa mauti halikuwa neno kwa Bwana Yesu, kwa sababu yeye ni Neno la Mungu; Uzima wenyewe wa Mungu aliyekuja toka mbingu. Kama Mungu alivyo na uzima ndani yake, vivyo hivyo Masiya ana uzima ndani yake. Na kama Mungu anavyoweza kufufua maiti na kuwapa uzima, vivyo hivyo Masiya anaweza kuleta uzima kwa mtu ye yote anayetaka, kwa sababu yeye ndiye **Asili ya Uzima**. Kwa sababu hii, wakati Yesu alipoita Lazaro kutoka, maiti alipata uzima tena, akafufuka na kutoka kaburini. Na kwa sababu hii vilevile Yesu aliweza kusema kwa ndugu mke ya Lazaro, ***"Mimi ni ufufuko na uzima: yeye ambaye ananiamini, hata anapokufa, ataishi!"***

Sasa tumalize habari hizi na kuona nini Wayuda walilofanya nyuma ya kuona Yesu akifufua Lazaro toka kaburi. Maandiko yanasema :

> (Yoane 11) *45 Basi Wayuda wengi waliokuja kwa Maria, na kutazama maneno aliyofanya Yesu,* ***walimwamini****. 46* ***Lakini wengine wao*** *wakakwenda zao kwa Wafarisayo, wakawaambia maneno aliyofanya Yesu. 47 Basi wakubwa wa makuhani na Wafarisayo wakakusanya baraza, wakasema: Tunafanya nini? Kwa sababu mtu huyu anafanya alama nyingi. 48 Kama tukimwacha hivi peke yake, watu wote watamwamini; na Waroma watakuja na wataondoa pahali petu na taifa letu vilevile.*
>
> *49 Na mmoja wao, jina lake* ***Kayafa****, aliyekuwa kuhani mkubwa mwaka ule, akawaambia:* ***Hamujui kitu,*** *50* ***wala hamufikili ya kwamba inafaa mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, wala taifa lote lisiangamie****. 51* ***Na neno hili hakusema kwa yeye mwenyewe; lakini akiwa kuhani mkubwa mwaka ule, alitabiri ya kwamba Yesu atakufa kwa ajili ya taifa lile;*** *52* ***wala si kwa ajili ya taifa hili tu, lakini akusanye pamoja watoto wa Mungu waliosambazwa mbali.*** *53 Basi tangu siku ile walifanya shauri la kumwua. 54 Hivi Yesu hakutembea tena waziwazi katikati ya Wayuda; lakini alikwenda zake kwa inchi karibu na jangwa, mpaka mji unaoitwa Efuraimu, na alikaa kule pamoja na wanafunzi wake.*
>
> *55 Na Pasaka ya Wayuda ilikuwa karibu: na wengi walipanda toka inchi ile kwenda Yerusalema mbele ya Pasaka, wapate kusafishwa. 56 Basi wakatafuta Yesu, wakasemezana wao kwa wao, wangali waliposimama katika hekalu: Munazania nini? Hatakuja kwa karamu? 57 Na wakubwa wa makuhani na Wafarisayo walikuwa wameleta amri, ya kwamba kama mtu akijua pahali alipokuwa, alete habari, wapate kumkamata.*
>
> (Yoane 12) *1 Basi Yesu, siku sita mbele ya Pasaka, alifika Betania, pahali alipokuwa Lazaro, yule ambaye Yesu alimfufua toka wafu. 2 Kule wakamfanyiza chakula cha mangaribi, na Marata alitumika; lakini Lazaro alikuwa mmoja wa wale waliokula chakula pamoja naye. 3 Basi Maria akatwaa ratli ya marasi ya nardo safi, ya bei gali, akapakaa miguu ya Yesu, na alipangusa miguu yake kwa nyole zake; nyumba ikajaa na harufu ya marasi. 4 Lakini Yuda Iskariota, mwana wa Simoni, mmoja wa wanafunzi wake, yeye aliyekuwa tayari kumtoa, akasema: 5 Kwa nini marasi hii haikuuzwa kwa dinari mia tatu, na kupewa masikini? 6 Alisema maneno haya, si kwa sababu ya*

Everyday Publications Inc @ 2010

*kuhurumia masikini; lakini kwa sababu alikuwa mwizi, na mwenye kushika mfuko, na alichukua vilivyotiwa ndani yake. 7 Basi Yesu alisema: Mumwache, ameiweka kwa siku ya maziko yangu. 8 Kwa maana muna masikini pamoja nanyi siku zote; lakini hamuna mimi pamoja nanyi siku zote.*

*9 Basi watu wengi wa Wayuda walijua ya kama alikuwa kule, wakakuja, si kwa sababu ya Yesu tu, lakini waone Lazaro vilevile, ambaye alimfufua toka wafu. 10 Lakini* ***wakubwa wa makuhani wakafanya shauri waue Lazaro vilevile, 11 maana kwa sababu yake wengi katika Wayuda walikwenda zao wakaamini Yesu.***

Mbele ya kumaliza somo hili kuna neno moja ambalo inatupasa kufikili juu yake. Uliona namna viongozi vya Wayuda kwa maneno ya dini walivyotenda wakati walipoona alama hii ya Yesu? Wao wote waliogopa kubisha ajabu Yesu alilotenda, kwa sababu watu wote waliweza kuona wao wenyewe mtu yule aliyefufuliwa toka wafu! Basi Kuhani Mkubwa na makuhani wengine walifanya nini? Walitubu zambi zao na kuamini ya kwamba Yesu alikuwa Masiya, Mwana wa Mungu Mjuu Sana, aliyekuja toka mbinguni? **Sivyo, hawakutubu!** Maajabu yote Yesu aliyofanya hayakufanyiza makuhani na wanafunzi wao kutubu na kupokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wao.

Everyday Publications Inc @ 2010

Halafu makuhani walifanya nini? Walichukia Yesu hata kupita, wakafanya shauri pamoja kumwua! Walikusudi kuua Lazaro ambaye Yesu alimfufua sasa tu, kwani kwa sababu ya Lazaro Wayuda wengi waliacha kufuata makuhani, wakaanza kufuata Yesu. Kweli viongozi hawa walikuwa mbali sana na Mungu, wenye mioyo iliyojaa udanganyifu! **Hawakupenda Mungu wala kweli.** Waliona bule maajabu yote ambayo Yesu alikuwa amefanya mbele yao. Waliweka roho tu juu ya anasa yao wenyewe, pahali pao pa heshima, faida yao wenyewe, na kujipatia mali. Hivi walifanya shauri pamoja kuua Yesu, kwa sababu waliogopa kama wakimruhusu kuendelea na kazi yake, Wayuda wote wataacha kuwafuata, na watafuata Yesu.

Unafikili nini juu ya viongozi hawa wa Wayuda? Nani aliweka ndani ya roho zao mawazo juu ya kuua Yesu? Shetani alikuwa akiwaongoza, kwa sababu anachukia Mungu na Masiya yake. Shetani alifikili kama viongozi vya Wayuda wakiua Yesu, Mungu hataweza kutimiza shauri lake kuokoa wana wa Adamu toka

uwezo wake. Lakini Shetani hakufahamu ya kwamba **Mungu alikusudi kutumia mauti ya Masiya kuokoa wana wa Adamu toka uwezo wa Shetani!** Vilevile, Shetani na wale waliofungana naye hawakufahamu ya kwamba uwezo wa mauti haukuweza kufunga Bwana Yesu kwa sababu **Yesu ni Ufufuko na Uzima**. Kwa sababu hii Yesu aliweza kusema na ndugu mke wa Lazaro, *"**Mimi ni ufufuko na uzima**. Yeye ambaye ananiamini, hata anakufa, ataishi . . . Unaamini haya?"* (Yoane 11:25,26)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Tumefikia mwisho wa somo la leo. Tunakuomba kufika tena mara ya nyuma wakati tutakapoendelea ndani ya Habari Njema na kusoma juu ya Yesu akiingia Yerusalema juu ya mwana-punda, na kutimiza maneno manabii wa Mungu waliyoandika juu ya Masiya miaka mingi mbele . . .

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya maana tamu sana ya masemo haya ya Yesu Masiya:

> *"**Mimi ni ufufuko na uzima**. **Yeye ambaye ananiamini, hata anakufa, ataishi . . . Unaamini haya?"*** (Yoane 11:25,26)

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## SOMO 79

# YESU ANAINGIA YERUSALEMA

## LUKA 18-20

Tunakusalimu tena kwa jina la Mungu. Ni furaha kuweza kuendelea tena na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo la mbele tuliona namna **Bwana Yesu alivyofufua maiti** aliyekuwa amelala kaburini kwa siku ine. Uwezo wa mauti si neno kwa Yesu kwani yeye mwenyewe ni Ufufuko na Uzima. Leo tunakusudi kuendelea ndani ya Habari Njema na kuona Yesu akiingia Yerusalema pahali atakapouawa. **Yesu alijua kila neno ambalo litampata.** Alijua ya kwamba viongozi wa dini ya Wayuda watamtoa kwa Waroma ambao watamtesa na kumfunga juu ya msalaba. Lakini kujua maneno haya hakumzuiza asiende Yerusalema. Juu ya neno hili Habari Njema inasema: *"Ikakuwa siku za kupokewa kwake juu zilipokuwa karibu kutimia,* ***akakaza uso wake kwenda Yerusalema."*** (Luka 9:51) Wakati alipotembea njiani kwenda Yerusalema, Yesu alisema na wanafunzi wake, *"Nina ubatizo [wa mateso] kubatizwa nao, na ninasongwa namna gani hata utakapotimizwa!"* (Luka 12:50)

Everyday Publications Inc. @ 2010

Kwa nini Yesu alikaza uso wake kwenda Yerusalema? Alifanya hivi ili aweze kujitoa kwa wale ambao walitaka kumwua! **Ajabu kabisa!** Kama ukijua ya kwamba, ndani ya mji fulani kulikuwa na watu waliotaka kukutesa na kukuua, utakwendea mji huu na roho moja? Hili ndilo neno Yesu Masiya alilofanya. Yesu alijua ya kuwa alizaliwa kusudi aweze kufa kwa zambi za dunia. Yesu hakufika duniani kutafuta mapenzi yake mwenyewe, lakini **kutimiza maneno manabii waliyoandika juu yake** miaka mingi mbele: ya kwamba Masiya atateswa na kumwanga damu yake inje ya Yerusalema juu ya mlima pahali Abrahamu alipotoa kondoo dume kwa pahali pa mwana wake. Ilikuwa lazima kwa mfano huu wa kondoo dume kutimizwa ndani ya Yesu. Kwa sababu hii Yesu alikwenda Yerusalema, mji uliokuwa kwaye kama pango la simba wenye njaa waliokuwa wakingoja chakula chao.

Sasa tuendelee na majifunzo yetu ndani ya kitabu cha Habari Njema. Maandiko yanasema:

> *"Na walikuwa njiani,* ***wakipanda kwenda Yerusalema:*** *na Yesu aliwatangulia; wakashangaa, nao ambao walimfuata wakaogopa.* ***Akatwaa tena kumi na wawili, akaanza kuwaambia habari za maneno yatakayofanywa juu yake****."* (Marko 10:32) *"Tunapanda Yerusalema,* ***na maneno yote yatatimizwa yaliyoandikwa na manabii juu ya Mwana wa watu****."* (Luka 18:31) *"Mwana wa watu* ***atatiwa katika mikono*** *ya wakubwa wa makuhani, na waandishi, nao* ***watamhukumu afe****,* ***watamtia katika mikono ya Mataifa****, na* ***watamzihaki*** *na* ***kumtemea mate,*** *na* ***kumpiga fimbo,*** *na* ***kumwua,*** *na* ***nyuma ya siku tatu atafufuka."*** (Marko 10:33,34)
>
> (Luka 18) *34* ***Nao hawakufahamu maneno haya hata kidogo;*** *na neno hili limefichwa kwao, wala hawakujua maneno yaliyosemwa. 35 Na alipokaribia Yeriko, kipofu mmoja alikaa kando ya njia akiomba zawadi. 36 Naye aliposikia makutano wanapita, akauliza habari zimekuwa nini. 37 Wakamwambia: Yesu wa Nazareti anapita. 38 Akapaza sauti yake, akisema: Yesu, Mwana wa Daudi, unirehemu. 39 Wale waliotangulia wakamhamakia anyamaze; lakini yeye akazidi kupaza sauti: Mwana wa Daudi, unirehemu. 40 Yesu akasimama, akaamuru wamlete mbele yake; naye alipokuja karibu, Yesu akamwuliza, 41 akisema: Unataka nikufanyie nini? Akasema: Bwana, nipate kuona. 42 Yesu akamwambia: Upate kuona, imani yako imekuponyesha. 43 Mara moja alipata kuona, akamfuata, akitukuza Mungu; watu wote walipoona wakasifu Mungu.*
>
> *(Matayo 21) 1 Na wakati walipokaribia Yerusalema na kufika Betifage, katika mlima wa Mzeituni, Yesu akatuma wanafunzi wawili, 2 akawaambia: Kwendeni katika kijiji kilicho mbele yenu, na mara moja mutakuta* ***punda*** *amefungwa, na mwana-punda pamoja naye; muwafungue na kuwaleta kwangu. 3 Na kama mtu akiwaambia ninyi neno, semeni: Bwana anawahitaji; na mara moja atawatuma. 4* ***Maneno haya yamekuwa hata litimie neno lililosemwa na nabii*** *akisema: 5 Mumwambie binti ya Sayuni, Tazama, mfalme wako anakuja kwako, mpole, naye amepanda punda, na mwana-punda, mtoto wa punda..*
>
> *6 Wanafunzi wakakwenda, wakafanya kama Yesu alivyowaamuru, 7 wakaleta punda na mwana-punda, wakaweka mavazi yao juu yao; akaketi juu yake. 8 Na watu wengi katika makutano wakatandika*

Everyday Publications Inc
@ 2010

*mavazi yao njiani. 9 Na makutano waliopita mbele yake, nao waliofuata wakapaza sauti wakisema: Hosana kwa Mwana wa Daudi; mbarikiwa anayekuja kwa jina la Bwana; Hosana juu mbinguni!*

(Luka 19) *39 Wengine wa Wafarisayo katikati ya makutano wakamwambia: Mwalimu, uhamakie wanafunzi wako. 40 Akajibu, akawaambia: Ninawaambia ninyi: Kama hawa wakinyamaza mawe yatapaza sauti. 41 Naye wakati alipokaribia, akaona mji* ***akalia juu yake,*** *42 akisema: Kama wewe ungejua siku hii, maneno yanayofaa salama yako; lakini sasa yamefichwa kwako 44 . . . kwa sababu* ***hukujua wakati Mungu alipokuja kwako.***

(Matayo 21) *10 Na wakati alipoingia Yerusalema, mji wote wakasukasuka, wakisema:* ***Huyu ni nani?*** *11 Makutano wakasema: Huyu ni nabii, Yesu toka Nazareti ya Galilaya. 12 Yesu akaingia hekaluni mwa Mungu, akafukuza wote waliouza na kununua ndani ya hekalu,* ***akapindua meza*** *ya wabadilisha feza, na viti vyao waliokuwa wakiuza hua; 13 akawaambia: Imeandikwa:* ***Nyumba yangu itaitwa nyumba ya maombi; lakini munaifanya kuwa pango la wanyanganyi.***

Everyday Publications Inc
@ 2010

*14 Vipofu na viwete wakakuja kwake katika hekalu, akawaponyesha. 15 Lakini wakati wakubwa wa makuhani na waandishi walipoona maajabu aliyofanya, na watoto wakilia hekaluni wakisema:* ***Hosana kwa Mwana wa Daudi;*** *wakakasirika, (Walikasirika kwa sababu maana ya "Hosana" ni "Mungu atuokoe" – ndilo neno lililotumiwa kwa kusifu Mungu peke yake.) 16 wakamwambia: Husikii maneno hawa wanayosema? Yesu akawaambia: Ndiyo, hamukusoma: Toka vinywa vya watoto wachanga nao wanaonyonya umepata sifa ya kutimia?*

(Marko 11:18) *Wakubwa wa makuhani na waandishi wakasikia, wakatafuta namna ya kumwua, maana walimwogopa sababu makutano walishangaa juu ya mafundisho yake.*

(Yoane 12) *23 Yesu akawaambia [wanafunzi wake], akisema:* ***Saa imekuja****, Mwana wa watu atukuzwe. 24 Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Kama punza ya ngano isipoanguka kwa udongo na kufa, inakaa peke yake; lakini kama ikikufa, inazaa matunda mengi . . .*

*27 Sasa roho yangu inafazaika; nami nitasema nini? Baba, uniokoe kwa saa hii.* ***Lakini ni kwa sababu hii nimefika kwa saa hii.*** *28 Baba, utukuze jina lako. Basi sauti ilitoka katika mbingu: Nimelitukuza, nami nitalitukuza tena. 29 Basi makutano waliosimama karibu wakasikia, wakasema ya kwamba kulikuwa ngurumo; wengine*

> *walisema: Malaika amesema naye. 30 Yesu akajibu, akasema: Sauti hii haikuwa kwa sababu yangu, lakini kwa sababu yenu. 31 Sasa ni hukumu ya dunia hii; sasa mkubwa wa dunia hii atatupwa inje. 32 Nami kama nikinyanyuliwa juu ya dunia, nitakokota watu wote kwangu. 33* ***Alisema maneno haya, akionyesha ni mauti gani ambayo atakufa.***

Tuache pale kwanza. Tuliona namna Yesu alivyoingia Yerusalema, akitembea juu ya mwana-punda, na ya kwamba makutano ya Wayuda walimsifu na kumshangilia, na kumfanyiza mfalme wao. Lakini watu hawakufahamu kwa sababu gani Yesu alikuwa ameingia Yerusalema. Hata wanafunzi wa Yesu hawakutambua nini itatokea. Walitaraji ya kwamba Yesu ataponyesha Wayuda toka utawala wa adui zao, ndio Waroma. Lakini Yesu hakufika duniani kwa sababu hii. **Yesu hakuja kuharibu ufalme wa Roma, lakini kuharibu ufalme wa Shetani.** Hakushuka kugeuza dunia hii mbovu, lakini **kugeuza mioyo ya watu**. Ndiyo, siku nyingine Kristo atarudi kuhukumu watu wa dunia. Lakini wakati alipokuja duniani mara ya kwanza **alifika kufa kama sadaka**. Alikuja kuokoa wana wa Adamu toka azabu ya zambi yao, kama Mungu alivyoahidi miaka mingi mbele kwa njia ya manabii wake.

Everyday Publications Inc.
@ 2010

Tukiendelea na habari hizi tusome tena ndani ya Maandiko,

> Luka 19: *47 [Yesu]* ***akafundisha*** *kila siku ndani ya hekalu. Lakini wakubwa wa makuhani na waandishi, na wakubwa wa watu,* ***walitafuta kumwua.*** *48 Nao hawakuona neno la kufanya; kwa sababu watu wote walitaka sana kumsikia.*
>
> (Luka 20) *1 Ilikuwa siku moja alipofundisha watu katika hekalu na kuhubiri Habari Njema, wakubwa wa makuhani na waandishi, pamoja na wazee, walikuja kwake, 2 wakisema: Utuambie, kwa mamlaka gani unafanya maneno haya? Na* ***ni nani aliyekupa mamlaka hii?*** *3 Akajibu, akawaambia: Nami nitawauliza ninyi neno moja, muniambie: 4 Ubatizo wa Yoane, ulitoka kwa mbingu au kwa watu? 5 Walibishana wao kwa wao wakisema: Kama tukisema, toka mbingu, yeye atasema: Kwa sababu gani hamukumwamini? 6 Lakini kama tukisema, toka watu; watu wote watatutupia mawe kwa sababu wanasadiki ya kuwa Yoane alikuwa nabii. 7 Wakajibu kwamba hawajui pahali unapotoka. 8 Yesu akawaambia: Wala mimi siwaambii ninyi kwa mamlaka gani ninafanya maneno haya.*
>
> *9 Akaanza kuwaambia watu mfano huu:* ***Mtu alipanda shamba la mizabibu****, akakopesha kwa walimaji, naye alisafiri katika inchi*

*nyingine kwa siku nyingi. 10 Na wakati wa mavuno akatuma mtumwa kwa wale walimaji ili wampe kipande cha matunda ya mizabibu; lakini walimaji wakampiga, wakamfukuza pasipo kumpa kitu. 11 Tena akatuma mtumwa mwingine, wakampiga huyu vilevile, wakamtukana, wakamfukuza pasipo kumpa kitu. 12 Na tena alituma wa tatu, wakamwumiza, wakamtupa inje. 13 Halafu bwana wa shamba la mizabibu alisema: Nitafanya nini? Nitatuma mwana wangu, mpendwa wangu, labda watamheshimu yeye. 14 Lakini wale walimaji walipomwona wakasemezana, wakisema: Huyu ndiye mriti, tumwue ili uriti upate kuwa wetu. 15 Wakamtupa inje ya shamba la mizabibu, wakamwua. Yule bwana wa shamba la mizabibu atawafanyia nini? 16 Atakuja na kuangamiza hawa walimaji, na lile shamba la mizabibu atawapa wengine. Waliposikia maneno haya wakasema: Hapana, hata kidogo. 17 Akawatazama, akasema: Basi andiko hili ni nini?* ***"Jiwe walilokataa wenye kujenga, hili limekuwa jiwe kubwa la pembeni. 18 Kila mtu anayeanguka juu ya jiwe hili atavunjikavunjika, na kila mtu ambaye litamwangukia, litamsagasaga."*** *19 Wakubwa wa makuhani na waandishi wakatafuta kumkamata saa ile ile; wakaogopa watu, kwa sababu* ***walitambua ya kuwa alisema ule mfano juu yao.***

Everyday Publications Inc
@ 2010

Yesu alionya wale waliofanya shauri kumwua kwa njia ya mfano wa walimaji waovu. Unafahamu maana ya mfano huu? Si nguvu kuutafsiri. Ndani ya mfano huu, Bwana Yesu anasawanisha **Mungu** na mwenye shamba. Shamba la mizabibu ni **taifa la Israeli**. Walimaji waovu ni mfano wa **viongozi wa Wayuda kwa maneno ya dini**. Watumishi waliotumwa na mwenye shamba kupokea zabibu na waliotendewa mabaya na walimaji, ni mfano wa **manabii**. Mwana wa mwenye shamba, aliyeuawa na walimaji, ni mfano wa **Masiya, Yesu**.

Tunaweza kufahamu kwa sababu gani manabii na walimu wa sheria walikasirika sana. Walijua vizuri ya kwamba Yesu alikuwa akisema juu yao! Walifahamu ya kwamba Yesu alikuwa akiwasawanisha na walimaji waovu waliotesa watumishi wa mwenye shamba, na, mwishoni, waliua mwana wake. Hivi Yesu aliwashitaki kama wale **walioona maneno ya manabii bule**, na kama wale **watakaoua Masiya, Mwana wa Aliye Juu sana**, Yesu hakuwaambia mfano tu, lakini alitaja vilevile maneno yaliyoandikwa juu yake mwenyewe ndani ya Zaburi, akasema: ***"Jiwe walilokataa wenye kujenga, hili limekuwa jiwe kubwa la pembeni.*** *Kila mtu anayeanguka juu ya jiwe hili atavunjikavunjika, na kila mtu ambaye litamwangukia,*

*litamsagasaga."* (Luka 20:17,18; Zaburi 118:22) Hivi Yesu alionya viongozi ya dini ya kwamba kwa mwisho Mwokozi ambaye walikataa na kukusudi kuua, atakuwa **Mwamuzi** wao!

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Rafiki, tumefikia mwisho wa somo hili. Mungu akitaka, ndani ya somo la nyuma, tutaendelea na habari za ajabu za Yesu na viongozi vya Wayuda . . .

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya maneno Maandiko yanayotangaza juu ya Masiya:

> ***"Alikuwa ulimwenguni, na ulimwengu ulifanywa naye na ulimwengu haukumtambua!"*** (Yoane 1:10)

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 80

# Masemo Magumu ya Kweli

### Matayo 22-25

Tunakusalimu tena leo kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tuendelee sasa na somo letu *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo la mbele tuliona namna Masiya, **Yesu, alivyoingia Yerusalema, akijua** ya kwamba Yerusalema ulikuwa mji wa makuhani na waandishi wa sheria, ndio wale waliokuwa wakifanya shauri pamoja kumwua! Yesu alijua kila kitu ambacho kitampata, lakini neno hili halikumzuiza asiendee Yerusalema. Alijua ya kwamba alizaliwa kusudi afe kama sadaka kwa zambi za dunia. Nyuma ya siku chache tu makuhani wataagiza akamatwe na kufungwa juu ya msalaba na misumari.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Hivi msomaji, pahali gani ulipo leo, tunakuomba kusikiliza vizuri pamoja na maombi maonyo ya Bwana Yesu kwa watawala wa Wayuda kwa maneno ya dini juu ya udanganyifu na uovu wao. **Maneno** utakayosoma leo ni maneno **magumu**—na **kweli.** Mara nyingine tunaumia wakati tunaposikia kweli. Somo letu la leo linajaa na maneno ya kuumiza namna hii. Kwa lugha ya Senegal wanasema: "Kweli ni pilipili ya kuchoma"!

Kama tulivyoona ndani ya somo la mbele, wakati Yesu alipokwisha kuingia Yerusalema, kila siku aliingia hekalu na kufundisha watu. Kila siku viongozi vya dini na walimu wa sheria walitafuta njia kumkwalisha ndani ya masemo yake ili wapate njia kumwua. Lakini waliogopa watu waliosikiliza Yesu karibu karibu, wakiweka roho juu ya kila neno alilosema.

Ndani ya Habari Njema ya Luka, sura 20, Maandiko yanasema:

> (Luka 20) *20 Wakamwangalia [wakubwa], wakatuma **watu kupeleleza** maneno yake, nao **wakajifanya kuwa wenye haki**, **ili wapate kumshika** kwa maneno yake, kusudi wamtie katika amri na*

*mamlaka ya mtawala. 21 Wakamwuliza wakisema: Mwalimu, tunajua ya kama unasema na kufundisha maneno ya kweli; wala hutazami uso wa mtu, lakini kwa kweli unafundisha njia ya Mungu. 22 Ni halali kwetu kumpa Kaisari kodi au sivyo? 23 Lakini akatambua udanganyifu wao, akawaambia: Sababu gani munanijaribu? 24 Unionyeshe dinari. Ina sura ya nani, na maandiko ya nani? Wakasema: Ya Kaisari. 25 Akawaambia:* ***Mumpe Kaisari vitu vya Kaisari na Mungu vitu vya Mungu.*** *Lakini hawakuweza kumkamata kwa maneno mbele ya watu; wakashangaa kwa jibu lake, wakanyamaza.*

(Matayo 22) *23 Siku ile* ***Wasadukayo*** *wanaosema ya kwamba hakuna ufufuko, walikuja kwake; wakamwuliza, 24 wakisema: Mwalimu, Musa alisema, kama mtu akikufa, naye hana watoto, ndugu yake ataoa mke wake ili apatie ndugu yake mzao. 25 Basi tulikuwa na ndugu saba; wa kwanza akaoa, akakufa, na kwa kuwa hana mzao, akaacha mke wake kwa ndugu yake; 26 vivyo hivyo wa pili vilevile, na wa tatu, hata wote saba. 27 Mwisho wa wote, yule mwanamke akakufa. 28 Basi katika ufufuko, atakuwa mke wa nani katika wale saba? Maana wao wote walikuwa naye. 29 Lakini Yesu akajibu, akawaambia:* ***Munakosa kwa sababu hamujui maandiko wala uwezo wa Mungu.*** (Luka 20) *34 Wana wa wakati huu wanaoa na kuolewa; 35 lakini wale wanaohesabiwa kuwa wamestahili kufikia wakati utakaokuja na kufufuka toka wafu, hawaoi wala hawaolewi. 36 Kwa sababu hawawezi kufa tena, kwa sababu wako sawasawa na malaika: tena ni wana wa Mungu, wakiwa wana wa ufufuko. 37 Hata Musa alionyesha katika pahali pa kijiti ya kuwa wafu wanafufuka, wakati alipoita Bwana kuwa Mungu wa Abrahamu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo. 38 Kwani yeye si Mungu wa wafu lakini wa walio hai; kwa sababu wote wanaishi kwake.*

(Matayo 22) *33 Na wakati makutano waliposikia, wakashangaa kwa mafundisho yake. 34 Lakini wakati* ***Wafarisayo*** *waliposikia ya kwamba alifunga kinywa cha Wasadukayo, wakakusanyika. 35 Mmoja wao, mwana-sheria, akamwuliza akimjaribu: 36 Mwalimu, katika torati, amri gani iliyo kubwa? 37 Akamwambia:* ***Upende Bwana Mungu wako na moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote.*** *38 Hii ni amri iliyo kubwa na ya kwanza. 39 Na ya pili inafanana nayo, ni hii:* ***Penda jirani yako kama wewe mwenyewe****. 40 Katika amri hizi mbili inategemea torati yote na manabii.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

*41 Wakati Wafarisayo walipokusanyika, Yesu akawauliza, 42 akisema:* ***Munafikili nini juu ya Kristo? Yeye ni mwana wa nani?*** *Wakamwambia: Mwana wa Daudi. 43 Yesu akawaambia: Basi namna gani Daudi katika Roho anamwita Bwana, akisema: 44 Bwana alimwambia Bwana wangu: Uketi kwa mkono wangu wa kuume, hata ninapoweka adui zako chini ya miguu yako. 45 Basi Daudi akimwita Bwana, yeye ni mwana wake namna gani? Wala hakuna mtu aliyeweza kumjibu neno, wala* ***tangu siku ile hakuna mtu aliyesubutu kumwuliza neno tena.***

(Matayo 23) *1 Halafu Yesu akawaambia makutano na wanafunzi wake, 2 akisema: Waandishi na Wafarisayo wanaketi katika kiti cha Musa; 3 . . . Musitende kwa mfano wa matendo yao; kwa maana* ***wanasema, lakini hawatendi.*** *4 Ndiyo, wanafunga mizigo mizito iliyo michungu kwa kuvumilia juu ya mabega ya watu, lakini wao wenyewe hawataki kuigusa hata na kidole chao. 5 Lakini matendo yao yote wanatenda ili watazamwe na watu; kwani wanafanya hirizi zao pana na wanaongeza pindo za mavazi yao, 6 na wanapenda pahali pa mbele katika karamu, na kuketi mbele katika masunagogi, 7 na kusalimiwa katika masoko, na kuitwa na watu: Rabi. 8 Lakini ninyi musiitwe Rabi, kwa maana mmoja ni mwalimu wenu; nanyi wote ni ndugu. 9 Wala musiite mtu 'baba' yenu duniani, kwa sababu mmoja ni Baba yenu, aliye mbinguni. 10 Wala musiitwe mwalimu; kwani mmoja ni mwalimu wenu, ndiye Kristo. 11 Lakini yeye aliye mkubwa katikati yenu atakuwa mtumishi wenu. 12* ***Naye anayejitukuza mwenyewe, atanyenyekezwa; naye anayejinyenyekeza mwenyewe, atatukuzwa.***

Everyday Publications Inc
@ 2010

*13 Lakini* ***ole kwenu****, waandishi na Wafarisayo, wadanganyifu! Kwa sababu munafungia watu ufalme wa mbinguni. Kwa maana ninyi hamwingii ninyi wenyewe, wala wale wanaoingia, hamuwaachi kuingia.*

*15* ***Ole wenu****, waandishi na Wafarisayo, wadanganyifu! Kwa maana munazunguka bahari na inchi kufanya mtu mmoja kuwa mgeuzi: na akikwisha kufanyiwa, munamfanya kuwa mwana wa Gehena mara mbili zaidi kuliko ninyi wenyewe. . .*

*23* ***Ole wenu****, waandishi na Wafarisayo, wadanganyifu! Kwa sababu munalipa zaka na mnanaa na bizari na jira, lakini mumeacha mambo makubwa kupita ya sheria, hukumu, na rehema, na imani; lakini imewapasa ninyi kufanya maneno haya pasipo kuacha yale mengine. 24 Ninyi viongozi wapofu, munaochuja imbo na kumeza ngamia.*

*25* ***Ole wenu****, waandishi na Wafarisayo, wadanganyifu! Maana munasafisha inje ya kikombe na sahani, lakini ndani zimejaa unyanganyi na tamaa. 26 Wewe Mfarisayo mpofu, safisha kwanza ndani ya kikombe na ya sahani, hata inje zao ziwe safi vilevile.*

*27* ***Ole wenu****, waandishi na Wafarisayo, wadanganyifu! Kwani munafanana na makaburi yaliyopakaliwa pembe, yanayoonekana vizuri sana kwa inje, lakini ndani yanajaa mifupa ya wafu, na uchafu wote. 28 Hivi ninyi vilevile kwa inje munaonekana kuwa wenye haki mbele ya watu, lakini ndani munajaa udanganyifu na uovu.*

*29* ***Ole wenu****, waandishi na Wafarisayo, wadanganyifu! Kwa sababu munajenga makaburi ya manabii, na kupamba makaburi ya wenye haki, 30 mukisema: Kama sisi tungalikuwa kwa siku za baba zetu, hatungalishirikiana nao katika damu ya manabii. 31 Hivi munajishuhudia wenyewe ya kwamba ninyi ni wana wao walioua manabii. 32 Jazeni basi kipimo cha baba zenu. 33 Ninyi nyoka, ninyi wana wa majoka, mutakimbia hukumu ya Gehena namna gani? . . . 37 Ee Yerusalema, Yerusalema, unaoua manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kukusanya watoto wako pamoja kama vile kuku anavyokusanya watoto wake chini ya mabawa yake, lakini ninyi* ***hamukutaka!***

Everyday Publications Inc @ 2010

(Matayo 24) *1 Yesu akatoka hekaluni, akakwenda zake; wanafunzi wake wakamkwendea kumwonyesha majengo ya hekalu. 2 Lakini akajibu na kuwaambia: Hamwoni maneno haya yote? Kweli ninawaambia ninyi,* ***Halitabaki jiwe juu ya jiwe pasipo kubomolewa.*** *3 Na wakati alipokuwa ameketi juu ya mlima wa mizeituni, wanafunzi wakamkwendea peke yao wakisema: Utuambie, maneno haya yote yatakuwa wakati gani? Nini alama ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?*

*4 Yesu akajibu, akawaambia:* ***Angalieni musidanganywe na mtu.*** *5 Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema: Mimi ndiye Kristo; na watadanganya watu wengi. 6 Na mutasikia habari za vita na matetesi ya vita; angalieni musiogope, kwani sharti maneno haya yatimie; lakini mwisho wenyewe haujakuja bado. 7 Maana taifa litapigana na taifa na ufalme kupigana na ufalme; yatakuwa njaa na matetemeko ya inchi kwa pahali mbalimbali. 8 Lakini maneno haya yote ni mwanzo wa uchungu. 9 Halafu watawatoa ninyi kuteswa na kuwaua ninyi; na mutachukiwa na mataifa yote kwa ajili ya jina langu. 10 Halafu watu wengi watakwaa, na watatoana na kuchukiana. 11* ***Na manabii wengi wa uwongo watasimama na kudanganya watu wengi*** *. . . 23 Na wakati mtu atakapowaambia*

*ninyi: Tazama, Kristo ni hapa, au kule; musiamini. 24 Kwa sababu wakristo wa uwongo watasimama, manabii wa uwongo, nao wataonyesha alama kubwa na maajabu wapate kudanganya kama ikiwezekana hata wachaguliwa. 25* ***Tazama, nimekwisha kuwaonya ninyi mbele.*** *26 Basi kama wakiwaambia ninyi: Tazama, yeye ni jangwani, musitoke; Tazama, yeye ni katika vyumba vya ndani nyumbani, musisadiki. 27 Kwa maana kama umeme unavyokuja toka mashariki na unaonekana hata mangaribi; hivi kuja kwa Mwana wa watu kutakavyokuwa vilevile.*

*29 Mara moja nyuma ya mateso ya siku zile, jua litatiwa giza, wala mwezi hautatoa nuru yake, na nyota zitaanguka toka mbinguni, na nguvu za mbingu zitatikisika; 30 halafu alama ya Mwana wa watu itaonekana mbinguni; na mataifa yote ya dunia wataomboleza, nao* ***wataona Mwana wa watu akikuja katika mawingu ya mbingu pamoja na uwezo na utukufu mkubwa****. 31 Naye atatuma malaika zake na sauti kubwa ya baragumu, nao watakusanya wachaguliwa wake toka pepo ine, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho ule.*

Everyday Publications Inc @ 2010

(Matayo 25) *31 Lakini wakati Mwana wa watu atakapokuja katika utukufu wake, na malaika yote pamoja naye, halafu ataketi juu ya kiti cha utukufu wake; 32 na mbele yake mataifa yote watakusanyika; naye atawatenga kama mchungaji anavyotenga kondoo na mbuzi; 33 na ataweka kondoo kwa mkono wake wa kuume, lakini mbuzi kwa mkono wake wa kushoto. 34 Halafu Mfalme atawaambia wale kwa mkono wake wa kuume: Kujeni, ninyi muliobarikiwa na Baba yangu, muriti ufalme muliotengenezewa tangu kuumbwa kwa ulimwengu; . . . 41 Kisha atawaambia wale kwa mkono wake wa kushoto: Ondokeni kwangu, ninyi muliolaaniwa, mwende katika moto wa milele uliotengenezwa kwa Shetani na malaika zake. . . . 46* ***Na hawa wote watakwenda kuingia katika azabu ya milele; lakini wenye haki watakwenda kuingia katika uzima wa milele.***

Inatupasa kuacha hapa kwa leo. Tumesikia Bwana Yesu aki**gombeza** viongozi vya dini juu ya udanganyifu wao na ugumu wa mioyo yao. Tulimsikia vilevile akionya wanafunzi wake juu ya wale watakaotokea nyuma yake, ambao watajiita manabii na kudanganya watu wengi. Mwishoni, tulisikia Bwana Yesu aki**tangaza** ya kwamba atarudi tena siku nyingine kwa dunia hii, akitoka mbinguni pamoja na malaika zake wenye uwezo, kuhukumu watu wale wanaokataa kutii Habari Njema ya Mungu juu ya Masiya, Mwokozi wa wenye zambi.

Ndiyo, tumesikia **maneno magumu** leo, lakini ni **maneno mazuri** vilevile kwa sababu ni **maneno ya kweli**. Na ni **maneno ya ajabu** kwa watu wote ambao wanayaamini, kwa sababu Bwana Yesu alisema, *"Nanyi mutajua kweli, na* ***kweli itawaweka ninyi huru****!* (Yoane 8:32)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Rafiki, kutana nasi tena mara ya nyuma kujifunza juu ya mmoja wa wanafunzi wa Yesu aliyefika karibu na Kuhani Mkubwa kwa kutoa Yesu kwa mikono ya wale waliotaka kumwua. . .

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya masemo haya ya Yesu:

> ***"Munakosa kwa sababu hamujui maandiko wala uwezo wa Mungu." Lakini "kweli itawaweka ninyi huru!"*** (Matayo 22:29; Yoane 8:32)

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 81

# Chakula cha Mwisho

### Matayo 26

Salama kwako, rafiki msomaji, kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuja tena leo na mfulizo wenu *Njia ya Haki*.

Ndani ya safari yetu katika Maandiko Matakatifu, tunakaa kusoma ndani ya Habari Njema {*Injil*}, ndiyo kitabu kitakatifu kinachopasha Habari Njema juu ya Yesu Masiya. Yesu ni Mkombozi Mtakatifu aliyefika duniani kuokoa wana wa Adamu toka utawala wa Shetani. **Mkombozi alikuwa namna nyingine na watu wote wengine; Yeye ni Neno la Mungu lililokuwa pamoja na Mungu katika mwanzo na aliyetokea duniani kama mtu.** Mtu Yesu alikuwa namna nyingine kwa maneno ya **kuzaliwa** kwake, kwa sababu alizaliwa na bikira kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Yesu alikuwa namna nyingine kwa **tabia** yake, kwa sababu alizaliwa na tabia takatifu; hakufanya zambi kamwe. Kazi zake zilikuwa namna nyingine vilevile; hakuna mtu aliyefanya maajabu tangu zamani kama yeye. Bwana Yesu alikuwa na uwezo juu ya Shetani na pepo wachafu wake, upepo na bahari, ugonjwa na mauti. **Mafundisho** yake yalikuwa namna nyingine na yale ya watu wote; hata adui zake walisema, *"Mtu hajasema bado kama mtu huyu anavyosema!"* (Yoane 7:46)

Everyday Publications Inc
@ 2010

Ndiyo, Yesu Kristo alikuwa namna nyingine kwa kuzaliwa kwake, tabia yake, kazi zake na masemo yake. Lakini maneno haya hayakusaidia watu wote kutambua ya kwamba Yeye alikuwa Mwokozi aliyetoka mbinguni. Zaidi ya wana wa Adamu hawakufahamu kama Yesu alikuwa nani. Walifikili yeye ni nabii, lakini hawakufahamu kwamba Mungu mwenyewe alikuwa amefika katikati yao! Viongozi vya Wayuda kwa maneno ya dini hawakufahamu kama Yesu alikuwa nani, lakini zaidi ya ile walifanya shauri pamoja kumwua! Ndani ya somo letu la mbele, tulisikia namna Yesu alivyohamakia viongozi vya Wayuda na walimu wa Sheria kwa sababu ya udanganyifu na uovu wao. Lakini maneno Yesu aliyosema

nao hayakuwafanyiza kutubu. Sivyo, lakini sasa viongozi hawa walitawaliwa na wazo moja tu: **Lazima Yesu auawe!**

Bwana Yesu alijua ya kwamba atakufa katika Yerusalema, na ya kwamba ndio viongozi hawa kwa maneno ya dini ambao watamwua. Hivi, tuliona kwamba Yesu alisema na wanafunzi wake ya kuwa makuhani na walimu wa sheria watamhukumu kufa. Watamtoa kwa Waroma, ili wamzarau. wamtemee mate, wampige na kumfunga juu ya msalaba. Lakini nyuma ya siku tatu atafufuliwa tena! Hivi Yesu alitabiri habari za kufa kwake msalabani na ufufuko wake toka kaburi. Na Yesu hakutangaza tu **namna gani** atakufa, na **pahali gani** atakapokufa, lakini ndani ya sura tutakayosoma leo, tutaona ya kwamba Yesu alitangaza vilevile **wakati gani** atakapokufa!

Sasa tuendelee ndani ya Habari Njema ya Matayo, sura 26, na kusikia namna Yesu alivyojitayarisha kwa kufa kwake juu ya msalaba. Neno la Mungu linasema: (Matayo 26) *1 Na ilikuwa wakati Yesu alipomaliza maneno haya yote, akawaambia wanafunzi wake: 2 Munajua ya kama nyuma ya siku mbili Pasaka inakuja, na Mwana wa watu atatolewa asulibiwe.*

Everyday Publications Inc.
@ 2010

Ulisikia maneno Yesu aliyosema na wanafunzi? Alisema nao ya kwamba wana wa Adamu watamfunga juu ya msalaba **siku ya karamu ya Pasaka**. Neno hili ni neno kubwa sana. Wakati tuliposoma ndani ya Tora tulijifunza juu ya siku ya Pasaka. Karamu ya Pasaka ilishikwa ndani ya mwezi wa kwanza ya calendrier ya Wayuda, ndiyo mwezi wa tatu au wa ine (Pasaka). Kila siku, kwa siku kubwa hii, Wayuda wanakumbuka maneno yaliyotokea kwa wakati wa Musa, wakati Waisraeli walipokuwa watumwa wa mfalme mkali Farao. Kwa wakati ule, Mungu, mwenye haki, alihukumu kila mume mzaliwa wa kwanza katika Misri kufa. Lakini Mungu alitayarisha njia ya wokovu vilevile kwa wale ambao walimwamini na kumtii. Mungu aliagiza kila jamaa ya Waisraeli kutoa sadaka ya mwanakondoo bila kipaku na kupakaa damu ya sadaka hii juu ya milango ya nyumba zao. Mungu alikuwa ameahidi kusema, ***"Wakati nitakapoona damu nitapita juu yenu!"*** (Kutoka 12:13) Waisraeli walifanya neno Mungu aliloagiza, hivi Mungu aliponyesha wana wao wazaliwa wa kwanza toka mauti. Mungu aliwaokoa kwa **damu ya kondoo**.

Kwa miaka 1500 Wayuda walitoa sadaka za wana-kondoo kwa karamu ya Pasaka, kukumbuka namna Mungu alivyowaponyesha toka tauni ya mauti iliyopata inchi ya Misri. Lakini Mungu hakutaka **waangalie nyuma tu** na kukumbuka maneno yaliyotokea zamani. Kwa njia ya wana-kondoo za sadaka, Mungu alitaka **waangalie**

**mbele** kwa siku Masiya atakapomwanga damu yake juu ya msalaba. Damu Masiya atakayomwanga itaokoa wenye zambi toka tauni iliyo mbaya kupita matauni yote mengine: moto wa milele wa jehanum! Mauti ya Mkombozi juu ya msalaba itakuwa sadaka ya mwisho na sadaka kamilifu iliyohitajiwa na sheria ya haki ya Mungu. Mungu kwa akili yake alifanya shauri kwa Mkombozi kumwanga damu yake siku ya Pasaka na kwa njia hii **kutimiza mfano wa sadaka ya mwana-kondoo.** Hivi Yesu Mkombozi atamaliza njia ambayo Mungu alitayarisha kuokoa wenye zambi toka hukumu yake ya haki.

Sasa turudi kwa Habari Njema ya Matayo, sura 26, tukianza na shairi tulilosoma mbele:

> (Matayo 26) *1 Na ilikuwa wakati Yesu alipomaliza maneno haya yote, akawaambia wanafunzi wake: 2* ***Munajua ya kama nyuma ya siku mbili Pasaka inakuja, na Mwana wa watu atatolewa asulibiwe.*** *3 Halafu wakakusanyika wakubwa wa makuhani, na wazee wa watu kwa kiwanja cha kuhani mkubwa, aliyeitwa Kayafa; 4 wakafanya shauri ili wakamate Yesu kwa hila na kumwua. Lakini wakasema:* ***Si*** *kwa wakati wa siku kubwa ili kelele lisitokee katika watu. . . 14 Halafu mmoja wa wale kumi na wawili aliyeitwa Yuda Iskariota, akakwendea wakubwa wa makuhani, 15 akasema: Mutanipa mimi nini, nami nitamtoa mikononi mwenu? Wakampimia vipande makumi tatu vya feza. 16 Toka wakati ule alitafuta njia kumtoa mikononi mwao.*
>
> (Marko 14) *12 Hata siku ya kwanza ya mikate isiyochawa, wakati walipoua mwana-kondoo wa Pasaka, wanafunzi wake wakamwambia: Unataka twende kutengeneza pahali upate kula karamu ya Pasaka? 13 Akatuma wawili wa wanafunzi, akawaambia: Kwendeni mjini, na mwanamume atakutana nanyi anayechukua chungu cha maji, na pahali atakapoingia, mumwambie mwenye nyumba: Mwalimu anasema: Wapi chumba changu cha wageni, pahali nitakapokula karamu ya Pasaka pamoja na wanafunzi wangu? 15 Naye atawaonyesha ninyi chumba kikubwa juu ya nyumba, kilichotandikwa tayari; kule mututengenezee. 16 Wanafunzi wakatoka, wakakwenda mjini, wakaona kama alivyowaambia, wakatengeneza karamu ya Pasaka.*
>
> (Luka 22) *14* ***Saa ilipofika****, akaketi pamoja na mitume yake kumi na wawili. 15 Akawaambia: Kwa hamu kubwa nimetaka kula Pasaka hii pamoja nanyi mbele ya kuteswa kwangu. 16 Kwani ninawaambia ninyi: Sitaikula tena kabisa hata itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu.* (Marko 14) *18 Walipokuwa wakiketi kula chakula, Yesu alisema: Kweli ninawaambia ninyi, Mmoja wenu anayekula pamoja*

Everyday Publications Inc
@ 2010

> *nami atanitoa. 19 Wakaanza kuhuzunika, wakamwambia mmoja mmoja: Ni mimi? 20 Naye aliwaambia: Ni mmoja wa kumi na wawili anayechovya pamoja nami katika sahani. 21 Kwa maana Mwana wa watu atakwenda zake kama ilivyoandikwa juu yake, lakini ole wake mtu yule anayetoa Mwana wa watu; ingalikuwa heri kwake yule mtu kama asingalizaliwa.* (Matayo 26) 25 *Yuda ambaye alimtoa, akajibu, akasema: Ni mimi, Rabi? Akamwambia: Wewe umesema.* (Yoane 13) 30 *Basi yeye akipokea tonge alitoka inje mara moja; na ulikuwa usiku.* (Marko 14) 22 *Angali walipokula, akatwaa mkate, akabariki, akavunja, akawapa, akasema: Twaeni, kuleni huu ndio mwili wangu. 23 Akatwaa kikombe, akashukuru, akawapa, wakakunywa wote. 24 Akawaambia: Hii ni damu yangu ya Agano iliyomwangika kwa ajili ya wengi . . .*

Haya ndiyo maneno yanayoandikwa ndani ya Habari Njema juu ya chakula cha mwisho Yesu alichokula pamoja na wanafunzi wake, mbele ya kumwanga damu yake kama sadaka inayofuta zambi. Yesu alijulisha wanafunzi wake kumi na wawili ya kwamba mmoja wao atamtoa kwa mikono ya adui zake. Alikuwa Yuda Iskariota. Kwa macho ya watu, Yuda alikuwa mwanafunzi mwaminifu, lakini moyoni mwake aliweka roho juu ya mali na vitu vya dunia tu. Kwa sababu hii alifika karibu na kuhani mkubwa akamwambia: *Mutanipa mimi nini, nami nitamtoa mikononi mwenu?* Hivi makuhani walimpimia vipande makumi tatu vya feza. Maneno haya yalitimiza maneno nabii Zekaria aliyotabiri mia za miaka mbele, wakati alipoandika ya kwamba Masiya atatolewa kwa mikono ya adui kwa vipande makumi tatu vya feza. (Ona Zekaria 11:12,13.)

Everyday Publications Inc
@ 2010

Halafu neno kubwa sana ndani ya habari tulizosoma sasa tu ni maneno Yesu aliyosema wakati aliposhiriki mkate na kikombe pamoja na wanafunzi wake. Ulisikia maneno aliyosema nao? Tuyasome tena:

> (Marko 14) 22 *Angali walipokula, akatwaa* ***mkate,*** *akabariki, akavunja, akawapa, akasema: Twaeni, kuleni huu ndio* ***mwili*** *wangu. 23 Akatwaa* ***kikombe****, akashukuru, akawapa, wakakunywa wote. 24 Akawaambia: Hii ni* ***damu*** *yangu ya Agano iliyomwangika kwa ajili ya wengi . . .*

Hivi tunaona ya kwamba Yesu aliweka **mifano miwili** mbele ya wanafunzi wake: mfano wa **mkate**, na mfano wa **kikombe**. Mkate Yesu aliovunja vipande vipande na kuwapa wanafunzi wake, ulikuwa **mfano** wa mwili wake ambao aliutoa kama sadaka.

Kikombe na maji ya zabibu ndani yake kilikuwa **mfano** wa damu ambayo Yesu Mkombozi alimwanga kulipa deni ya zambi ya wana wa Adamu waweze kukaa mbele ya Mungu kwa milele.

Kwa njia ya **mfano wa mkate** na **mfano wa kikombe**, Yesu alifundisha wanafunzi wake ya kwamba alifika duniani **kutoa uzima wake**—mwili wake na damu yake—kama sadaka kwa wenye zambi. Na kama ikipasa kila mtu duniani **kula chakula na kunywa maj**i asife, vivyo hivyo inapasa kila mtu anayetaka kuishi kwa milele mbinguni pamoja na Mungu **kuamini** ya kwamba Yesu Kristo alitoa mwili wake na kumwanga damu yake kwa kutupa sisi uzima wa milele. Bwana Yesu peke yake anaweza kuleta uzima wa milele, na damu aliyomwanga ni dawa ya pekee kutuokoa wewe na mimi toka laana iliyo tunda la zambi.

Ee, msikiaji mwenzetu, ukikumbuka neno moja tu la mafundisho la leo, liwe neno hili: **Yesu Kristo alikuja duniani kubeba mzigo wa zambi yako**. Hili ndilo **tangazo** la manabii wa Mungu. Hii ndiyo **maana** ya kondoo ndume ambaye Abrahamu alitoa kama sadaka kwa pahali pa mwana wake. Njia ya usamehe ndiyo njia ya Sadaka Mkamilifu. Mungu anaweza kusamehe zambi zako kwa njia ya sadaka ya Mkombozi Mtakatifu aliyemwanga damu yake kwa ajili yako. Kwa elfu za miaka Mungu alihitaji sadaka za nyama ili aweze kupita juu ya (kufunika) zambi za wana wa Adamu. Hili ndilo Agano la Zamani ambalo Mungu alilowekea amana manabii wake. Lakini Yesu Masiya ndiye aliyeleta Agano Jipya. Ndiye aliyekuja **kutimiza mfano wa sadaka za nyama**. Yesu Kristo ni yeye mwenyewe Mwana-Kondoo wa mwisho wa Pasaka aliyeuawa, ili mtu ye yote ambaye anamwamini aweze kuokolewa toka hukumu ya haki ya Mungu. Kwa sababu hii Maandiko Matakatifu yanasema: *"Kristo, Pasaka yetu amekwisha kutolewa kwa ajili yetu."* (1 Wakorinto 5:7) ***"Maana yeye asiyejua zambi alimfanya kuwa zambi kwa ajili yetu ili sisi tuwe haki ya Mungu katika yeye."*** (2 Wakorinto 5:21)

Everyday Publications Inc
© 2010

**Damu ya Yesu ina faida bila mwisho, bila mpaka**. Sikiliza maneno Neno la Mungu anayosema juu ya uwezo wa kusafisha wa damu ya Yesu. Maandiko yanasema:

> ***"Damu yake Yesu Kristo . . inatusafisha zambi zote."*** (1 Yoane 1:7) *"Mukijua mumekombolewa, si kwa vitu vinavyoharibika, kwa feza au zahabu, mupate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa muliopokea kwa baba zenu;* ***lakini kwa damu ya damani, kama ya kondoo asiye na kilema wala alama, damu ya Kristo****. Naye*

*amejulikana kweli mbele ya kuwekwa kwa misingi ya dunia, lakini amefunuliwa kwa mwisho wa nyakati kwa ajili yenu, nanyi kwa njia yake munaamini Mungu ambaye alimfufua toka wafu na kumpa utukufu; hata imani yenu na tumaini lenu ziwe* ***katika Mungu****!"* (1 Petro 1:18-21)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Waza sana juu ya maneno uliyosikia leo, kwa sababu Mungu anataka ufahamu kweli hizi kubwa. Ndani ya somo la nyuma tunataka kumaliza habari za chakula cha mwisho na kuona namna watawala wa dini walifunga Yesu kusudi waweze kumwua . . .

Mungu akubariki wakati unapokaa kufikili juu ya maana ya ndanindani na baraka kubwa ndani ya shairi hili toka Neno la Mungu,

***"Damu yake Yesu Kristo . . . inatusafisha zambi zote!"*** (1 Yoane 1:7; Yoane 1:29)

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

SOMO 82

# YESU ANAKAMATWA

YOANE 14; MATAYO 26

Salama iwe kwako, rafiki. Tunakusalimu tena kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele.

Ndani ya somo la mbele la mfulizo *Njia ya Haki* tulisoma juu ya **chakula cha mwisho** ambacho Yesu alikula pamoja na wanafunzi wake wakati kufa kwake kulipokuwa karibu. Tulisikia Yesu akiwaambia wanafunzi wake kumi na wawili ya kwamba mmoja wao atamtoa kwa mikono ya adui zake. Tuliona Yesu akipitisha mkate na kikombe kwa wanafunzi wake, akiwaambia ya kwamba mkate aliovunja ulikuwa mfano wa mwili wake aliokuwa karibu kutoa kama sadaka, na kikombe chenye maji ya mizabibu kilikuwa mfano wa damu atakayomwanga. Hivi, Yesu alionyeshea wanafunzi wake tena ya kwamba sababu kwa kuja kwake duniani ilikuwa kumwanga damu yake kama sadaka inayoondosha zambi na inayoleta uzima wa milele.

Everyday Publications Inc @ 2010

Leo tunakusudi kuendelea ndani ya Habari Njema na kuona masemo mengine **ya ajabu na yenye maana sana** Bwana Yesu aliyosema **usiku walinzi wa hekalu walipokuja kumkamata.**

Tunasoma ndani ya Habari Njema, sura 14.

> (Yoane 14) *1 Musifazaike mioyoni mwenu; munaamini* ***Mungu****, muniamini mimi vilevile. 2* ***Katika nyumba ya Baba yangu ni makao mengi; kama sivyo ningaliwaambia ninyi; ninakwenda kuwatengenezea ninyi pahali.*** *3 Na kama ninakwenda kuwatengenezea ninyi pahali, nitakuja tena, na nitawakaribisha ninyi kwangu; pahali ninapokaa mimi, mukae vilevile. 4 Na pahali ninapokwenda munajua, na njia munajua.*
>
> *5 Tomasi akamwambia: Bwana, hatujui pahali unapokwenda na tutajua njia namna gani? 6 Yesu akamwambia:* ***Mimi ndimi njia,***

> ***na kweli, na uzima: mtu hakuji kwa Baba, ila kwa mimi.*** *7 Kama mungalinijua mimi, mungalijua Baba yangu vilevile; na tangu sasa munamjua na mumemwona. 8 Filipo akamwambia: Bwana, utuonyeshe Baba, basi inatufaa. 9 Yesu akamwambia: Nimekuwa pamoja nanyi wakati mrefu na hukunijua, Filipo?* ***Ambaye aliniona mimi, ameona Baba****; namna gani unasema: Utuonyeshe Baba? 10 Huamini kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani yangu? Maneno ninayosema kwenu, sisemi kutoka kwangu mwenyewe; lakini Baba anayekaa ndani yangu anafanya kazi zake. 11 Muniamini ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani yangu; au muniamini kwa sababu ya kazi zenyewe.*
>
> *15 Kama mukinipenda mutatii amri zangu. 16 Na nitaomba Baba, naye atawapa ninyi* ***Msaidizi mwingine****, akae nanyi hata milele, 17 hata* ***Roho ya kweli*** *ambaye dunia haiwezi kumpokea; kwani haimwoni wala haimjui; lakini ninyi munamjua, kwa sababu anakaa pamoja nanyi, naye atakuwa ndani yenu. 18 Sitawaacha ninyi yatima: nitakuja kwenu. 19 Angali wakati mdogo, na dunia hainioni tena; lakini munaniona; kwa sababu mimi ni hai, nanyi mutakuwa hai vilevile... 20 Katika siku ile mutajua ya kwamba mimi ni ndani ya Baba yangu, na ninyi ndani yangu, na mimi ndani yenu. Aliye na amri zangu, na kuzitii, yeye ndiye mwenye kunipenda; naye ambaye ananipenda atapendwa na Baba yangu, nami nitampenda na kujionyesha mwenyewe kwake. . . 23 Kama mtu akinipenda, atatii neno langu, na Baba yangu atampenda, nasi tutakuja kwake, na tutafanya makao yetu kwake. 24 Mtu ambaye hanipendi, hatii maneno yangu, na neno munalosikia si langu, lakini lake Baba ambaye alinituma. 25 Maneno haya nimewaambia ninyi nikikaa pamoja na ninyi. 26 Lakini* ***msaidizi, Roho Mtakatifu,*** *ambaye Baba atamtuma kwa jina langu, yeye atawafundisha yote, na kuwakumbusha ninyi yote ambayo niliwaambia ninyi. 27 Salama ninawaachia ninyi, salama yangu ninawapa ninyi; nami ninawapa ninyi si kama dunia inavyotoa. Musifazaike mioyoni mwenu, wala musiwe na woga.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

Hivi Bwana Yesu alifariji mioyo ya wanafunzi wake na kuwatayarisha kwa maneno yatakayotokea. Ulisikia neno Yesu alilotangaza juu ya **Msaidizi**? Ni lazima kwa wewe kufahamu neno hili, kwa sababu kwa wakati wa sasa watu wengine wanaharibu maana ya maneno ya Yesu na wanajaribu kuaminisha watu ya kwamba Yesu alikuwa akitangaza kufika kwa nabii mwingine. Lakini haiwezekani kwa maneno Yesu aliyosema juu ya Msaidizi kuwa juu ya nabii au mtu ye yote, kwa sababu Yesu alisema Msaidizi huyu alikuwa roho

ambaye watu hawawezi kuona na atakuja kukaa ndani ya wafuata wa kweli wa Yesu.

Basi Msaidizi huyu ni nani? Bwana Yesu anatuambia wazi kama yeye ni nani. Sikiliza tena maneno Yesu aliyosema,

> *"Nitaomba Baba, naye atawapa ninyi* ***Msaidizi mwingine, Roho ya kweli*** *. . . naye atakuwa ndani yenu. Sitawaacha ninyi yatima: nitakuja kwenu . . . Msaidizi,* ***Roho Mtakatifu****, ambaye Baba atatuma* ***kwa jina langu****, yeye atawafundisha yote, na kuwakumbusha ninyi yote ambayo niliwaambia ninyi."* (Yoane 14:16-18,26)

Tunauliza tena: Msaidizi huyu ambaye Yesu aliahidi kutuma kwa wanafunzi wake ni nani? Yeye ni **Roho Mtakatifu**, anayetoka kwa Mungu na aliyekuwa ndani ya Yesu. Yeye ni Roho ya Mungu na Yesu. Yeye ni Roho Mtakatifu, ambaye Mungu ataweka ndani ya mioyo ya wote wanaoamini Yesu kama Mwokozi na Bwana wao. Yesu aliahidi wanafunzi wake ya kwamba wakati atakapokwisha kufa, kufufuka, na kurudia mbingu, atatuma Roho Mtakatifu ndani ya mioyo yao, ili aweze kuwazaa mara ya pili, kuwasafisha, kuwapatisha nguvu, na *"kuwaongoza katika yote yaliyo kweli."* (Yoane 16:13; ona vilevile Tito 3:4-7) Nyuma ya masomo machache mengine, Mungu akitaka, tutaona ya kwamba maneno haya yalitokea kweli kwa Yerusalema wakati siku makumi ine nyuma ya kupanda kwa Yesu mbinguni Roho Mtakatifu aliposhuka na kuishi ndani ya mioyo ya wanafunzi wote wa Yesu, kama alivyoahidi.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Ndani ya somo lingine nyuma tutasikia kupita juu ya Mlinzi, ndiye Roho Mtakatifu, anayeweza kugeuza mwenye zambi anayejifikili mwenyewe tu kuwa mtu anayependa Mungu na anayetaka kumpendeza. Lakini sasa turudi tena kwa Matayo 26 na kuona nini ilitokea usiku ule wakati Yesu alipokwisha kula chakula cha mwisho pamoja na wanafunzi wake.

Maandiko yanasema:

> (Matayo 26) *30 Wakati walipokwisha kuimba,* ***wakatoka inje*** *kwenda mlima wa Mizeituni. 31 Halafu Yesu akawaambia: Nyinyi wote mutaanguka kwa ajili yangu usiku huu; kwa sababu imeandikwa: Nitapiga mchungaji, na kondoo za kundi watasambazwa. 32 Lakini nyuma ya ufufuko wangu nitawatangulia ninyi kwenda Galilaya. 33 Lakini Petro akajibu, akamwambia: Hata wote wakianguka kwa ajili yako, mimi sitaanguka kamwe. 34 Yesu akamwambia: Kweli ninakuambia ya kama usiku huu mbele ya kuwika jogoo, utanikana*

*mara tatu. 35 Petro akamwambia: Hata ikinipasa kufa pamoja nawe,
sitakukana kabisa. Na wanafunzi wote walisema vivyo hivyo.*

*Kisha Yesu akakwenda pamoja nao hata pahali pamoja jina lake
**Getesemane**, akawaambia wanafunzi wake: Ketini hapa angali
ninapokwenda kule kuomba. 37 Akatwaa Petro na wana wawili wa
Zebedayo pamoja naye, akaanza kuhuzunika na kufazaika sana. 38
Halafu akawaambia: **Roho yangu ina huzuni saa hata kufa**; kaeni
hapa na kuangalia pamoja nami. 39 Akakwenda mbele kidogo, aka-
anguka kifudifudi, akaomba akisema: **Ee Baba yangu, kama iki-
wezekana kikombe hiki kinipitie; lakini si kama ninavyotaka
mimi, lakini kama wewe unavyotaka.***

Tusimame hapa kidogo. Kikombe kile cha mateso ambacho Yesu alichoogopa kunywa kilikuwa nini? Kwa nini Yesu alikuwa na huzuni sana hata kufa? Yesu alitaabishwa sana rohoni kwa sababu alijua saa kwa yeye kubeba azabu kwa zambi za wana wa Adamu ilikuwa imefika. **Saa ambayo manabii wote wa Mungu walitabiri juu yake ilikuwa imefika!** Watu watatesa Mkombozi na kumfunga juu ya msalaba, lakini neno la kuogofya zaidi kwa Yesu lilikuwa kujua ya kwamba Mungu, Baba yake mbinguni ambaye alimpenda (na yeye alimpenda vilevile) atavimbisha juu yake azabu kwa zambi za dunia nzima! Kwa sababu hii Yesu aliomba: *"Baba yangu, kama ikiwezekana kikombe hiki kinipitie; lakini si kama ninavyotaka mimi, lakini kama wewe unavyotaka."*

Everyday Publications Inc
© 2010

Halafu Maandiko yanasema:

(Matayo 26) *40 [Yesu] akakuja kwa wanafunzi wake, akawakuta
wakilala, akamwambia Petro: Hamukuweza kuangalia pamoja nami
saa moja? 41 Angalieni na kuomba, musiingie katika majaribu; roho
ni tayari lakini mwili ni zaifu. 42 Akakwenda tena **mara ya pili**,
akaomba akisema: Ee Baba yangu, kama haiwezekani kwa kikombe
hiki kunipitia ila nikikikunywa, mapenzi yako yatimizwe. 43 Akakuja
tena, akawakuta wakilala, maana macho yao yamekuwa mazito. 44
Akawaacha tena, akakwenda na kuomba **mara ya tatu,** akisema
maneno yale tena. 45 Halafu akakuja kwa wanafunzi, akawaambia:
"Laleni sasa na kupumzika; tazama, saa imekaribia na Mwana wa
watu ametolewa mikononi mwa wenye zambi. 46 Simameni twe-
ndeni; tazama, yule ambaye ananitoa ni karibu.*

*47 Na wakati alipokuwa akisema, tazama, **Yuda [Iskariota]**,
mmoja wa wale kumi na wawili akakuja, na pamoja naye, makutano
makubwa na panga, na magongo, waliotoka kwa wakubwa wa*

*makuhani na wazee wa watu. 48 Na yule ambaye alimtoa akawapa alama akisema: Yeye ambaye nitambusu, huyu ndiye; mumkamate. 49 Basi akakwendea Yesu mara moja, akasema: Salamu, Rabi; akambusu. 50 Yesu akamwambia: Rafiki, fanya neno ulilokuja kufanya. Halafu wakakuja na kunyosha mikono juu ya Yesu, wakam**kamata**.*

*51 Na tazama, mmoja wao waliokuwa pamoja na Yesu, akanyosha mkono wake, akafuta upanga wake, akapiga mtumwa wa kuhani mkubwa, akamkata sikio. 52 Halafu Yesu akamwambia: Rudisha upanga wako pahali pake; kwani wote wanaoshika upanga wataharibiwa kwa upanga. 53 **Au unazania ya kuwa mimi siwezi kusihi Baba yangu, naye atanitumia sasa zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika?** 54 **Basi maandiko yatatimizwa namna gani ya kama sharti itokee hivi?***

*55 Kwa saa ile Yesu aliwaambia makutano: Mumetoka kunitwaa kama juu ya mnyanganyi, wenye panga na magongo? Kila siku niliketi hekaluni, lakini hamukunikamata. 56 Lakini **maneno haya yote yamekuja ili maandiko ya manabii yatimizwe.** Halafu wanafunzi wote wakamwacha, wakakimbia. 57 Nao waliokamata Yesu wakampeleka kwa nyumba ya Kayafa, kuhani mkubwa, pahali waandishi na wazee walipokusanyika.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

Hivi tumeona leo namna Yesu alivyojitoa kwa mikono ya wale waliotaka kumwua. Labda mtu mwingine atauliza: "Kwa sababu gani Yesu alikubali kutolewa kwa mikono ya adui zake? Yeye aliyetuliza tufani, kutoza pepo kwa watu, kuponyesha vipofu na kufufua wafu—**kwa nini hakujiponyesha mwenyewe toka adui zake?** Yesu mwenyewe alituambia kwa sababu gani hakujiponyesha mwenyewe. Wakati mmoja wa wanafunzi wake alipojaribu kumlinda, Yesu alimwambia,

> *"Rudisha upanga wako pahali pake . . . Unazania ya kuwa mimi siwezi kusihi Baba yangu, naye atanitumia sasa zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika? **Basi maandiko yatatimizwa namna gani ya kama sharti itokee hivi?"*** (Matayo 26:52-54)

Kwa nini Yesu aliruhusu adui zake kumfunga? Alifanya hivi kwa **kutimiza Maandiko ya Manabii** waliotabiri tena na tena ya kwamba ni lazima kwa Masiya kuteswa na kumwanga damu yake kama sadaka inayoondoa zambi. Sharti Mkombozi mwenye haki afe kwa ajili ya wasio haki kusudi kutuleta kwa Mungu. Yesu Masiya alikuja duniani kutimiza maneno ya manabii. Alikuja kutimiza

mfano na maana ya kondoo za sadaka. Alikuja kutuokoa wewe na mimi toka zambi zetu. **Yesu alitoa uzima wake kwa ajili yako na yangu**. Haleluya kwa Mungu aliyetutumia Mwokozi namna hii!

~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Rafiki, ni sharti kwetu kuacha hapa leo. Kwa somo la nyuma tutasoma mafundisho kuona namna gani wakubwa wa makuhani na watu wa Yerusalema na viongozi wao walivyofungana pamoja kukata maneno ya Yesu na kumhukumu, na kwa njia hii kutimiza maneno ya manabii . . .

Mungu akubariki wakati unapokaa kukumbuka na kuwaza juu ya maneno ambayo Yesu aliwaambia wanafunzi wake:

> ***"Ninatoa uzima wangu . . . na kuutwa tena. Hakuna mtu anayeuondoa kwangu, lakini mimi mwenyewe ninautoa!"*** (Yoane 10:17,18)

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 83

# Yesu Anahukumiwa

### Matayo 26,27; Yoane 18,19

Tunafurahi kukusalimu tena kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele.

Kwa safari yetu ndani ya Maandiko Matakatifu tulisikia namna manabii wa Mungu walivyotangaza **njia ya wokovu** Mungu aliyotayarisha kuokoa wenye zambi toka azabu ya milele. Shauri hili la wokovu ni nini? Ni mauti ya Masiya juu ya msalaba. Manabii wa Mungu walishuhudu ya kwamba inapasa Masiya mwenye haki kufa kumwanga damu yake kwa wazalimu, na kubeba kwa ajili yetu hukumu kwa zambi zetu, kama kondoo ya sadaka asiyekuwa na zambi. Hii ilikuwa njia ya pekee kwa Mungu kuweza kutusamehe zambi zetu na kutuhesabu kama wenye haki pamoja na kubaki mwenye haki yeye mwenyewe. Ndani ya masomo yetu ya Maandiko kwa namna matukio yanavyofuatana tuko karibu kufikia habari kubwa zaidi, ndizo habari za mauti na ufufuko wa Masiya. Mungu akitaka tutaangalia leo na ndani ya masomo yanayofuata, namna Masiya, Yesu alivyotoa uzima wake kubeba zambi za dunia.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Ndani ya somo letu la mbele, tuliona namna makuhani walivyonunua mwenye kutoa Yesu kwa mikono yao na kuwafikisha pahali Yesu na wanafunzi wake walipokuwa. Tuliona namna **walivyokamata** Yesu, kumfunga, na kwenda naye. **Habari za kushangaza**! Kwa nini Yesu, aliyejaa uwezo wa Mungu aliruhusu adui zake kumkamata? Aliwaruhusu kumkamata ili aweze **kutimiza maneno yaliyotabiriwa ndani ya maandiko ya manabii** ya kwamba itakuwa lazima kwa Masiya kuteswa, kufa na kufufuliwa toka wafu siku ya tatu, ili mtu ye yote ambaye anamwamini aweze kupokea usamehe wa zambi. Kama manabii walivyotabiri, Masiya *atapelekwa kuchinjwa kama mwana-kondoo* (Isaya 53:7).

Sasa tuendelee ndani ya Habari Njema kuona nini ilitokea **usiku**

**ule wa giza**, nyuma ya kufungwa kwa Yesu na watawala wa dini. Maandiko yanasema:

(Marko 14) *53* ***Wakapeleka Yesu mbele ya kuhani mkubwa;***
***wote wakakusanyika, wakubwa wa makuhani, na wazee na***
***waandishi.*** *54 Naye Petro alimfuata kwa mbali hata ndani ya*
*kiwanja cha kuhani mkubwa, akaketi pamoja na watumishi, akiota*
*moto.*

*55 Wakubwa wa makuhani na baraza wote* ***walitafuta ushuhu-***
***da*** *juu ya Yesu kumwua,* ***lakini hawakuona****. 56 Maana wengi*
*walimshuhudia kwa uwongo lakini ushuhuda wao haukupatana. 57*
*Wengine wakasimama, wakamshuhudia uwongo wakasema: 58 Sisi*
*tulimsikia akisema: Mimi nitavunja hekalu hili lililofanyika kwa*
*mikono, na katika siku tatu nitajenga lingine lisilofanyika kwa*
*mikono. 59 Hata hivi ushuhuda wao haukupatana. 60 Kuhani mku-*
*bwa akasimama katikati, akauliza Yesu, akisema: Hujibu neno? Watu*
*hawa wanakushuhudia nini? 61 Lakini akanyamaza, wala hakujibu*
*neno. Tena kuhani mkubwa akamwuliza, akamwambia: Wewe ndiwe*
*Kristo, mwana wake Mbarikiwa? 62 Yesu akasema:* ***Mimi ni yeye****.*
*Nanyi mutaona Mwana wa watu ameketi mkono wa kuume wa*
*nguvu akikuja na mawingu ya mbingu. 63 Naye kuhani mkubwa ali-*
*pasua nguo zake akisema: Tunahitaji tena ushuhuda namna gani? 64*
*Ninyi munasikia kufuru yake; munazani nini?* ***Nao wote wali-***
***mhukumu kuwa amestahili kuuawa****. 65 Wengine wakaanza*
*kumtemea mate, na kumfunika uso, na kumpiga makonde, na*
*kumwambia: Tabiri! Nao watumishi walimpiga makofi.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

*66 Na* ***Petro*** *alikuwa chini katika kiwanja; akakuja mmoja wa*
*vijakazi vya kuhani mkubwa, 67 akaona Petro akiota moto, akamwa-*
*ngalia, akasema: Nawe ulikuwa pamoja na yule Mnazareti, Yesu. 68*
*Akakana, akasema: Sijui wala sisikii maneno unayosema. Akatoka*
*inje hata ukumbi: jogoo akawika. 69 Na yule kijakazi alimwona tena,*
*akaanza kuwaambia waliosimama pale: Huyu ni mmoja wao. 70*
*Akakana tena. Nyuma ya wakati kidogo waliosimama wakamwambia*
*Petro tena: Hakika wewe mmoja wao kwa sababu wewe Mgalilaya. 71*
*Akaanza kulaani na kuapiza: Sijui mtu huyu ambaye munamsema.*
*72 Mara moja jogoo akawika mara ya pili. Petro akakumbuka lile neno*
*ambalo Yesu alimwambia, kwamba: Mbele ya kuwika jogoo mara*
*mbili utanikana mara tatu. Na wakati alipofikili, akalia.*

(Matayo 27) *1 Na wakati ilipokuwa asubui, wakubwa wote wa*
*makuhani na wazee wa watu wakafanya shauri juu ya Yesu kumwua;*

*2 wakamfunga, wakamchukua na kumpeleka kwa Pilato aliyekuwa liwali. 3 Kisha **Yuda** ambaye alimtoa, wakati alipoona ya kuwa amekwisha kuhukumiwa, akatubu, akarudishia wakubwa wa makuhani na wazee vipande makumi tatu vya feza, 4 akasema: Nimekosa wakati nilipotoa damu isiyo na kosa. Lakini wale wakasema: Hili ni nini kwetu? Uliangalie wewe mwenyewe. 5 Akatupa vipande vya feza katika pahali patakatifu, akaondoka; akatoka inje akajitundika mwenyewe.*

(Yoane 18) *28 Basi **walipeleka Yesu** kutoka kwa Kayafa* (Kuhani Mkubwa) ***hata nyumba ya hukumu**; na ilikuwa mapema; lakini wao wenyewe hawakuingia ndani ya nyumba ya hukumu wasiwe wakachafuka, lakini wapate kula Pasaka. 29 Basi **Pilato** akawatokea inje, akasema: Ni mashitaki gani munayoleta juu ya mtu huyu? 30 Wakajibu, wakamwambia: Kama huyu asingekuwa mwenye kufanya uovu, tusingemleta kwako. 31 Basi Pilato akawaambia: Mumkamate ninyi wenyewe na kumhukumu kwa torati yenu. Basi Wayuda wakamwambia: Sisi hatuna ruhusa ya kuua mtu; 32 hata neno lake Yesu litimizwe alilosema, akionyesha ni kufa gani atakakokufa.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

*33 Basi Pilato akaingia nyumba ya hukumu tena, akaita Yesu, akamwambia: Wewe ni mfalme wa Wayuda? 34 Yesu akajibu: Wewe unasema hivi wewe mwenyewe, au watu wengine walikuambia habari zangu? 35 Pilato alijibu: Mimi Myuda? Taifa lako na wakubwa wa makuhani walikuleta kwangu; umefanya nini? 36 Yesu akajibu: Ufalme wangu si wa dunia hii; kama ufalme wangu ungekuwa wa dunia hii, watumishi wangu wangenipigania nisitolewe kwa Wayuda; lakini sasa ufalme wangu si wa dunia hii. 37 Basi Pilato akamwambia: Wewe mfalme basi? Yesu akajibu: Wewe unasema ya kwamba mimi ni mfalme. Kwa ajili ya maneno haya nilizaliwa, na kwa ajili ya maneno haya nilikuja katika dunia, ili nishuhudie kweli. Kila mtu wa kweli anasikia sauti yangu. 38 Pilato akamwambia: Kweli ni kitu gani? Na wakati alipokwisha kusema neno hili, alitokea Wayuda tena, akawaambia: **Mimi sioni hata kosa moja kwake**.* (Luka 23) *5 Nao wakazidi kusema: Anakoroga watu na kufundisha katika Yudea yote, akianza kutoka Galilaya hata hapa. 6 Pilato aliposikia neno hili akauliza kama alikuwa mtu wa Galilaya. 7 Alipojua ya kama ni mtu chini ya mamlaka ya Herode, akamtuma kwa Herode; naye alikuwa katika Yerusalema siku zile.*

(Luka 23) *8 **Herode** alipoona Yesu, akafurahi sana, kwa sababu tangu zamani alitaka kumwona, kwa sababu amesikia habari zake; akataka sana kuona alama inayofanyika naye. 9 Akamwuliza kwa maneno*

*mengi, lakini hakumjibu hata neno moja. 10 Wakubwa wa makuhani,*
*na waandishi walisimama, wakamshitaki kwa nguvu. 11 Halafu Herode*
*pamoja na askari zake wakamzihaki, wakamcheka; wakamvika mavazi*
*mazuri, wakamrudisha kwa Pilato. 12 Siku ile Pilato na Herode waka-*
*patana kuwa rafiki, maana mbele walikuwa na fitina kati yao.*

*13 Pilato akaita pamoja wakubwa wa makuhani, na wakubwa, na*
*watu, 14 akawaambia: Mumeniletea mtu huyu kama mmoja anayegeuza*
*watu kuwa wabaya, na tazama, nimemwuliza yeye mbele yenu,*
***sikuona kosa katika mtu huyu katika maneno yale ambayo***
***mulimshitaki;*** *15 wala hata Herode; kwani amemrudisha kwetu;*
*wala tazama hakufanya hata neno moja la kustahili kufa.* (Yoane 18)
*39 Lakini kuna desturi kwenu, mimi kuwafungulia ninyi mtu mmoja*
*wakati wa Pasaka; basi munataka niwafungulie ninyi Mfalme wa*
*Wayuda? 40 Basi wote wakalalamika tena, wakisema: Hapana mtu*
*huyu, lakini **Baraba**.* (Luka 23) *19 Naye alitiwa katika kifungo kwa*
*sababu alifanya fitina katika mji, naye aliua mtu kwa kusudi. 20 Pilato,*
*akitaka kufungua Yesu, akasema nao tena. 21 Lakini wakapaza sauti,*
*wakisema: **Umsulibishe, umsulibishe**. 22 Akawaambia mara ya tatu:*
*Kwa sababu gani? Alifanya ubaya gani? Sikuona neno moja kwake*
*kufaa kufa; nitampiga fimbo na kumfungua.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

(Yoane 19) *1 Hivi basi Pilato alitwaa Yesu, akam**piga na mije-***
***lele**. 2 Na askari walisokota **taji ya miiba**, wakaitia kwa kichwa*
*chake, wakamvika na vazi jekundu; 3 wakakuja kwake, wakasema:*
*Salamu, Mfalme wa Wayuda! **Wakampiga makofi.***
*[**Wakamtemea mate**, wakatwaa lile tete na kumpiga kichwani.*
*(Matayo 27:30)] 4 Pilato akatoka tena inje, akawaambia: Tazama*
*ninamleta inje kwenu, mujue ya kuwa sioni neno baya kwake. 5 Basi*
*Yesu akatoka inje, akivaa taji ya miiba, na vazi jekundu. Pilato*
*akawaambia: Tazama mtu huyu. 6 Basi wakati wakubwa wa*
*makuhani na wa askari walipomwona, wakapaza sauti, wakisema:*
***Umsulibishe, umsulibishe!*** *Pilato akawaambia: Mumtwae ninyi*
*wenyewe na kumsulibisha; kwa maana mimi sioni neno baya kwake.*
*7 Wayuda wakamjibu: **Sisi tuna sheria, na kwa sheria ile imem-***
***pasa kufa, kwa sababu alijifanya kuwa Mwana wa Mungu.***

*8 Basi wakati Pilato aliposikia neno hili, akazidi kuogopa; 9 aka-*
*ingia tena nyumba ya hukumu, akamwambia Yesu: **Unatoka wapi?***
*Lakini Yesu hakumjibu neno. 10 Basi Pilato akamwambia: Husemi*
*na mimi? Hujui ya kama nina mamlaka ya kukusulibisha, na nina*
*mamlaka ya kukufungua? 11 Yesu akamjibu: Hungekuwa na mamla-*
*ka juu yangu hata kidogo, kama usingepewa toka juu; kwa sababu hii*

*yeye ambaye alinitia mikononi mwako ana zambi kubwa zaidi. 12 Kutoka saa ile Pilato akatafuta kumfungua; lakini Wayuda wakapaza sauti, wakisema: Kama ukifungua mtu huyu, wewe si rafiki ya Kaisari; kila mtu ambaye anajifanya kuwa mfalme anakataa Kaisari.*

(Matayo 27) *24 Basi wakati Pilato alipoona ya kuwa hakuweza kufanya neno, lakini kama kelele lilizidi, akatwaa maji, akanawa mikono yake mbele ya makutano, akisema: Mimi sina kosa katika damu ya mtu huyu mwenye haki; ninyi mwangalie maneno haya ninyi wenyewe. 25 Watu wote wakajibu, wakasema: Damu yake iwe juu yetu na juu ya watoto wetu!* (Marko) 15:15 ***Pilato akipenda kupendeza makutano akawafungulia Baraba, akatoa Yesu, nyuma ya kumpiga mijeledi, ili asulibiwe.***

Hivi maneno yote yalitokea namna nabii Isaya alivyotabiri miaka karibu mia saba mbele, wakati alipoandika juu ya Masiya: ***"Alionewa, na aliteswa; lakini hakufungua kinywa chake; kama mwana-kondoo anayepelekwa kuchinjwa, na kama mwana-kondoo anavyonyamaza mbele yao wanaokata manyoya yake hakufungua kinywa chake."*** (Isaya 53:7) Isaya aliandika vilevile maneno haya ya Masiya: ***"Niliwatolea mgongo wangu wale wenye kunipiga, na mashavu yangu wale wanaongoa ndevu; sikuficha uso wangu usipate haya na kutemewa mate."*** (Isaya 50:6)

Everyday Publications Inc
© 2010

Leo tumeona namna viongozi vya dini vya Wayuda walitimiza Maandiko ya Manabii wakati walipotesa na kuonea Masiya mtakatifu na mwenye haki na kumhukumu kufa. Kwa nini viongozi vya dini walihukumu Masiya kufa? Walimhukumu kwa sababu **hawakuweza kuvumilia nuru ya kweli.** Yesu alikuwa amewaambia kweli, na kweli ile ilifunua udanganyifu na uovu wao. Yesu mwenyewe alikuwa kweli! Nuru ilikuwa imefikia dunia, lakini watu walipenda zaidi giza kwa sababu kazi zao zilikuwa mbovu. Na kwa sababu wana wa Adamu hawakuweza kuvumilia Nuru, hivi walijaribu kuzima nuru yenyewe. Kwa sababu hii Maandiko yanatangaza:

*"Nuru ilingaa katika giza na giza halikuishinda. . . Hata mmoja wa watawala wa dunia hii hakuijua; kwa sababu kama wangalijua wasingalisulibisha Bwana wa utukufu … Alikuwa ulimwenguni, na ulimwengu ulifanywa naye na ulimwengu haukumtambua. Alikuja kwake, nao walio wake hawakumpokea.* ***Lakini wote ambao walimpokea aliwapa uwezo wa kuwa watoto wa Mungu, ndio wale walioamini jina lake.****"* (Yoane 1:5; 1 Wakorinto 2:8; Yoane 1:10-12)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Asante, rafiki kwa kujifunza pamoja nasi. Usikose kukutana nasi kwa somo la nyuma wakati tutakapoona namna wana wa Adamu walivyotimiza maneno ambayo nabii Daudi aliandika ndani ya Zaburi juu ya Masiya, akisema: *"Wametoboa mikono yangu na miguu yangu."* (Zaburi 22:16)

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya maneno nabii Isaya aliyotabiri miaka mingi mbele juu ya mateso ya Masiya:

> ***"Alionewa, na aliteswa; lakini hakufungua kinywa chake; kama mwana-kondoo anayepelekwa kuchinjwa, na kama kondoo anavyonyamaza mbele yao wanaokata manyoya yake hakufungua kinywa chake."*** (Isaya 53:7)

Everyday Publications Inc
@ 2010

## Somo 84

# Yesu Anasulibishwa

### Matayo 27; Marko 15; Luka 23; Yoane 19

Salama kwako, rafiki. Umekwisha kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo Mungu wa salama ametayarisha, uweze kukaa na salama ya kweli naye kwa milele? Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea tena leo na somo lingine la mfulizo *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo letu la mbele tuliona namna watawala wa Wayuda kwa maneno ya dini walivyofunga Yesu, wakampeleka kwa nyumba ya kuhani mkubwa usiku, wakam**hukumu,** na kumpeleka kwa Pilato, mtawala wa inchi ili waweze kumsulibisha. Askari walimpiga sana na ukali, wakatengeneza taji ya miiba na kuiweka juu ya kichwa chake, wakimzarau, wakimpiga usoni, wakimtemea mate, na kumpiga kichwani na fimbo. **Kwa njia hii wana wa Adamu walikataa mwenye haki, Bwana wa utukufu, aliyekuja toka mbinguni.** Watu wale waliotesa Yesu hawakujua maneno ya manabii; hata hivi walikuwa wakitimiza maneno manabii waliyotangaza ya kwamba ilikuwa lazima kwa Masiya kuteswa hivi kwa mikono ya wenye zambi.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Leo tutaendelea ndani ya kitabu cha Habari Njema {*Injil*} na kuona **namna Yesu Masiya alivyoteswa na kufa** juu ya msalaba, **na kutimiza kwa njia hii shauri kubwa la Mungu, shauri la wokovu,** ambalo manabii yake walitangaza miaka mingi mbele. Mbele ya kuanza mafundisho ya leo, vizuri ujue ya kwamba wakati Yesu alipoishi duniani, ilikuwa desturi ya serikali ya Waroma kuhukumu waasi fulani wa sheria kwa njia ya kuwafunga juu ya mti na misumari, au juu ya miti iliyofungwa pamoja kuwa msalaba. Mauti namna hii yaliitwa *kusulibiwa*. Waasi wabaya zaidi tu waliuawa hivi, ndiyo mauti ya maumivu makubwa na haya sana.

Labda unafazaika kwa sababu gani Mungu aliamuru kwa Masiya mwenye haki kufa hivi na maumivu na haya nyingi. Ilipasa Yesu kufa mauti mabaya hivi kwa sababu zambi ni uasi wa kuogofya sana. **Zambi ndiyo shina la mabaya yote duniani**. Sisi sote ni wenye

zambi na zambi zetu zinachukiza Mungu mtakatifu na mwenye haki! Kwa Mungu kuweza kutusamehe wewe na mimi zambi zetu, pamoja na kukaa mwenye haki yeye mwenyewe, **ilipasa Mungu kuhukumu zambi zetu na hukumu timilifu na ya haki**. Hawezi kusamehe zambi zetu kwa njia yo yote nyingine. Mungu ni Mwamuzi wa haki na ni lazima kwake kuazibu **kila** zambi. Azabu kwa zambi ni mauti na moto wa milele wa jehanum. Sharti azabu hii **nzima** ilipwe. Habari Njema ndiyo ya kwamba Mungu ametuma kwetu Mkombozi mwenye haki kulipa azabu nzima ya zambi zetu. Alikuja kutuokoa toka gazabu ya Mungu ingaliyopasa kutuangukia sisi kwa sababu ya zambi zetu.

Sasa, rafiki zetu, tunawaita ninyi kusikiliza na nia na roho tayari wakati tutakaposoma toka Habari Njema **habari takatifu za Yesu na mauti yake juu ya msalaba**. Maandiko yanasema:

> (Yoane 19) *16 **Hivi basi [Pilato] akamtia katika mikono yao asulibiwe**. Na walikamata Yesu, wakampeleka; 17 akatoka akibeba msalaba wake, hata pahali panapoitwa pahali wa Mfupa wa Kichwa, na kwa Kiebrania Golgota.*
>
> (Luka 23) *26 Ilipokuwa wakimpeleka, wakakamata mtu mmoja jina lake Simoni Mkurene, naye alitoka kwa mashamba, wakaweka msalaba juu yake auchukue nyuma yake Yesu. 27 Makutano makubwa ya watu wakamfuata, na wanawake waliojipigapiga na kumwomboleza . . . 32 Na wawili wengine, watenda mabaya, walipelekwa pamoja naye kuuawa. 33 Wakati walipofika pahali palipoitwa Mfupa wa Kichwa, kule walimsulibisha, na wale watenda mabaya, mmoja kwa mkono wa kuume, na mmoja kwa mkono wa kushoto. 34 Yesu akasema: **Baba, uwasamehe, kwa sababu hawajui neno wanalofanya** . . . 35 Watu wakasimama wakitazama. Lakini wakubwa wakamzihaki, wakisema: Aliokoa wengine, ajiokoe yeye mwenyewe kama yeye ni Kristo wa Mungu. 36 Askari vilevile wakamzihaki, wakakuja kwake wakimpa siki, 37 na kusema: Kama wewe ni mfalme wa Wayuda, ujiokoe wewe mwenyewe.*
>
> (Yoane 19) *19 Pilato akaandika anwani na akaiweka juu ya msalaba. Na imeandikwa, YESU MNAZARETI, MFALME WA WAYUDA. 20 Basi wengine katika Wayuda walisoma anwani hii, kwa sababu pahali aliposulibiwa Yesu, palikuwa karibu na mji; na iliandikwa kwa Kiebrania, na Kiroma, na Kiyunani. 21 Basi wakubwa wa makuhani wa Wayuda walimwambia Pilato: Usiandike, Mfalme wa Wayuda, lakini ya kwamba alisema: Mimi Mfalme wa*

Everyday Publications Inc
@ 2010

*Wayuda. 22 Pilato akajibu: Niliyoandika nimeyaandika. 23 Basi askari, wakati waliposulibisha Yesu, wakatwaa mavazi yake, wakayatenga sehemu ine, kwa kila askari sehemu moja; na kanzu yake vilevile; na kanzu ile haikushonwa, imesukwa pia toka juu hata chini. 24 Basi wakasemezana: Tusiipasue, lakini tuipigie kura, itakuwa ya nani; andiko* ***litimizwe*** *linalosema [na nabii Daudi katika Zaburi]: Waligawanya nguo zangu katikati yao, na vazi langu walilipigia kura. Basi maneno haya waliyafanya askari.*

(Luka 23) *39 Mmoja wa wale watenda mabaya waliotundikwa pamoja naye akamtukana, akisema: Si wewe uliye Kristo? Ujiokoe mwenyewe pamoja nasi. 40 Lakini wa pili akamhamakia, akisema: Huogopi hata Mungu, maana wewe ni katika hukumu ile ile? 41 Na sisi kwa kweli sababu tunapokea malipo yanayostahili kwa matendo yetu, lakini mtu huyu hakufanya neno lisilofaa. 42 Akamwambia Yesu: Bwana, unikumbuke wakati unapokuja katika ufalme wako. 43 Yesu akamwambia:* ***Kweli ninakuambia, Leo utakuwa pamoja nami katika Paradiso.***

Everyday Publications Inc
© 2010

(Marko 15) *33 Na ilipokuwa saa sita, giza lilikuwa juu ya inchi yote hata saa tisa. 34 Na saa tisa Yesu alipaza sauti kubwa;* ***Eloi, Eloi, lama sabaktani****; maana yake:* ***Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha?*** *35 Nao waliposimama pale walisema: Tazama anaita Elia. 36 Na mmoja . . . alisema: Acheni, tuone kama Elia atakuja kumshusha.* (Watu walisema hivi kwa sababu hawakufahamu maneno yaliyokuwa yakitokea. Inchi nzima iligeuka giza kabisa—toka saa sita ya mchana kufika karibu saa tisa. Ndani ya saa zile za giza **Mungu alivimbisha azabu ya zambi za wana wote wa Adamu juu ya Mkombozi Mtakatifu,** ili mtu ye yote ambaye anamwamini hatapotea kamwe! Hatuwezi hata kidogo kujua ukubwa wa mateso ya Yesu kwa ajili yetu.)

(Yoane 19) *28 Nyuma ya maneno haya Yesu akijua ya kama maneno yote yamekwisha kumalizwa, ili andiko litimizwe, akasema:* ***Nina kiu****. 29 Palikuwa kule chombo kimejaa siki; wakajaza sifongo na siki, wakatia juu ya hisopo, wakatia kwa kinywa chake. 30 Basi wakati Yesu alipopokea siki, akasema;* ***Imekwisha.*** (Luka 23) *Yesu alipolia kwa sauti kubwa, akasema:* ***Baba, katika mikono yako ninaweka roho yangu****; na alipokwisha kusema maneno haya akatoa roho.*

(Marko 15) *38* ***Pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini.*** *39 Yule akida aliyesimama mbele yake [Yesu], wakati alipoona alikata roho namna hii, akasema: Hakika mtu huyu*

*alikuwa Mwana wa Mungu. 40 Wanawake walikuwa pale vilevile wakitazama kwa mbali: katika hawa walikuwa Maria Magdalene, na Maria mama ya Yakobo mdogo na wa Yose, na Salome. Hawa ambao walimfuata na kumtumikia wakati alipokuwa katika Galilaya; na wengine wengi waliokwenda pamoja naye hata Yerusalema.*

(Yoane 19) *31 Basi Wayuda, kwa sababu ilikuwa Maandalio, miili isikae juu ya msalaba siku ya sabato (kwa sababu siku ya sabato ile ilikuwa siku kubwa), wakaomba Pilato, miguu yao ivunjwe, na waondolewe. 32 Basi askari walikuja, wakamvunja miguu wa kwanza, na wa pili, aliyesulibiwa pamoja naye; 33 lakini wakati walipofika kwa Yesu, wakaona ya kama amekwisha kufa, hawakuvunja miguu yake; 34 lakini* ***mmoja wa askari alimchoma mbavu yake kwa mkuki, na mara moja ilitoka damu na maji.*** *35 Naye aliyeona alishuhudia, na ushuhuda wake ni kweli; na yeye anajua ya kwamba anasema kweli, ninyi mupate kuamini. 36 Kwa maana maneno haya yalifanyika,* ***ili andiko litimie****: Hapana mfupa wake utakaovunjwa. 37 Na tena andiko lingine linasema: Watamtazama yeye ambaye walimchoma.*

*38 Nyuma ya maneno haya,* ***Yosefu mtu wa Arimatea,*** *akiwa mwanafunzi wa Yesu, lakini kwa siri (maana aliogopa Wayuda)* ***akaomba Pilato ruhusa aondoe mwili wa Yesu****, na Pilato alimpa ruhusa. Basi alikuja akaondoa mwili wake. 39 Na Nikodemo alikuja vilevile, yule aliyekuja kwanza kwa Yesu usiku, na alileta machanganyiko ya manemane na uude, karibu na ratli mia. 40 Basi wakakamata mwili wa Yesu, wakaufunga na sanda ya kitani pamoja na yale manukato, kama desturi ya Wayuda katika maziko. 41 Na pahali pale aliposulibiwa palikuwa shamba; na ndani ya shamba lilikuwa kaburi jipya, bado hajatiwa mtu ndani yake. 42 Basi kule waliweka Yesu kwa sababu ya Maandalio ya Wayuda, kwa sababu kaburi ilikuwa karibu.*

Everyday Publications Inc
© 2010

Rafiki, inatupasa kumaliza masomo yetu hapa kwa leo, hata kama habari za Masiya hazikwishi ndani ya kaburi! Sivyo! Tunafurahi sana kwa sababu ndani ya somo la nyuma tutaona ya kwamba **Yesu amefufuka!**

Maneno tuliyosikia leo ni kweli habari za kushangaza! Tumeona namna wana wa Adamu walivyozarau Masiya, Bwana wa uzima, na kumwua kwa njia ya kumfunga juu ya msalaba na misumari. Lakini, sharti tukumbuke ya kwamba mauti ya Masiya yalitimiza shauri la njia ya wokovu ambayo Mungu alitayarisha mbele ya kuumbwa kwa dunia.

Ulisikia neno Bwana Yesu alilotangaza toka msalaba mbele ya kufa kwake? Alisema, *"**Imekwisha!**"* Kwa sababu gani Yesu alisema, *"Imekwisha!"*? Alisema, *"Imekwisha!"* kwa sababu alikuwa ametimiza kazi ya wokovu. Kweli, dini za dunia **haziwezi** kusema "Inakwisha!" Wangesema: "Hakuna neno linalokwisha! Sharti ujiokoe mwenyewe kwa njia ya kazi zako njema! Sharti utumike sana kuzima zambi zako mwenyewe! Kaa kutumika; usiache; hakuna neno linalokwisha! Ukitaka kuingia Paradiso, sharti ufanye kazi, kutoa sadaka, kutimiza desturi za dini yako, kuomba, kufunga chakula, kutesa mwili wako, vivi hivi!"

Lakini Habari Njema ya Mungu kwa watu ni **"I-me-kwisha!!!"** Amini na kuokolewa! Masiya amelipa deni yako ya zambi na damu yake mwenyewe! Damu ya Yesu inaweza kusafisha na kugeuza mwenye zambi zaidi! Kwa sababu hii Yesu aliweza kusema kwa mnyanganyi aliyetubu na aliyekuwa akikufa kando yake, *"Kweli ninakuambia, Leo utakuwa pamoja nami katika Paradiso."* (Luka 23:43)

Rafiki, kazi inayoweza kukuokoa toka azabu ya zambi imefanywa na inakwisha kabisa. Mungu anakubali sadaka ya Yesu. Hatuhitaji kutoa sadaka za kondoo kama wazazi wetu walivyofanya walioishi mbele ya wakati wa Masiya. Yesu Kristo ni Sadaka kamilifu na ya mwisho ya Mungu. Hakuna neno linalobaki kwa sisi kufanya ila kuamini ushuhuda wa Mungu juu ya Masiya na sadaka yake. ***"Imekwisha!"*** Yesu ametimiza maneno ambayo manabii walitabiri juu ya mateso na mauti ya Mkombozi mwenye haki! Miaka mia saba mbele ya kuja kwa Yesu duniani, nabii Isaya aliandika:

Everyday Publications Inc. @ 2010

> *"Wakamfanya [Masiya] kaburi pamoja na waovu; na pamoja na matajiri katika kufa kwake; hata yeye hakufanya jeuri, wala hila haikuonekana kinywani mwake. . .* ***Lakini aliumizwa kwa makosa yetu, alichubuka kwa maovu yetu. Azabu ya salama yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote, kama kondoo tumepotea; tumegeuka kila mmoja kwa njia yake mwenyewe; na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote!"*** (Isaya 53:9,5,6)

Wewe unayesikiliza leo, **unaamini manabii kweli kweli**? Unaamini ya kwamba Yesu ndiye aliyemaliza kazi ya wokovu ambayo manabii wa Mungu waliandika juu yake? Unafahamu sababu kwa mauti ya Mkombozi mwenye haki juu ya msalaba? **Wewe na mimi** ni sababu yenyewe! Alikufa kwa sababu ya zambi zetu, kama kondoo ya sadaka bila kipaku. Sisi tunastahili kupokea azabu ya milele

katika jehanum, lakini Mungu, kwa sababu ya mapendo yake makubwa kwa sisi, alituma Yesu (ambaye alimwita Mwana wake mpendwa) ili aweze kubeba azabu na hukumu kwa zambi zetu. Hili ndilo neno Maandiko Matakatifu yanatangaza, wakati yanaposema:

> *"Kwa maana ni ugumu kwa mtu kufa kwa ajili ya mtu wa haki: lakini inawezekana mtu kusubutu kufa kwa ajili ya mtu mwema.* ***Lakini Mungu anaonyesha mapendo yake kwetu, wakati tulipokuwa tungali wenye zambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu.*** (Waroma 5:7,8) *"Maana yeye asiyejua zambi [Mungu] alimfanya kuwa zambi kwa ajili yetu* ***ili sisi tuwe haki ya Mungu katika yeye.****"* (2 Wakorinto 5:21)

Utukufu uwe kwa Mungu, Mwenye Rehema, Mwenye Huruma . . . ***"Imekwisha!"*** Mungu ametimiza mfano wa sadaka ya Abrahamu {*Id al-Adha*}! Kwani kwa pahali Abrahamu alipotoa sadaka ya kondoo ndume kwa pahali pa mwana wake, Yesu, Mkombozi asiyekuwa na zambi, alikubali kutolewa kama sadaka kwa pahali petu— *"ili* ***kila mtu akimwamini*** *asipotee, lakini apate uzima wa milele!"* (Yoane 3:16)

Everyday Publications Inc
@ 2010

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya neno lenye maana sana, neno la uwezo kabisa ambalo Yesu alisema toka msalaba muda mfupi tu mbele ya kufa kwake. Alisema,

> ***"Imekwisha!"*** (Yoane 19:30)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Somo 85

# Yesu Amefufuka!

Matayo 28; Luka 24; Yoane 20

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele.

Ndani ya somo letu la mbele tuliona namna **Yesu Masiya alivyomwanga damu yake** juu ya msalaba pahali alipofungwa na misumari, kulipa kwa zambi za dunia na **kufungulia wenye zambi mlango wa salama ya milele.** Kila neno lilitokea namna manabii walivyotabiri: Masiya alizarauliwa, alipigwa fimbo na kufungwa juu ya msalaba na misumari. Kama kondoo ndume asiyekuwa na kosa alivyokufa kwa pahali pa mwana wa Abrahamu, Yesu, Mkombozi asiyekuwa na zambi, alikufa kwa pahali petu. Dakika mbele ya kufa kwake Yesu alilalamika, ***"Imekwisha!"*** Mungu asifiwe kwani Bwana Yesu ametimiza shauri la Mungu kwa wokovu wa watu!

Everyday Publications Inc @ 2010

Kufa kwa Masiya juu ya msalaba ni habari kubwa zaidi ndani ya Maandiko Matakatifu mazima, kwani ni kwa sababu ya mauti ile Mungu anaweza kutusamehe zambi zetu pamoja na kubaki mwenye haki yeye mwenyewe. Lakini, hata kama mauti ya Masiya ni **habari *kubwa* zaidi,** maneno ambayo tutasoma juu yao leo ni **habari za *kushangaza* zaidi,** kwani tutasikia namna **Mungu alivyofufua Yesu toka wafu.**

Kama tulivyosoma mbele, nyuma ya kufa kwa Yesu juu ya msalaba, askari alikamata mkuki na kuchoma mbavu za Yesu nayo, na kufungua njia kwa damu na maji kutoka, ndilo neno lililohakikisha ya kwamba alikuwa amekufa. Tuliona vilevile ya kwamba mtajiri mmoja alitwaa mwili wa Yesu na kuuweka ndani ya kaburi jipya ambalo alikuwa amechimba toka mawe kwa maiti yake mwenyewe. Jiwe kubwa lilifingirishwa kwa pahali pa kuingia kaburi. Maneno yote yalitokea namna manabii wa Mungu walivyotabiri.

Hivi, ndani ya Habari Njema imeandikwa:

(Matayo 27) *62 Basi kesho yake, iliyo siku nyuma ya Matengenezo, wakubwa wa makuhani na Wafarisayo walikusanyika kwa Pilato, 63 wakisema: Bwana, tunakumbuka ya kama yule mdanganyifu alisema wakati alipokuwa angali hai:* ***Nyuma ya siku tatu nitafufuka tena.*** *64 Agiza basi kaburi lilindwe hata siku ya tatu, wanafunzi wake wasije na kumwiba na kuwaambia watu: Amefufuka toka wafu; na udanganyifu wa mwisho utapita wa kwanza. 65 Pilato akawaambia: Muna askari walinzi; kwendeni mulilinde kwa kadiri munavyoweza. 66 Basi wakakwenda, wakalinda kaburi wakitia lile jiwe mhuri, pamoja na wale askari walinzi.*

(Matayo 28) *1 Basi wakati sabato ilipokwisha, ikipambazuka* ***siku ya kwanza ya juma****, Maria Magdalene na Maria mwingine wakakuja kuona kaburi. 2 Na tazama, palikuwa na tetemeko kubwa la inchi; kwani* ***malaika ya Bwana akashuka toka mbinguni, akakuja na kufingirisha jiwe toka mlango, akaketi juu yake****. 3 Na sura yake ilikuwa kama umeme, na mavazi yake meupe kama theluji. 4 Na kwa kumwogopa, wale walinzi wakatetemeka, wakakuwa kama wafu.*

Everyday Publications Inc.
@ 2010

Hivi wakati wanawake walipofika pahali pa maziko, (Luka 24) *2 wakaona jiwe limefingirishwa mbali na kaburi. 3 Wakaingia, lakini hawakuona mwili wa Bwana Yesu. 4 Na wakishangaa juu ya maneno haya, tazama, watu wawili wakasimama karibu nao, wamevaa nguo za kungaa sana. 5 Nao walikuwa na woga sana wakainama kifudifudi hata udongo, na wale waliwaambia:* ***Kwa nini munatafuta yeye aliye hai katikati ya wafu? 6 Hayuko hapa, lakini amefufuka****; kumbukeni namna alivyosema. . . 7 Imepasa Mwana wa watu kutiwa katika mikono ya watu wenye zambi na kusulibiwa, na kufufuka siku ya tatu. 8 Wakakumbuka maneno yake, 9 wakarudi toka kaburi, maneno haya yote wakawaambia wale kumi na mmoja, na wengine wote. 10 Maria Magdalene na Yoana na Maria mama ya Yakobo, na wanawake wengine pamoja nao, waliwaambia mitume mambo haya. 11 Maneno yao yalionekana kuwa bule kwao, wala hawakuwasadiki. 12 Lakini Petro akaondoka, akakwenda mbio hata kaburi, akasimama, akachungulia ndani, akaona vile vitambaa vimewekwa peke yao; akakwenda kwake akishangaa kwa maneno yaliyotokea.*

*13* ***Na tazama, siku ile ile wawili wao walikuwa wakikwenda hata kijiji jina lake Emau****, kilichokuwa mbali na Yerusalema kama mwendo wa saa mbili. 14 Nao wakazungumuza habari za maneno haya yote yaliyofanyika. 15 Walipokuwa wakizungumuza na*

*kuulizana,* ***Yesu mwenyewe alikaribia, akakwenda pamoja nao. 16 Lakini macho yao yalifungwa wasipate kumtambua.***

*17 Akawaambia: Maneno gani munayosemezana wakati munapotembea? Walisimama wenye huzuni. 18 Mmoja wao, jina lake Kleopa, akamjibu, akamwambia: Wewe mgeni peke yako katika Yerusalema, usijue maneno yaliyofanyika kule siku hizi? 19 Akawaambia: Maneno gani? Wakamwambia: Maneno ya Yesu wa Nazareti, aliyekuwa nabii, mwenye nguvu kwa tendo na kwa neno mbele ya Mungu na watu wote, 20 na namna wakubwa wa makuhani na maliwali yetu walivyomtoa kwa hukumu ya kufa, wakamsulibisha. 21 Lakini tulitumaini ya kuwa yeye atakomboa Israeli. Na tena juu ya maneno haya, leo ni siku ya tatu tangu yalipofanyika maneno haya yote. 22 Tena wanawake fulani wa kwetu walitushitusha, walikwenda kaburi asubui mapema. 23 Lakini hawakuona mwili wake, wakakuja, wakasema waliona maono ya malaika ambao waliwaambia ya kama yeye ni hai. 24 Tena wengine waliokuwa pamoja nasi, walikwenda kaburini, wakaona vivyo kama wanawake walivyosema, lakini hawakumwona. 25 Akawaambia:* ***Wenye upumbavu na wenye mioyo mizito katika kuamini yote ambayo walisema manabii****. 26* ***Haikupasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake?*** *27 Akaanza toka kitabu cha Musa na manabii yote, akawaelezea maana ya maneno yote yaliyoandikwa* ***juu yake****.*

Everyday Publications Inc @ 2010

*28 Wakakaribia kijiji walipokwenda; naye alifanya kama alitaka kwenda mbele. 29 Lakini wakamshurutisha, wakisema: Ukae pamoja nasi, kwani usiku unataka kuingia na mchana unakwisha sasa. Akaingia kukaa pamoja nao. 30 Ilikuwa alipokaa pamoja nao kula chakula, akatwaa mkate, akaubariki, akavunja, akawapa wale. 31 Macho yao yakafunguliwa, wakamjua; akatoweka asionekane nao. 32 Wakasemezana: Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu angali alipokuwa kusemezana nasi katika njia, na kutufunulia maana ya maandiko? 33 Wakakwenda saa ile ile, wakarudi Yerusalema, wakakuta wale mitume kumi na mmoja wamekusanyika, nao waliokuwa pamoja nao, 34 wakisema:* ***Kweli Bwana amefufuka, ameonekana na Simoni.*** *35 Nao wakawasimulia habari za maneno ya njia, na namna alivyotambuliwa nao kwa kuvunja mkate.*

*36 Na waliposema maneno haya,* ***Yesu mwenyewe akasimama katikati yao*** *akawaambia: Salamu kwenu. 37 Lakini wakafazaika, wakaogopa, wakazania ya kama waliona roho. 38 Yesu akawaambia: Munafazaika sababu gani? Na kwa nini mashaka yanatoka katika mioyo yenu? 39* ***Tazameni mikono yangu na miguu yangu*** *ya*

*kuwa ni mimi mwenyewe. Munipapase, mutazame; kwani roho haina mwili na mifupa, kama munavyoniona mimi kuwa nayo. 40 Aliposema vile akawaonyesha mikono yake na miguu yake. 41 Walikuwa hawakuamini kwa sababu ya furaha, wakishangaa, akawaambia: Muna kitu cha kula hapa? 42 Wakampa kipande cha samaki iliyopikwa, na asali kidogo. 43 Akatwaa, akakula mbele yao.*

*44 Kisha akawaambia: Haya ndiyo maneno yangu ambayo niliwaambia ninyi wakati nilipokuwa kwenu, ya kwamba **maneno yote yatatimizwa yaliyoandikwa juu yangu katika torati ya Musa, na katika manabii, na katika Zaburi.** 45 **Halafu akafungua akili zao wapate kufahamu maana ya maandiko.***

*46 **Akawaambia: Ndivyo ilivyoandikwa, na ndivyo ilivyopasa Kristo kuteswa na kufufuka toka wafu siku ya tatu.** 47 **Na maneno ya toba na kusamehe zambi yahubiriwe kwa jina lake katika mataifa yote, kwanza kutoka Yerusalema.** 48 **Nanyi ni washuhuda wa maneno haya.***

(Yoane 20) *24 Lakini Tomasi, mmoja wa wale kumi na wawili, anayeitwa Mpacha, hakuwa pamoja nao wakati alipokuja Yesu. 25 Basi wanafunzi wengine wakamwambia: Tumeona Bwana. Lakini akawaambia: Nisipoona katika mikono yake alama za misumari, na kutia mkono wangu katika mbavu zake, sitaamini hata kidogo.*

Everyday Publications Inc. © 2010

*26 Na nyuma ya siku nane wanafunzi wake walikuwa ndani tena, na Tomasi pamoja nao. Yesu akakuja, milango imefungwa, akasimama katikati, akasema: Salama kwenu. 27 Basi akamwambia Tomasi: Leta hapa kidole chako, na tazama mikono yangu. Na leta hapa mkono wako uutie katika mbavu zangu; usiwe asiyeamini, lakini mwenye kuamini. 28 Tomasi akajibu, akamwambia: **Bwana wangu, na Mungu wangu**. 29 Yesu akamwambia: Tomasi, kwa sababu umeniona, umeamini; **heri wale wasioona, lakini wameamini.***

*30 Basi alama nyingi nyingine Yesu alifanya mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki; 31 l**akini hizi zimeandikwa mupate kuamini ya kwamba Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mupate uzima kwa jina lake**.*

Kweli tumesoma habari za kutoa furaha kabisa leo! **Yesu alifufuka toka wafu!** Alishinda moja ya adui kubwa zaidi ya mtu: mauti. Kaburi halikuweza kumfunga. Siku ya tatu, Yesu alitoka ndani ya nguo ambazo alizikwa ndani yao, namna kipepeo kinavyotoka ndani ya kifuniko chake. Nguo za maziko tu zilibaki pahali mwili wa Yesu ulipolala. Bwana Yesu Kristo alifufuka ndani ya mwili wa utukufu

namna kila mtu ambaye anamwamini atapokea siku nyingine! Kwa sababu hii Maandiko yanasema:

> *"Lakini sasa Kristo amefufuliwa toka wafu, **malimbuko** yao waliolala. Maana kwa kuwa kufa kuliletwa na mtu, hivyo ufufuko wa wafu uliletwa na mtu. **Kwa sababu kama katika Adamu wote wanakufa, hivyo wote katika Kristo watapatizwa uhai!**"* (1 Wakorinto 15:20-22)

Ufufuko wa Yesu unahakikisha ya kwamba maneno Yesu aliyosema juu yake mwenyewe ni kweli. Unakumbuka ya kwamba Yesu alisema, ***"Mimi ni ufufuko na uzima. Yeye ambaye ananiamini, hata anapokufa, ataishi!"*** (Yoane 11:25) Yesu aliahidi kuleta uzima wa milele kwa wote ambao wanamwamini, lakini kama yeye mwenyewe asiposhinda mauti, namna gani angaliweza kuokoa wengine toka uwezo wa mauti na zambi na jehanum?

Labda **mfano huu** utasaidia. Mtoto anacheza ndani ya mawimbi kwa pwani ya bahari. Gafula maji yanampeleka kwa nguvu mbali na pwani. Anajaribu sana sana kurudia pwani, lakini inamshinda. Mtoto atakufa isipokuwa mtu mwingine anamponyesha. Kuna mwanamume kwa pwani anayeona mtoto, na kulalamika: "Usiogope. Nitakuponyesha!" Hivi mwanamume mwenyewe anaogelea kwa pahali mtoto alipokuwa, lakini uwezo wa mawimbi yanamshinda. Wao wawili, yeye na mtoto, wanazama. Mwanamume alikusudi kuponyesha mtoto lakini alikosa uwezo kutimiza makusudi yake. Uwezo wa mawimbo ulimshinda. Vivyo hivyo, tunasikia juu ya watu ambao wanajiita waokozi na kuwaambia watu: "Munifuate, muniamini, na mutafikia Paradiso." Wale wanaosema maneno namna hii wanakusudi yaliyo mema, lakini hawawezi kutimiza maneno wanayoahidi. Hawawezi kujiokoa wenyewe, kwa sababu hawawezi kushinda uwezo wa zambi na mauti. Uwezo wa mauti unawashinda kabisa, na wakati wanapokufa wanazikwa, miili yao itaoza ndani ya kaburi, na roho zao zitangojea siku ya hukumu.

Everyday Publications Inc @ 2010

Lakini haikuwa hivi na Bwana Yesu. **Yeye ni kweli Mwokozi kama alivyosema!** Maneno yote yalitokea namna alivyotabiri. Yesu alikufa kama sadaka kuondoa zambi, alizikwa, na halafu siku ya tatu, alitoka kaburini! Hakuna nabii ye yote hata mmoja aliyekufa, kuzikwa, na halafu kutoka kaburini asife tena kamwe! Lakini hili ndilo neno Yesu Masiya alilofanya! Alishinda mauti na kaburi! Alishinda zambi na Shetani na mauti na Hadeze! Na neno la ajabu zaidi ndilo ya kwamba **mtu ye yote anayeamini habari hizi njema**

**kweli kweli** juu ya kufa na ufufuko wa Yesu Kristo atashiriki ndani ya ufukufu wake kwa milele. Hili ndilo neno Bwana Yesu alilotangaza nyuma ya kufufuka toka wafu, akisema, ***"Usiogope, mimi ni wa kwanza na wa mwisho; na aliye hai; nami nilikuwa nimekufa, na tazama mimi ni hai hata milele na milele. Nami nina funguo za mauti, na za Hadeze!"*** (Ufunuo 1:17,18)

Mungu alifufua Yesu ili uweze kujua hakika ya kwamba yeye ni Mwokozi na Mwamuzi wa dunia, aliyewekwa na Mungu. Hii ndiyo maana ya maneno ambayo Maandiko yanasema:

> *"**Wala hakuna wokovu katika mwingine,** kwa maana hakuna jina lingine chini ya mbingu walilopewa watu tupate kuokolewa nalo! . . . [Mungu] ameweka siku wakati atakapohukumu dunia kwa haki, kwa mtu yule ambaye alimweka kwa kazi hii, **naye aliwapa watu wote hakika ya mambo haya kwa kumfufua toka wafu** . . . **Ukikiri kwa kinywa chako ya kuwa Yesu ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua toka wafu, utaokolewa! . . . Kila mtu anayeitia jina la Bwana ataokolewa!"*** (Matendo 4:12; 17:31; Waroma 10:9,13)

Everyday Publications Inc
@ 2010

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Mungu akitaka, ndani ya somo la nyuma tutaona namna Bwana Yesu alivyopanda mbinguni nyuma ya kutokea wanafunzi wake kwa muda wa siku makumi ine na kuhakikisha kwa njia mbalimbali ya kwamba yeye alikuwa hai. . .

Mungu akupe ufahamu kwa maneno yote uliyosikia leo, na tunakusihi kuwaza sana juu ya shairi hili toka Neno lake takatifu:

> ***[Yesu] "alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili tuhesabiwe haki."*** (Waroma 4:25)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 86

# Yesu Anakwenda Mbinguni

### Matayo 28; Luka 24; Matendo 1

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuja tena leo na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Kwa siku nyingi sasa tumesoma ndani ya Habari Njema takatifu {*Injil*}, ndicho kitabu ndani yake tunapata habari za Mwokozi mwenye uwezo wote, ndiye Yesu Kristo. Kama tulivyoona mbele, maana ya **Yesu** ni *Mungu anaokoa*. **Kristo** ni neno kwa Kiyunani kwa *Masiya* maana yake *Mpakaliwa wa Mungu.* Yesu Kristo ndiye Mungu ali*weka* ku**okoa** wana wa Adamu toka utawala wa zambi.

Lakini, kama tulivyoona, **zaidi ya watu hawakutambua kama Yesu alikuwa nani**. Wengine walifikili yeye ni nabii, lakini hawakufahamu ya kwamba yeye ndiye Neno la Mungu mwenyewe {*Kalimat Allah*} aliyekuja toka mbinguni na kutokea duniani kama mtu. Wengine, kama wakubwa wa makuhani na watawala wa Wayuda, walimwonea wivu sana na mwishoni walimwua kwa njia ya kumtundika juu ya msalaba. Lakini Mungu alishauri na kujua maneno haya yote mbele. Mauti ya Masiya juu ya msalaba yalipatana kabisa na shauri la Mungu alilotangaza zamani kwa njia ya manabii yake. Ndani ya somo la mbele tuliona ya kwamba Mungu alifufua Yesu tena siku ya tatu. Ufufuko wa Yesu unahakikisha ya kwamba Mungu alikubali damu ambayo Yesu alimwanga kulipa kabisa kwa wokovu wa wana wa Adamu toka uwezo wa zambi, woga wa mauti, na azabu ya jehanum.

Nyuma ya kufufuliwa toka wafu Yesu alionekana kwa wanafunzi wake, akawaonyesha alama za vilonda pahali askari walipoingiza misumari kwa mikono na miguu yake. Tunasoma vilevile ya kwamba Yesu alikula pamoja na wanafunzi wake kuhakikisha ya kwamba alikuwa hai kweli. Kitabu cha Habari Njema {*Injil*} kinapasha vilevile ya kwamba Yesu alionekana kwa wanafunzi wake katika muda wa siku makumi ine na alisema nao juu ya ufalme wa Mungu. Siku moja Yesu alionekana kwa zaidi ya 500 wa wanafunzi

Everyday Publications Inc @ 2010

wake (1 Wakorinto 15:6). Lakini neno linalohakikisha kupita maneno yote mengine ya kwamba Yesu ni hai leo ni ya kwamba anaishi ndani ya mioyo ya wale ambao wanamwamini na kunyenyekea amri yake.

Leo, Mungu akitusaidia, tutasikia juu ya **mamlaka kubwa ambayo Mungu alimpa Bwana Yesu** na tutaona **Yesu akilagana na wanafunzi wake na kupanda mbinguni.** Tutaanza kusoma leo ndani ya sura ya mwisho ya Habari Njema ya Matayo. Maandiko yanasema:

> (Matayo 28) *16 Lakini wale wanafunzi kumi na mmoja wakakwenda*
> *Galilaya, mpaka mlima ambao aliwaagiza Yesu. 17 Na wakati*
> *walipomwona, wakamwabudu; lakini wengine waliona shaka. 18*
> *Yesu akakuja kwao, akawaambia akisema: Nimepewa* ***mamlaka yote***
> *mbinguni na duniani. 19 Kwendeni basi mukafanye mataifa yote*
> *kuwa wanafunzi, mukiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la*
> *Roho Mtakatifu; 20 mukiwafundisha kushika maneno yote ambayo*
> *niliwaamuru ninyi; na tazama, mimi ni pamoja nanyi siku zote hata*
> *mwisho wa dunia.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

Ulisikia neno Yesu alilosema na wanafunzi? Alisema nao, "***Nimepewa mamlaka yote*** *mbinguni na duniani. Kwendeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi."* Kwa nini Yesu alisema alikuwa na mamlaka yote mbinguni na duniani?

Ndani ya mafundisho yetu katika Torati ya Musa tuliona namna Mungu alivyoumba mwanamume wa kwanza. Tulisoma ya kwamba Mungu alimpa Adamu mamlaka kutawala juu ya kila kitu Mungu alichokwisha kuumba. Mungu alitaka Adamu kuishi pamoja naye na kutawala pamoja naye kwa milele. Lakini Adamu alipotewa mamlaka ile siku alipoasi agizo la Mungu na alipokula tunda la mti wa kujua uzuri na ubaya. Adamu ni babu yetu na kwa sababu hii sisi vilevile tumepotewa mamlaka ya kuishi na kutawala pamoja na Mungu. Kama Adamu, sisi sote ni wenye zambi, tumezaliwa ndani ya ufalme wa zambi, mbali na Mungu na utukufu na enzi yake.

Lakini tunasifu Mungu, kwa sababu Maandiko ya Manabii yanaonyesha ya kwamba Mungu alitayarisha njia kwa wana wote wa Adamu, **mlango** kwa njia yake waliweza kurudi karibu na Mungu na kushiriki katika utukufu na ufalme wake. **"Mlango"** huyu ni **Masiya mtakatifu** aliyetoka mbinguni kumwanga damu yake kama sadaka kusafisha watu toka zambi zao na kuwarudisha karibu na Mungu. Yesu Masiya alijaribiwa kama Adamu, lakini Yesu haku-

fanya zambi. Alikuwa mkamilifu na mtakatifu, kama Mungu ni mkamilifu na mtakatifu. Kwa sababu hii Mungu hakuwa na haya kumwita **Mwana wake**. Hivi wakati Yesu alipokwisha kutoa uzima wake kama sadaka kuondoa zambi, Mungu alimfufua toka wafu, akamweka kuwa Bwana juu ya vyote na kumpa *"mamlaka yote mbinguni na duniani."*

Labda wengine wangependa kuuliza, "Kama Yesu ni Bwana juu ya vyote, kwa sababu gani dunia yetu hii inakaa kujaa taabu na zambi?" Maandiko Matakatifu yanajibu ulizo hili wakati yanaposema:

> *"Kwa sababu kama **katika Adamu** wote wanakufa, hivyo wote **katika Kristo** watapatizwa uhai. Lakini kila mtu kwa pahali pake; Kristo malimbuko; kisha watu wa Kristo kwa kutokea kwake. Halafu mwisho utakuja, wakati atakapotoa ufalme kwa Mungu Baba; atakapoondosha utawala wote, na mamlaka yote, na uwezo wote."* (1 Wakorinto 15:22-24) *"Naye **atapungusa** kila chozi katika macho yao; wala mauti **haitakuwa** tena; wala maombolezo, wala kilio, wala uchungu hautakuwa tena; kwa maana maneno ya kwanza yamekwisha kupita."* (Ufunuo 21:4)

Everyday Publications Inc
@ 2010

Kwa njia ya mashairi haya na mashairi mengi mengine ndani ya Neno la Mungu tunajifunza ya kwamba Mungu amempa Yesu mamlaka yote ili aweze kutawala maneno yote, na kuhukumu kila mtu. Lakini kufika sasa hayaanza kutawala kila kitu, wala hayahukumu watu wa dunia. Siku nyingine Yesu atarudi duniani. Wakati atakaporudi, ataanza kutawala dunia hii na kufanyiza maneno yote kuwa mapya tena.

Hivi, si neno kama wewe ni nani au kama ukiwa pahali gani, Mungu anakuagiza ku**tubu** zambi zako, kugeuka kwake na **kuamini** Habari Njema ya wokovu inayotegemea mauti na ufufuko wa Bwana Yesu Kristo. Ukiamini kweli kweli, Mungu atasamehe zambi zako zote kwa jina la Yesu, atafanyiza mpya moyo wako kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, na kukupa salama na Mungu kwa milele. Ukiamini Kristo, atakuja kwako kwa njia ya Roho Mtakatifu wake na kusimamisha **ufalme wake ndani ya moyo wako**. Yesu hatageuza dunia kufika wakati atakaporudi yeye mwenyewe kuihukumu. Lakini anaweza kukugeuza wewe leo! Utamruhusu kusimamisha ufalme wake ndani ya moyo wako?

Rafiki, Mungu ametuma kwako Mwokozi anayeweza kuondoa zambi zako na kukupa moyo ulio mpya na safi. Unaweza **kujua** ya kwamba utashinda milele pamoja na Mungu katika utukufu wa

Paradiso, kama **ukiamini** kweli juu ya Yesu Kristo, Mwokozi wa dunia! Lakini kama **ukiona bule** Mwana wa Mungu ambaye Mungu alituma, atageuka Mwamuzi wako siku nyingine! Haya ndiyo maneno Maandiko yanayosema kwa 2 Watesalonika 1:7-10,

> *". . . wakati wa ufunuo wa Bwana Yesu kutoka mbingu pamoja na malaika za uwezo wake, katika moto wa kuwaka* ***akiwalipa kisasi wao wasiojua Mungu, na wao wasiotii Habari Njema ya Bwana wetu Yesu Kristo****; na watakaoazibiwa kwa uharibifu wa milele na kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake, wakati atakapokuja kutukuzwa katika watakatifu wake, na kushangiliwa katika wote walioamini!" (*2 Watesalonika 1:7-10)

Rafiki, Neno la Mungu ni wazi. Linatupasha ya kwamba mtu ye yote **anayeamini** kwelikweli Habari Njema juu ya mauti ya Yesu Kristo juu ya msalaba na juu ya ufufuko wake toka wafu ataokolewa! Lakini, mtu ye yote **asiyeamini atahukumiwa**! Yesu alimwanga damu yake kama sadaka inayoweza kufutia mbali deni yako ya zambi kwa milele. Lakini damu ambayo Yesu alimwanga kwa wewe haina faida kama usipoamini kwelikweli moyoni mwako. Kwa sababu Maandiko yanasema:

Everyday Publications Inc @ 2010

> *"Kwa maana Mungu alivyopenda ulimwengu, hata kutoa Mwana wake wa pekee, ili* ***kila mtu akimwamini asipotee,*** *lakini apate uzima wa milele. . .* ***asiyemwamini amekwisha kuhukumiwa****, kwa sababu hakuamini jina la Mwana wa pekee wa Mungu."* (Yoane 3:16,18)

Ndiyo, ukiamini Habari Njema ya Yesu Kristo, uta**okolewa**, lakini kama usipoamini, uta**potea** katika zambi zako. Hili ndilo neno la wokovu ambalo Mungu alituma kwa wana wa Adamu. Kwa sababu hii Yesu aliagiza wanafunzi wake, akisema: *"Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Kwendeni basi mukafanye mataifa yote kuwa wanafunzi."* (Matayo 28:18,19)

Sasa tuendelee na habari hizi. Yesu alionekana kwa wanafunzi wake kwa siku zaidi ya makumi ine nyuma ya kufufuliwa toka wafu. Maandiko yanasema:

> (Matendo 1) *4 Hata, akikutana nao [wanafunzi wake] akawaagiza wasitoke Yerusalema, ila wangoje ahadi ya Baba muliyosikia kwangu; 5 kwani Yoane alibatiza kwa maji, lakini ninyi mutabatizwa katika* ***Roho Mtakatifu*** *nyuma ya siku si nyingi."*

Ulisikia maneno Yesu aliyosema? Tumesoma mbele (ndani ya Habari Njema ya Yoane 14-16) ya kuwa Yesu aliahidi wanafunzi wake kwamba Baba yake mbinguni atatuma kwao Msaidizi mwingine, Roho Mtakatifu, atakayekaa ndani ya mioyo yao, akiwasafisha, akiwapatisha nguvu, na kuwaingiza katika kweli yote. Sasa tunasikia Yesu akiagiza wanafunzi wake kungoja katika Yerusalema kwa Roho Mtakatifu atakayekuja nyuma kidogo. Ndani ya somo letu la nyuma, Mungu akitaka, tutaona namna Roho Mtakatifu alivyoshuka kujaza mioyo ya wanafunzi wote wa Yesu, kama alivyoahidi.

Tusome sasa namna Yesu alivyoondokea wanafunzi wake na kupanda mbinguni. Maandiko yanasema:

> (Matendo 1) *6 Wakati walipokutanika, wakamwuliza, wakisema: Bwana, utarudishia Waisraeli ufalme wao tena wakati huu? 7 Akawaambia: Si maneno yenu kujua nyakati wala majira Baba aliyoweka katika mamlaka yake mwenyewe. 8 Lakini mutapokea nguvu wakati Roho Mtakatifu anapokuja juu yenu, nanyi mutakuwa washuhuda wangu katika Yerusalema, na katika Yudea yote, na Samaria, hata mpaka wa dunia.*
>
> *9 Akikwisha kusema maneno haya,* ***akanyanyuliwa, nao wakitazama, wingu likampokea toka macho yao.*** *10 Wakati walipokuwa wakikaza macho mbinguni, yeye alipokuwa akikwenda zake, tazama, watu wawili wenye nguo nyeupe walisimama karibu nao, 11 wakasema: Ninyi watu wa Galilaya, kwa sababu gani mumesimama mukitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa toka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja namna hii sawasawa mulivyomwona akikwenda zake mbinguni."*

Everyday Publications Inc
@ 2010

Hivi Yesu alipanda mbinguni na kurudia nyumba ya Baba yake ambayo aliiondokea karibu miaka makumi tatu na tatu mbele. Kweli kwenda kwake kulikuwa kwa enzi mbele ya macho ya wanafunzi wake wachache. Bila shaka Yesu huyu ambaye walikuwa wamemfuata kwa miaka mitatu alikuwa kweli Masiya ambaye manabii walitabiri juu yake! Ndani ya kuzaliwa kwake, maisha yake, mauti, maziko na ufufuko na kwenda kwake mbinguni—Yesu wa Nazareti **alikuwa ametimiza** maneno yote ambayo manabii walitabiri juu yake, hata kupanda mbinguni kama nabii Daudi alivyotabiri ndani ya Zaburi.

Rafiki, unajua pahali Bwana Yesu ni leo? Maandiko Matakatifu

yanatujulisha ya kwamba *"Yesu Kristo . . . aliye kwa mikono wa kuume wa Mungu, akiwa amekwenda mbinguni: malaika na mamlaka na nguvu zikikwisha kutiishwa chini yake."* (1 Petro 3:21,22) Ndiyo, Yesu ni mbinguni, kwa mkono wa kuume wa Mungu na viumbe vyote wanatiishwa mbele yake. **Wote walio kweli watu wa Mungu wanatiishwa mbele ya Bwana Yesu.** Basi wewe? Umejiweka chini ya Yesu Masiya, yule aliyechaguliwa na Mungu kuwa Mwokozi na Mwamuzi wa dunia?

Kama tulivyosoma sasa tu, wakati Bwana Yesu alipokwisha kupanda na kurudi mbinguni, malaika wawili walionekana kwa wanafunzi wake, wakasema nao, *"kwa sababu gani mumesimama mukitazama mbinguni? **Huyu Yesu aliyechukuliwa toka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja namna hii sawasawa mulivyomwona akikwenda zake mbinguni.**"* Ndiyo, siku nyingine Yesu Kristo atarudi katika mawingu. Wewe ni tayari kwa kurudi kwake? **Siku ile watu wote watamwona, na kila mtu atajua ya kwamba yeye ndiye Mungu alimweka kuwa Mwokozi, na Mwamuzi wa dunia!** Hii ndiyo maana ya Maandiko katika Wafilipi 2, kuanza na shairi 6:

Everyday Publications Inc
© 2010

> (Wafilipi 2) *6 Ndiye aliyekuwa na namna ya Mungu, hakuona kuwa sawa na Mungu kuwa kitu cha kushikamana nacho, 7 lakini alijifanya mwenyewe kuwa hana utukufu, akitwaa namna ya mtume, akakuwa na mfano wa mtu; 8 naye akionekana na sura ya mtu, alijinyenyekeza mwenyewe, akakuwa mwenye kutii hata mauti, ndiyo mauti ya msalaba. 9 Kwa hivi Mungu vilevile alim**tukuza sana**, na kumpa **jina lililo juu ya kila jina;** 10 hata kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni na vya duniani, na chini ya dunia, 11 na **kila ulimi** ukiri ya kuwa Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba.*

~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Rafiki, inatupasa kuacha hapa kwa leo, lakini ndani ya somo la nyuma tutasoma namna Mungu alivyotuma Roho Mtakatifu kuishi ndani ya moyo wa kila mtu anayepokea Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wake.

Mungu akubariki wakati unapokaa kukumbuka neno ambalo malaika wawili waliwaambia wanafunzi:

> ***"Huyu Yesu aliyechukuliwa toka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja namna hii sawasawa mulivyomwona akikwenda zake mbinguni."*** (Matendo 1:11)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 87

# Roho Mtakatifu Amekuja

### Matendo 1,2

Salama kwako, rafiki. Ni furaha kuweza kuendelea leo na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Kwa masomo machache yanayopita ndani ya Habari Njema {*Injil*} tumesikia **namna Bwana Yesu alivyotimiza maneno yote ambayo manabii wa Mungu waliandika miaka mingi mbele juu ya kufa na ufufuko wa Masiya.** Tulisoma ya kwamba Yesu alimwanga damu yake takatifu juu ya msalaba ambao alifungwa juu yake na misumari, kulipa deni ya zambi kwa wana wa Adamu. Tuliona ya kwamba alishushwa toka msalaba na kuwekwa ndani ya kaburi. Lakini, siku ya tatu, Mungu alimfufua toka wafu! Nyuma ya ufufuko wa Yesu, alionekana kwa wanafunzi wake kwa siku makumi ine, akihakikisha mbele yao ya kwamba yeye ni hai kweli kweli. Halafu ndani ya somo la mwisho tuliona Yesu akipanda mbinguni mbele ya macho ya wanafunzi wake.

Everyday Publications Inc
@ 2010

**Unakumbuka neno la mwisho Yesu aliloagiza wanafunzi wake mbele ya kupanda mbinguni yeye mwenyewe?** Tusome tena maneno aliyosema:

> (Matendo 1) *4 . . . akawaagiza wasitoke Yerusalema, ila* ***wangoje ahadi ya Baba*** *muliyosikia kwangu; 5 kwani Yoane alibatiza kwa maji, lakini ninyi* ***mutabatizwa katika Roho Mtakatifu*** *nyuma ya siku si nyingi. . . 8* ***Mutapokea nguvu wakati Roho Mtakatifu anapokuja juu yenu, nanyi mutakuwa washuhuda wangu katika Yerusalema, na katika Yudea yote, na Samaria, hata mpaka wa dunia.*** *9 Akikwisha kusema maneno haya, akanyanyuliwa, wao wakitazama, wingu likampokea toka macho yao. 10 Walipokuwa wakikaza macho mbinguni, yeye alipokuwa akikwenda zake, tazama, watu wawili wenye nguo nyeupe wakasimama karibu nao, 11 wakisema: Ninyi watu wa Galilaya, kwa sababu gani mumesimama muk-*

*itazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa toka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja namna hii sawasawa mulivyomwona akikwenda zake mbiunguni.*

Hivi Yesu aliachana na wanafunzi wake, akarudia Paradiso pahali alipotoka kufika duniani, akaketi kwa mkono wa kuume wa Mungu. Yeye ni pale hata leo, akingojea saa atakaporudi kuhukumu dunia kwa haki.

Ulisikia maneno Yesu aliyoagiza wanafunzi wake mbele ya kupanda mbinguni? Aliwaagiza kukaa katika Yerusalema kufika wakati Roho Mtakatifu atakayetoka mbinguni atakapokuja juu yao. Labda ungali unafazaika na kuuliza: **Roho Mtakatifu ni nani?** Roho Mtakatifu ni Roho ya Mungu na Roho ya Yesu. Yeye ni mmoja nao na hata hivi mbalimbali nao. Ndiye aliyeongoza manabii kuandika na kutangaza Neno la Mungu zamani. Roho Mtakatifu ndiye Roho ya Mjuu sana aliyekuja juu ya bikira jina lake Maria na kumwezesha kuzaa Mtoto mtakatifu Yesu. Yeye ndiye Msaidizi ambaye Yesu aliahidi wanafunzi wake wakati aliposema nao,

Everyday Publications Inc @ 2010

*"Nitaomba Baba, naye atawapa ninyi Msaidizi mwingine, akae nanyi hata milele, Roho ya kweli ambaye dunia hawezi kumpokea, kwani haimwoni wala haimjui; lakini ninyi munamjua; kwa sababu anakaa pamoja nanyi, naye atakuwa ndani yenu."* (Yoane 14:16,17)

Sharti tufahamu vizuri maneno Yesu aliyoahidi wanafunzi wake juu ya Msaidizi huyu, kwa sababu kwa wakati wa sasa watu wengine wanataka watu kuamini ya kwamba Yesu alitangaza kwamba nabii mwingine atakuja. Lakini yule Msaidizi ambaye Bwana aliahidi hawezi kuwa mtu, kwa sababu Yesu alisema wazi ya kwamba Msaidizi alikuwa **Roho,** na **hakuna mtu ambaye ataweza kumwona**, na ya kwamba **ataishi ndani ya wanafunzi wa Kristo kwa milele**. Hivi Roho Mtakatifu ni nani? Ni Roho ya Mungu ambaye Mungu anaweka ndani ya mioyo ya wote wanaoamini Masiya. Anawazaa mara ya pili, anawasafisha, anawapatisha nguvu, na anawaweka kuwa mali yake.

Leo tutaona Mungu akitolea wanafunzi wa Yesu Roho Mtakatifu siku ya Pentekote. Pentekote ndiyo siku kubwa moja Mungu aliyosimamisha kwa Waisraeli kwa wakati wa nabii Musa. Unaweza kusoma juu yake ndani ya Tora. Siku ile Waisraeli walishukuru Mungu kwa usitawi waliopata kwa njia ya mavuno ya ngano yao. Lakini siku kubwa ya Pentekote ilikuwa na maana hata kubwa kupita.

Mungu alichagua siku ya Pentekote zamani kuwa siku atakapotuma Roho Mtakatifu kuishi ndani ya wana wote wa Adamu wanaoamini Masiya kweli kweli. Siku kubwa ya Pentekote ilikuwa siku 50 nyuma ya siku kubwa ya Pasaka; vivyo hivyo Mungu alikusudi kutuma Roho Mtakatifu siku 50 nyuma ya kufa na ufufuko wa Yesu Masiya.

Sasa tuendelee ndani ya Neno la Mungu kuona nini ilitokea wakati Yesu alipokwisha kulagana na wanafunzi wake na kurudi mbinguni. Maandiko yanasema:

> (Matendo 1) *12* ***Kisha [wanafunzi wa Yesu] wakarudia Yerusalema toka mlima ulioitwa Zeituni,*** *ulio karibu na Yerusalema kama kilomètre moja. 13 Wakati walipoingia walipanda chumbani mwa juu walipokuwa wakikaa; Petro na Yoane, na Yakobo, na Anderea, Filipo na Tomasi, Bartolomayo, na Matayo, Yakobo, mwana wa Alfayo, na Simoni-Zelote, na Yuda wa Yakobo. 14 Hawa wote walishinda katika kuomba kwa moyo moja, pamoja na wanawake, na Maria mama ya Yesu, na ndugu zake.*
>
> (Matendo 2) 1 ***Hata ilipotimia siku ya Pentekote walikuwa wote na moyo mmoja pahali pamoja.*** *2 Gafula uvumi ukatoka mbinguni kama wa upepo unaovuma na nguvu sana, ukajaza nyumba yote walipokuwa wameketi. 3 Na zilionekana kwao ndimi kama za moto, zilizogawanyika zikawakalia kila mmoja wao. 4* ***Wakajazwa wote Roho Mtakatifu*** *wakaanza kusema kwa lugha nyingine kama Roho Mtakatifu alivyowapa kusema.*
>
> *5 Na walikuwa katika Yerusalema Wayuda wakikaa, watu wenye haki toka mataifa yote chini ya mbingu. 6 Basi, sauti hii iliposikiwa, makutano walikusanyika, wakafazaika, kwa sababu kila mmoja aliwasikia wakisema lugha yake mwenyewe. 7 Wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana: Si hawa wote wanaosema Wagalilaya? 8 Kwa namna gani basi sisi tunasikia kila mtu kwa lugha yetu tuliyozaliwa nayo? 9 Waparti na Wamedi, na Waelamu, nao wanaokaa Mesopotamia, Yudea na Kapadokia, Ponto na Asia, 10 Furugia na Pamfilia, Misri, na pande za Libia karibu na Kurene, na Waroma wageni, Wayuda na wageuzi, 11 Wakrete na Waarabu: tunawasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makubwa ya Mungu. 12 Wakashangaa wote wakaingiwa na mashaka, wakaambiana: Maana ya neno hili nini? 13 Wengine walizihaki, wakisema: Wamelewa na mvinyo mpya.*
>
> *14* ***Lakini Petro akasimama pamoja na wale kumi na mmoja, akapaza sauti yake, akawaambia:*** *Ninyi wanaume wa Yudea, na ninyi wote munaokaa katika Yerusalema: neno hili liju-*

Everyday Publications Inc © 2010

*likane kwenu, musikilize maneno yangu. 15 Kwani watu hawa hawalewi kama munavyozania, kwa sababu ni saa tatu ya mchana; 16 lakini neno lile ndilo lililosemwa na nabii Yoeli: 17 Itakuwa katika siku za mwisho, Mungu anasema, Nitamwanga Roho Mtakatifu yangu juu ya watu wote. Na wana wenu na binti zenu watatabiri, na vijana vyenu wataona maono, na wazee wenu wataota ndoto: 18 na katika siku zile nitamwanga Roho yangu juu ya watumishi wangu, wanaume na wanawake, nao watatabiri. . . . 21 Na itakuwa kila mtu anayeita jina la Bwana ataokolewa.*

*22 Ninyi wanaume wa Israeli, sikieni maneno haya: Yesu wa Nazareti, mtu aliyeonyeshwa kwenu na Mungu kwa matendo ya uwezo, maajabu na alama alizofanya Mungu kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenyewe munavyojua; 23* ***huyu alitwaliwa nanyi kwa shauri lililokusudiwa, na kwa kujua kwa Mungu tangu zamani, nanyi mulimsulibisha, mukamwua kwa mikono ya watu wabaya. 24 Lakini Mungu alimfufua****, akilegeza uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao.*

*25 Maana [nabii] Daudi anasema juu yake: Niliona Bwana mbele yangu siku zote, kwa kuwa yuko kwa mkono wangu wa kuume, nisitikisike. 26 Kwa hili, moyo wangu ulipendezwa, ulimi wangu ukafurahi; tena mwili wangu nao utakaa katika matumaini. 27 Kwa maana hutaniacha roho yangu katika Hadeze, wala hutatoa Mtakatifu wako aone uharibifu. . .*

Everyday Publications Inc
© 2010

*29 Ndugu, muniruhusu niseme pasipo woga mbele yenu habari za baba yetu mkubwa, Daudi, ya kuwa alikufa, akazikwa, na kaburi lake ni kwetu hata leo. 30 Basi kwa sababu alikuwa nabii, akajua ya kuwa Mungu alimwapia kwa kiapo, ya kwamba toka uzao wake, kwa namna ya mwili, atanyanyua Kristo akae katika kiti chake cha ufalme. 31 Akitangulia kuona maneno haya, alisema habari za ufufuko wake Kristo, ya kama nafsi yake haikuachwa katika Hadeze wala mwili wake haukuona uharibifu.*

*32 Huyu Yesu, Mungu alimfufua, na sisi sote tuko washuhuda wake. 33 Basi akikwisha kupandishwa hata mkono wa Mungu, na kupokea kwa Baba ahadi ile ya Roho Mtakatifu, amemwanga hili munaloona sasa, na kulisikia. 34 Maana Daudi hakupanda katika mbingu lakini yeye mwenyewe alisema: "Bwana alimwambia Bwana wangu, Keti kwa mkono wangu wa kuume hata niweke adui zako chini ya miguu yako ... 36* ***Basi kila nyumba yote ya Israeli ijue kwa kweli, Mungu amefanya huyu Yesu ambaye mulimsulibisha kuwa Bwana na Kristo.***

> *37 Wakati waliposikia maneno haya wakachomwa katika mioyo yao, wakawaambia Petro na mitume wengine: Ndugu zetu, tutafanya nini? 38 Petro akawaambia: Tubuni mukabatizwe kila mmoja* ***kwa jina lake Yesu Kristo, mupate ondoleo la zambi zenu, nanyi mutapokea zawadi ya Roho Mtakatifu.*** *39 Kwa sababu ahadi hii ni kwa ajili yenu, na watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu. 40 Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi, na kuwaonya, akisema: Mujiponyeshe wenyewe na kizazi hiki kipotevu.* Amina.

Msikilizaji mwenzangu, ulisikia hotuba ya Petro vizuri? Kwa ufupi alitangaza kwa makutano katika Yerusalema ya kwamba Mungu alikuwa Masiya, Yesu, kama alivyoahidi miaka mingi mbele kwa njia ya manabii yake. Petro aliwaambia: Mulizarau Masiya ambaye Mungu alituma toka mbinguni! Mulimwua kwa njia ya kumfunga juu ya msalaba na misumari, lakini Mungu alimfufua toka wafu. Sisi sote ni washuhuda wa neno hili! Mungu ametukuza Yesu kwa mkono wake wa kuume na ametuma Roho Mtakatifu ambaye aliahidi kutuma! Mutubu na kugeuka kwa Mungu! Mwamini habari za manabii! Mwamini Yesu aliyewekwa na Mungu kuwa Mwokozi na Mwamuzi wa dunia! ***"Huyu manabii yote wanamshuhudia ya kwamba kwa jina lake kila mtu ambaye anamwamini atapewa usamehe wa zambi!"*** (Matendo 10:43)

Everyday Publications Inc. © 2010

Hivi mtume Petro alitangaza **Habari Njema ya wokovu** kwa njia ya imani kwa Yesu Masiya. Wakati makutano waliposikia maneno ya Petro, waliumia sana mioyoni mwao kwa sababu walifahamu sasa ya kwamba Yesu wa Nazareti, ambaye walimfunga juu ya msalaba, alikuwa Bwana wa Utukufu toka mbinguni! Yesu huyu, ambaye walimzarau na kuchukia, alikuwa Masiya ambaye Mungu aliahidi miaka mingi mbele kwa njia ya manabii yake! Hivi, siku ile, watu wengi **walitubu** zambi zao, wakageuka kwa Mungu na **kuamini** jina la Bwana Yesu Kristo. Wanafunzi hawa wapya walibatizwa ndani ya maji kama ushuhuda mbele ya watu wengine ya kwamba walikuwa wamesafishwa toka zambi kwa njia ya kuamini mauti, kuzikwa na kufufuliwa kwa Yesu Kristo. Ubatizo ndani ya maji haukuwasafisha toka zambi zao—ulikuwa **alama tu** ya kwamba walikuwa wamesafishwa ndani**, rohoni.**

Hivi, Maandiko Matakatifu yanasema:

> *"Nao waliopokea neno lake kwa furaha wakabatizwa; na siku ile wakazidishwa watu kama elfu tatu. Walikuwa wakidumu katika*

> ***mafundisho ya mitume*** *na katika* ***ushirika****, na katika* ***kuvunja mkate*** *na* ***kuomba****. . . . Na wanafunzi walijaa furaha na Roho Mtakatifu."* (Matendo 2:41,42; 13:52)

Hivi, siku ile ya Pentekote, **kanisa**—kusanyiko la wale walioamini Yesu Kristo—lilizaliwa. Kanisa la Yesu Kristo si jengo wala dini. Neno kwa kanisa kwa lugha ya Kiyunani ni *"Ekklesia"*, maana yake *"wale walioitwa kutoka."* Kama kwa wakati wa sasa kuna waamini wa kweli na wa uwongo duniani, kuna kanisa la kweli na kanisa la uwongo. Kanisa la kweli la Yesu Kristo ndio watu wote ambao tangu siku ile ya Pentekote walihamishwa toka **jamaa ya Adamu** kuingia **jamaa ya Kristo** kwa njia ya kuamini na imani ya kweli ndani ya sadaka kamilifu na iliyotimia ya Kristo.

Matukio ya Pentekote tuliyosikia juu yao leo yalitokea karibu miaka elfu mbili mbele. Hivi labda wengine wanasema: "Habari hizi si neno kwangu! Mimi si mmoja wa watu wale waliosulibisha Masiya! Wayuda na Waroma walimsulibisha! Sina neno na habari hizi hata kidogo!" Lakini Neno la Mungu linatuambia ya kwamba Masiya *"aliumizwa kwa makosa* ***yetu****, alichubuka kwa maovu* ***yetu!****"* (Isaya 53:5) **Zambi zetu** ndizo sababu ya mauti yake. Ni kwa sababu ya makosa yetu Mungu alikubali watu kusulibisha Mwana wake mpendwa! **Watu walisulibisha Yesu, lakini Mungu alimfufua toka wafu, kuwa Mwokozi** wa wote **wanaoamini,** na **Mwamuzi** wa wote **wasioamini.** Hivi Maandiko yanatangaza:

Everyday Publications Inc.
© 2010

> *"Sasa [Mungu] ameamuru watu wote pahali po pote watubu, kwa maana ameweka siku wakati atakapohukumu dunia kwa haki, kwa mtu yule ambaye alimweka kwa kazi hii, naye aliwapa watu wote hakika ya mambo haya kwa kumfufua toka wafu."* (Matendo 17:30,31)

Waza sana juu ya maneno haya, kwa sababu **neno unalofanya juu yao litachagua pahali gani utakapokaa kwa milele.**

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Mungu akubariki wakati unapofikili juu ya neno Petro, mtume wa Kristo alilotangaza, akisema, ***"Huyu [Yesu] manabii yote wanamshuhudia ya kwamba kwa jina lake kila mtu ambaye anamwamini atapewa usamehe wa zambi . . . na . . . zawadi ya Roho Mtakatifu!"*** (Matendo 10:43; 2:38)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 88

# Yesu Atarudi Tena!

## Ufunuo 19-22

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuja tena leo na mfulizo *Njia ya Haki.*

Tumefika leo kwa somo la 88 ndani ya **mafundisho yetu ya Neno la Mungu kwa taratibu ya miaka**. Kama tulivyoona, ndani ya muda wa mia za miaka Roho ya Mungu aliongoza manabii kupita makumi tatu kuandika sehemu ya kwanza ya Maandiko Matakatifu, ndiyo Tora, Zaburi, na vitabu vya manabii. Sehemu ya kwanza ya kitabu cha Mungu inaitwa **Agano la Kale.** Ndani ya sehemu ile, manabii wote walitangaza neno moja, ndilo ya kwamba Mungu ni mtakatifu na mwenye haki, na hivi inampasa kuhukumu kila zambi. Lakini, Mungu ni mwenye rehema nyingi vilevile na hataki wana wa Adamu kupotea katika zambi zao. Hivi tuliona namna Mungu, kwa njia ya manabii wake, aliahidi kwamba Mkombozi atakuja, Masiya Mtakatifu, atakayezaliwa na bikira, kuishi maisha matakatifu, na halafu kumwanga damu yake juu ya msalaba kulipa kwa zambi za wana wa Adamu. Manabii wote wa Agano la Kale waliandika juu ya Masiya huyu atakayekuja.

Everyday Publications Inc @ 2010

Ndani ya sehemu ya pili ya Maandiko Matakatifu, **Agano Jipya,** Kitabu cha Habari Njema, tuliona ya kwamba wakati saa iliyochaguliwa na Mungu ilipokuwa imefika, Mungu alileta Masiya, Mwokozi wa dunia, kama alivyoahidi kwa njia ya manabii wake. Masiya alikuwa Yesu wa Nazareti—Mwenye ukamilifu kabisa aliyeishi duniani tangu zamani. Yesu alijaa uwezo wa Mungu, kwa sababu alikuwa Neno la Mungu kabisa kwa mwili wa mtu. Mungu alisema juu yake, *"Huyu ni Mwana wangu, mpenda wangu, ninapendezwa naye!"* (Matayo 3:17) Lakini wanaume wenzetu waliua Mtakatifu wa Mungu kwa njia ya kumfunga juu ya msalaba. Lakini Mungu ali-

mfufua tena siku ya tatu. Nyuma yake washuhuda wengi walimwona, na Mungu alimtukuza na kumpa pahali pa juu zaidi mbinguni. Lakini huu si mwisho wa habari zake.

Habari za ajabu za njia ya haki ya wokovu wa Mungu zina mwanzo na mwisho. **Dunia hii mbovu itaona maneno mengine juu ya Yesu Masiya!** Neno la Mungu linatupasha ya kwamba Bwana Yesu atarudi tena duniani kutupa Shetani na malaika zake mabaya ndani ya ziwa la moto, kuhukumu wana wa Adamu siku ya hukumu, na kuumba tena dunia hii ya zamani. Somo letu la leo linaitwa "**Yesu atakuja tena!**"

Tutasoma ndani ya sehemu ya mwisho ya Agano Jipya, toka kitabu kinachoitwa ***Ufunuo***. Ufunuo ni kitabu chenye habari za ndani ndani, za uwezo mkubwa, kwa sababu kinatangaza maneno yatakayotokea kwa wakati wa mwisho, wakati dunia hii (muda wa sasa) itakapokwisha. Kitabu cha Ufunuo kina sura 22, sura zinazotangaza kushinda kwa utukufu kwa wote wanaoamini. Lakini sura hizi zinatangaza habari za kuogopesha kabisa kwa wale wasioamini, kwa sababu kitabu cha Ufunuo kinafunua ya kwamba ukikataa kupokea Yesu Kristo kuwa **Mwokozi** wako, atakuwa **Mwamuzi** wako wakati wa mwisho! Kama usipopokea **Mwana-Kondoo wa Mungu**, utakutana na **Simba wa Mungu**, kwa sababu Bwana Yesu, aliyekufa kama mwana-kondoo wa sadaka kuondoa zambi, atarudi kama simba ya kunguruma kwa hukumu. Hii ndiyo maana ya Maandiko yanayosema juu ya *"wakati wa ufunuo wa Bwana Yesu kutoka mbingu pamoja na malaika za uwezo wake, katika moto wa kuwaka akiwalipa kisasi wale wasiojua Mungu, na wao wasiotii Habari Njema ya Bwana wetu Yesu Kristo!"* (2 Watesalonika 1:7,8)

Everyday Publications Inc @ 2010

Sasa, tusikilize vizuri wakati tunaposoma sehemu za kitabu cha Ufunuo. Nyuma ya kurudi kwa Bwana Yesu kwenda mbinguni, alituma malaika yake karibu na mtume Yoane, kumfunulia maneno yatakayotokea kwa mwisho wa dunia. Ndani ya sura ya kwanza, Yoane aliandika:

> (Ufunuo 1) 1 ***Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu aonyeshe watumishi wake maneno yaliyopasa kuwa upesi;*** *naye akatuma kwa malaika yake kuonyesha mtumishi wake Yoane; 2 aliyeshuhudia Neno la Mungu na ushuhuda wa Yesu Kristo, maneno yote aliyoona. 3 Heri anayesoma nao wanaosikia maneno ya unabii huu, na kushika maneno yaliyoandika ndani yake; kwa maana wakati ni karibu. 4 Mimi Yoane . . . ninawaandikia ninyi . . . Neema iwe*

*kwenu, na salama zinazotoka kwake yeye aliye sasa na aliyekuwa, na atakayekuja; na zinazotoka kwa roho saba zilizo mbele ya kiti chake cha ufalme 5 . . .* ***Kwake yeye ambaye alitupenda na kutuosha zambi zetu kwa damu yake, 6 na kutufanya kuwa ufalme wa makuhani kwa Mungu na Baba yake; kwa yeye utukufu na uwezo hata milele na milele! Amina. 7 Tazama, anakuja na mawingu; na kila jicho litamwona, na wale ambao walimchoma; na mataifa yote ya dunia wataomboleza kwa ajili yake. Ndiyo. Amina.*** *8 Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, anasema Bwana Mungu, yeye aliye sasa, na aliyekuwa, na atakayekuja, Mwenyezi.*

Ndani ya sura 19 Yoane aliandika:

(Ufunuo 19) 1 *Nyuma ya maneno haya nikasikia sauti kama sauti ya makutano makubwa, sauti kubwa mbinguni ikisema: Haleluya, Wokovu, na utukufu na nguvu ni za Bwana Mungu wetu; 2 kwa sababu hukumu zake ni za kweli . . . 6 Nikasikia sauti kama sauti ya makutano makubwa, na kama sauti ya maji mengi, na kama sauti ya ngurumo yenye nguvu, ikisema: Haleluya; kwa sababu Bwana Mungu wetu, Mwenyezi, ametawala. [**Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atatawala hata milele na milele!*** (11:15)]

*11 Nikaona mbingu zimefunguliwa, na tazama, farasi mweupe, na yeye ambaye alimpanda, anayeitwa* ***Mwaminifu na wa Kweli****, naye kwa* ***haki*** *anahukumu na kufanya vita. 12 Na macho yake yalikuwa kama mwako wa moto, na juu ya kichwa chake mitama mingi; naye ana jina lililoandikwa, ambalo mtu halijui ila yeye mwenyewe. 13 Naye amevikwa vazi lililochovywa katika damu; na* ***jina lake linaitwa Neno la Mungu****. 14 Na majeshi yaliyo mbinguni wakamfuata, wamepanda farasi weupe, na kuvikwa kitani nzuri, nyeupe na safi. 15 Na upanga mkali unatoka katika kinywa chake, ili apige mataifa kwa huu; naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, naye anakanyaga kikanyagio cha matunda cha gazabu ya kasirani ya Mungu Mwenyezi. 16 Naye ana jina linaloandikwa katika vazi lake na paja lake,* ***MFALME WA WAFALME NA BWANA WA WABWANA****.*

(Ufunuo 20) *1 Kisha nikaona malaika akishuka toka mbingu, mwenye ufunguo wa shimo pasipo mwisho, na mnyororo mkubwa katika mkono wake. 2 Akashika yule joka mkubwa, yule nyoka ya zamani, anayeitwa Diabolo na Shetani, akamfunga miaka elfu, 3*

Everyday Publications Inc
@ 2010

*akamtupa katika shimo pasipo mwisho, akamfunga, akatia muhuri juu yake, asipate kudanganya mataifa tena, hata ile miaka elfu itimie; na nyuma ya haya imepasa afunguliwe wakati kidogo. 4 Nikaona viti vya ufalme, nao wakakaa juu yao, nao wakapewa hukumu; nikaona roho zao waliokatiwa vichwa kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu, na kwa Neno la Mungu . . . wakatawala pamoja na Kristo miaka elfu.*

*7 Na wakati itakapokwisha ile miaka elfu, Shetani atafunguliwa katika kifungo chake, 8 naye atatoka kudanganya mataifa walio katika pembe ine za dunia . . . kuwakusanya kwa vita, hesabu yao ni kama mchanga wa bahari. 9 Wakapanda juu ya upana wa dunia, wakazunguka kambi ya watakatifu, na mji huu uliopendwa. Moto ukashuka toka Mungu mbinguni, ukawateketeza. 10* ***Na yule Diabolo, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti, pahali wanapokaa yule nyama na yule nabii wa uwongo. Na watateswa mchana na usiku hata milele na milele.***

*11 Nikaona* ***kiti cha ufalme, kikubwa, cheupe,*** *naye anayeketi juu yake, dunia na mbingu zikakimbia uso wake; na pahali pao hapakuonekana. 12 Nikaona wafu, wakubwa na wadogo, wamesimama mbele ya Mungu, na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, kilicho cha uzima; na wafu wakahukumiwa katika mambo haya yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao. 13 Bahari ikatoa wafu waliokuwa ndani yake. 14 Mauti na Hadeze zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili, hili ziwa la moto. 15 Na ikiwa* ***mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.***

(Ufunuo 21) *1 Nikaona* ***mbingu mpya na dunia mpya****; kwa maana mbingu za kwanza na dunia ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana habari tena. . . 3 Nikasikia sauti kubwa toka mbinguni, ikisema: Tazama, hema ya Mungu ni pamoja na watu, naye atakaa pamoja nao, nao watakuwa watu wake, na Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao, atakuwa Mungu wao. 4 Naye atapangusa kila chozi katika macho yao; wala* ***mauti haitakuwa tena:*** *wala maombolezo, wala kilio, wala uchungu hautakuwa tena; kwa maana maneno ya kwanza yamekwisha kupita. 5 Na yeye anayeketi juu ya kiti cha ufalme akasema: Tazama, ninafanya yote kuwa mapya. Akaniambia: Andika, kwa maana maneno haya ni amina na ya kweli. 6 Akaniambia: Imekwisha kuwa. Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho.* ***Mimi nitampa yeye mwenye kiu, ya chemchemi ya maji ya uzima, bule.*** *7 Yeye anayeshinda atariti maneno haya, nami*

Everyday Publications Inc. @ 2010

*nitakuwa **Mungu wake**, naye atakuwa **mwana wangu.** 8 Lakini wenye woga, na wasioamini, na wanaoabudu sanamu, na wawongo wote, **sehemu yao** ni katika lile ziwa linalowaka moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili.*

(Ufunuo 22) *1 Kisha akanionyesha mto wa maji wa uzima wenye kungaa kama bilauri, ukitoka katika **kiti cha ufalme cha Mungu, na cha Mwana-Kondoo.** 2 Katikati ya njia yake ya ule mto, upande ngambo na ngambo, ulikuwa mti wa uzima, unaozaa matunda namna kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila mwezi . . 3 Wala haitakuwa laana yo yote tena. Na kiti cha ufalme cha Mungu, na cha Mwana-kondoo kitakuwa ndani yake. Na watumishi wake watamtumikia; 4 nao wataona uso wake, na jina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao. 5 Wala hautakuwa usiku tena; wala hawahitaji taa, wala nuru ya jua; kwa maana Bwana Mungu anawatia nuru, nao watatawala hata milele na milele. 6 Akaniambia: Maneno haya ni amina na kweli. Na Bwana, Mungu wa manabii watakatifu alituma malaika yake kuonyesha watumishi wake mambo yaliyopaswa kuwa upesi.*

Everyday Publications Inc
@ 2010

*[Mimi Yesu, ninasema:] 12 **Tazama, ninakuja upesi,** na mshahara wangu ni pamoja nami, kulipa kila mtu kama ilivyo kazi yake. 13 Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, wa kwanza na wa mwisho. 14 Heri wale wanaofua nguo zao, wawe na amri kwendea mti wa uzima, na kuingia katika mji kwa milango yake. 15 Lakini inje ni . . . kila mtu anayependa uwongo na kuufanya, 16 Mimi, Yesu, nimetuma malaika yangu kuwashuhudia ninyi mambo haya katika makanisa. Mimi ndimi Shina na Mzao wa Daudi, ile nyota yenye kungaa ya asubui. 17 Na Roho na bibi-arusi wanasema: Kuja. Naye mwenye kusikia aseme: **Kuja. Naye mwenye kiu, aje; na yeye anayetaka atwae maji ya uzima bule.***

*18 Nikashuhudia kila mtu anayesikia maneno ya unabii wa kitabu hiki, **mtu ye yote akiyaongezea,** Mungu atamwongezea mapigo haya yaliyoandikwa katika kitabu hiki 19 Na **mtu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki,** Mungu atamwondolea sehemu yake katika kitabu cha uzima, na katika ule mji mtakatifu, ndizo habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki. 20 Yeye anayeandika maneno haya anasema: **Ndiyo, ninakuja upesi.** Amina, kuja Bwana Yesu. 21 Neema ya Bwana Yesu Kristo iwe pamoja nanyi wote. Amina.*

Hivi Mungu anamaliza kitabu chake cha ajabu na anaahidi ya kwamba Bwana Yesu Kristo ambaye wana wa Adamu walifunga juu

ya msalaba na misumari, atarudia dunia siku nyingine. Atarudi na uwezo na utukufu mkubwa, kuwapeleka wale ambao walimwamini kuwa pamoja naye, na kuwahukumu wale ambao hawamwamini! Rafiki, unakaa na tumaini wakati unapowaza juu ya kurudi kwa Bwana Yesu toka mbinguni? Wewe ni katikati ya wale ambao walimpokea kuwa Mwokozi na Bwana wao? Unaamini moyoni mwako ya kwamba Mungu aliweka zambi zako juu ya Bwana Yesu Kristo, asiyefanya zambi kamwe, ili kwa njia yake Mungu aweze kukuhesabu kuwa mwenye haki? **Jina lako limeandikwa ndani ya Kitabu cha Uzima?** Bwana Yesu Kristo ni **Mwokozi wako**? Au atakuwa **Mwamuzi** wako?

Wewe ni tayari kwa kurudi kwa Kristo? Kama ungesikia sauti ya Mungu leo, usifanye mgumu moyo wako, kwa sababu Maandiko yanasema:

> *"Kwa Bwana . . . miaka elfu moja ni kama siku moja. Bwana hakawii kutimiza ahadi yake, kama wengine wanavyozania kukawia; lakini ni vumilivu kwetu asiyetaka mtu mmoja* ***kupotea****, lakini wote wafike* ***kutubu****. Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwizi; katika siku hii mbingu zitatoweka na sauti kubwa, na viumbe vya asili vitayeyushwa kwa moto mkali, na inchi na kazi zilizo ndani yake zitateketezwa.* (2 Petro 3:8-10) *"****Sasa*** *ni wakati wa kukubaliwa; tazama* ***sasa*** *ni siku ya wokovu!"* (2 Wakorinto 6:2) ***"Basi sisi tutapona namna gani tusipochunga wokovu mkubwa namna hii?"*** (Waebrania 2:3)

Everyday Publications Inc © 2010

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Rafiki, asante kwa kusoma pamoja nasi. Tunaomba Mungu hata kila neno ulilojifunza juu ya *Njia ya Haki* litakuwa baraka ndani ya maisha yako na kukuongoza kupokea "*wokovu mkubwa*" wa Mungu anaotoa bila bei kwa watu wote wanaoamini Neno lake kwelikweli.

Mungu akubariki wakati unapokumbuka masemo ya mwisho ya Yesu ndani ya Maandiko Matakatifu. Bwana Yesu Kristo alisema:

> ***"Ndiyo, ninakuja upesi!"*** (Ufunuo 22:20).
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

# Sehemu 4

## Njia ya Haki
## **Muhtasari**

Everyday Publications Inc
@ 2010

***"Tutapona namna gani tusipochunga wokovu mkubwa namna hii?'***

Waebrania 2:3

Everyday Publications Inc
@ 2010

Somo 89

# Habari Njema

Salama iwe kwako, rafiki. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea pamoja leo na mfulizo huu *Njia ya Haki.*

Ndani ya mafundisho yetu ndani ya kitabu cha Injil {*Habari Njema* kwa Kiarabe} tuliona ya kwamba Bwana Yesu Kristo, nyuma ya ufufuko wake, aliagiza wanafunzi wake akisema, ***"Kwendeni katika dunia pia, mukihubiri Habari Njema kwa kila mtu."*** (Marko 16:15) Na wakati Yesu alipokwisha kupanda mbinguni, mtu mmoja, jina lake Paulo (aliyekuwa mwenye kutesa watu wa dini nyingine na ukali sana mbele ya kugeuka mwenye kufuata Kristo na bidii) aliandika:

> *"[Mungu aliniita kuwa mtume wake na kunipa kazi ya kutangaza* ***habari njema yake*** *– ndiyo* **Habari Njema***] aliyoahidi mbele kwa vinywa vya manabii yake katika Maandiko matakatifu . . . Sioni haya kwa* ***Habari Njema*** *[ambayo ninahubiri] kwani ni uwezo wa Mungu hata wokovu, kwa kila mtu anayeamini . . . Kwa sababu haki ya Mungu inaonekaa ndani yake, toka imani hata imani."* (Waroma 1:1,2,16,17).

Everyday Publications Inc
@ 2010

**Habari njema, habari njema, habari njema! Habari njema** hii inayotangazwa tena na tena ndani ya Neno la Mungu ni nini? Leo, Mungu akitusaidia, tunataka kusemezana juu ya **Habari Njema** hii inayotangazwa ndani ya Maandiko Matakatifu. Lakini mbele ya kusemezana juu ya **Habari *Njema*,** inatupasa kukumbuka ***habari mbaya.***

**Habari mbaya** ni nini? Labda unakumbuka ya kwamba, katika mwanzo, nyuma ya kuumba mbingu na dunia, Mungu alifanya Adamu na Hawa na kuwaweka ndani ya shamba la Paradiso hapa duniani. Mungu aliwaumba ili waweze kumjua, kumpenda, kumtii na kumtukuza kwa milele. Lakini kwa kuwapima, Mungu alisema na Adamu: "Unaweza kukamata matunda ya miti yote shambani, ila toka mti ulio katikati ya shamba. Huna ruhusa kula matunda yake, kwa sababu siku unapoyakula utakufa!" Habari mbaya ndiyo ya kwamba Adamu na Hawa walisikiliza masemo ya nyoka, ndiye Shetani, ambaye aliwajaribu kula matunda ya mti ambao Mungu alikataza. Zambi ya Adamu na

Hawa iliingiza taabu na mauti duniani, ikiwachafua wenyewe pamoja na wazao wao wote. Kama tunavyosikia mara nyingi: "Tauni haikwishi na yule ambaye anaianza!" Neno la Mungu linatujulisha habari mbaya wakati linaposema:

> *"Na sawasawa watu wanavyowekwa kufa mara moja, na* ***nyuma ya kufa hukumu*** *. . . Bwana alikuja . . . ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuazibisha wote wasioogopa Mungu, kwa ajili ya matendo yao yote ya upotevu waliyotenda pasipo kuogopa Mungu, na kwa ajili ya maneno magumu yote wakosaji hawa wasioogopa Mungu waliyosema juu yake!"* (Waebrania 9:27; Yuda 15)

Hivi **habari mbaya** ndizo ya kwamba **sisi sote ni wenye zambi na inatupasa kukaa tayari kupokea hukumu ya haki ya Mungu!**

Lakini, **Habari Njema** ni ya kwamba palepale ndani ya shamba la Paradiso, Mungu, aliye mwenye rehema nyingi, alitangaza ya kwamba siku nyingine atatuma Mtu duniani asiyechafuwa na zambi, aliyezaliwa na bikira. Mtu huyu Mtakatifu, **Mkombozi** huyu mwenye haki, atajitoa mwenyewe kuuawa kama sadaka kulipa kwa zambi za Adamu na wazao wake. Azabu kwa zambi ambayo sisi tunastahili kupata itamwangukia yeye. Hizi ndizo Habari Njema Mungu alizotangaza siku Adamu na Hawa walipofanya zambi.

Mungu alitumia watu wengi kutangaza kuja kwa Mkombozi huyu, anayeitwa **Masiya** vilevile. Kila nabii wa Mungu alitangaza neno fulani juu ya Masiya, ili wakati alipokuja, watu wote waliweza kutambua ya kwamba ndiye aliyewekwa na Mungu. Kwa mfano, nabii Isaya, aliyeishi karibu miaka mia saba mbele ya wakati Masiya atakapozaliwa, alitabiri: *"Tazama, bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana, nao watamwita jina lake Emanueli; maana yake Mungu pamoja nasi."* (Matayo 1:23; Isaya 7:14) Nabii mwingine, jina lake Mika, alitabiri ya kwamba Masiya atatoka mbinguni na kuzaliwa duniani ndani ya kijiji cha **Betelehemu**. Na kweli Masiya alizaliwa palepale tu. Mika alitabiri neno hili mia za miaka mbele ya kuja kwa Masiya.

Lakini manabii hawakutangazwa kuzaliwa kwa Masiya tu. Walitabiri vilevile ya kwamba Masiya **atateswa na kufa** kwa pahali pa wenye zambi. Kwa mfano, nabii Daudi aliandika ya kwamba watu watazarau Masiya, watamtesa, kutoboa mikono na miguu yake, na kumwua. Na Daudi hakutangaza mauti tu ya Masiya, lakini alitabiri vilevile ya kwamba **Mungu atafufua Masiya** toka wafu na kuhakikisha ya kwamba alikuwa Mwokozi, ndiyo Mwokozi wa pekee aliyetumwa kuokoa wana wa Adamu toka azabu ya zambi.

Everyday Publications Inc @ 2010

Watu hawabishani sana juu ya kuzaliwa kwa Masiya, lakini watu wengi wanakwalishwa na habari za mauti na ufufuko wake. Hawawezi kufahamu namna gani Mungu aliweza kuangalia tu wakati watu walipohayarisha Masiya ambaye alimtuma. Lakini neno inaloshinda zaidi ya watu kufahamu ni ya kwamba Mungu, ambaye anatupenda, ndiye alikusudi kwa Masiya kuteswa hivi **kwa zambi zetu.** Kwa sababu hii manabii walitangaza, wakisema: *"Ilipendeza Bwana kumchubua [Masiya - kama sadaka **kulipa kwa zambi]!**"* (Isaya 53:10)

Tunaamini manabii? Tunasema tunawaamini. **Tukiamini manabii kweli kweli,** inatupasa **kuamini vilevile maneno waliyoandika**. Sharti tukumbuke ya kwamba manabii hawakutangaza mawazo yao wenyewe. Mungu aliweka ndani ya roho zao maneno ambayo iliwapasa kusema. Hivi, tukikataa kuamini manabii wale, kabisa kabisa tunakataa nani? Tunakataa **Mungu**—kwani ni yeye aliyeongoza manabii kutabiri ya kwamba Masiya atakufa kama sadaka kuondoa zambi.

Mungu alifanya shauri kwa Masiya kufa kwa sababu anapenda dunia na hataki mtu ye yote kupotea kwa sababu ya zambi zake. Ilikuwa lazima kwa Mwenye haki kufa kwa wazalimu ili kuwaokoa toka hukumu ya Mungu. Hii ndiyo maana ya sadaka za kondoo na mbuzi kwa miaka iliyopita. **Yesu Kristo** aliyezaliwa na bikira, kwa uwezo wa Mungu, ni **sadaka kamilifu na ya mwisho** ambayo Mungu alitoa. Yeye ni Sadaka kamilifu na ya daima kwa zambi na hatuhitaji kusumbuka kukaa kutoa sadaka zisizo kamilifu na zilizo alama tu. Unakumbuka maneno Bwana Yesu aliyotangaza juu ya msalaba saa ndogo mbele ya kufa kwake? Alisema, ***"Imekwisha!"*** (Yoane 19:30) Alilipa deni yetu mara moja na kwa milele. Linabaki neno moja tu kwa sisi kufanya, ndilo kuliamini! Kama tulivyosoma mbele, Maandiko yanasema: Habari Njema ya mauti na ufufuko wa Yesu Kristo *"ni uwezo wa Mungu hata wokovu, kwa **kila mtu anayeamini**."* (Waroma 1:16)

Everyday Publications Inc @ 2010

Ni huzuni kubwa kwa sababu watu wengi wanakataa kuamini ndani ya Kristo, wakisema habari hizi juu ya kufa na ufufuko wake ni habari zilizotungwa na watu tu. Lakini wakati tunapojifunza Habari Njema, tunaona ya kwamba kila neno ambalo manabii walitabiri juu ya Masiya **lilitimizwa** ndani ya Yesu Kristo. Ndiyo, **kila neno**! . . . juu ya kuzaliwa kwake, maisha yake, mauti yake, ufufuko wake na kupanda kwake kwenda mbingu. Hivi, Habari Njema inatangaza ya kwamba *"Kristo alikufa kwa sababu ya zambi zetu kama maandiko [ya manabii] yanavyosema; na ya kama alizikwa, akafufuka siku ya tatu, kama maandiko [ya manabii] yanavyosema."* (1 Wakorinto 15:3,4) **Kila neno lililotokea namna manabii walivyotabiri**. Watu waliochukia Yesu walimzarau,

walimtesa na kumwua, na watu ambao walimpenda walimzika. Lakini mauti haikuweza kumfunga ndani ya kaburi. Tuliona ya kwamba, siku ya tatu nyuma ya kusulibishwa kwake, wanawake wengine waliamka asubui mapema, wakakwendea kaburi pahali Yesu alipozikwa, wakakuta kaburi lilikuwa wazi na maiti haikuwa ndani! Nyuma ya kufa na ufufuko wake Yesu alijionyesha kwa wanafunzi wake kwa muda wa siku makumi ine. Zaidi ya watu mia tano walimwona nyuma ya ufufuko wake. Ndiyo, alifufuka kweli! Masiya alikuwa ameshinda mauti, moja ya adui kubwa zaidi za mtu. Na ufufuko wa Yesu ulihakikisha ya kwamba Mungu alikubali na kupokea sadaka yake kama malipo ya kutosha kwa zambi za wana wa Adamu, ili kila mtu anayemwamini aweze kushiriki ndani ya uzima wa milele ambao alinunua.

Hizi ndizo Habari Njema. **Bwana Yesu Kristo alikufa kuondoa zambi zako, na alitoka kaburini siku ya tatu kukupa uzima wa milele.** Kusudi la Habari Njema hii ni kuokoa wote ambao wanaziamini. Hivi inakupasa kujibu ulizo hili: **"Unaamini habari hizi?"** Neno la Mungu linasema: "Leo ni siku ya wokovu! Ukisikia Habari Njema, usifanyize moyo wako kuwa mgumu! Amini!" Wokovu si tunda la kazi sisi tunazofanya, kwa sababu **hakuna mtu anayeweza kufanya kazi za kutosha kumstahilisha kuingia Paradiso.** Mungu hataku**uza** wokovu wake mkubwa kamwe; anataka ku**toa** kwako kama **zawadi**! Labda matendo mema, maombi na kufunga chakula kunafurahisha roho yako lakini hakuwezi kutosha kwa haki ya Mungu. Kuna njia moja tu kwa wewe kuingia Paradiso ya Mungu, ndiyo hii:

Everyday Publications Inc @ 2010

1) Inakupasa ku**kubali** ya kwamba wewe ni mwenye zambi na huna nguvu kupendeza Mungu.

2) Kisha inakupasa ku**amini** ya kwamba Yesu Kristo ni Mwokozi ambaye Mungu alituma kukufia juu ya msalaba kuondoa zambi zako na kufufuliwa toka wafu kukupa uzima wa milele.

Ukiamini Habari Njema hizi, **unaweza kujua hakika ya kwamba utapelekwa kwa Paradiso nyuma ya kufa kwako**, kwa sababu Mungu mwenyewe ameahidi ndani ya Neno lake ya kwamba tunaweza kujua kwamba tuna uzima wa milele, **kama tukiamini** jina la Bwana Yesu Kristo. (1 Yoane 5:9-13)

{Maneno yanayofuata ni ushuhuda wa Malick, mtangazaji wa masomo haya kwa radio kwa Senegal} Uniruhusu kukupasha namna gani niligeuka mwamini ndani ya Yesu Kristo. Wakati nilipokuwa kijana nilikuwa mwaminifu kwa dini ya Islam na niliomba mara tano kila siku. Nilishika vilevile siku kubwa (karamu) ya kila mwaka, lakini sikujua

pahali gani nitakapokwenda nyuma ya kufa kwangu. Niliulizana na watu wengine, lakini hakuna mtu aliyeweza kunijibu waziwazi. Lakini wakati niliposoma Habari Njema {*Injil*}, niliona ya kwamba **niliweza kujua pahali nitakapokwenda nyuma ya kufa kwangu** kwa sababu Yesu Masiya mwenyewe alisema ndani ya Habari Njema: *"Kweli, kweli ninawaambia ninyi, yeye anayesikia neno langu na kumwamini yeye ambaye alinituma* ***ana uzima wa milele; hafiki kwa hukumu, lakini amepita kutoka mauti kuingia uzima."*** (Yoane 5:24) Alisema vilevile: *"Mimi ni ufufuko na uzima; yeye ambaye ananiamini, hata anapokufa* ***anaishi!****"* (Yoane 11:25) Hivi nilitubu masumbuko yangu kujiokoa mwenyewe na niliamini Masiya juu yake manabii wote walitabiri wakisema, ***"kwa jina lake kila mtu ambaye anamwamini atapewa usamehe wa zambi."*** (Matendo 10:43) Niliweka tumaini langu lote ndani ya Bwana Yesu Kristo. Na tangu siku ile kufika sasa Mungu ameleta salama kwa roho yangu. Damiri yangu hainisumbushi tena. Wakati ulio mbele unaonekana mzuri sana kwa sababu ya mauti ya Yesu juu ya msalaba. Kwa wakati wa maisha yangu ya sasa kama mwanafunzi wa Kristo ninapata taabu na mateso mara nyingine kwa sababu imani yangu haipatani na mawazo ya ndugu na rafiki zangu, lakini nina salama rohoni. Salama ya Mungu inajaza moyo wangu na nia yangu. Na Yesu ambaye alinipa salama hii anasema: *"Kama dunia ikiwachukia ninyi, munajua ya kama imenichukia mimi mbele . . . Salama ninawaachia ninyi; salama yangu ninawapa ninyi; nami ninawapa ninyi si kama dunia inavyotoa. Musifazaike mioyoni mwenu, wala musiwe na woga."* (Yoane 15:18; 14:27)

Na rafiki, maneno Bwana aliyofanya kwa mimi na ndani yangu anaweza kufanya kwa ninyi wote mmoja mmoja. Anaomba neno moja tu kwako: Anaomba **umpe roho yako nzima**. Yeye atafanya mambo yote mengine. Kwani Bwana Yesu mwenyewe alisema, *"Kujeni kwangu, ninyi wote munaosumbuka na wenye mzigo mzito, nami nitawapumzisha ninyi. Tieni nira yangu juu yenu, na mufundishiwe nami, kwa sababu mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; na mutapata raha kwa nafsi zenu."* (Matayo 11:28,29)

**Wewe unachoka na kusumbushwa kwa sababu ya mzigo wa zambi zako?** Unataka kupata raha kwa roho yako? Kama ukiamini Habari Njema ya kwamba Masiya alikukufia na kufufuka tena kwa wewe, Mungu atasamehe zambi zako, atakuhesabu kuwa haki na ataandika jina lako ndani ya kitabu cha uzima. Ukiamini Habari Njema hizi, Mungu atakutia mhuri kuonyesha kwamba wewe ni mali yake, na atatuma Roho ya Yesu kuingia ndani ya moyo wako. Roho Mtakatifu, anayeishi ndani yako, atageuza moyo wako, maisha yako na mwenendo wako, kwa sababu Maandiko yanasema: *"Kama mtu akiwa ndani ya Kristo,*

Everyday Publications Inc @ 2010

*yeye ni kiumbe kipya; maneno ya zamani yamepita; tazama maneno yote yamekuwa mapya!"* (2 Wakorinto 5:17)

Rafiki, pahali gani ulipo, hata hali yako ni nini, si neno kama ukiwa mwanamume na mwanamke, mzee au kijana, Bwana Yesu Kristo anaweza kukupa uzima mpya—**kama ukimwamini**. Alikukufia ili uweze kuishi pamoja na Mungu kwa milele. **Unaamini Habari Njema hizi?**

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Mungu akubariki. Tunaachana nawe na mashairi mawili toka Maandiko yanayosema juu ya matumaini ya ajabu ambayo Mungu anawapa watu wote wanaoamini Habari Njema ya Mungu. Maandiko yanasema:

> ***"[Mungu] alituokoa, akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu, lakini kwa kadiri ya kusudi lake mwenyewe na neema yake, tuliyopewa katika Kristo Yesu mbele ya nyakati za zamani, na sasa imefunuliwa na kuonekana kwa Mwokozi wetu Yesu Kristo, aliyebatili kufa, na kufunua uzima na maisha yasiyokoma kwa njia ya Habari Njema."***
>
> (2 Timoteo 1:9,10)

Everyday Publications Inc @ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 90

# Maulizo ya Watu na Majibu ya Mungu

### Sehemu 1

Salama iwe kwako, rafiki unayejifunza pamoja nasi. Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea tena na mfulizo *Njia ya Haki.*

Ndani ya somo letu leo tunataka kufanya neno lililo namna nyingine na maneno tunayofanya kila mara. Tunataka kushiriki nawe **maulizo** mengine tuliyopokea toka watu wengine. Kwa kujibu kila ulizo **tutatumika na mashairi toka Maandiko Matakatifu tu,** kwani Neno la Mungu ndilo nuru ya pekee ya hakika ambayo inaweza kutuongoza katika giza. Kama ilivyoandikwa ndani ya Zaburi: *"Neno lako ni taa kwa miguu yangu, na nuru kwa njia yangu.* (Zaburi 119:105) Sasa tusikilize maulizo hata.

Everyday Publications Inc © 2010

1) Ulizo la kwanza tuliyopokea ndani ya barua ndiyo hii: **Dini ya wale waliotayarisha mfulizo *Njia ya Haki* ni nini?**

Zamani sana Mungu aliweka ndani ya mioyo yetu hamu kutafuta kweli—**kweli *yake***. Tulitaka kujua kwa faida yetu wenyewe Neno la Mungu wa pekee wa kweli. Wakati tuliposoma Biblia, maana Tora {*Taurat*}, Zaburi, vitabu vya Manabii, na Habari Njema {*Injil*}, tulitambua ya kwamba Yesu Kristo ni Mwokozi Mtakatifu ambaye manabii wote waliandika habari zake. Yesu ndiye sadaka kamilifu na ya mwisho ambayo Mungu alitoa kufutia mbali deni ya zambi ya wana wa Adamu ili kila mtu ambaye anamwamini aweze kuishi mbele ya Mungu kwa milele. Yesu Kristo tu, aliyetoka kwa Mungu, anaweza kutuleta kwa Mungu. Tumeweka tumaini letu nzima ndani yake.

Basi, sisi ni nani? Sisi ni **wanafunzi wa Yesu Kristo**. Qur'an kinatuita "*Ahl al-kitab*," maana yake *Watu wa Kitabu*. Wengine wanatuita *Wakristo*, maana yake, *watu wa Kristo*. Wakati tunapokujulisha ya

kwamba tuko Wakristo, tunakukumbusha ya kwamba kuna watu wengi ambao wanajiita Wakristo, lakini si kusema ya kwamba wao ni kweli watu wa Kristo. Mti haugeuki mamba kwa njia ya kulala ndani ya maji saa ndefu (mfano wa watu wa Senegal), vivyo hivyo mtu hageuki Mkristo kwa njia ya kufanya tu maneno Wakristo wanayofanya. Kufuata dini hakuwezi kutuingiza ndani ya jamaa ya Mungu. Yesu Kristo tu anaweza kutuleta kwa Mungu. Tumebarikiwa sana kwa sababu Kristo ni Mwokozi na Bwana na Rafiki yetu! Ametuingiza ndani ya jamaa ya Mungu na kutupa sisi tumaini kwa wakati wa kufa. Kila siku anatuonyesha uaminifu na mapendo yake. Ndani ya Bwana Yesu Kristo, Mungu ametupa sisi yote yanayohitajiwa kwa uzima wa milele! Ndani yake tunapata vyote mioyo yetu inavyohitaji!

2) Ulizo la nyuma ni ulizo kubwa na linastahili jibu wazi. Mtu huyu anasema: **Kuna neno moja ambalo linanisumbusha sana. Nimesoma ndani ya Qur'an pahali nabii wetu, Muhamedi, anapoagiza wafuata wote wa Islam kuamini vitabu vingine ndani ya Biblia kama Tora na Habari Njema. Ninaheshimu Biblia na nilianza kuisoma. Lakini, rafiki zangu wananiambia ya kwamba hatuwezi kuamini Biblia, kwa sababu imechafuwa na kugeuzwa. Wanasema Biblia ambayo ninasoma ni namna nyingine na Biblia ya kwanza. Unafikili nini juu ya neno hili?**

Everyday Publications Inc @ 2010

Mbele ya kujibu ulizo hili, tuna maulizo machache kwa wale wanaosema vitabu vya zamani vya manabii "vimechafuwa na kugeuzwa." Pahali gani mulipata mawazo ya kwamba Biblia imegeuzwa? Munasimamisha mashitaki makubwa namna hii juu ya nini? Mutuambie kama Biblia iligeuzwa **wakati gani**? **Nani** aligeuza? Iligeuzwa **pahali gani**? **Maneno gani** yaligeuzwa? Munajua neno hili **namna gani**? Munaweza kuonyesha hata neno moja tu linalohakikisha ya kwamba Maandiko yamechafuwa?

**Mukitafuta na roho ya kweli mambo ya hakika** juu ya Biblia, mutaona ya kwamba Mungu amelinda Neno lake takatifu ambalo aliongoza manabii wake kuandika. Wale wanaosema Biblia imegeuzwa na kusudi la kudanganya wanaamini masemo ya watu tu. Hakuna neno linalohakikisha ya kwamba Biblia imegeuzwa. Lakini kuna maneno mengi yanayoshuhudia na kuhakikisha ya kwamba Biblia **haikugeuzwa.**

Leo, ndani ya nyumba kubwa zenye vitu kuonyesha maendeleo ya maneno mbalimbali, na ndani ya universités za dunia, wenye

elimu wamelinda **vitabu vingi vya zamani sana,** (hati za kuvingirisha na karatasi zenye maandiko ya mkono) vya Maandiko ya Habari Njema {Injil}, maana yake, Agano Jipya. Vitabu hivi vilikuwa mia za miaka mbele ya wakati wa Muhamedi na vilevile vitabu vya Agano la Kale kama Tora na Zaburi. Mukifananisha vitabu hivi vya zamani na vile tunavyoshika mikononi mwetu leo, mutaona ya kwamba Mungu amelinda Neno lake kwa sisi. Biblia tunayosoma leo inalingana na Biblia iliyokuwa kwa wakati wa Muhamedi.

Manabii waliandika maneno ya Mungu juu ya hati za kuvingirisha zilizofanywa toka ngozi za nyama au utembwe wa mapando. Waandishi Wayuda walifanya miigo ya Neno la Mungu juu ya hati mpya. Walijifunza kazi hii sana na waliweka roho kabisa **ili miigo yao iwe sawasawa kabisa na kitabu walichofuatisha.** Walifanya hesabu ya herufi ndani ya kitabu na kuonyesha herufi ya katikati kabisa kwa kuhakikisha ya kwamba kitabu na mwigo wake ilikuwa sawasawa. Kosa likipatikana, hati nzima iliharibiwa! Waandishi hawa Wayuda waliamini ya kwamba kugeuza Neno la Mungu ni sawasawa na kugusa Mungu mwenyewe! Labda umesikia habari za **Hati za Bahari ya Chumvi** zinazojulikana sana na zilizovumbuliwa kwa mwaka 1947. Ulijua ya kwamba miigo hii ya Agano la Kale ilifanywa miaka mia moja mbele ya kuzaliwa kwa Yesu? Hata hivi hati hizi zinalingana sawa na hati za miigo iliyofanywa miaka elfu moja nyuma ya wakati ule! Biblia haikugeuzwa!

Everyday Publications Inc @ 2010

Kabisa kabisa hakuna mtu anayeweza kugeuza Biblia. Mtu fulani akitaka kugeuza Biblia, ingempasa kugeuza miigo yote ya Biblia, ndilo neno lisilowezekana. Biblia iliandikwa kwanza kwa lugha za Kiebrania, Kiaramaic na Kiyunani. Ndani ya wakati uliofuata miaka Kristo alipokuwa duniani, wenye elimu walianza kutafsiri Biblia toka lugha hizi kwa **lugha mbalimbali nyingi**. Hakuna mtu anayeweza kugeuza Biblia hizi zote katika dunia nzima! Kwa wakati wa sasa Biblia (Biblia nzima au sehemu yake), iliandikwa ndani ya kupita lugha mbalimbali elfu mbili. Mungu amelinda Neno lake na watumishi wake wanalitafsiri kwa lugha za makabila ya dunia, kwa sababu Mungu anataka kila mtu kuisikia na masikio yake mwenyewe, kuifahamu na nia yake mwenyewe, kuipokea ndani ya moyo wake kabisa na kuokolewa.

Mungu anaweza kulinda Neno lake hata Shetani na wale ambao wanataka kuigeuza na kuiharibu wasiweze kufanya hivi? Ndiyo, **anaweza** kufanya hivi na kweli **amefanya** vile! *Allahu Akbar!* Mungu ni mkubwa! Ndiyo tunajua ya kwamba tangu mwanzo wa dunia

kufika leo Shetani amejaribu kugeuza Neno la Mungu—ndani ya nia za watu. Kwa mfano, ndani ya kitabu cha kwanza cha Biblia, tulisikia Mungu akisema na Adamu, *"Siku unapokula [wa mti wa kujua uzuri na ubaya] hakika **utakufa**!"* Lakini Shetani alikana neno Mungu alilosema, akawaambia Adamu na Hawa, *"**Hamutakufa!**"* Hivi Shetani alijaribu kugeuza Neno la Mungu. Kama unavyojua, Adamu na Hawa walichagua kuamini Shetani, na kula matunda waliyokatazwa kula. Hivi roho zao zilikufa, na miili yao ilianza kuchakaa na kufa, kama Mungu alivyokwisha kusema. Rafiki, Neno la Mungu ni neno la hakika. Shetani ni mwongo na mdanganyi. Anataka kudanganya watu na kuwaaminisha ya kwamba Biblia imegeuzwa. Lakini Bwana Yesu Kristo anasema, *"Maandiko **hayawezi** kuvunjika!"* (Yoane 10:35) *"Mbingu na dunia zitapita, lakini maneno yangu **hayatapita kamwe**!"* (Matayo 24:35)

3) Ulizo la tatu ndilo hili: **Kwa sababu gani unaita Yesu *Mwana wa Mungu*? Mungu hazai, na Mungu hakuzaliwa, basi namna gani Yesu anaweza kuwa Mwana wake?**

Everyday Publications Inc @ 2010

Tumejibu ulizo hili kubwa mara nyingi mbele, lakini tunafurahi kulijibu tena. Ujinga juu ya neno kubwa namna hii unaweza kuzaa mauti! Uliuliza, "Kwa nini unaita Yesu *Mwana wa Mungu*?" Kwanza ni lazima kwa sisi kukumbusha wasikiaji wetu ya kwamba sisi hatukumpa Yesu jina hili la heshima "*Mwana wa Mungu!*" Ni **Mungu** ambaye anaita Yesu **Mwana wake**. Neno la pili ambalo inatupasa kukumbuka ni ya kama maana ya "Mwana wa Mungu" **si kusema** ya kwamba Mungu alikamata mke na kuzaa mwana! Kama tulivyoona mbele, Yesu alikuwa na mia za majina ndani ya Biblia. Majina haya yanatusaidia kufahamu kama Yesu ni nani. Kwa mfano, aliitwa ***"mlango"*** lakini maana ya jina hili haiko ya kwamba Yesu alikuwa mlango wa mti au chuma. Aliitwa vilevile ***"Chakula kinacholeta Uzima"*** (Mkate wa Uzima), lakini maana yake haiko ya kwamba Yesu ni chakula, kama mboga au samaki tunachokula. Manabii wa Mungu waliita Masiya ***"Mwana-Kondoo wa Mungu",*** lakini si kusema ya kwamba alikuwa kondoo. Vivyo hivyo, wakati Mungu anapoita Yesu Mwana wake, ingekupasa kufahamu ya kwamba maana yake haiko ya kwamba Mungu alikamata mke na kuzaa mtoto naye! Masemo namna hii ni makufuru! Nikitoka inchi yangu, wananiita "mwana wa Congo" kwa sababu niko Mkongomani. Maana yake haiko kusema Congo ilikamata mke na kuzaa mtoto! Vivyo hivyo, Mungu na malaika na manabii waliita Masiya "Mwana wa Mungu" kwa sababu alitoka kwa Mungu. Yesu alizaliwa na biki-

ra. Hakuwa na baba ya dunia. Hata mbele ya kuzaliwa kwake aliishi mbinguni, kwa sababu yeye ni *"Kalimat Allah"*, maana yake ***Neno*** aliyekuwa pamoja na Mungu katika mwanzo. Hili ndilo neno Maandiko yanayotangaza:

> *"Katika mwanzo alikuwa Neno, na Neno alikuwa pamoja na Mungu, na Neno alikuwa Mungu. Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu, tukatazama utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee akitoka kwa Baba, amejaa neema na kweli. . . Hakuna mtu aliyeona Mungu wakati wo wote; Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye alimfunua!"* (Yoane 1:1,14,18)

Yesu ni Mwana wa milele wa Mungu, Neno la Mungu aliyetokea duniani kwa mwili wa mtu.

Neno la Mungu ni nini? Labda utajibu kusema Neno la Mungu ni Maandiko Matakatifu ambayo Mungu aliongoza manabii kuandika. Ni kweli. Maandiko ya manabii wa Mungu ni Neno la Mungu kwa sisi—kama barua zinazotumwa kwetu na Mungu. Lakini uturuhusu kukuuliza juu ya rafiki yako anayeishi ndani ya mji mwingine. Ungependa nini zaidi: kwa rafiki yako kukuandikia **barua** tu, au kwa **yeye mwenyewe kufika kukuona**? Bila shaka ungependa kwa yeye kufika yeye mwenyewe ili muweze kuzungumuza uso kwa uzo. Basi Mungu ni mkubwa na hakuna neno ambalo linamshinda. Akitaka watu kujua kama yeye ni namna gani, na mapenzi yake kwa sisi watu, unafikili atatuandikia barua tu au atatufikia yeye mwenyewe? Rafiki, habari njema ambazo manabii walitangaza ni ya kwamba **Mungu atakuja yeye mwenyewe kwa sisi watu wenye zambi!**

Everyday Publications Inc. © 2010

Ndani ya Habari Njema, tunaona ya kwamba Mungu alituma Neno lake kama Mtu kukaa katikati ya watu ili aweze kuwaokoa toka zambi zao. Yule Mtu toka mbingu ni Yesu Kristo. Yesu anastahili kuitwa Mwana wa Mungu, kwa sababu yeye ni Neno aliyekuwa pamoja na Mungu katika mwanzo. Yesu ni Mwana wa Milele wa Mungu, mfano mkamilifu wa Mungu—mwenye kufunua tabia ya Mungu kwa watu. Mara nyingi tunasema juu ya kijana, "Anafanana sana na baba yake!" Ni vivyo hivyo na Yesu. Yesu ni namna ya Mungu. Kujua Yesu ni kujua kama Mungu ni namna gani. Hivi Maandiko yanasema:

> ***"Mungu, aliyesema zamani na baba zetu katika manabii*** *kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi,* ***katika siku hizi za mwisho***

> ***amesema nasi katika Mwana,*** *ambaye alimweka kuwa mriti wa vitu vyote, kwa yeye aliyefanya ulimwengu. Yeye akiwa kungaa kwa utukufu wake, na chapa ya nafsi yake mwenyewe, akichukua vitu vyote kwa Neno la uwezo wake, akikwisha kufanya katika yeye utakaso wa zambi zetu, aliketi mkono wa kuume wa Mwenye ukuu."* (Waebrania 1:1-3) Amina.

Neno moja lingine kwa kumaliza: Mungu hasemi ni lazima kwa wewe **kufahamu kwa sababu gani** anaita Yesu Mwana wake—lakini ya kwamba lazima **uamini neno hili.** Kumbuka, Mungu ndiye aliyeongoza nabii Daudi kuandika ndani ya Zaburi: *"Busuni **Mwana*** {maana kumpa heshima} *asikasirike, nanyi munapotea njiani, kwa kuwa hasira yake itawaka upesi. Heri wote ambao wanamkimbilia."* (Zaburi 2:12) Na ni Mungu aliyeongoza mtume Yoane kuandika ndani ya Habari Njema:

> *"Alama nyingi nyingine Yesu alifanya mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki;* ***lakini hizi zimeandikwa mupate kuamini ya kwamba Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mupate uzima kwa jina lake"*** (Yoane 20:30,31) ***"Anayeamini Mwana ana uzima wa milele; na asiyetii Mwana hataona uzima, lakini gazabu ya Mungu inakaa juu yake!"*** (Yoane 3:36)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, tutaendelea na maulizo na majibu mengine . . .

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya tangazo hili ndani ya Biblia:

> ***"Miili yote ni kama majani, na utukufu wao wote kama ua la majani. Majani yanakauka, na ua lake linaanguka; lakini Neno la Bwana linadumu kwa milele!"*** (1 Petro 1:24,25)

Everyday Publications Inc @ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Somo 91

# Maulizo ya Watu na Majibu ya Mungu

Sehemu 2

Salama iwe kwako rafiki msomaji. Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuja tena leo na mfulizo *Njia ya Haki.*

Leo tutaendelea na maneno tuliyoanza ndani ya somo la mbele—ndiyo kujibu **maulizo** tuliyopokea toka wasomaji. Mbele ya kuanza, kuna neno moja tunalohitaji kusema waziwazi, ndilo hili: Hatuna ukaramisu kutegemea akili yetu wenyewe au akili ya watu wengine kwa kujibu maulizo haya. Tunategemea **Neno la Mungu peke yake**. Sisi hatuna majibu, lakini **Mungu** ana majibu na ametupa sisi majibu haya ndani ya Maandiko Matakatifu. Biblia inasema: *"Neno la Mungu ni hai, lenye nguvu na ukali wa upanga unaokata ngambo mbili likitoboa hata kutenga nafsi na roho, na viungo na mafuta ndani ya mifupa; nalo ni jepesi kufahamu mawazo na makusudi ya moyo."* (Waebrania 4:12) Basi, sasa tuanze na maulizo haya.

Everyday Publications Inc. © 2010

1) Ndani ya barua hii msomaji anaandika: **Tulisoma ndani ya somo moja: "Maneno maovu hayawezi kutoka kwa Mungu." Sikubali neno hili, kwani ninaamini ya kwamba Mungu aliumba kwanza yaliyo maovu mbele ya kufanya yaliyo mema**.

Acha nijibu ulizo hili na ulizo ndani ya Biblia: *"Kuna chemchemi inayotoa maji matamu na machungu katika kisima kimoja?"* (Yakobo 3:11) Sivyo, hata moja. Kama chemchemi au kisima haviwezi kutoa maji matamu pamoja na maji ya chumvi, vivyo hivyo Mungu si mwanzo wa mema *na* maovu. Maandiko Matakatifu yanasema:

> *"Mungu ni **nuru**, wala **giza si ndani yake** kabisa!"* (1 Yoane 1:5)
> *"Mtu akijaribiwa, asiseme: Ninajaribiwa na Mungu: maana **Mungu***

> ***hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hajaribu mtu.*** *Lakini kila mtu anajaribiwa akivutwa na kudanganywa na tamaa yake mwenyewe. . . Ndugu zangu wapenzi, musidanganyike. Kila* ***zawadi njema, na kila zawadi timilifu*** *inatoka juu, inashuka kwa Baba ya nuru kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeukageuka. Kwa mapenzi yake mwenyewe alituzaa sisi kwa neno la kweli, tuwe kama malimbuko ya viumbe vyake."* (Yakobo 1:13,14,16-18)

Nabii wa Mungu, ndiye Habakuki, aliandika: *"Wewe si tangu milele hata milele, Ee Bwana Mungu wangu, mtakatifu wangu? . . . Wewe uliye na macho safi zaidi hata usiweze kutazama mabaya, na* ***usiyeweza kutazama ukaidi.*** *. ."* (Habakuki 1:12,13) Hivi kama Mungu hawezi kutazama maovu, haifai tuamini ya kwamba anaweza ku**umba** yaliyo maovu. Mungu aliumba malaika aliyeitwa Lusifero, lakini Lusifero aligeuka Shetani kwa njia ya kuchagua kuasi Mungu. Mungu aliumba Adamu, lakini Adamu aligeuka mwenye zambi kwa njia ya kuchagua kuasi Mungu. Neno la Mungu linatufundisha ya kwamba uovu unatoka kwa Shetani na moyo mzalimu wa mtu, lakini wema unatoka kwa Mungu na Neno lake.

Everyday Publications Inc @ 2010

2) Ulizo lingine: **Mungu akiwa mtakatifu na mwenye rehema, kwa nini anaangalia tu na macho magomvi na vita na wauaji na uovu duniani? Hawezi kufanya kitu kusaidia watu walio katika taabu?**

Kweli Mungu ni Bwana wa Rehema, na **amekwisha kufanya** neno ambalo ilimpasa kufanya kusaidia watu walio na taabu. Alituma Mkombozi mwenye haki, Yesu Kristo, kupatanisha watu na yeye mwenyewe, kisha kupatanisha watu na wenzao. Lakini, mbele ya watu kuweza kupatanishwa kabisa na wenzao, inawapasa kuamini kwanza Mwokozi ambaye Mungu alituma, na kumnyenyekea yeye. Tukiwa na ushirika mzuri na Mungu, tunaweza kuwa na ushirika mzuri na watu vilevile. Saa ile ile tunaweza kuwa na salama ya kweli. Hivi **ni kazi yetu kuchagua**. Sharti tupokee wokovu ambao Mungu aliweka tayari kwa sisi. Kumbuka vilevile ya kwamba Mungu atahukumu dunia hii kwa sababu ya uovu wake. Neno la Mungu linasema ya kwamba Bwana Yesu atarudi kwa mwisho wa muda huu na kuhukumu kila mtu anayekataa kweli na anayejifurahisha na uzalimu. Wakati Bwana Yesu atakapokwisha kushinda adui zote za Mungu, maneno haya yanayoandikwa ndani ya Maandiko yatatimizwa: ***"Haitakuwa laana yo yote tena*** *. . . mauti*

*haitakuwa tena; wala maombolezo, wala kilio, wala uchungu, kwa maana maneno ya kwanza yamekwisha kupita."* (Ufunuo 22:3; 21:4)

3) Ulizo la tatu leo ndilo hili: **Kuna neno moja ambalo linanisumbusha. Tangu zamani niliamini ya kwamba nikifanya zambi, zambi hii inaniumiza mimi tu, lakini ya kwamba haitaumiza watoto wangu kwa sababu wao hawakufanya zambi yenyewe. Lakini ndani ya kitabu hiki nilisoma ya kwamba zambi ambayo mzazi wetu Adamu alitenda ndani ya shamba la Paradiso ilienea kwa wazao wake wote, na ya kwamba ni lazima kwa Mungu kuwahukumu. Neno hili linawezekana namna gani?**

Watu wa kabila moja la Senegal wanasema: "Tauni halikwishi na mtu ambaye alilianza!" na "Paa mwenye kurukaruka hazai nyama mwenye kuchimba udongo tu." Maneno ya kweli kabisa, sivyo? Sisi sote tunajua ya kwamba ukizaa mtoto, na kumlea nyumbani mwako mwenyewe, ataanza kuonyesha tabia yako wewe mwenye kumzaa, kama ni tabia nzuri au mbaya, ataanza kusema kama wewe, kuishi na kuwaza na kufanya maneno namna wewe unavyoyafanya. Sisi sote ni ndani ya jamaa ya Adamu na Hawa. Tuko wazao wa wale walioasi agizo la Mungu. Sisi si sawasawa na wazazi wetu? Nani katikati yetu anayeweza kusema ya kwamba hajakwenda mbali na maagizo ya Mungu hata mara moja? Sisi sote tuna hatia. Tulizaliwa na tabia inayoasi maagizo ya Mungu. Tuliriti tabia hii toka nani? **Toka Adamu**. Kama ugonjwa mbaya, zambi ya Adamu imeenea kutupata sisi sote. Si neno kama tukikubali au sivyo, ni kweli kabisa hata hivi. Ni kweli inayotangazwa na Neno la Mungu wakati linaposema: *"Kwa* ***mtu mmoja zambi*** *iliingia ulimwenguni, na* ***kufa kwa njia ya zambi;*** *na hivi* ***kufa kulikuja juu ya watu wote****, kwa sababu* ***wote wamefanya zambi."*** (Waroma 5:12) Lakini kuna tumaini hata hivi kwa sababu Neno la Mungu linasema vilevile: *"Kama vile kwa* ***kosa moja*** *(la Adamu) watu wote walihukumiwa azabu, hivi kwa* ***tendo moja la haki*** *(la Yesu Kristo), watu wote walipewa haki yenye uzima."* (Waroma 5:18)

Everyday Publications Inc @ 2010

4) Sikia ulizo lingine: **Kwa nini Biblia ina sehemu mbili: Agano la Kale na Agano Jipya?**

Kwa ufupi, inakupasa kufahamu ya kwamba maneno ambayo manabii waliandika ndani ya Agano la Kale, ndiyo ndani ya **Agano la Kwanza**, waliandika **mbele ya** kuzaliwa kwa Masiya. Lakini maneno yote ndani ya **Agano Jipya** waliyaandika **nyuma ya** kuzali-

wa kwa Masiya. Hivi habari za manabii wa Mungu walioandika Agano la Kwanza zilikuwa: “Mungu **atatuma** Masiya!” Lakini, habari za Agano Jipya ni: “Mungu **ametuma** Masiya, kama alivyo-ahidi kwa njia ya manabii yake!” Hivi, inatupasa kushukuru Mungu kwa sababu Biblia ina sehemu mbili—Agano la Kanza **NA** Agano Jipya. Ndani ya sehemu hizi mbili, tunaweza kuona ya kwamba Mungu alitimiza ahadi aliyotoa zamani! Mungu ametuma Mwokozi, Yesu Kristo, kama alivyoahidi wazazi wetu ndani ya Tora, Zaburi na maandiko mengine ya manabii. Kama maji ya mito yanavyopita kwa bahari, vivyo hivyo Maandiko ya manabii yalitimizwa ndani ya Kristo.

5) Ulizo lingine: **Watu wanasema ya kwamba mtu hawezi kujua kama atafikia mbinguni au hadeze. Mungu tu anajua. Lakini wewe unasema unajua ya kama ukikufa leo, utakwenda mbinguni. Unaweza kusema hivi namna gani?**

Uturuhusu kujibu ulizo hili na ulizo lingine. **Mungu anaweza kuvunja ahadi yake?** Au Mungu ni mwaminifu na anatimiza neno lake? Neno la Mungu linasema:

Everyday Publications Inc
@ 2010

> *“Huyu [Yesu] manabii yote wanamshuhudia ya kwamba kwa jina lake* ***kila mtu ambaye anamwamini atapewa usamehe wa zambi.****”* (Matendo 10:43) *“Ninawaandikia ninyi wenye kuamini jina la Mwana wa Mungu, maneno haya,* ***ili mujue ya kuwa muna uzima wa milele****.”* (1 Yoane 5:13)

Mungu yeye mwenyewe alisema ya kwamba unaweza kujua kwamba una uzima wa milele. Basi namna gani tutabisha neno lake na kusema hakuna mtu anayeweza kujua pahali gani atakaposhinda kwa milele? Ndiyo, rafiki, **unaweza kujua** pahali gani utakapokwenda nyuma ya mauti. Tunakuuliza basi: Unaamini ndani ya Bwana Yesu Kristo na sadaka yake kamilifu kweli kweli? Au unategemea kazi zako “njema”? Watu wale tu wanaoamini Kristo kweli kweli wanaweza kusema na roho ya kweli, “**Ninajua** ya kwamba nina uzima wa milele!”

6) Mtu huyu anauliza: **Yesu alitangaza ya kwamba Msaidizi, “Parakletos,” atakuja nyuma yake. Alisema juu ya nani?**

“Parakletos” ni neno la Kiyunani, maana yake *mshauri, msaidizi,* au *mwombezi.* Ndani ya Maandiko Matakatifu neno hili linasema juu ya Yesu na Roho Mtakatifu vilevile (ona 1 Yoane 2:1). Kama tuli-

vyosoma ndani ya Habari Njema, mbele ya kurudi mbinguni, Bwana Yesu alitolea wanafunzi wake ahadi, akisema:

> *"Nitaomba Baba, naye atawapa ninyi* ***Msaidizi mwingine****, akae nanyi hata milele,* ***Roho ya kweli,*** *ambaye dunia haiwezi kumpokea; kwani haimwoni wala haimjui; lakini ninyi munamjua, kwa sababu anakaa* ***pamoja nanyi,*** *naye atakuwa* ***ndani*** *yenu. . . Msaidizi,* ***Roho Mtakatifu,*** *ambaye Baba atamtuma* ***kwa jina langu****, yeye atawafundisha ninyi yote, na kuwakumbusha ninyi yote ambayo niliwaambia ninyi. . . Wakati anapokuja, atahakikisha dunia maneno ya zambi, na maneno ya haki, na maneno ya hukumu; kwa maneno ya zambi, kwa sababu hawaniamini mimi . . . [Hivi] akawaagiza wasitoke Yerusalema, ila wangoje* ***ahadi*** *ya Baba muliyosikia kwangu; kwani Yoane alibatiza kwa maji, lakini ninyi mutabatizwa katika* ***Roho Mtakatifu*** *nyuma ya siku si nyingi."* (Yoane 14:16,17,26; 16:8,9; Matendo 1:4,5)

Maneno Bwana Yesu aliyosema yanatufahamisha ya kwamba Mshauri huyu **si mtu**, lakini **Roho**—Roho Mtakatifu wa Mungu—ambaye hakuna mtu anaweza kuona. Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi wake ya kwamba nyuma ya kurudi kwake mbinguni Mungu atatuma Roho Mtakatifu kuishi ndani ya mioyo yao. Masomo machache mbele tulisoma ya kwamba hili ndilo neno lililotokea siku ya Pentekote, siku kumi nyuma ya kupanda kwa Yesu mbinguni.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Kwa ufupi, Mshauri ni Roho ya Kristo atakayekuja kuishi ndani ya mioyo ya wote wanaoamini Habari Njema. Kama wewe ukiamini na roho ya kweli, Roho Mtakatifu atasafisha na kufanya mpya moyo wako. Atakutia alama (au muhuri) kuonyesha kwamba wewe ni mtoto wa Mungu kabisa, na atakuwezesha kukaa mbele ya Mungu Mtakatifu kwa milele. Haya ndiyo maneno Maandiko yanayotangaza:

> *"Ndani yake ninyi vilevile, wakati muliposikia neno la kweli, Habari Njema ya wokovu wenu . . . mumekwisha kuamini vilevile na* ***kutiwa muhuri wa Roho Mtakatifu ya ahadi . . . aliye arabuni ya uriti wetu,*** *ili kuleta ukombozi kwa mali yake mwenyewe, kuwa sifa ya utukufu wake."* (Waefeso 1:13,14)

Kwa sisi tunaoamini, Roho Mtakatifu ni msaidizi wetu, mwongozi, nguvu, mwalimu, na maneno mengi mengine. Anafanya maneno mengi kwa sisi—hatuwezi kuyataja yote. Neno moja ndilo

maombi. Kuna tofauti kabisa katikati ya *kusema tu ombi fulani* na *kuomba kweli kwa Mungu*. Roho Mtakatifu anatusaidia kuomba maombi ya kweli kwa Mungu. Tunasoma ndani ya Maandiko: *"Roho anasaidia uzaifu wetu; kwa maana hatujui kuomba kitu namna inavyotupasa, lakini Roho mwenyewe anatuombea kwa kuugua kusikoweza kusemwa."* (Waroma 8:26) Wote wanaoamini Habari Njema ya Yesu Kristo kweli wana Mgeni huyu toka mbingu, Roho Mtakatifu akiishi ndani yao. Maandiko yanasema: ***"Mtu ye yote asipokuwa na Roho ya Kristo huyu si mtu wake."*** (Waroma 8:9)

7) Mwenye maulizo ya mwisho anaandika: **Nimefahamu kwa njia ya mafundisho yako ya kuwa nitakwenda Paradiso kama nikipokea Yesu Kristo kuwa Mwokozi wangu. Ni kusema ya kwamba ninaweza kuishi namna ninavyotaka na kufanya maneno maovu na kufikia Paradiso hata hivi wakati nitakapokufa? Biblia inafundisha nini?**

Maandiko yanajibu ulizo hili waziwazi ndani ya kitabu cha Waroma, sura 6, pahali tunaposoma, *"Tudumu katika zambi, neema izidi sana? Hapana, hata kidogo. Sisi tuliokufia zambi, namna gani tutakaa ndani yake tena?"* (Waroma 6:1,2) Habari za mauti ya Yesu Masiya juu ya msalaba na ufufuko wake toka kaburi ni shauri la haki la Mungu **kuokoa wenye zambi** si toka **azabu ya zambi** tu lakini toka **uwezo wa zambi** vilevile! Ukipokea Habari Njema moyoni mwako na imani ya kweli, Neno la Mungu linafundisha ya kwamba, kwa dakika ile ile unapoamini, Mungu atafanya kazi mbili ndani yako:

Everyday Publications Inc @ 2010

**Kwanza: Mungu atasamehe zambi zako zote** kwa jina la Kristo, kama alivyoahidi.

**La pili: Mungu atakupa moyo mpya** kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Halafu utaanza kupenda haki na kuchukia uovu, kwa sababu Mungu ameweka tabia yake takatifu ndani yako. Hivi, Maandiko yanaahidi:

> *"Kama mtu akiwa ndani ya Kristo, yeye ni kiumbe kipya; maneno ya zamani yamepita; tazama, maneno yote yamekuwa mapya!"* (2 Wakorinto 5:17) *"Yesu Kristo . . . ambaye alijitoa mwenyewe kwa ajili yetu atukomboe* ***toka uovu wote****, na* ***kujisafishia*** *watu wawe mali yake mwenyewe,* ***wenye bidii sana katika kazi njema.****"* (Tito 2:14)

Wakati mtu anapoamini Bwana Yesu Kristo kweli kweli, hataweza kuishi namna inavyompendeza na kutenda maovu, kwa

sababu Mungu aliweka **Roho Mtakatifu** ndani yake—na *"matunda ya Roho ni mapendo, furaha, salama, uvumilivu, neema, wema, uaminifu, upole, ujizuiza."* (Wagalatia 5:22,23)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, tutawaza tena juu ya ulizo hili, ndilo kama inapasa mfuata wa Kristo kuishi namna gani.

Mungu akubariki. Tunaagana nawe leo na shairi hili la nabii Daudi toka Zaburi:

> ***"Mungu, njia yake ni kamilifu, neno la Mungu limejaribiwa; yeye ni ngabo kwao ambao wanamwekea tumaini lao."*** (Zaburi 18:30)

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## SOMO 92

# INAPASA MWANAFUNZI WA KRISTO KUISHI NAMNA GANI?

Salama kwako, rafiki. Tunakukumbusha tena kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, kuweka roho juu ya kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, ili uweze kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tuendelee sasa na somo lingine la mfulizo *Njia ya Haki.*

Kama tulivyosema ndani ya somo la mbele, tunakusudi kuwaza juu ya **namna gani inapasa wafuata wa Yesu Kristo kutembea kwa kupendeza Mungu.** Ingepasa imani ambayo mwanafunzi ana moyoni mwake kuonekana ndani ya mawazo yake, ndani ya matendo na masemo yake, ndiyo, kwa maneno yote ya maisha yake.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Mbele ya kuwaza juu ya mwenendo wa mwanafunzi wa Kristo, tujikumbushe tena kama nini inageuza mtu kugeuka mwanafunzi wa kweli wa Kristo. Kama tulivyoona mbele, mwanafunzi wa Kristo ndiye mtu aliyekubali ya kwamba yeye ni mwenye zambi mbele ya Mungu, na asiye na tumaini kufikia Paradiso kwa njia ya kazi zake mwenyewe. Ni mtu anayeamini shauri ambayo manabii wote wa Mungu walitangaza—shauri linalowezesha Mungu kusamehe zambi za wana wa Adamu. Shauri hili lilikuwa mauti ya Yesu Kristo juu ya msalaba. Mungu alitoa Mkombozi asiye na zambi afe kwa zambi zetu na kumfufua tena kusudi aweze kutuhesabu kuwa wenye haki.

Kwa kujumlisha, **mwanafunzi wa Kristo ndiye mtu anayeamini Habari Njema ya Yesu Masiya na roho yake yote** na anayejua kabisa ya kwamba zambi zake zote zimesamehewa, kama Mungu alivyoahidi ndani ya Neno lake. Mungu anaingiza mwamini namna hii ndani ya jamaa yake kama mtoto wake. Hivi iliandikwa ndani ya Habari Njema: Wale wanaopokea Yesu Masiya na kuamini jina lake wamepewa *"uwezo wa **kuwa watoto wa Mungu**, waliozaliwa si . . . kwa mapenzi ya mwili . . . lakini kwa Mungu."* (Yoane 1:12,13) Rafiki,

Mungu anataka ujue ya kwamba ukigeuka mtoto wa Mungu kwa njia ya imani ndani ya Kristo na sadaka yake, hutapotea milele, naye atakupa haki kwa kuishi mbele yake kwa milele, katika Paradiso!

Labda wengine wangependa kubishana na neno hili, wakisema: Lakini kama ni nyepesi hivi kwa mwanafunzi wa Kristo kuingia Paradiso, halafu ataweza kuishi namna yeye anavyotaka na kutenda zambi kama ikimpendeza, bila kuogopa hukumu, kwa sababu Mungu anakwisha kusamehe zambi zake zote! Rafiki, mawazo namna hii ni **mapumbavu.** Wale wanaofikili hivi hawajafahamu bado kama zambi ni nini, wala hawajui Mungu Mtakatifu. Zambi ni neno baya. Yesu Kristo alikuja kutu**ponyesha** toka utumwa wa zambi; hakuja kutupa sisi ruhusa kukaa kuendelea ndani ya zambi. Mtu ye yote anayeamini Kristo **si mtumwa wa zambi tena.** Ndiyo, wale tu walio watu wa Shetani wanaweza kufurahi kutenda zambi. Mungu akiokoa mtu, anageuza roho yake. Anaiosha na kuisafisha. Mtu aliyetendewa hivi na Mungu ataepuka uchafu wo wote. Kwa sababu hii, Maandiko yanatangaza: *"Kama mtu akiwa ndani ya Kristo, yeye ni kiumbe kipya; maneno ya zamani yamepita; tazama, maneno yote yamekuwa mapya!"* (2 Wakorinto 5:17)

Everyday Publications Inc
@ 2010

Unafikili nini? Ukivaa vazi safi jeupe, utaketi au kutembea kwa pahali pachafu? Sivyo, utaepuka kitu cho chote kinachoweza kuchafua mavazi yako. Ni vivyo hivyo na kila mtu aliyesafishwa na Mungu toka zambi zake. Hutataka kufungana tena na neno lo lote lisilopendeza Mungu. Uta**taka** kupendeza Bwana. Mtu akisamehe deni yako kubwa sana, utatenda na kusudi neno ambalo itamwumiza? Sivyo, utafanya neno lo lote unaloweza kufanya kumpendeza. Vivyo hivyo, ikiwa Bwana Mungu amesamehe deni yako kubwa ya zambi na kukuokoa toka azabu ya milele, hutamshukuru na kumheshimu ndani ya mawazo na masemo ya matendo yako maisha yako mazima?

Sikiliza maneno Habari Njema inayotangaza juu ya wale walio watu wa Bwana Yesu, Katika Tito 3 tunasoma:

> (Tito 3) *3 Kwa sababu zamani sisi vilevile tulikuwa pasipo akili, wenye kuasi, tumedanganywa, tukitumikia tamaa na anasa za namna nyingi, tukiishi katika uovu na hasidi, tukichukiza na kuchukiana. 4 Lakini wakati wema wa Mungu Mwokozi wetu, na mapendo yake kwa watu yalipoonekana, 5 si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyofanya lakini kwa rehema yake alituokoa, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa mpya na kufanywa upya na Roho Mtakatifu; 6 ambaye alimwan-*

*ga juu yetu, kuzidi sana, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu; tukihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa wariti kwa tumaini la uzima wa milele.* Na kwa 1 Petro imeandikwa: *14 Kama wana wa kutii musijifananishe na tamaa zenu za kwanza, za ujinga wenu; 15 lakini kama yeye ambaye aliwatia ninyi ni mtakatifu, ninyi vilevile muwe watakatifu katika mwenendo wenu wote; 16 maana imeandikwa:* ***Muwe watakatifu: kwa kuwa mimi ni mtakatifu."***

Tunaweza kujumlisha mwenendo wa mwanafunzi wa Yesu namna gani? Tunaweza kusema ya kwamba Mungu anataka watoto wake kuonyesha tabia yake ndani ya mwenendo wao hapa duniani. **Ndiyo, Mungu anataka watoto wake kuwa sawasawa naye**. Basi, Mungu ni namna gani? Ndani ya majifunzo katika Maandiko Matakatifu tumeona ya kwamba maneno makubwa mawili ya tabia ya Mungu ni utakatifu na mapendo. Yeye ni Mungu Mtakatifu. Yeye ni Mungu wa mapendo vilevile. Hivi mapenzi yake kwa sisi tulio mali yake ni nini? **Anataka tuwe watakatifu, kama yeye ni mtakatifu, na kupendana namna yeye anavyotupenda sisi.**

Everyday Publications Inc
@ 2010

Hivi kwa njia ya kuwa na mwenendo mtakatifu na roho ya mapendo wale walio mali ya Mungu ni mbali na wale wasio watu wake. Juu ya neno hili, Neno la Mungu linasema:

(1 Yoane 3) *10 Hivi watoto wa Mungu wanaonekana wazi, na watoto wa Shetani; mtu ye yote asiyetenda haki hatoki kwa Mungu, wala yeye asiyependa ndugu yake.* (Tito 2) *11 Kwa sababu neema ya Mungu inayoleta wokovu kwa watu wote, imeonekana, 12* ***ikitufundisha sisi kukataa ubaya na tamaa ya dunia,*** *na kuishi na kiasi kwa haki na utawa, katika ulimwengu wa sasa, 13 tukitazamia tumaini la baraka, na kuonekana kwa utukufu wa Mungu mkubwa, Mwokozi wetu Yesu Kristo; 14 ambaye alijitoa mwenyewe kwa ajili yetu* ***atukomboe toka uovu wote, na kujisafishia watu wawe mali yake mwenyewe, wenye bidii sana katika kazi njema.***

(Waefeso 4) *25 Kwa hivi,* ***mukiondosha uwongo****, museme kweli kila mtu na jirani yake; kwa maana sisi ni viungo, kila mmoja kiungo cha mwenzake. 26 Mukasirike na musifanye zambi; jua lisishuke na uchungu wenu haujakwisha bado; 27 wala musimpe Shetani nafasi. 28 Yeye aliyeiba* ***asiibe tena****; lakini zaidi atumike akifanya kazi njema kwa mikono yake, awe na* ***kitu cha kugawia mwenye kuhitaji****. 29 Masemo maovu yasitoke vinywani mwenu, lakini yaliyo mema kwa kujenga kama inavyohitajiwa, yawape neema wale wanaosikia. 30*

*Wala* ***musihuzunishe Roho Mtakatifu ya Mungu,*** *ndani yake mulitiwa mhuri hata siku ya ukombozi. 31* ***Uchungu wote na hasira na kasirani na kelele na matukano yaondoshwe kwenu,*** *pamoja na kila namna ya ubaya, na mwonyeshe mema ninyi kwa ninyi, muwe wenye huruma, mukisameheana, kama Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.*

(Waefeso 5) *1 Basi* ***mufuate Mungu*** *kama watoto wanaopendwa; 2 na mutembee katika mapendo, kama Kristo vilevile alivyowapenda ninyi na kujitoa mwenyewe kwa ajili yetu, toleo na zabihu kwa Mungu, kuwa harufu ya manukato. 3 Lakini uasherati* ***usitajwe*** *katikati yenu, wala uchafu wo wote wala kutamani, kama inavyostahili watakatifu; 4 wala aibu wala masemo yasiyo na maana, wala maneno ya kuchekesha yasiyofaa; lakini zaidi maneno ya kushukuru. 5 Maana munajua kabisa, ya kwamba hakuna mwasherati wala mtu mchafu wala mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu, ana uriti katika ufalme wa Kristo na Mungu. . . 8 kwa maana zamani mulikuwa giza, lakini sasa mumekuwa nuru katika Bwana;* ***mutembee kama watoto wa nuru.*** (1 Yoane 4) *7 Wapenzi, tupendane; kwa kuwa mapendo ni ya Mungu, na kila mtu anayependa amezaliwa na Mungu. 20 Kama mtu akisema: Ninapenda Mungu, naye anachukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyependa ndugu yake ambaye alimwona, hawezi kupenda Mungu ambaye hamwoni. 21 Na amri hii tumepewa naye;* ***mwenye kupenda Mungu inampasa kupenda ndugu yake vilevile.***

Everyday Publications Inc @ 2010

Haya ndiyo maneno Maandiko yanayosema juu ya mwenendo wa wale wanaofuata Yesu Kristo. Ni kusema ya kwamba mfuata wa Kristo hawezi kufanya zambi tena, au ya kwamba anapenda jirani yake kama yeye mwenyewe kila mara? Sivyo! Anakaa kufanya zambi, lakini hakwamani na zambi. Wakati anapofanya zambi, anaweza kutumia ahadi ndani ya Neno la Mungu linalosema: (1 Yoane 1) *7 . . . damu yake Yesu Kristo . . . inatusafisha zambi zote. 8 Kama tukisema kwamba hatuna zambi, tunajidanganya wenyewe, wala kweli si ndani yetu. 9* ***Tukikiri zambi zetu****, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee zambi zetu, na kutusafisha na uzalimu wote.* Amina.

Kuwa mtu wa Yesu Kristo **si dini tu**—ni **undugu**. Wakati mtu ni mali ya Kristo, anaingizwa ndani ya **ushirika na Mungu mtakatifu wa mapendo.** Adamu na Hawa walipoteza undugu huu na Mungu wakati walipofanya zambi, lakini undugu huu unarudishwa kwetu kwa njia ya damu ambayo Yesu alimwanga juu ya msalaba. Mungu hatakumbuka makosa yetu tena kwa sababu Yesu alitulipia deni

yetu ya zambi. Kwa sababu sisi ni ndani ya Kristo, Mungu ni Baba yetu ya mapendo, na sisi ni watoto wake. Hii ndiyo maana ya Maandiko wakati yanaposema: *"Kwa maana kwa yeye [Kristo] sisi sote tumepata njia ya kukaribia Baba katika Roho mmoja. Basi tangu sasa sisi si* ***wageni*** *na wasafiri tena, lakini wenyeji pamoja na watakatifu, na* ***watu wa nyumba ya Mungu.****"* (Waefeso 2:18,19)

Wale walio ndani ya Kristo wanaweza kufurahi ndani ya ushirika mtamu duniani na kutazamia uriti wa milele mbinguni. Lakini labda unauliza, namna gani mwanafunzi wa Kristo anaweza kufurahi ndani ya ushirika huu na Mungu wakati yeye ni duniani? Namna gani tunaweza kupata nguvu ndani ya ushirika wetu na Mungu? Juu ya neno hili, Neno la Mungu linataja **maneno mane** ambayo yatatusaidia kutambua mapenzi ya Mungu na kuishi maisha yanayopatana na mahali yetu ya wana wa Mungu ili tuweze kumpendeza ndani ya maneno yote na kuongezeka katika kujua Mungu.

1) Neno la kwanza ndilo hili: Inapasa mwanafunzi wa Kristo **kujikulisha na Neno la Mungu** kila siku, akiwaza juu yake na kulipokea moyoni mwake na hamu ya kulitii. Maandiko Matakatifu yanafunua mapenzi ya Mungu. Mungu anasema nasi kwa njia ya Neno lake. Neno la Mungu linalisha roho yetu na kuipatisha nguvu. Ni chakula cha ajabu. Mtu ye yote anayependa Mungu kweli hahitaji maonyo kusikiliza Neno la Mungu, kwa sababu atakuwa na njaa kwa Neno la Mungu namna alivyo na njaa kwa chakula cha mwili. Nabii Yobu alisema, *"Nimefikili maneno ya kinywa chake [Mungu] kuliko chakula changu!"* (Yobu 23:12)

Everyday Publications Inc @ 2010

2) Neno la pili ni **kuomba kwa Mungu**, Baba yetu aliye mbinguni. Mtu ye yote anayetaka kupata nguvu ndani ya ushirika wake na Mungu atataka kusemezana naye mara nyingi. Kwa mwanafunzi wa Kristo, maombi ni kusemezana na Mungu, namna unayoweza kusema na rafiki yako ya karibu zaidi. Hakuna saa fulani inapotupasa kuomba. Tunaweza kusemezana na Baba yetu ya mbinguni saa yo yote ya usiku au mchana! Ingepasa awe ndani ya mawazo yetu saa zote. Anataka tukae kumshukuru na kumpa asante daima kwa sababu yeye ni Mungu na kwa maneno makubwa ambayo ametufanyia. Anataka tumwambie vilevile maneno ambayo yanatusumbusha. Mwanafunzi wa Kristo anajua kwamba maombi yana uwezo. Bwana Yesu aliahidi wanafunzi wake ya kwamba *"mukiomba neno gani kwa jina langu, nitalifanya."* (Yoane 14:14) na, *"Musijisumbushe wenyewe kwa neno lo lote; lakini katika kila neno kwa kuomba na kusihi pamoja na kushukuru maombi yenu yajulikane na Mungu [Baba yenu]"* (Wafilipi 4:6)

3) Neno kubwa la tatu ni **ushirika** na wengine wanaoamini na kupenda Bwana Yesu Kristo. Kama kala linavyokaa na moto muda mrefu kupita kama likiachwa ndani ya moto pamoja na makala mengine, vivyo hivyo ushirika wetu na waamini wengine utatusaidia kuishi kwa Kristo na kuwapa waamini wengine hamu kufanya vivyo hivyo. Neno la Mungu linasema:

> *"Tuangaliane kwa njia ya kusukumana katika mapendo na kazi nzuri; tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; lakini tukionyana, zaidi sana munavyoona siku ile inakaribia."* (Waebrania 10:24,25)

4) Neno la ine linalofaa kwa wanafunzi wa Kristo ni kuwa **washuhuda wake**. Sikiliza maneno ambayo Yesu aliwaambia wanafunzi wake mbele ya kupanda mbinguni: *"Hili ndilo manabii waliyoandika: Itapasa Kristo kuteswa na kufufuliwa.* Inapasa wanafunzi kuwaambia wengine juu ya Mwokozi wao, wakieleza Habari Njema ya Yesu Kristo aliyekufa kuwapa wote ambao wanamwamini upatano wa karibu wa ajabu sana na Mungu kwa milele. Ndiyo, haitoshi kwa sisi kutoa ushuhuda na masemo tu, lakini pamoja na masemo haya tuwe na maisha matakatifu na mapendo. Kristo akigeuza maisha na mwenendo wetu, ushuhuda wetu utakuwa na uwezo. Maana Maandiko yanasema: *"Ufalme wa Mungu si katika neno, lakini katika uwezo!"* (1 Wakorinto 4:20)

Everyday Publications Inc
@ 2010

Msomaji, kuna siku moja katika maisha yako wakati ulipokutana na Mwokozi Yesu Kristo, siku wakati aliposamehe zambi zako na kufanya mpya moyo wako? **Maisha yako yanajaa sasa na utakatifu na mapendo ya Mungu?** Wewe ni mwanafunzi wa kweli wa Bwana Yesu?

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Mungu akubariki wakati uanpowaza juu ya neno Maandiko Matakatifu yanalotangaza:

> ***"Mungu ni nuru, wala giza si ndani yake kabisa. Kama tukisema ya kwamba tunashirikiana naye, tena tukitembea katika giza, tunasema uwongo, wala hatufanyi yaliyo kweli."***
>
> (1 Yoane 1:5,6)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Somo 93

# Ukumbusho #1
# Adamu, Neno Gumu la Zambi

Mwanzo 1-4, na nyingine

Salama iwe kwako, rafiki msomaji. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuja tena leo kuendelea na mfulizo *Njia ya Haki.*

Tumejifunza sasa Maandiko ya Manabii kwa siku nyingi. Tumeona ya kwamba Mungu aliongoza zaidi ya watu makumi ine (katika muda wa kupita miaka 1500) kuandika Kitabu chake—Kitabu kinachofunua njia ya haki kwa njia yake wenye zambi wanaweza kugeuka wenye haki mbele ya Mungu. Tuliona ya kwamba manabii wote wa kweli wa Mungu walishiriki wazo moja na tangazo moja juu ya njia ya wokovu. Maneno waliyoandika hayakutoka ndani ya nia zao wenyewe, lakini yalitoka kwa Roho ya Mungu. Mungu akitusaidia, **leo na ndani ya masomo matatu mengine,** tunakusudi kufanya **ukumbusho** na jumlisho la maneno yote tuliyojifunza ndani ya Maandiko Matakatifu. Somo letu la leo linaitwa **"Neno gumu la zambi."**

Everyday Publications Inc @ 2010

Sasa turudi kwa **msingi Mungu alioweka yeye mwenyewe**, sehemu ya kwanza ya Neno la Mungu, ndiyo **Tora**, Mungu aliyoweka ndani ya nia ya Musa, nabii wake. Unakumbuka shairi la kwanza? Linasema: ***"Katika mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia."*** Ndani ya shairi hili tuliona ya kwamba, katika mwanzo, wakati ulimwengu na malaika na watu wasipoumbwa bado, **Mungu tu alikuwa.** Mungu ni Bwana wa milele, Roho ya milele. Hana mwanzo wala mwisho. Yeye ni mwenye uwezo wote anayeona maneno yote na kujua maneno yote.

Ndani ya sura ya kwanza, tulisoma namna Mungu, ndani ya siku sita, aliumba mbingu, dunia, bahari na viumbe vyote ndani yao. Mungu alikusudi kuumba mtu na alitayarisha dunia kwaye kukaa ndani yake. Kwa sababu hii alisema, siku ya sita,

> *"Tufanye mtu kwa mfano wetu, mwenye sura yetu, na watawale juu ya samaki za bahari na juu ya ndege za hewa na juu ya ngombe, na juu ya inchi nzima, na juu ya kila mtambazi anayetambaa juu ya inchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake mwenyewe . . ."* (Mwanzo 1:26,27)

Mtu **anajulikana kupita viumbe vyote vingine ambavyo Mungu aliumba**, kwa sababu Mungu alimwumba kwa sura yake mwenyewe! Mungu alikusudi kuwa na ushirika wa karibu, wa ajabu sana na mtu. Kwa sababu hii aliweka ndani ya nafsi wa mwanamume na mwanamke, **roho** kusudi waweze kujua Mungu, aliwapa **moyo** kusudi waweze kupenda Mungu, na **uwezo wa kuchagua** wao wenyewe kama watatii Mungu au kama watamwasi.

Ndani ya sura 2, tulisoma ya kwamba Mungu aliweka mwanamume wa kwanza, Adamu, ndani ya shamba zuri, lenye miti iliyozaa matunda yaliyoonekana mazuri sana na yaliyokuwa matamu kwa kula. Tuliona vilevile ya kwamba Mungu alifanya mwanamke toka mfupa wa mbavu ya Adamu, na kumleta kwa Adamu. Adamu alimwita Hawa. Mungu alibariki mwanamume na mwanamke na kuwapa vyote walivyohitaji. Lakini kulikuwa kitu kimoja Mungu alichotaka kupokea toka kwao. Mungu alitaka nini toka watu hawa wawili ambao aliumba kwa sura yake mwenyewe? Alitaka **wampende** na nia, moyo, na kutaka kwao wenyewe, na kwa njia hii kuwa na ushirika mtamu na wa ajabu sana naye kwa milele. Hivi Mungu aliwapa **pimo** kufunua kama nini ilikuwa ndani ya mioyo yao. Mungu alitolea Adamu agizo hili: *"Wa kila mti wa shamba unaweza kula; lakini wa mti wa kujua uzuri na ubaya usile kwa maana siku unapokula **hakika utakufa**!"* (Mwanzo 2:16,17) Hivi Mungu alipima Adamu na kumwonya ya kwamba mwisho wa kuasi sheria utakuwa mauti, maana **kutengwa na Mungu kwa milele.**

Everyday Publications Inc
@ 2010

Ndani ya sura 3, Maandiko yanapasha ya kwamba siku moja Shetani, malaika aliyeasi Mungu mbele, alifikia Adamu na Hawa kama nyoka ya hila. Alisema na mwanamke,

> *"Mungu amesema: Musile ya miti yote ya shamba? Mwanamke akamwambia nyoka: Matunda ya miti ya shamba tunaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya shamba Mungu amesema: Musile yake wala musiyaguse, musife. Nyoka akamwambia mwanamke: Hakika hamutakufa, kwani Mungu anajua ya kama siku mutakapokula matunda yake, macho yenu yatafunguliwa, na mutakuwa kama Mungu mukijua uzuri na ubaya."* (Mwanzo 3:1-5)

Mungu alisema na Adamu na Hawa nini itatokea kama wakikula ya mti ambao aliwakataza kula? Alisema nao, "Muta**kufa!**" Shetani alisema nini? Alisema, "**Ha**mutakufa!" Adamu na Hawa walichagua kuamini na kufuata neno la nani? Walichagua neno la Mungu, au neno la Shetani? **Walichagua neno la Shetani, adui ya Mungu!**

Halafu Mungu alifanya nini? Alitazama Adamu na Hawa na macho tu? Sivyo. Alifanya neno lile lile ambalo aliwaonya mbele kwamba atafanya. Aliwaita, aliwahukumu, aliwalaani pamoja na udongo, kisha aliwaweka inje ya shamba lile zuri ambalo alikuwa amewatengenezea. Siku ile ya huzuni, Adamu na Hawa walikufa ndani ya roho zao. **Walitengwa na Mungu**, mwenye kutoa uzima. Waliweza kungojea neno moja tu sasa, ndilo mauti ya mwili na azabu ya milele, kwa sababu malipo kwa zambi ni mauti ya milele, kama Mungu alivyosema.

Kweli, zambi ni msiba mkubwa. Adamu na wazao wake wote walitengwa na Mungu kwa sababu ya zambi moja tu! Zambi inafanana na ugonjwa unaoitwa AIDS kwa njia nyingine. Kama munavyojua, AIDS ni ugonjwa watu wanaosambaza katikati yao. Ni msiba duniani pote. Wakati virus ya AIDS inapokwisha kuingia mwili wa mtu, haitamwondokea tena kamwe. Wale walio na AIDS wanaweza kuieneza kwa watoto wao. AIDS ni mwuaji na inaua watu wote walio na ugonjwa huu. **Zambi** ni hivi. Zambi ni pahali po pote, ndani ya kila mtu na inafanyiza watu kupotea kwa milele. Lakini asante kwa Mungu, kuna tofauti kwa gonjwa hizi mbili, ugonjwa wa zambi na ugonjwa wa AIDS. Hakuna dawa kwanza kuponyesha AIDS, lakini kuna njia ku**ponyesha watu wanaochafuwa na zambi**! Mungu yeye mwenyewe alitayarisha njia kwa sisi kupona na kusafishwa toka zambi kwa milele, kama tukiipokea.

Unakumbuka **ahadi ya ajabu** Mungu aliyotoa siku Adamu na Hawa walipofanya zambi? Ndiyo, siku ile ile zambi ilipoingia duniani, Mungu aliahidi kutuma duniani Mkombozi mtakatifu, atakayekomboa wana wa Adamu toka uwezo wa kuharibu wa Shetani na zambi. Tulisoma vilevile tangazo la Mungu ya kwamba Mkombozi huyu atazaliwa na mwanamke bikira, kwa sababu Mwokozi wa wenye zambi hakuweza kuja toka wazao wa Adamu waliochafuwa wote na zambi. Sharti aje toka Roho safi na takatifu ya Mungu.

Hivi tuliona ndani ya Habari Njema {*Injil*} ya kwamba elfu za miaka nyuma ya ahadi ya Mungu kutuma Mkombozi huyu, wakati

Everyday Publications Inc @ 2010

saa ilipokubaliwa na Mungu ilipofika, Mwanamume mwenye haki kabisa alizaliwa duniani; hakuwa na baba ya dunia; alizaliwa na bikira. Jina lake lilikuwa **Yesu**, maana yake *Mungu anaokoa*. Ndiyo, Yesu Kristo ni Mkombozi mtakatifu ambaye Mungu aliahidi kutuma siku ile wakati Adamu na Hawa walipofanya zambi. Yeye ni Mwokozi wa pekee.

Sasa turudi tena kwa ukumbusho wetu wa maneno yaliyotokea siku zambi ilipoingia duniani. Unakumbuka kama Adamu na Hawa walifanya nini nyuma ya kula tunda la mti wa kujua uzuri na ubaya? Walishona majani ya mtini pamoja kuwa mavazi kufunika haya yao, kwa sababu mbele ya kufanya zambi walikuwa watupu. Mungu alikubali mavazi ambayo walijifanyia? Alitaka kuwafundisha ya kwamba hakuna tendo la mtu linaloweza kufunika haya ya zambi yake mbele ya Mungu! Hivi Mungu alifanya kitu kimoja kwa Adamu na Hawa. Tuliona namna Mungu alivyochagua nyama wasiokuwa na zambi, akawachinja, akaondosha ngozi zao, akafanya mavazi kwa Adamu na Hawa, akawavalisha nao. Kwa njia hii Mungu alifundisha Adamu na Hawa ya kwamba **malipo kwa zambi ni mauti**! Ndiyo, Mungu alifanya sadaka ya nyama, na aliagiza Adamu na wazao wake kuua nyama wasiokuwa na kipunguo na kuzitoa kama sadaka kufunika zambi, kufika wakati Mungu atakapotuma Mkombozi mtakatifu, Masiya, Mwokozi toka mbinguni.

Everyday Publications Inc @ 2010

Hivi Mungu aliwaonyesha wazi ya kwamba kuna **njia moja tu ya wokovu: njia ya sadaka bila kipunguo**. Njia ya haki ambayo Mungu aliamuru iliagiza mtu kuchagua nyama bila kipunguo na kuzichinja kama sadaka zinazofunika zambi. Sadaka hizi zilikuwa **mfano wa Mkombozi mtakatifu**, atakayekuja na kumwanga damu yake juu ya msalaba kulipa deni ya zambi ya wazao wa Adamu. Hivi, kwa njia ya sadaka zile za nyama, Mungu alionyeshea wenye zambi mfano wa Yesu Masiya atakayekufa kama sadaka inayoondoa zambi. Kwa njia hii Mungu alihakikisha ya kwamba yeye ni mwenye haki, hata kama katika uvumilivu wake aliachilia zambi zilizofanywa zamani (Waroma 3:25,26).

Ndani ya sura inayofuata habari za zambi ya Adamu na ahadi ya ajabu ya Mungu kutuma Mkombozi, tulisoma juu ya wana wawili wa kwanza wa Adamu, Kaina na Abeli. Tuliona namna Abeli alivyotolea Mungu mwana-kondoo bila kipunguo na kumchinja kuwa sadaka kufunika zambi, kama Mungu alivyokwisha kuagiza. Kaina aljaribu kukaribia Mungu na kazi zake mwenyewe, akaletea Mungu zawadi ya matunda ambayo alipanda ndani ya udongo uliokwisha

kulaaniwa. Hivi, Maandiko yanasema, *"Bwana akaheshimu Abeli na zabihu yake, lakini hakuheshimu Kaina na zabihu yake."* (Mwanzo 4:4,5) Kwa nini Mungu hakupokea zabihu ya Kaina? Kama tulivyoona, njia ya haki ambayo Mungu aliamuru ilitangaza ya kwamba ***"pasipo kumwanga damu hakuna ondoleo."*** (Waebrania 9:22) Lakini Kaina aliona bule njia ya sadaka ambayo Mungu alitayarisha. Kaina alitenda sawasawa aliamini Mungu, lakini matendo yake yalikana neno hili kwa sababu hakutoa sadaka ya nyama ambayo Mungu aliagiza. Kwa sababu hii Mungu alikataa Kaina na sadaka yake. Lakini Mungu alipendezwa na sadaka ya Abeli, akamsamehe zambi zake zote, kwani Abeli aliamini neno la Mungu na kumtolea sadaka ya nyama ya mwana-kondoo.

Abeli ni mfano wa wale ambao Mungu anahesabu kuwa wenye haki kwa sababu ya imani yao ndani ya Masiya Yesu, aliyemwanga damu yake kulipa kwa zambi. Kaina ni mfano wa wale wanaojaribu kuwa wenye haki mbele ya Mungu kwa njia ya kazi zao wenyewe, na wanaokataa sadaka ya Mkombozi ambaye Mungu alituma toka mbinguni. Kufika leo, kuna **njia hizi mbili** tu: Njia ya Abeli na njia ya Kaina. Wewe unafuata njia ya nani? Umekubali njia ya Abeli, maana **njia ya haki,** inayotegemea sadaka ya Masiya mtakatifu ambaye Mungu alituma toka mbingu? Au unakaa kufuata njia ya Kaina, **njia ya uzalimu** inayotegemea kazi za mtu na maagizo ya dini?

Rafiki, tafazali fahamu kabisa ya kwamba **Mungu ni mwenye haki** na hawezi kuvumilia zambi! Mungu hakuweza kusema na Adamu na Hawa, Kaina na Abeli, na wazao wao wote: "Ninajua kwamba mumefanya zambi, basi si neno kubwa! Nitasahau tu ya kwamba mulifanya zambi!" Mungu aliweza kusamehe zambi hivi? Sivyo! Kama Mungu angalifanya hivi, namna gani wenye zambi watatambua utakatifu wake? Mungu ni mwamuzi wa haki na ni lazima kwake kuazibu zambi. Azabu kwa zambi ni mauti! Kwa sababu hii ilipasa Mkombozi mtakatifu kufa kwa zambi zetu. Wakati alipokufa juu ya msalaba alilipa azabu kwa zambi zangu na zambi zako.

Sikiliza maneno yaliyoandikwa ndani ya Habari Njema juu ya **njia ya haki** ambayo Mungu aliamuru. Maandiko yanasema:

> *"Kama kwa mtu mmoja zambi iliingia ulimwenguni, na kufa kwa njia ya zambi; na hivi kufa kulikuja juu ya* ***watu wote****, kwa sababu wote wamefanya zambi."* (Waroma 5:12) *"Hakuna tofauti, kwa sababu* ***wote wamefanya zambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu; wanahesabiwa haki bule kwa neema yake, kwa njia***

Everyday Publications Inc. @ 2010

> ***ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu****: naye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake, kusudi aonyeshe haki yake kwa sababu ya kuachilia zambi zilizofanywa zamani, katika uvumilivu wa Mungu: apate kuonyesha haki yake katika wakati huu, ili awe mwenye haki, na mwenye kuhesabia haki mtu anayeamini Yesu."* (Waroma 3:22-26) *"Kwa maana* ***mshahara wa zambi ni mauti,*** *lakini* ***zawadi ya Mungu ni uzima wa milele*** *katika Yesu Kristo Bwana wetu."* (Waroma 6:23)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutaendelea na ukumbusho wa habari za unabii na kujikumbusha namna Mungu alivyoita Ahrahamu kuwa sehemu ya shauri lake la ajabu kutuma Mwokozi duniani . . .

Mungu akubariki wakati unapokaa kuwaza juu ya shairi hili toka Neno la Mungu linaloweza kugeuza maisha yako:

> ***"Mshahara wa zambi ni mauti, lakini zawadi ya Mungu ni uzima wa milele katika Yesu Kristo Bwana wetu****."* (Waroma 6:23)

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 94

# Ukumbusho #2
# Abrahamu, Haki kwa Njia ya Imani

(Mwanzo 6-22, na nyingine)

Salama iwe kwako, rafiki msomaji, kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka ufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Mfulizo wetu *Njia ya Haki* unaeleza maneno haya wazi.

Leo tunaendelea na **ukumbusho** wetu wa habari za manabii ya Mungu. Habari za manabii ni habari za ajabu **za Mungu** juu ya neno alilofanya kutafuta na kuokoa wana wa Adamu wanaopotea ndani ya zambi. **Kwa ufupi, habari za manabii wa Mungu ni Habari Njema juu ya namna wazalimu wanaweza kufanyizwa haki mbele ya Mungu.** Somo letu la ukumbusho linaitwa: **"Haki kwa njia ya Imani."**

Everyday Publications Inc. @ 2010

Ndani ya Ukumbusho #1 tulikumbushwa namna mtu wa kwanza, Adamu, alivyochagua kufuata Shetani, adui ya Mungu. Zambi moja ya Adamu ilifanyiza wazao wake wote kuzaliwa katika zambi, kwa njia inayofikisha watu kwa jehanum. Watu wengine wanajaribu kubisha neno hili, wakisema: *"Zambi ya Adamu ni neno lake mwenyewe. Haitugusi sisi!"* Lakini wale wanaosema hivi hawaweki roho juu ya Maandiko ya Manabii yanayosema: ***"Kwa mtu mmoja zambi iliingia ulimwenguni,** na kufa kwa njia ya zambi; na hivi kufa kulikuja juu ya watu wote, kwa sababu wote wamefanya zambi!"* (Waroma 5:12)

Watu wa kabila moja wanasema "Tauni haikwishi na mtu kwa njia yake tauni ilianza!" Vivyo hivyo, laana ya zambi ya Adamu haikwisha kwake tu lakini ilienea kwa sisi sote, kama ugonjwa wa kuenea. Kwa sababu ya zambi ya Adamu kwa mwanzo watu wote wanazaliwa na tabia ya zambi. Sisi sote tumeriti tabia ya baba yetu Adamu. Neno la hakika ndilo ya kwamba tabia ya zambi ndani yetu itatuhukumu kupotea kwa milele—isipokuwa Mungu anatayarisha njia kwa sisi kupona. Habari Njema ndiyo ya kwamba Bwana

Mungu alitayarisha kweli **njia ya kupona** kwa sisi. Kama tulivyosoma ndani ya Tora, siku Adamu na Hawa walipokufa, Mungu, kwa rehema yake, alitoa ahadi. Aliahidi kutuma duniani Mkombozi wa haki atakayezaliwa na bikira. Mkombozi huyu atamwanga damu yake kama zabihu itakayolipa deni ya zambi za wana wa Adamu.

Wakati tuliposoma ndani ya kitabu cha Habari Njema {*Injil*} tuliona ya kwamba kwa saa aliyoweka mbele, Mungu alitume Yule ambaye aliahidi kutuma. Mwokozi huyu ambaye Mungu aliahidi kutuma ni nani? Ni Mtu mkamilifu na wa haki kabisa, ndiye **Yesu Kristo**. Sikia namna Maandiko ya Mungu yanavyoonyesha tofauti kati ya Adamu aliyefanya zambi na Kristo asiyefanya zambi. Maandiko yanasema:

> *"Kwa maana kama, kwa njia ya kosa la mtu mmoja, **kufa** kulitawala kwa ajili ya mtu mmoja, zaidi sana wao wanaopokea neema ya kuzidi sana na zawadi ya haki watatawala katika **uzima** kwa yule mmoja, Yesu Kristo. Basi hivi, kama vile kwa kosa moja **watu wote walihukumiwa azabu,** hivi kwa tendo moja la haki watu wote walipewa **haki ya uzima**. Kwa sababu, kama kwa kuasi kwa mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya **wenye zambi**, hivi kwa kutii kwake mtu mmoja, wengi wameingizwa katika hali ya **wenye haki.**"* (Waroma 5:17-19)

Everyday Publications Inc @ 2010

Haya ndiyo mafundisho ya Maandiko juu ya wale walio **ndani ya Adamu** na wale walio **ndani ya Kristo.**

Sisi sote tume**zaliwa** na sura ya Adamu. Lakini Mungu anaita wana wa Adamu **kuzaliwa tena** mioyoni mwao, kuondosha **sura ya Adamu** na kuvaa **sura ya Kristo**. Neno hili linawezekana namna gani? Kwa **njia ya imani** tu! Maandiko yanasema ya kama ukiamini moyoni mwako ya kwamba Bwana Yesu Kristo alilipa kwa zambi yako, Mungu atakufanyiza kuzaliwa tena kwa njia ya kusafisha moyo wako na kukufanyiza mpya kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Utageuka kiumbe kipya ndani ya Kristo; hutaishi kwa faida yako mwenyewe tena lakini kwa Bwana Yesu aliyekufa na kufufuliwa tena kwa ajili yako.

Sasa turudi kusoma katika Tora na kuendelea ndani ya ukumbusho wetu kwa njia ya kuwaza tena juu ya namna Mungu alivyoendesha **shauri lake** kutuma Mkombozi duniani. Ndani ya masomo yetu ya namna habari zilivyofuatana tuliona wana wawili wa kwanza wa Adamu, Kaina na Abeli. Abeli aliamini maneno Mungu aliyoahidi juu ya Mkombozi, atakayekuja kumwanga damu yake

kama zabihu, lakini Kaina hakuamini. Mungu alihamakia Kaina kusudi aweze kutubu, lakini Kaina alikasirika tu na aliua Abeli, mdogo wake.

Tuliona ya kwamba zaidi ya wana wa Adamu walifuata njia ya Kaina, wakifurahi sana kutenda zambi. Kwa sababu hii, wakati tunapofika kwa wakati wa Noa, Maandiko yanasema: *"Bwana akaona ya kama uovu wa watu ulikuwa mkubwa duniani, na ya kama mawazo yote ya **mafikili ya mioyo yao yalikuwa mabaya tu siku zote.**"* (Mwanzo 6:5) Tuliona kusudi la Mungu kuharibu wana wa Adamu kwa njia ya garika. Kwa wakati ule mwovu sana Noa peke yake aliamini maneno Mungu aliyoahidi juu ya Mkombozi atakayekuja. Basi Mungu aliagiza Noa kujenga safina kubwa kusudi Noa na jamaa yake na nyama wingi waweze kuponyeshwa. Kwa miaka mia moja Mungu alivumilia na saburi uovu wa watu wakati Noa alipokuwa akijenga safina. Lakini hakuna mtu aliyetubu na kuamini neno la Mungu ila Noa na jamaa yake. Hivi mwishoni Mungu, anayetimiza kila mara maneno anayosema, alifanya yote aliyoahidi, akaharibu kabisa wote waliokataa kuingia safina ambayo aliwatayarishia.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Nyuma yake, tuliona ya kwamba wazao wa Noa walisahau Neno la Mungu polepole, kwa sababu wao vilevile walikuwa wana wa Adamu na wenye tabia ya zambi. Hivi tulisoma juu ya mnara wa Babeli na ya kwamba watu walijaribu kukutanisha watu wote wa dunia kwa pahali pamoja na kujenga mji na mnara unaokwenda juu sana. Walifanya hivi kwa kuasi Mungu, lakini Mungu aliwahukumu kwa njia ya kuchanganyisha lugha yao na kuwasambaza pahali pote katika dunia nzima.

Halafu tulifikia habari nzuri sana za **nabii Abrahamu**. Kweli Abrahamu alijulikana sana ndani ya shauri la Mungu kukomboa wana wa Adamu toka utumwa wa zambi. Baba ya Abrahamu aliabudu sanamu na Abrahamu mwenyewe alikuwa mwenye zambi, kama wazao wote wa Adamu. Lakini tuliona ya kwamba Mungu alitokea kwa Abrahamu, akamwagiza kuondokea nyumba ya baba yake, na kutoka katika inchi yake. Mungu alikusudi kwa Abrahamu kuwa mtu wa kwanza wa taifa jipya kwa njia yake Mkombozi mtakatifu atakapofika duniani. Kwa sababu hii tulisoma ndani ya kitabu cha Mwanzo, sura 12 juu ya wakati Mungu alipoita Abrahamu, akisema naye:

> *"Toka wewe katika inchi yako na katika ndugu zako, na nyumba ya baba yako hata inchi ambayo nitakuonyeshea; na nitakufanya wewe*

> *kuwa taifa kubwa, na nitakubariki, nitatukuza jina lako, nawe uwe baraka; na nitawabariki ambao wanakubariki; naye ambaye anakulaani nitamlaani vilevile, na* ***ndani yako jamaa zote za inchi watabarikiwa."*** (Mwanzo 12:1-3)

**Kwa nini Mungu aliagiza Abrahamu kuhama kwa inchi nyingine?** Mungu alitaka kufanya t**aifa jipya kwa njia yake. Kwa sababu gani Mungu alitaka kufanya taifa jipya kwa njia ya Abrahamu?** Kwa njia ya taifa lile jipya Mungu alikusudi kuleta manabii watakaoandika Maandiko Matakatifu. Na kwa njia ya taifa lile lile, Mungu alikusudi kutuma **Mkombozi** duniani. Kwa sababu hii Mungu aliahidi Abrahamu akisema, *"nawe uwe baraka . . . na ndani yako jamaa zote za inchi watabarikiwa."*

**Mungu alitimiza ahadi aliyotolea Abrahamu?** Ndiyo! Wakati Abrahamu alipokuwa na miaka mia moja, na Sara, mke wake alikuwa na miaka makumi tisa, Mungu aliwapa mwana, Isaka, kama aliyoahidi. Isaka alizaa Yakobo, na Yakobo alizaa wana kumi na wawili waliokuwa mwanzo wa taifa jipya, ndilo taifa la **Israeli**. Wale katikati yenu munaojua Maandiko Matakatifu, munajua ya kwamba Mkombozi alikuja kwa njia ya taifa la Israeli, kwa sababu Maria, mama ya Yesu, na Yosefu aliyehesabu Yesu kama mwana wake, walikuwa wazao wa Abrahamu. Hivi, shairi la kwanza ndani ya Habari Njema linasema: *"Kitabu cha kizazi cha Kristo, mwana wa Daudi,* ***mwana wa Abrahamu.****"* (Matayo 1:1) Kwa neno la mwili wake wa dunia, Yesu alikuja kwa njia ya wazao wa Abrahamu, Isaka na Yakobo. Lakini kwa neno la nafsi yake takatifu—Yeye ni Mwana wa Mjuu sana, Neno la Mungu kabisa {*Kalimat Allah*} aliyekuja toka mbinguni kuzaliwa duniani.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Turudi kwanza kwa habari za Abrahamu, kwa sababu kuna neno kubwa lingine ambalo inatupasa kukumbuka juu yake. Tuliona ya kwamba Abrahamu alizaliwa ndani ya zambi, kama wana wote wa Adamu. Lakini, Maandiko Matakatifu yanatupasha ya kwamba leo Abrahamu ni mbinguni, mbele ya Mungu Mtakatifu na atakuwa pale kwa milele. Sasa tunauliza: **Abrahamu alifanya nini ili Mungu asamehe zambi zake, kumhesabu kuwa haki na kumkaribisha mbinguni?** Maandiko Matakatifu yanasema nini juu yake? Yanasema, *"Abrahamu aka****amini*** *Bwana; akamhesabia kwa* ***haki****."* (Mwanzo 15:6)

Abrahamu aliamini **Mungu**—Mungu mwenyewe. Abrahamu **aliamini maneno ambao Mungu alimwambia**. Kwa sababu hii Mungu alimhesabu kuwa haki. Wewe unayesikiliza leo, **unaamini**

**Neno la Mungu kama Abrahamu alivyoliamini**? Hatuulizi kama unaamini kwamba kuna Mungu, au kwamba Mungu ni Mmoja. Shetani anajua ya kwamba Mungu ni mmoja! Neno Mungu analotaka ni kwa wewe kuamini **maneno anayosema** juu ya njia ya wokovu ambayo aliamuru, kama Abrahamu alivyoamini! Abrahamu alituambia neno ambalo inatupasa kuamini. Unakumbuka neno kubwa Abrahamu alilosema juu ya mlima ule siku alipotoa kondoo ndume kwa pahali pa mwana wake? Alisema, *"Mungu atajipatia mwenyewe mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa."* (Mwanzo 22:8) Na nyuma ya kuchinja kondoo ndume, aliita mlima ule *Yehova-Yire*, maana yake "*Bwana a**ta**weka tayari*." (Mwanzo 22:14) Kwa nini Abrahamu aliita mlima ule *"**Bwana ataweka tayari**,"* wakati Mungu alipokwisha kuweka tayari kondoo ndume kwa sadaka? Abrahamu, kama nabii, alikuwa akitangaza neno litakalotokea nyuma. Wakati Abrahamu aliposema, "***Bwana ataweka tayari**,"* alitoa habari mbele ya neno litakalotokea juu ya mlima ule pahali kondoo alipokomboa mwana wake juu ya mazabahu. Alitazama mbele kwa siku ile wakati Mkombozi atakapomwanga damu yake juu ya mlima ule — **kuokoa wote ambao wanamwamini** toka hukumu ya haki ya Mungu.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Wakati tulipojifunza ndani ya Habari Njema mbele, tuliona ya kwamba Yesu Kristo alifika duniani karibu miaka elfu mbili nyuma ya wakati wa Abrahamu, na ya kwamba alitimiza unabii wa Abrahamu. Ndiyo, inje ya Yerusalema, juu ya mlima pahali Abrahamu alipotoa sadaka ya kondoo kwa pahali pa mwana wake, Mkombozi, Yesu alimwanga damu yake kukomboa wana wa Adamu. Kwa sababu hii, wakati walipokwisha kufunga Yesu juu ya msalaba na misumari, na mbele ya kufa kwake, tulimsikia akisema na sauti kubwa, ***"Imekwisha!"*** Maana ya ime*kwisha* ni ime*timizwa*. Kwa sababu gani Yesu alisema "Imetimizwa!"? Alisema hivi kwa sababu **mauti yake juu ya msalaba ilitimiza njia ya wokovu** ambalo Mungu alitangaza miaka mingi mbele kwa njia ya manabii yake. **Mauti ya Yesu ilimaliza na kutimiza mfano wa sadaka ya Abrahamu na ya sadaka zote za nyama!**

Wewe unayesikiliza leo, unaamini ya kwamba Yesu Kristo mwenyewe ni kondoo wa sadaka mkamilifu na wa mwisho {*Id al-Adha*} aliyetumwa na Mungu toka mbingu? **Una imani ya Abrahamu?** Sikia maneno Habari Njema inayosema juu ya imani ya Abrahamu. Inasema:

> (Waroma 4) *1 Basi tuseme nini, Abrahamu . . . amepata nini kwa njia ya mwili? 2 Kwa maana kama Abrahamu alihesabiwa haki kwa*

*ajili ya matendo, ana maneno ya kujisifia; lakini si mbele ya Mungu. 3 Kwa maana maandiko yanasema nini?* ***Abrahamu aliamini Mungu, na ilihesabiwa kwake kuwa haki*** *. . . 22 Kwa hii ilihesabiwa kwake kuwa haki. 23 Lakini* ***haikuandikwa kwa ajili yake tu*** *kwamba ilihesabiwa kwake, 24* ***lakini kwa ajili yetu vilevile****. Itahesabiwa kwetu kama tukimwamini yeye aliyefufua Yesu Bwana wetu toka wafu; 25 aliyetolewa* ***kwa ajili ya makosa yetu****, na kufufuliwa* ***ili tuhesabiwe haki.*** Amina!

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutaendelea na ukumbusho wetu wa habari za manabii na kuona nabii mkubwa mwingine ambaye Mungu alichagua kutayarisha njia kwa kuja kwa Mwokozi duniani. Nabii huyu alikuwa Musa.

Mungu akubariki na kukusaidia kufahamu vizuri maneno Maandiko yanayotangaza, ya kwamba

***"Abrahamu aliamini Mungu, na ilihesabiwa kwake kuwa haki."*** (Waroma 4:3)

Everyday Publications Inc
@ 2010
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Somo 95

# Ukumbusho #3
# Musa, Sheria takatifu ya Mungu

Kutoka 1-20, na nyingine

Tunakusalimu tena kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka sisi sote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele.

Basi tuendelee sasa na **ukumbusho** wetu wa habari za manabii ya Mungu, ndizo Habari Njema zinazoonyesha namna wenye zambi wanavyoweza kugeuka haki mbele ya Mungu. Ukumbusho wetu ungali ndani ya Tora, kitabu Mungu alichoweka ndani ya nia ya nabii wake Musa. Kama tulivyoona mbele, Tora ya Musa ina faida kubwa kwa watu wote wanaotaka kujua kweli; ni msingi Mungu alioweka ili tuweze kuhakikisha kila neno tunalosikia kama likitoka kwa Mungu au sivyo.

Everyday Publications Inc.
@ 2010

Katika mwanzo wa Tora, tuliona ya kwamba mzazi wetu **Adamu** alifanya zambi. **Zambi yake ilienezwa** kwa wazao wake wote kama ugonjwa wa kuenea, na ilileta taabu, mauti, na azabu ya milele, kama Bwana Mungu alivyoonya mbele. Lakini tunashukuru Mungu kwa sababu Maandiko yanasema, *"Pahali zambi zilipozidi, neema ilizidi zaidi sana."* (Waroma 5:20) Ndiyo, siku ile ile Adamu na Hawa walipofanya zambi, Mungu, kwa neema yake, alitangaza ya kwamba siku nyingine atatuma **Mkombozi** duniani, kukomboa wana wa Adamu toka laana ambayo zambi ilileta.

Ndani ya somo la ukumbusho la mbele, tuliona namna Mungu alivyoita **Abrahamu,** akiahidi kumfanya kuwa **taifa jipya**, na ya kwamba manabii na Mkombozi watatoka kwa taifa lile. Hivi Abrahamu alizaa Isaka, Isaka alizaa Yakobo, na Yakobo alizaa wana kumi na wawili waliokuwa mwanzo wa makabila kumi na mawili ya **Israeli**.

Sasa tuendelee na ukumbusho wetu kuona namna Mungu ali-

vyotumika na wazao wa Adamu, ndio Waisraeli, kufundisha wanadamu kama Bwana Mungu ni namna gani na kama ikipasa wenye zambi kufanya nini kwa kuepuka hukumu ya haki ya Mungu. Somo letu la leo linaitwa "**Sheria Takatifu ya Mungu."**

Wakati tulipojifunza ndani ya Tora, tuliona ya kwamba Mungu aliruhusu wana wa Israeli kugeuka watumwa ndani ya inchi ya Misri kwa miaka mia ine, kama alivyojulisha Abrahamu miaka mingi mbele. Kwa wakati Mungu aliochagua mbele, alituma **Musa** kwa Waisraeli. Musa alikuwa Mwisraeli aliyepata nguvu ndani ya nyumba ya Farao, mfalme mwovu wa Misri.

Mungu alituma Musa karibu na Farao kumwambia, "Bwana Mungu anasema: '**Ruhusu watu wangu** waende na kunifanyia siku kubwa jangwani!'" (Kutoka 5:1) Lakini Farao alikataa pamoja na kuzarau, akisema, "Bwana ni nani? Sitaruhusu watu wa Israeli kwenda kamwe!" Halafu Mungu alijulisha Farao na Wamisri uwezo na utukufu wake kwa njia ya mapigo tisa ya kuogofya sana yaliyopata inchi nzima ila Waisraeli. Lakini alama na maajabu Mungu aliyofanya mbele ya Farao hayakumsukuma kutubu na kutii neno la Musa. Mungu alisema na Musa, "Nitaleta pigo moja lingine juu ya Farao na Misri. Nyuma yake, atawaruhusu ninyi kwenda!" Unakumbuka kama pigo hili lilikuwa nini? Ndiyo, lilikuwa **mauti ya mzaliwa wa kwanza** ndani ya kila nyumba.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Hivi tuliona ya kwamba Mungu aliua mzaliwa wa kwanza ndani ya nyumba ya Farao na ndani ya nyumba zote za Misri. Lakini aliponyesha wazaliwa wa kwanza wa Waisraeli kwa sababu ya **damu ya mwana-kondoo** waliyopakaa juu ya milango ya nyumba zao. Maana Mungu yeye mwenyewe alikuwa ameahidi, akisema: *"Damu itakuwa alama kwenu juu ya nyumba pahali mutakapokuwa; na **wakati nitakapoona damu, nitapita juu yenu**, wala pigo halitakuwa juu yenu kuwaharibu ninyi."* (Kutoka 12:13) Hivi, kwa sababu ya damu ya mwana-kondoo, Mungu alipita juu ya nyumba za Waisraeli, bila kuua wazaliwa wa kwanza. Kwa njia hii Mungu aliponyesha Waisraeli toka mkono wa Farao.

Kama tulivyoona, habari za siku ya Pasaka ina **maana kubwa kupita** kuokolewa kwa wana wa Israeli toka utawala wa Farao. Maana Maandiko yanasema: *"Maneno haya yote yaliwapata kama mifano, yakaandikwa kutuonya sisi tuliofikiliwa mwisho wa siku."* (1 Wakorinto 10:11) Habari za damu ya mwana-kondoo ambayo Waisraeli walipakaa juu ya milango ya nyumba zao ili Mungu aponyeshe wazaliwa kwanza **wasife**, na kuwafungua toka utawala wa Farao ni

mfano. Ni **mfano wa njia ya wokovu** ambayo Mungu alitengeneza kuokoa wenye zambi toka bwana wa kazi aliye mwovu kupita Farao, ndiye Shetani!

Neno la Mungu linaonyesha ya kwamba wana wote wa Adamu ni kama watumwa! Labda unafikili, "Ndiyo, ninajua tuko watumwa wa Mungu!" Lakini wazo hili halipatani na maneno Bwana Yesu aliyosema ndani ya Habari Njema {*Injil*}, akisema: *"Kweli, kweli ninawaambia ninyi, Kila mtu anayefanya zambi ni* ***mtumwa wa zambi.****"* (Yoane 8:34) Na kwa sababu wana wote wa Adamu ni watumwa wa zambi, wao ni watumwa wa Shetani vilevile kwani Shetani ni bwana wa zambi. Na tunajua neno moja bila shaka, ndilo ya kwamba mtu aliye mtumwa wa zambi hawezi hata kidogo kujifungua toka utumwa ule! Inawezekana kwa mtumwa kujifungua? Anaweza kumpa bwana wake kitu fulani ili bwana yule aweze kumfungua toka utumwa wake? Labda neno hili linawezekana na bwana mzuri, lakini si na bwana mbaya kama Shetani. Kama Farao, Shetani hawezi kukubali kamwe kufungua watumwa wake na kutaka kwake mwenyewe! Ndiyo, hatakubali kamwe! Kweli sisi wana wa Adamu, tumelaaniwa kabisa! Kuna njia yo yote kutuokoa toka utawala wa Shetani ambaye alitufanyiza kuwa watumwa wake? Ndiyo, Mungu asifiwe, **kuna Mwokozi**! Mungu ametuma kwetu Mmoja anayeweza kutuweka huru! Ni Mwokozi mwenye uwezo na haki aliyetoka mbinguni, ndiye manabii wote wa Mungu walimshuhudia.

Everyday Publications Inc @ 2010

Ndani ya **Tora**, tunasoma namna Mungu alivyoahidi kuponda kichwa cha Shetani kwa njia ya Mkombozi mtakatifu atakayezaliwa na bikira. Ndani ya **Zaburi**, tulisikia maneno nabii Daudi aliyoandika ya kwamba Mkombozi huyu, ambaye Mungu anaita Mwana wake, atauawa kwa njia mbaya sana—ya kwamba atateswa, na mikono na miguu yake itatobolewa! Ndani ya kitabu cha **Habari Njema**, tunasoma maneno mengi juu ya Mkombozi huyu wa ajabu. Yeye ni Yesu, mwana wa Maria, aliyeishi maisha makamilifu, kisha alikufa juu ya msalaba kwa zambi zetu na alifufuliwa tena toka kaburi. Ndiyo, Yesu alitimiza maneno ambayo manabii wa Mungu waliandika zamani juu ya Mwokozi wa wenye zambi.

Neno la Mungu linaita Yesu Kristo **"Mwana-kondoo wa Mungu."** Kama wana-kondoo waliochinjwa siku ya Pasaka, Yesu alimwanga damu yake kutuokoa toka hukumu. Karibu miaka elfu moja mia tano nyuma ya wakati Mungu alipookoa Waisraeli kwa njia ya damu ya mwana-kondoo siku ya Pasaka, Mungu aliruhusu wana wa Adamu kufunga Yesu, Masiya mwenye haki, kwa msalaba

na misumari. Na ilikuwa siku ya karamu ya Pasaka alipofungwa kwa msalaba. Hivi, kama Yesu alivyotimiza mfano wa sadaka ya Abrahamu {*Id al-Adha*}, vivyo hivyo, Yesu **alitimiza mfano wa mwana-kondoo wa Pasaka**. Watu ambao walimsulibisha siku ile walitenda hivi kwa ujinga, lakini Mungu alikusudi hata mbele ya kuumba dunia kwa Masiya kutolewa kama sadaka (ona Ufunuo 13:8; Matendo 3:17).

Yesu ni sadaka kamilifu na ya mwisho kwa zambi. **Damu ya Yesu Kristo ni bei iliyohitajiwa na sheria** kwa Mungu kukomboa wana wa Adamu toka utawala wa zambi. Hivi Maandiko yanasema:

> *"Kristo, Pasaka yetu, amekwisha kutolewa kwa ajili yetu."* (1 Wakorinto 5:7) *"Kwa maana tungali tulipokuwa pasipo nguvu, kwa wakati wa kutimia, Kristo alikufa kwa ajili yao wasioogopa Mungu. Kwa maana ni ugumu kwa mtu kufa kwa ajili ya mtu wa haki: lakini inawezekana mtu kusubutu kufa kwa ajili ya mtu mwema. Lakini Mungu anaonyesha mapendo yake kwetu, wakati tulipokuwa tungali wenye zambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu."* (Waroma 5:6-8)

Everyday Publications Inc
@ 2010

Tuache sasa habari za Pasaka, na tujaribu kukumbuka maneno tuliyojifunza juu ya sheria takatifu ambayo Mungu alitolea Waisraeli. Wakati tulipojifunza juu ya sheria tuliona namna Mungu alivyofunua utakatifu na utukufu wake kwa Musa na Waisraeli jangwani, akishuka juu ya Mlima Sinai ndani ya moto na ngurumo na lalo. Hivi Mungu aliwapa Waisraeli Amri zake Kumi na maagizo mengi mengine. Yote pamoja yanaitwa *Torati ya Musa*. Mungu aliwaagiza, akisema: **"Utapenda Bwana Mungu wako na moyo wako wote, na roho yako yote,** na **na nia yako yote;** usiwe na miungu mingine ila mimi! Haifai ufanye sanamu! Usitumie jina la Bwana Mungu wako bule! Kumbuka siku ya sabato na kuitakasa! **Penda jirani yako kama wewe mwenyewe!** Heshimu baba na mama yako! Usiue! Usizini! Usiibe! Usishuhudie jirani yako uwongo! Usitamani cho chote kilicho cha jirani yako!" Na kwa maagizo haya matakatifu, Mungu aliongeza maneno haya: *"Mtu anayeshika sheria yote, lakini akakosa katika **neno moja tu**, amekosa juu ya yote!"* (Yakobo 2:10) *"Amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika **yote** yaliyoandikwa katika kitabu cha torati ayafanye."* (Wagalatia 3:10) Hili ndilo tangazo kubwa la sheria takatifu ambayo Mungu alitolea Musa!

Wewe msomaji, **umeshika sheria hii takatifu ya Mungu ambayo inakuagiza kuwa kamilifu kabisa ndani ya mawazo na maneno na matendo—kuanza na siku ya kuzaliwa kwako kufika**

**siku ya kufa kwako?** Kila siku na kila saa, usiku na mchana, inakupasa kupenda Bwana Mungu ni moyo wako **wote**, nafsi yako **yote**, na nia yako **yote**. Na vilevile, inakupasa kupenda jirani yako **kama wewe mwenyewe**! Umetimiza sheria hii takatifu? Wewe na mimi tunajua ya kwamba **hatukuitimiza**! Maandiko yanasema: *"Hakuna mwenye haki, hata mmoja!* (Waroma 3:10) *"Kama tukisema kwamba hatuna zambi, tunajidanganya wenyewe, wala kweli si ndani yetu."* (1 Yoane 1:8) Hakuna mtu hata mmoja aliyetimiza maneno yote ambayo Mungu anaagiza, kwa sababu sisi sote tumezaliwa na tabia ya zambi.

Labda wengine wangependa kuuliza: Kama sisi sote tusipoweza kutimiza sheria ya Musa, kwa sababu gani Mungu alitutolea sheria ile? Mungu ni Mungu anayetaka watu wote kupotea? Sivyo, Mungu ni mapendo, na **hataki mtu ye yote** kupotea! Basi Mungu alitolea wenye zambi sheria zake takatifu wakati alipojua vizuri ya kwamba hakuna mtu hata mmoja atakayeweza kuzitimiza? Kusudi la maagizo yale ni nini? Mungu anajibu ulizo hili wakati anaposema,

> *"Kwa kazi ya sheria hapana mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele yake; kwa sababu* ***kwa njia ya sheria zambi inajulikana****."* (Waroma 3:20) *"Maandiko yalifunga wote chini ya zambi, kusudi wenye kuamini wapewe ahadi kwa imani ya Yesu Kristo."* (Wagalatia 3:22)

Everyday Publications Inc @ 2010

Hivi tuliona ya kwamba Mungu aliwekea wenye zambi amana amri zake takatifu, kutuonyesha ukosefu na upungufu wetu mbele yake, na ya kwamba tunahitaji Yesu Kristo aliyebeba kwa sisi laana ambayo zambi ilileta. Katikati ya watu, **Bwana Yesu Kristo ndiye wa pekee aliyeshika na kutii kabisa sheria takatifu** ambayo Mungu aliwekea Musa amana. Kama tulivyoona, Yesu alikuwa namna nyingine kabisa na wazao wa Adamu, kwa sababu hakushiriki tabia yao ya zambi. Yesu ni Neno la Milele la Mungu, aliyeshuka mbinguni, na aliyezaliwa na bikira. Yesu alikamata mwili namna ya miili yetu, lakini hakukamata tabia yetu ya zambi. Kwa sababu hii, wakati alipokuwa duniani, aliweza kusema: *"Musizanie nilikuja kuharibu torati au manabii; sikuja kuharibu, lakini* ***kutimiliza****."* (Matayo 5:17) Ulisikia neno Yesu alilosema? Ni kweli kubwa na ya ajabu sana. Yesu alisema alikuja duniani ku**timiza** sheria takatifu ambayo Mungu aliwekea Musa amana! Unafahamu maana ya maneno haya? **Yesu alifanya kwa sisi neno ambalo sisi wana wa Adamu, hatukuweza kufanya kamwe kwa sisi wenyewe!** Alitimiza **sheria takatifu ya Mungu**, na nyuma yake, alimwanga damu yake juu ya msalaba

**kubeba laana ya sheria kwa sisi** na kutuokoa toka hukumu ya haki ya Mungu!

Yesu hakustahili kufa, kwa sababu hakufanya zambi kamwe. Lakini kwa kutimiza njia ya wokovu ambayo Mungu alikuwa ameahidi kwa njia ya manabii, Bwana Yesu, na kutaka kwake mwenyewe alitoa uzima wake kwa sisi. Na nyuma ya kumwanga damu yake kulipa deni yetu ya zambi, Mungu alimfufua toka wafu siku ya tatu! Sikiliza neno Maandiko Matakatifu yanalosema juu ya neno hili. Yanasema:

> *"[Sheria takatifu ya Mungu **haiwezi kuleta hukumu ya azabu**] juu yao walio katika Yesu Kristo! . . . Maana yale yasiyowezekana kufanywa kwa sheria kwa sababu ilikuwa zaifu kwa sababu ya mwili, Mungu alituma Mwana wake mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa zambi, na kwa sababu ya zambi, alihukumu zambi katika mwili."* (Waroma 8:1,3)

Rafiki unayesikiliza, unatumainia nini? Unategemea Habari Njema ya Mungu juu ya Mkombozi mwenye haki aliyebeba azabu kwa zambi zako? Au ungali unategemea kazi "njema" wewe unazotenda? Usisahau tangazo la Neno la Mungu, ya kwamba:

Everyday Publications Inc @ 2010

> *"Wale wote walio wa matendo ya sheria ni chini ya laana, maana imeandikwa: Amelaaniwa kila mtu asiye**dumu katika yote** yaliyoandikwa katika kitabu cha torati ayafanye. . . [Lakini] Kristo **alitukomboa** kwa laana ya torati, akiwa alifanywa laana kwa ajili yetu . . . ili **kila mtu** akimwamini asipotee, lakini apate uzima wa milele!"* (Wagalatia 3:10,13; Yoane 3:16)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Ndani ya somo la nyuma, Mungu akitaka, tutatimiza ukumbusho wetu wa Maandiko ya Manabii na tutaona ya kwamba Yesu Masiya alitimiza kila neno manabii walilotabiri juu yake, na kwa njia hii kufungulia wana wa Adamu mlango wa wokovu na salama!

Mungu akusaidie kufahamu maneno tuliyojifunza leo. Na kumbuka ahadi hii toka Mungu mwenyewe:

> ***"[Sheria takatifu ya Mungu haiwezi kuleta hukumu ya azabu] juu yao walio katika Yesu Kristo!"*** (Waroma 8:1)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 96

# Ukumbusho #4
# Yesu Kristo : "Imekwisha!"

(Yoane 19, Waebrania 10)

Salama iwe kwako rafiki msomaji. Tunasalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tuendelee sasa na mfulizo wetu *Njia ya Haki*.

Ndani ya masomo matatu yanayopita tulifanya ukumbusho wa habari za manabii ya Mungu. Leo, Mungu akitusaidia, **tutamaliza ukumbusho huu**. Somo hili linaitwa: **"Imekwisha!"**

Everyday Publications Inc
© 2010

Kama tulivyoona, Mungu aligawa kitabu chake kwa **sehemu** kubwa mbili, Agano la Kale, na Agano Jipya. **Agano la Kale** ni sehemu ya kwanza ya kitabu cha ajabu cha Mungu. Ndani yake ni Tora {*Taurat*}, Zaburi {*Zabur*}, na Maandiko ya Manabii. Tuliona ndani ya sehemu hii ya kwanza ya Kitabu cha Mungu namna mzazi wetu, Adamu, alivyoasi Mungu, na kuingiza wazao wake wote ndani ya ufalme wa Shetani. Lakini, tulijifunza vilevile ya kwamba Mungu aliahidi kutuma Mwokozi mwenye uwezo kwa wana wa Adamu, kuokoa wote wanaoamini, na kuwaingiza ndani ya ufalme wa Mungu. Ahadi hii ilikuwa sehemu kubwa ya Agano la Kale.

**Kwa kuanza kutimiza shauri lake** kutuma Mwokozi, Mungu aliita Abrahamu wakati alipokuwa mzee, akasema naye, *"Nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa . . . na ndani yako jamaa zote za inchi watabarikiwa."* (Mwanzo 12:2,3) Hivi tuliona ya kwamba Mungu alifanyiza Abrahamu kuwa baba ya taifa la Israeli. Aliwekea amana taifa hili Maandiko ya Manabii. Kwa miaka elfu mia tano Mungu alitumia Waisraeli neno lake aliloweka ndani ya nia za watu mbalimbali—toka nabii Musa kufika nabii Yoane. Kwa njia ya manabii hawa, Mungu alihamakia uzalimu wa wana wa Adamu na aliwafunulia habari za kuja kwa Mkombozi wa haki atakayemwanga damu yake kulipa deni yao ya zambi.

Kama tulivyoona, Agano la Kale ambalo Mungu alisimamisha na wenye zambi, lilihitaji sadaka za nyama. Tulisikia ya kwamba “bila kumwanga damu hakuna usamehe wa zambi—kwa sababu **malipo kwa zambi ni mauti!**” Lakini sadaka ya nyama watu walizotoa tangu kizazi cha kwanza, hazikuweza kulipa kamwe kwa zambi, kwa sababu **thamani ya nyama** na **thamani ya mtu** si sawasawa. Kwa mfano, nikiwa na motakaa namna ya michezo ya watoto, ninaweza kwenda kwa duka na kuibadilisha kwa motakaa ya hakika? Sivyo, hata kidogo! Kwa nini? Kwa sababu bei ya motakaa yangu ya michezo si kipimo kimoja na ile ya motakaa ya hakika. Vivyo hivyo sadaka za nyama ambazo Mungu alitaka katika vizazi vya mbele hazikuweza kuondosha zambi, kwa sababu bei ya nyama na bei ya mtu si sawasawa. Kama tulivyoona, sadaka za nyama zilikuwa mifano tu ikingojea wakati Mungu atakapotuma sadaka ya hakika: Mkombozi wa haki atakayeleta Agano Jipya. Sadaka za nyama ziliweza kufunika tu zambi kwa wakati; hazikuweza kuondosha zambi kabisa.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Sehemu ya pili ya Kitabu cha Mungu inaitwa **Agano Jipya**, au Habari Njema {*Injil*}. Inatupasha juu ya agano (mapatano) Mungu alilosimamisha na watu kwa njia ya damu ya Mkombozi aliyetoka mbinguni. Kitabu cha Habari Njema ni habari za **Yesu** Mkombozi **aliyetimiza mfano wa sadaka zote za nyama** wakati alipomwanga damu yake juu ya msalaba ili sisi tuweze kupokea usamehe wa zambi. Kwa nini ilipasa Mkombozi kufika toka mbinguni? Kwa sababu kila mzao wa Adamu anabeba mzigo wa zambi. **Mwenye zambi hawezi kukomboa mwenye zambi mwingine.** Kwa mfano, inawezekana kwa mwanamke anayebeba chungu cha maji kichwani kubeba chungu cha pili kwa mtu mwingine vilevile? Sivyo. Vivyo hivyo mwenye zambi hawezi kubeba azabu ya Mungu kwa mwenye zambi nyingine. Lakini, Mkombozi, Yesu Kristo, aliyetumwa na Mungu, hakubeba mzigo wa zambi, kwa sababu alikuwa Mwana safi wa kweli wa Roho toka Mungu, Neno lililokuwa pamoja na Mungu katika mwanzo. Kwa sababu hii aliitwa Mwana wa Mjuu Sana. Alizaliwa na bikira. Hivi, alikuwa na mwili namna ya miili yetu, lakini hakuwa na tabia yetu ya zambi. Hakuwa na mzigo wa zambi. Kwa sababu hii Mungu aliweza kuweka juu yake mzigo wa zambi zetu zote. Yesu Mtakatifu alikufa kwa makosa yetu. Kisha, nyuma ya siku tatu, alifufuka toka wafu kutupa sisi uzima mpya. Alishinda mauti, kaburi, Shetani na zambi!

Sisi sote tulizaliwa ndani ya shimo kubwa la zambi, na hakuna

anayeweza kutuokoa, ila Masiya aliyekuja toka juu. Ukiweka tumaini lako ndani yake, atakuondosha ndani ya shimo la zambi. Alikuja toka mbingu kuokoa wana wa Adamu toka shimo la zambi. Na sasa amerudi mbinguni, kuwa mpatanishi kwa wote ambao wanamwamini. Kwa sababu hii Maandiko yanasema:

> *"Mungu ni mmoja tu, na mpatanishi katikati ya Mungu na watu ni mmoja, yule mtu Kristo Yesu, ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote!"* (1 Timoteo 2:5,6) *"Maana kuhani mkubwa wa namna hii alitufaa sisi sana, aliye mtakatifu, pasipo uovu, wala alama ya uchafu, aliyetengwa na wenye zambi . . . akikwisha kufanya katika yeye utakaso wa zambi zetu, aliketi mkono wa kuume wa Mwenye Ukuu."* (Waebrania 7:26; 1:3)

Kama tulivyoona ndani ya Habari Njema, wengine waliamini Yesu Masiya wakati alipokuwa duniani. Wale waliotambua kama Yesu ni nani walifurahi sana. Walijua ya kwamba kwa elfu za miaka manabii ya Mungu walikuwa wakitangaza kuja kwa Masiya; sasa walimwona na macho yao wenyewe! Tulisikia ya kwamba katikati ya wanafunzi wa Yesu wengine walikwenda kutafuta ndugu na rafiki zao na kuwaambia: ***"Tumeona Masiya . . . Tumeona Yeye aliyeandikwa na Musa katika torati, na manabii waliandika juu yake!"*** (Yoane 1:41,45)

Everyday Publications Inc © 2010

Ni huzuni kubwa kuona ya kwamba zaidi ya watu walioishi kwa wakati Yesu alipokuwa duniani, **hawakujua kama alikuwa nani.** Hili ndilo neno Maandiko yanalosema wakati yanapotangaza:

> *"Katika mwanzo alikuwa Neno, na Neno alikuwa pamoja na Mungu . . . Na Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu . . . nuru iliingia katika giza na giza halikuifahamu . . . Alikuwa ulimwenguni, na ulimwengu ulifanywa naye na ulimwengu haukumtambua. Alikuja kwake, nao walio wake hawakumpokea."* (Yoane 1:2,14,5,10,11)

Kama tulivyoona, watu wengi waliona alama na maajabu ambayo Masiya alifanya. Yesu alishinda gonjwa, tufani, pepo wachafu, zambi na mauti, lakini hata hivi zaidi ya watu hawakutambua kama alikuwa nani kwa sababu Shetani alipofusha nia zao. Makutano walimgusa na kumsonga lakini hawakum**jua** kweli kweli! Walifikili yeye ni mmoja wa manabii, lakini hawakuamini ya kwamba kutimia kwa Mungu kulikuwa ndani yake.

Tuliona ya kwamba viongozi wa Wayuda kwa maneno ya dini

walikataa Yesu kabisa kabisa. Walimwonea wivu sana na mwishoni walimwua kwa njia ya kumfunga juu ya msalaba na misumari! Lakini Mungu alikusudi neno hili tangu mwanzo; mauti ya Masiya juu ya msalaba ilitimiza **shauri lake takatifu** alilotangaza miaka mingi mbele kwa njia ya manabii wake. Kwa sababu hii, siku makuhani walipofunga Yesu aweze kuuawa, Yesu alisema na Petro aliyetaka kumlinda, *"Unazania ya kuwa mimi siwezi kusihi Baba yangu, naye atanitumia sasa zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika? Basi **maandiko yatatimizwa namna gani ya kama sharti itokee hivi?**"* (Matayo 26:53,54)

Yesu alijua kwa sababu gani alikuwa amefika duniani. Alikuja aweze kutoa uzima wake, kumwanga damu yake kwa wenye zambi, kama manabii walivyotangaza zamani. Yesu alikuja kutimiza mfano wa sadaka ya kondoo ya Abrahamu na wa sadaka zote nyingine za nyama. Unakumbuka neno la mwisho Yesu alilosema juu ya msalaba mbele ya kutoa roho yake kwa Mungu? Ndiyo, Maandiko yanatujulisha ya kwamba alisema na sauti kubwa, ***"Imekwisha!"*** Kisha alikufa. Wakati alipokufa, pazia la hekalu lilipasuka vipande viwili toka juu hata chini. (Yoane 19:30; Marko 15:37,38) Kwa nini Yesu alitoa sauti kubwa kusema, *"Imekwisha!"*? Na kwa sababu gani pazia la Patakatifu pa Patakatifu hekaluni lilipasuka vipande viwili, ndipo pahali waliponyunyiza damu ya sadaka za nyama kufunika zambi? Ni Mungu aliyepasua pazia vipande viwili, na Yesu alitangaza, *"Imekwisha!"* ili watu wote waweze kujua ya kwamba kwa njia ya **damu ya Yesu Mungu anaweza kusamehe** wana wa Adamu zambi zao na kuwapa ruhusa kukaa mbele ya Mungu mtakatifu kwa milele!

Everyday Publications Inc @ 2010

**Kwa njia ya mauti yake, Bwana Yesu Kristo alitimiza maneno ya manabii na mfano wa sadaka za nyama**. Na kama tulivyoona, ufufuko wake siku ya tatu ulihakikisha wazi ya kwamba Mungu alipokea sadaka yake kama bei nzima kulipa kwa zambi kwa milele! Yesu Kristo ni sadaka kamilifu ambayo Mungu alitoa kwa watu wa dunia, ili mtu ye yote ambaye anaamini yeye hatapotea lakini atakuwa na uzima wa milele!

Sasa, kwa kumaliza ukumbusho wetu wa habari za manabii, tunakuita kusikiliza mashairi mengine ya ajabu na yenye maana sana toka Neno la Mungu juu ya zabihu kamilifu na ya mwisho ambayo Yesu Masiya alitoa wakati alipomwanga damu yake juu ya msalaba kulipa kwa zambi. Maandiko yanasema:

(Waebrania 10) *1 Kwa kuwa **torati ni kivuli cha yale mema***
***yatakayokuwa, wala si sura yao yenyewe,** haiwezi hata mara*
*moja kwa zabihu ambazo wanazitoa kila mwaka daima, kukamilisha*
*wenye kukaribia. 2 Kama sivyo, wangeacha kuzitoa; kwa maana*
*wenye kuabudu wakikwisha kusafishwa mara moja, kama wasingejua*
*zambi tena mioyoni? 3 Lakini katika zabihu zile ni ukumbusho wa*
*zambi kila mwaka, 4 **maana haiwezekani kwa damu ya ngombe***
***na mbuzi kuondoa zambi.***

*5 Kwa sababu hii wakati anapokuja katika dunia anasema: Zabihu*
*na sadaka hukutaka, lakini mwili uliniwekea tayari; 6 sadaka za*
*kuteketezwa, na sadaka za zambi hukuzitaka. 7 Halafu nilisema:*
*Tazama, nimekuja (Katika gombo la kitabu nimeandikiwa) nifanye*
*mapenzi yako, Mungu . . . 9 Ameondoa la kwanza, kusudi asimamishe*
*la pili. 10 Katika mapenzi haya **tumepata utakaso kwa kutolewa***
***mwili wa Yesu Kristo mara moja.** 11 Na kila kuhani anasimama*
*kila siku akitumika, na kutoa zabihu zile zile mara nyingi nazo hazi-*
*wezi kabisa kuondoa zambi. 12 Lakini yeye wakati alipokwisha kutoa*
*zabihu moja kwa zambi hata milele, aliketi mkono wa kuume; 13 aki-*
*ngojea mpaka adui zake wawekwe kuwa chini ya miguu yake. 14*
***Maana kwa toleo moja amekamilisha hata milele wenye***
***kutakaswa.** 15 Na Roho Mtakatifu anatushuhudia vilevile, kwa*
*maana nyuma ya kusema: 16 Hili ni agano nitakalofanya nao:*
*Nitatia sheria zangu ndani ya mioyo yao, na katika akili zao*
*nitaziandika; 17 na zambi zao na maovu yao sitayakumbuka tena. 18*
*Basi pahali maneno haya yanaposamehewa, hapana toleo tena kwa*
*zambi.*

*19 Basi, ndugu, kwa sababu tuna uhodari wa kuingia Pahali*
*Patakatifu **kwa damu ya Yesu,** 20 njia ile aliyoanza kwa ajili yetu,*
*mpya, na hai, katika pazia, ndio mwili wake; 21 na tukiwa na kuhani*
*mkubwa juu ya nyumba ya Mungu; 22 tukaribie **kwa moyo wa***
***kweli, kwa utimilifu wa imani** . . . 23 Tushike sana kukiri kwa*
*tumaini letu, kusudi lisigeuke; maana yeye aliyeahidi ni mwaminifu;*
*24 na tuangaliane kwa njia ya kusukumana katika mapendo na kazi*
*nzuri . . . 26 Kama tukifanya zambi kusudi nyuma ya kupokea kujua*
*kwa kweli, haibaki tena zabihu kwa ajili ya zambi; 27 lakini kutaza-*
*mia hukumu kwa woga, na ukali wa moto ulio tayari kula adui. 28*
*Mtu aliyezarau sheria ya Musa alikufa pasipo huruma kwa neno la*
*washuhuda wawili au watatu. 29 Munazania nini? **Haikupasa***
***azabu kubwa zaidi kwa mtu yule aliyekanyaga Mwana wa***
***Mungu,** na kuhesabu damu ya agano aliyotakaswa nayo kuwa kitu*

Everyday Publications Inc @ 2010

> *kichafu, na kutukana Roho ya neema? 30 Maana tunamjua yeye aliyesema: Malipizi kisasi ni juu yangu, mimi nitalipa, Bwana anasema. Na tena: Bwana atahukumu watu wake. 31 Ni neno la kuogopa kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai.*
>
> ***"Sisi tutapona namna gani tusipochunga wokovu mkubwa namna hii?"*** (Waebrania 2:3)

Na maneno haya, Mungu anatuonya sisi sote tusikose kuangalia na kuchunga njia ya pekee ya wokovu, iliyo ndani ya damu ya Yesu Masiya. Lazima **kila mtu anayezarau Zabihu ambayo Mungu Mwenyewe alitoa ajue ya kwamba hakuna zabihu nyingine kwa zambi;** inabaki hukumu ya Mungu tu, hukumu bila rehema! Yesu Kristo ni Sadaka kamilifu, ambayo Mungu Mwenyewe alitoa, ili **kila mtu ambaye anamwamini** asipotee lakini awe na uzima wa milele. Juu ya msalaba Yesu alisema, *"Imekwisha!"* Basi Yesu akiwa Neno la Mungu—wakati Yesu aliposema, *"Imekwisha,"* alikuwa Mungu Mwenyewe akisema, ***"Imekwisha!"*** Na nyuma ya siku tatu Mungu alifufua Yesu toka mauti, na kuhakikisha kwa dunia ya kama anakubali kabisa sadaka ya Yesu kwa zambi.

Everyday Publications Inc
@ 2010

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Rafiki, unafahamu ya kwamba Yesu alilipa bei kwa zambi zako? Unaamini ya kwamba Yesu Kristo alimaliza kazi ya wokovu kwa wewe? Au unakaa kujaribu kujiokoa mwenyewe kwa njia ya kazi zako njema?

Kufika mara ya nyuma, Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya maana ya ndani ya tangazo la Masiya toka msalaba, wakati aliposema,

***"Imekwisha!"*** (Yoane 19:30)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Somo 97

# Hadeze!

Luka 16

Salama iwe kwako, rafiki. Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuja tena leo na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Maandiko Matakatifu yanasema:

> *"Wenye woga, na wasioamini, na wenye machukio . . . na wawongo wote . . sehemu yao ni katika lile* ***ziwa linalowaka moto na kiberiti****."* (Ufunuo 21:8) *"Watatupwa katika giza la inje . . . katika moto wa milele uliotengenezwa kwa Shetani na malaika zake; kutakuwa kulia na kusaga meno."* (Matayo 8:25; 25:41) *"Hawa wote watakwenda kuingia katika* ***azabu ya milele****; lakini wenye haki watakwenda kuingia katika uzima wa milele!"* (Matayo 25:46)

Everyday Publications Inc
@ 2010

**Hadeze!** Inaitwa **Jehanum** vilevile. Hakuna mtu anayetaka kusema juu yake. Hatutaki hata kufikili juu yake! Hata hivi, tunakusudi kusema juu ya Hadeze leo, kwa sababu Mungu anasema maneno mengi juu yake. Ndani ya Maandiko Matakatifu kuna mia za maonyo kuzuiza watu wasiende pale. Leo na ndani ya somo la nyuma tunakusudi kujifunza juu ya mafundisho ya Maandiko juu ya hadeze (jehanum) na mbingu (Paradiso), na namna gani tunaweza kujua kabisa ya kwamba tutakwenda mbinguni na hatutatumwa kwa hadeze. Watu wengi wanafikili ya kwamba haiwezekani kwao kujua nini itatokea nyuma ya kufa kwao, au kama watashinda milele kwa pahali gani. Wanafikili hivi kwa sababu hawajui njia ya wokovu ambayo Mungu alitayarisha, wala ahadi za ajabu ya Mungu ambazo zinatuwezesha kujua kabisa kwamba tutakwenda mbinguni. Neno la Mungu linatuambia namna gani tunaweza kujua kwa hakika ya kwamba tutakwenda Paradiso? Ndiyo! Neno la Mungu linasema:

*"Ninawaandikia ninyi wenye kuamini jina la Mwana wa Mungu, maneno haya* ***ili mujue ya kuwa muna uzima wa milele!"*** (1 Yoane 5:13)

Rafiki, una uzima wa milele ambao Mungu alitangaza? Siku unapokufa, una**jua** pahali gani roho yako itakapokwenda? Unajua **kabisa** ya kwamba utaingia Paradiso, na hutatumwa kwa hadeze? Kama usipojua maneno haya kabisa, somo letu la leo litakuwa na faida kubwa kwawe.

Kama tulivyoona ndani ya Habari Njema, wakati Yesu Mwokozi alipokuwa duniani, alifundisha watu mara nyingi juu ya pahali panapoitwa **Mbingu** na pahali panapoitwa **Hadeze**. Lakini Yesu alifundisha juu ya hadeze kupita juu ya mbingu, kwa sababu anajua kwamba azabu ya hadeze ni ya kuogofya sana, na hataki mtu ye yote kwenda pale.  Basi sasa tugeuke kwa Habari Njema na kusikia maneno Yesu aliyofundisha makutano juu ya hadeze. **Sikiliza habari hizi za kweli** juu wa watu wawili waliokufa. Tunasoma ndani ya Habari Njema ya Luka, sura 16. Yesu alisema na makutano:

> (Luka 16)  *19 "Kulikuwa* ***mtu tajiri*** *fulani, amevaa nguo nyekundu na bafuta, na kila siku alifurahi na anasa.  20 Na inje ya mlango wake* ***masikini mmoja*** *alilala,* ***jina lake Lazaro****, naye alikuwa na vidonda vibaya,  21 akataka sana kushibishwa na makombo yaliyoanguka toka meza ya yule tajiri; hata imbwa walikuja wakaramba vidonda vyake.*
>
> *22 Halafu yule masikini alikufa, akachukuliwa na malaika katika* ***kifua cha Abrahamu****. Yule tajiri alikufa vilevile, akazikwa. 23* ***Katika hadeze*** *akiwa katika azabu akanyanyua macho yake, akaona Abrahamu mbali na Lazaro katika kifua chake."*

Everyday Publications Inc
© 2010

Tuache kwanza. Ulifahamu maneno yaliyopata tajiri na mtu masikini, Lazaro? Mtu masikini alikwenda wapi wakati alipokufa? Roho yake ilikuwa mara moja katika **Paradiso**, mbele ya Mungu, pahali Abrahamu, nabii wa Mungu, alipofika miaka mingi mbele. Na yule tajiri, alikwenda wapi? Roho yake ilikuwa mara moja katika **hadeze**, pahali alipokuwa katika maumivu.

Kwa nini mtu masikini, Lazaro, alikwenda Paradiso na tajiri alikwenda hadeze? Kwanza, tufahamu ya kwamba si kusema mtu akiwa masikini ataokolewa, na akiwa na mali nyingi si kusema ya kwamba atapotea! Lazaro, mtu masikini alikwenda Paradiso kwa sababu **aliweka roho juu ya njia ya wokovu** ambayo Mungu alitangaza ndani ya Maandiko ya Manabii. Lakini yule tajiri, **hakuwe-**

**ka roho juu ya Neno la Mungu**, Anafanana na watu wengi kwa wakati wa sasa wanaoonekana kuwa watu wa dini. Wanajua kuna Mungu mmoja na ya kwamba kuna Maandiko ya Manabii, lakini wanafuata njia ya hadeze kwa sababu hawakuamini kamwe njia ya wokovu ambayo manabii wote wa Mungu walishuhudia ndani ya Maandiko. Kama tajiri ndani ya habari zetu za leo, wanaweka roho juu ya kujifurahisha wenyewe na kujivimbishia mali kupita juu ya kusikiliza Neno la Kweli linaloweza kuokoa roho zao.

Tuendelee na habari zetu na kusikia namna gani Mungu aliruhusu tajiri, aliyekuwa katika hadeze, kusemezana kidogo na nabii Abrahamu, aliyekuwa katika Paradiso. Mungu anataka sisi kupata ufahamu toka maneno mtu huyu aliyosema katika hadeze. Bwana Yesu aliendelea na habari hizi akisema,

> (Luka 16) *23 Katika Hadeze [tajiri] akiwa katika azabu, akaona Abrahamu mbali na Lazaro katika kifua chake. 24 Akalalamika, akasema: Baba Abrahamu, unirehemu, utume Lazaro atie ncha ya kidole chake katika maji apoleshe ulimi wangu; kwani ninateswa katika moto huu.*
>
> *25 Lakini Abrahamu alisema: Mwana, kumbuka ya kuwa ulipokea vitu vizuri katika maisha yako, kama vilevile Lazaro alivyopokea vitu vibaya; lakini sasa anafarijiwa, na wewe unateswa. 26 Na zaidi ya maneno haya yote, shimo kubwa limewekwa kati yetu, sisi na ninyi; hata watu wanaotaka kutoka hapa kupita kwenu hawawezi, wala wanaotaka kutoka kule kupita hapa kwetu.*
>
> *27 Halafu akasema: Ninakuomba, baba, umtume nyumbani mwa baba yangu, 28 kwani nina ndugu watano; awashuhudie, wasifike vile pahali hapa pa azabu.*
>
> *29 **Abrahamu akamwambia**: **Wana Musa na manabii, wawasikilize wao**.*
>
> *30 Akasema: Sivyo, baba Abrahamu; lakini kama mmoja atakwenda kwao toka wafu, watatubu.*
>
> *31 Akamwambia: **Wasiposikia Musa na manabii, hawatasadikishwa kama mmoja akifufuka toka wafu.***

Everyday Publications Inc
@ 2010

Huu ndio mwisho wa habari za tajiri na Lazaro. Kweli pahali panapoitwa Hadeze ni pahali pa kuogofya, pahali panapokosa rehema. Tajiri katika Hadeze alitaabishwa na hakuna mtu aliyeweza kupunguza maumivu yake kwa njia ya kumpa hata maji kidogo! Na neno lililo la kuogofya zaidi ndilo hili, tajiri huyu ni pale hata leo!

Yeye ni katika Hadeze akingojea Siku ya Hukumu wakati nafsi yake na roho yake zitakapotupwa ndani ya **ziwa linalowaka moto**. Atakuwa pale kwa milele pamoja na **kila mtu aliyekataa kutii mafundisho ya manabii**—Habari Njema ya Yesu Masiya. Haya ndiyo maneno Maandiko yanayosema: *"Na ikiwa mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, atatupwa katika lile ziwa la mto . . . Na moshi wa mateso yao ulipanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku!"* (Ufunuo 20:15; 14:11) Fikili kwanza! Kila mtu anayeona bule njia ya haki ya wokovu Mungu aliyotayarisdha, na kuingia Hadeze, hatakufa kamwe (maana yake hataacha kuwa), hataweza kutoka kule **kamwe**, na moto ule hautazimishwa **kamwe! Kamwe! Kamwe! Kwa milele!**

Watu wengine wanafikili ya kwamba wenye zambi, nyuma ya kuteswa kwa wakati katika Hadeze watatoka kule na watakwenda Paradiso. Lakini mawazo haya hayapatani na Neno la Mungu linaloeleza Hadeze kuwa pahali pa *"azabu ya **milele**."* (Matayo 25:46) Hivi, hakuna maombi kwa wafu ndani ya Maandiko ya Manabii. Kuombea wafu ni desturi ya watu tu, na hakutoki kwa Neno la Mungu linalosema watu wanawekwa kufa mara moja, na nyuma ya kufa hukumu! (Waebrania 9:27) Kuombea wafu hakuwezi kupunguza maumivu yao katika Hadeze wala kuwaponyesha Siku ya Hukumu. Na wale walio mbinguni hawahitaji maombi yetu, kwa sababu wao ni pale mbele ya Mungu na katika raha ya kutimia!

Everyday Publications Inc
@ 2010

Wasikiaji wenzangu, **Musiache mtu ye yote kuwadanganya ninyi na masemo ya bule.** Watu wengine wanasema, "Eh, Mungu ni mwema! Asingaliumba watumishi wake, kisha kuwateketeza! Ataturehemu sisi sote na kutupokea katika Paradiso!" Lakini wale wanaosema hivi hawana msingi kwa mawazo yao. Wanasema hivi kwa kutuliza damiri zao kwa sababu kwa kutaka kwao wenyewe wanaona bule njia ya wokovu ambayo Mungu alitayarisha. Kama wasipoacha mawazo yao mabaya na kugeuka kwa Mungu na kupokea njia ya haki ambayo aliwatayarishia, watajua siku nyingine ya kwamba Hadeze iko! Lakini saa ya kutubu itakuwa **imepita**!

Ulisikia neno tajiri aliloomba Abrahamu (katika Luka 16)? Alimwomba kutuma Lazaro kwa nyumba ya baba yake kuonya ndugu zake watano wasiokufa bado, *"wasifike vile pahali hapa pa azabu!"* Abrahamu alimjibu nini? Alimwambia, ***"Wana Musa na manabii, wawasikilize wao!"*** Lakini tajiri alijibu, *"Sivyo, baba*

*Abrahamu, lakini kama mmoja atakwenda kwao toka wafu, watatubu." Abrahamu alisema naye,* ***"Wasiposikia Musa na manabii, hawatasadikishwa kama mmoja akifufuka toka wafu."***

Wewe msomaji, unajua Habari Njema ya manabii ya Mungu inayoweza kukuokoa toka Hadeze? Habari Njema hii ndiyo habari unayosoma ndani ya masomo ya *Njia ya Haki*. Kwa kujumlisha tumeona ya kwamba habari njema ya manabii ni Habari Njema juu ya Mkombozi mtakatifu ambaye Mungu alituma duniani kufa juu ya msalaba kwa kulipa kwa zambi zako, na kufufuliwa toka wafu siku ya tatu **ili ukimwamini moyoni mwako usiende hadeze!** Hizi ndizo Habari Njema ambazo zinaweza kukuokoa toka hukumu ya haki ya Mungu.

Kama tulivyoona ndani ya somo letu la kwanza, Mungu hakuumba hadeze kwa watu, lakini kwa Shetani na malaika zake maovu. Lakini kwa sababu ya zambi ya baba yetu Adamu sisi sote tulizaliwa mbali na Mungu, inje ya Shamba la Paradiso (Edeni) hapa duniani, katika ufalme wa Shetani, kwa njia pana inayofikisha watu kwa hadeze. Bila shaka tabia ya zambi ndani yetu ingalitu**haribu kwa milele**, isipokuwa Mungu ametutayarishia njia ya ku**okolewa**, kwa sababu malipo kwa zambi ni mauti na hadeze kwa milele. Haiwezekani kwetu kuepuka zambi kwa nguvu yetu wenyewe! Lakini, tunashukuru Mungu aliyefanya shauri na kwa njia ya shauri hili anaweza kutusamehe zambi zetu! Shauri hili ni nini? Ni **kufa kwa Masiya mtakatifu**. Juu ya msalaba. Mungu aliweka juu ya Yesu Kristo azabu kwa zambi zetu, mara moja na kwa milele. Kama ilivyoandikwa: *"Yeye [Kristo] asiyejua zambi [Mungu] alimfanya zambi kwa* ***ajili yetu*** *ili sisi tuwe haki ya Mungu katika yeye."* (2 Wakorinto 5:21)

Tuliona namna watu walivyotesa Yesu, wakimpiga, kutia taji ya miiba juu ya kichwa chake, wakimzarau na kumpiga usoni, wakimtemea mate na kumfunga juu ya msalaba na misumari. Mungu aliruhusu watu kutesa Mwana wake mpendwa namna hii, kwa kuonyesha azabu sisi tuliyostahili kupata kwa zambi zetu. Ingalitupasa sisi kutendewa kila kitu ambacho watu walitendea Yesu. Lakini Mungu, kwa sababu ya mapendo yake makubwa kwasi, aliweka azabu kwa zambi zetu juu ya Masiya mtakatifu, Mwana wake mpendwa. Na kumbuka ya kwamba mateso Yesu aliyopata si maneno ambayo watu walimtendea tu. Maandiko ya Manabii yanaonyesha ya kwamba wakati Yesu alipokuwa akiteswa juu ya msalaba, Mungu yeye mwenyewe aliweka juu yake maumivu

Everyday Publications Inc @ 2010

ambayo sisi watu hatuwezi kufahamu. Mungu aliweka juu ya Yesu malipo kwa zambi zetu, maana yake, **hadeze yetu**! Nabii Yobu alitabiri mateso makali sana ambayo Masiya atavumilia toka Mungu wakati alipoandika, *"Mungu amenitoa kwao wasio haki, na kunitupa mikononi mwa waovu. . .* ***[Mungu] amenipasua katika gazabu yake, na kunitesa; amenisagia meno yake; mtesi wangu amenikazia macho yake.****"* (Yobu 16:11,9)

Malipo kwa zambi ni mauti na kupokea gazabu ya Mungu na kuingia katika giza la hadeze, ndipo pahali Mungu anapoweka wote wanaokataa kuamini Habari Njema! Lakini Yesu alivumilia gazabu ya Mungu kwa ajili yetu, ili sisi tuweze kupokea neema ya Mungu. Kama tulivyoona, wakati Yesu alipokuwa akikufa msalabani, inchi nzima iligeuka giza nyeusi kama hadeze—toka azuhuri kufika saa tatu. Ndani ya saa hizi, Yesu aliita na sauti kubwa, **"Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha?"** Basi kwa sababu gani Mungu aliacha Masiya, mpendwa wake, juu ya msalaba? **Kwa sababu yako na yangu**. Kwa sababu ya zambi zetu! Wakati Yesu alipokuwa juu ya msalaba, Mungu aliweka juu yake azabu kwa zambi zetu, **hadeze yetu!** Hii ni kweli ya maana sana tusiyoweza kufahamu na nia zetu. Lakini kuna neno moja la hakika kabisa, ndilo hili: **Ukiamini Bwana Yesu na roho ya kweli, utaokolewa, na hutakwenda hadeze kamwe,** kwa sababu umepokea zabihu ya Mkombozi ambaye Mungu alimtoa kukukomboa. Kama kondoo ya sadaka, iliyokomboa mwana wa Abrahamu asife, Yesu Masiya alikufa kukuokoa wewe toka mauti isiyokwisha kwamwe katika pahali panapoitwa **hadeze**!

Everyday Publications Inc
@ 2010

Mungu aliweka hadeze yako juu ya Yesu Kristo. **Unaamini neno hili?** Unaamini ya kwamba Yesu Kristo Mwenye haki, alilipa deni yako kwa wewe? Au utakwenda hadeze kulipa deni yako ya zambi wewe mwenyewe kwa milele? **Ni maneno yako kuchagua**. Utachagua nini? **Paradiso**? Au **hadeze**?

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Asante kwa kusoma pamoja nasi. Usikose kufika tena mara ya nyuma wakati tutakapojifunza juu ya neno lililo namna nyingine kabisa na neno tulilojifunza leo, kwani, Mungu akitaka, tutajifunza juu ya pahali pazuri sana panapoitwa Paradiso . . .

Mungu akubariki. Tunaagana nawe na masemo haya toka Bwana Yesu:
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

*"Ingieni kwa mlango ulio mwembamba; kwani mlango ni mpana na njia ni pana inayokwenda hata upotevu, nao ni wengi wanaoingia kwa mlango huu. Lakini mlango ni mwembamba, na njia imesongwa inayokwenda hata uzima, nao ni wachache ambao wanaiona."* (Matayo 7:13,14)

Everyday Publications Inc
@ 2010

## Somo 98

# Paradiso

### Ufunuo 21,22

Tunakusalimu tena kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele.

Ndani ya soma la mbele, tuliwaza juu ya pahali azabu isipokwisha kamwe, ndipo **hadeze**. Hadeze ni pahali pabaya sana, palipoumbwa kwa Shetani na malaika zake. Ni pahali kila mtu asiyeweka roho juu ya njia ya wokovu ambayo Mungu alitayarisha atalazimishwa kwenda, akitengwa na Mungu kwa milele! Hili ndilo neno Maandiko Matakatifu yanatangaza, yakisema: *"Ikiwa mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto!"* (Ufunuo 20:15)

Everyday Publications Inc. @ 2010

Kweli hadeze ni habari za kuogofya sana ambazo mtu anaweza kufikili. Lakini leo, tunataka kuangalia neno zuri zaidi ambalo roho ya mtu anaweza kufikili, ndilo **mbingu**, zinazoitwa ***Paradiso*** vilevile.

Watu wana mafikili mbalimbali juu ya Paradiso, na juu ya maneno inayopasa mtu kufanya kuingia pale. Kwa mfano, wale wanaoshika dini za mashariki wanafikili kuna mbingu (paradiso) nyingi zenye vipimo mbalimbali vya anasa, na ya kwamba kwa kipimo cha kazi zake kila mtu atakwenda kwa mbingu fulani. Watu wengine wanafikili ya kwamba inapasa mtu kufika kwa hadeze kwanza, na wakati anapokwisha kulipa deni yake ya zambi, atahamishwa kwa Paradiso. Na wengine wanafikili ya kwamba Paradiso ndipo pahali Mungu alipoweka mbali kwa wale wanaofanya kazi za dini yao na uaminifu, na ya kwamba ni pahali watu wanaposhikana na anasa, wakikula, kunywa na kulala na wanawake wa kuonekana vizuri sana. Ndiyo, watu wana mawazo mengi juu ya Paradiso na namna gani kufika pale. Lakini leo hatutaki kufikili zaidi juu ya **mawazo ya watu** juu ya Paradiso, lakini juu ya **maneno**

**Mungu anayosema** ndani ya Neno lake takatifu!

Pahali pa Paradiso pana majina mengi ndani ya Maandiko ya Manabii. Panaitwa *mbingu; kiti cha ufalme cha Mungu; pahali Mungu alipo; nyumba ya Mungu; kao la Mungu Mtakatifu; mji mtakatifu; mji wa Mungu aliye hai; Yerusalema wa mbingu; kao la malaika watakatifu na Mwana-kondoo; pahali Bwana Yesu na utukufu wake mkubwa alipo; na kao la watu wa Mungu, wenye majina yaliyoandikwa mbinguni.* Bwana Yesu aliita Paradiso, *"Nyumba ya Baba yangu,"* kwa sababu ndipo pahali alipokuwa mbele ya kuzaliwa duniani.

Kwa kujumlisha, Paradiso ni **kao la Mungu**. Kama tulivyoona, Mungu ni pahali pote; hata hivi kuna pahali pamoja palipo patakatifu, na kungaa na kuonekana vizuri sana. Pahali pale ni mbali sana, kupita malaika; pahali Mungu anapokaa katika utukufu wake. Pahali pale ndipo pahali Mwana wa Mjuu sana, Yesu anapoketi juu ya kiti cha ufalme, kwa mkono wa Mwenyezi, akingoja wakati atakaporudi kuhukumu dunia na kuitengeneza. Vile, Paradiso ndipo pahali elfu elfu za malaika wanapozunguka kiti cha ufalme, pamoja na makutano makubwa sana ya watu ambao Mungu alikomboa kwa yeye mwenyewe kwa njia ya damu ya Mwana-kondoo, Bwana Yesu Kristo.

Everyday Publications Inc @ 2010

Kwa mwisho wa kitabu cha Agano Jipya, ndani ya sura mbili za mwisho za kitabu cha Ufunuo, Mungu alitolea Yoane, mtume wake, ono kumwonyeshea Mji Mtakatifu wa Paradiso, ambao Bwana amefanya kwa wale wenye majina ndani ya kitabu cha uzima wa milele. Sikia maneno Maandiko yanayosema juu ya Mji wa Paradiso.

> (Ufunuo 21) *10 Akanichukua katika Roho, mpaka mlima mkubwa, akanionyesha ule **mji mtakatifu** . . . 11 wenye **utukufu wa Mungu;** mwangaza wake ulikuwa mfano wa jiwe la bei kubwa, kama jiwe la yaspi, safi kama bilauri. 12 Ulikuwa na ukuta mkubwa, na mrefu, wenye milango kumi na miwili, na kwa ile milango malaika kumi na wawili . . .*
>
> *16 Na ule mji ni mraba, na urefu wake sawasawa na upana wake. . . 19 Na misingi ya ukuta wa mji ilikuwa imepambwa kwa mawe ya bei ya damani ya kila namna . . . 21 Na ile milango kumi na miwili ni lulu kumi na mbili; kila mlango ni lulu moja. Na njia ya mji ni zahabu safi kama kioo waziwazi. 22 Nami sikuona hekalu ndani yake, kwa maana **Bwana Mungu Mwenyezi na Mwana-kondoo** ndio hekalu lake. 23 Na mji ule hauhitaji jua wala mwezi kuuangaza, kwa maana **utukufu wa Mungu** unautia nuru, na taa yake ni Mwana-*

*Kondoo. 24 Na mataifa ya wale waliookolewa wanatembea katika nuru yake . . 25 Na milango yake haitafungwa kabisa mchana, kwa maana kule hakuna usiku . . . 27 Na* ***ndani yake hakitaingia kabisa kitu cho chote kilicho kichafu, wala yeye anayefanya machukizo na uwongo, lakini wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo.***

(Ufunuo 22) *1 Kisha akanionyesha mto wa maji wa uzima wenye kungaa kama bilauri, ukitoka katika* ***kiti cha ufalme cha Mungu, na cha Mwana-Kondoo****. 2 Katikati ya njia yake ya ule mto, upande ngambo na ngambo, ulikuwa mti wa uzima, unaozaa matunda namna kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila mwezi . . . 3 Wala haitakuwa laana yo yote tena [wala mauti haitakuwa tena, wala maombolezo, wala kilio, wala uchungu, Ufunuo 21:4]. Na* ***kiti cha ufalme cha Mungu, na cha Mwana-Kondoo*** *kitakuwa ndani yake. Na watumishi wake watamtumikia. 4 Na wataona* ***uso wake,*** *na* ***jina lake*** *litakuwa katika vipaji vya nyuso zao. 5 Wala hautakuwa usiku tena; wala hawahitaji taa, wala nuru ya jua;* ***kwa maana Bwana Mungu*** *anawatia nuru, nao watatawala hata milele na milele.* Amina.

Everyday Publications Inc @ 2010

Hili ndilo ono Mungu aliloonyeshea Yoane, ono la Mji Mtakatifu anaotayarishia wale wanaochagua njia yake ya wokovu. Ndani ya saa inayobaki leo, tunataka kufikili kidogo juu ya maneno Mungu anayosema ndani ya Neno lake juu ya **njia inayofika Paradiso**. Namna gani tunaweza kujua hakika ya kwamba tutakwenda Paradiso, si hadeze?

Unakumbuka maneno Masiya, Yesu aliyosema na wanafunzi wake juu ya nyumba ya Mungu Baba yake na njia inayofika kule? Alisema nao:

(Yoane 14) *1 Musifazaike mioyoni mwenu: munaamini Mungu, muniamini mimi vilevile. 2 Katika nyumba ya Baba yangu ni* ***makao mengi****: kama sivyo ningaliwaambia ninyi;* ***ninakwenda kuwatengenezea ninyi pahali.*** *3 Na kama ninakwenda kuwatengenezea ninyi pahali, nitakuja tena, na nitawakaribisha ninyi kwangu; pahali ninapokaa mimi, ninyi mukae vilevile. 4 Na pahali ninapokwenda munajua, na njia munajua . . . 6 Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima:* ***mtu hakuji kwa Baba, ila kwa mimi.***

Haya ndiyo maneno Bwana Yesu aliyosema. Yeye mwenyewe ni **Njia**. Mtu ye yote asiyefika kwa njia ya Mwana wa Mjuu sana, ndiye

Mkombozi mtakatifu, hataingia mbele ya Mungu Mtakatifu **kamwe!** Ndiyo, **KAMWE!** Hili ndilo neno Maandiko yanatangaza wakati yanaposema:

> *"Wala hakuna wokovu* ***katika mwingine,*** *kwa maana hakuna jina lingine chini ya mbingu walilopewa watu tupate kuokolewa nalo."* (**Ma**tendo 4:12) *"Kwa sababu Mungu ni mmoja tu, na mpatanishi katikati ya Mungu na watu ni mmoja, yule mtu Kristo Yesu, ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote . . ."* (1 Timoteo 2:5,6)

Mpatanishi, Yesu Kristo, aliyetoka kwa Mungu, ni **Njia ya Wokovu** inayofikisha watu kwa Paradiso. Kwa kuleta wenye zambi kwa Mungu, Kristo alizaliwa duniani, aliishi maisha matakatifu duniani, alimwanga damu yake kama zabihu kamilifu kwa zambi, kisha alifufuka toka wafu siku ya tatu. Hakuna mtu anayefika kwa Mungu ila kwa njia yake. Unaamini neno hili? Unafahamu ya kwamba Yesu Masiya ni **Njia ya pekee** inayoleta wenye zambi mbele ya Mungu? Labda tunaweza kueleza neno hili wazi zaidi kwa njia ya **hadizi hii ndogo**:

Everyday Publications Inc @ 2010

Mtu mmoja aliishi ndani ya kijiji kidogo mbali sana polini. Watu wa kabila lake hawakuvaa mavazi. Walivaa tu kitu kama kamba kwa viuno vyao. Mtu huyu alikuwa na shamba, lakini mtu mwingine mwenye uwezo kupita yeye alikuja, akanyanganya shamba lake naye hakubaki na shamba alipoweza kulima. Watu wote walikataa kumsaidia kukamata shamba lake tena kwa sababu hakuwa na mali kuwalipa.

Siku moja alifikili vizuri aende kwa mji mkubwa kuona Président, ndiye mtawala wa inchi, na kumwomba kumsaidia, kwa sababu alikuwa amesikia ya kwamba Mtawala alikuwa mtu wa haki na huruma. Hivi aliondoka, akatembea na kutembea na kutembea kufika wakati alipofikia mji mkubwa na nyumba kubwa ya Président. Ilikuwa nyumba ya mapambo mengi! Wakati alipofika, na ku**jaribu kuingia** na uchafu na utupu wake, mlinzi alisema naye: "Ee wewe! Unataka kufanya nini?" Alijibu, "Ninataka kuona Président." Mlinzi alisema nawe, "Unazania ya kwamba mtu ye yote anayetaka anaweza kuingia hapa kama akitaka? Ujiangalie kwanza! Hujui ya kwamba huwezi kuingia hapa na uchafu na bila mavazi? Ondoka hapa, au nitakufunga gerezani!"

Basi yule mtu masikini aligeuka, akakwenda, lakini hakushu-

shwa moyo. Alikwenda na kuomba mali karibu na watu toka asubui kufika mangaribi. Kisha alinunua mavazi ya bei chini, akaoga na kuvaa mavazi yake, akarudi kwa nyumba ya Mtawala. Wakati alipofika tena, mlinzi alisema naye, “Unavaa mavazi, lakini mavazi haya hayatoshi kukuruhusu kutokea mbele ya Mtawala wa inchi. Na hata kama mavazi yako yangalitosha, huwezi kuingia kwa sababu **unahitaji ruhusa** kuingia nyumba ya Président. Hivi huwezi kuingia! Basi kwenda zako!”

Halafu mtu masikini alishushwa moyo, akisema, ”Ni faida gani? Hata nyuma ya masumbuko haya yote, siwezi kufika karibu na Mtawala wa inchi!” Hakuwa na tumaini tena, hivi aliketi kando ya njia na uchungu mkubwa. Lakini, wakati maneno haya halipokuwa yakitokea, Mtawala wa inchi alimwona. Mwana mzaliwa wa kwanza wa Mtawala alikuwa pale vilevile. Mtawala alisema na mwana wake, “Kwenda na kuuliza kama mtu huyu akitaka nini.” Wakati mwana wa Mtawala alipofikia mtu masikini, alikaa kitako karibu naye, akamwuliza, “Bwana, ninaweza kukusaidia? Ulifika hapa mjini kwa sababu gani, na kwa nini una huzuni hivi?” Masikini alimwambia, “Ninataka kuona Mtawala wa inchi, lakini haiwezekani. Nilipima kwa kila njia, lakini **yote ni bule!”**

Everyday Publications Inc
@ 2010

Kijana alisema naye, “Mimi ni mwana wa Mtawala wa inchi, na baba yangu alinituma hapa kukusaidia. Unifuate.” Hivi alikwenda pamoja naye kwa lango la nyumba ya Président. Wakati walipofika mlinzi aliyezuiza masikini mbele asiingie, aliwasalimu na heshima kubwa nao waliingia lango na kiwanja cha nyumba kubwa. Mwana alimpa mtu masikii vazi zuri sana, na pamoja waliingia nyumba ya Mtawala. Hivi, mtu masikini aliweza kuingia nyumba ya Président na kuona Mtawala wa inchi, kwa sababu ya **kusaidia na amri ya mwana wa Mtawala.**

Rafiki, ni hivi na wale wanaotaka kuingia Paradidso, pahali pa Mfalme wa wafalme. ndiye Mungu. Mtawala wa ulimwengu ni mtakatifu na mjuu sana. Hatuwezi kuingia mbele yake kwa njia yo yote sisi tunayotaka. Kazi zetu haziwezi kutufungulia njia kufika mbele yake. Sisi ni kama yule mtu masikini aliyejaribu kuingia mbele ya président kwa njia ya kazi zake zaifu. Maandiko yanasema: *“Sisi sote tumekuwa kama kitu kichafu, na haki zetu zote ni kama vitambaa vya kupasukapasuka vya taka.”* (Isaya 64:6) Paradiso ni pahali patakatifu na *“ndani yake hakitaingia kitu cho chote kilicho kichafu, wala yeye anayefanya machukizo na uwongo!”* (Ufunuo 21:7) **Hakuna mtu anayeweza kutuingiza ndani ya pahali pale patakatifu ila Yule Mtakatifu**

**aliyetoka kule!** Mtakatifu huyu ni **Yesu Kristo**, Mwana wa Mungu Mjuu, Mwana-Kondoo wa Mungu, aliyetoka Paradiso, aliyekufa kama sadaka kuondoa zambi, aliyefufuka toka wafu na kurudia Paradiso!

Basi, nani anaweza kuingia Paradiso? Wale tu waliosafishwa **kwa njia ya imani** ndani ya Yesu Mkombozi na damu yake aliyomwanga. Wale tu wataingia Paradiso! Haya ndiyo maneno Maandiko yanatangaza:

> *"Hapana tofauti, kwa sababu wote wamefanya zambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu; wanahesabiwa haki bule kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Yesu Kristo: naye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake.* (Waroma 3:22-25) *"Kama tukipokea ushuhuda wa watu, ushuhuda wa Mungu ni mkubwa zaidi; kwa maana ushuhuda wa Mungu ndio huu, kwamba ameshuhudia Mwana wake. Yeye anayeamini Mwana wa Mungu ana ushuhuda huu ndani yake. Asiyeamini Mwana wa Mungu amemfanya kuwa mwongo, kwa kuwa hakuamini ushuhuda Mungu alioshuhudia Mwana wake mwenyewe.* ***Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu ni katika Mwana wake. Yeye aliye na Mwana ni mwenye uzima; lakini yeye asiye na Mwana wa Mungu hana uzima.*** *Ninawaandikia ninyi wenye kuamini jina la Mwana wa Mungu, maneno haya, ili* ***mujue*** *ya kuwa muna uzima wa milele."* (1 Yoane 5:9-13)

Everyday Publications Inc
© 2010

Wewe **unajua** ya kwamba una uzima wa milele? Unajua kabisa ya kwamba utaingia Paradiso, na kufurahi mbele ya Mungu kwa milele? Umeamini jina la Mwana wa Mungu? Jina lako limeandikwa ndani ya kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo?

Waza sana juu ya maneno tuliyosoma leo, kwa sababu Mungu anataka kukupa ufahamu.

Mungu akubariki wakati unapofikili juu ya shairi hili tamu sana toka Neno lake takatifu:

> ***"Jicho halikuona, wala sikio halikusikia, wala hayakuingia katika moyo wa mtu, maneno Mungu aliyotengenezea wenye kumpenda.."*** (1 Wakorinto 2:9)

## SOMO 99

# UNAFIKILI NINI JUU YA YESU?

## SEHEMU 1

Salama iwe kwako, rafiki. Tunakusalimu kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele. Tunafurahi kwa sababu tunaweza kuendelea na mfulizo wetu *Njia ya Haki.*

Kwa siku nyingi sasa tumeangalia Maandiko ya Manabii kuona njia ya haki iliyotengenezwa na Mungu, kwa njia yake wenye zambi wanaweza kugeuka wenye haki mbele yake. Tumeona namna Yesu Masiya alivyotimiza maneno ya manabiii ya Mungu. **Leo, na ndani ya somo la nyuma,** tunakusudi kufanya ukumbusho wa utukufu wa Yule ambaye manabii wote walisema juu yake. Hivi, jina la masomo haya mawili ya mwisho ya mafundisho yetu ya MAANDIKO YA MANABII ni, **"Unafikili nini juu ya Yesu?"**

Everyday Publications Inc @ 2010

Wakati tuliposoma ndani ya Habari Njema {*Injil*}, tulisikia Yesu akiuliza watu, ***"Munafikili nini juu ya Kristo? Yeye ni mwana wa nani?"*** (Matayo 22:42) Hili ndilo ulizo kubwa zaidi ambalo sisi sote mmoja mmoja tunapaswa kujibu tungali hai. Pahali tutakapokaa kwa milele panafuatana na namna tunavyojibu ulizo hili! Nyuma kidogo Yesu Masiya atarudi, na wakati atakapokuja, atakuuliza wewe namna alivyouliza watu wa wakati ule, akisema, "Basi wewe, unafikili nini juu yangu?"

Ni kusudi letu kukujulisha kama Yesu alikuwa nani. Hatutaki hata kidogo kwa mtu ye yote kukuongoza kwa njia mbaya ndani ya neno hili. Tunakuonya usifikili ya kwamba Yesu Kristo alikuwa mmoja wa manabii tu, au mtu mwema. Sivyo, **alikuwa namna ya peke yake asiye na kifani!** Hakuna mwingine sawaswa naye ndani ya dunia hii au katika dunia ya kuja. Unafikili nini juu yake? Unafikili yeye ni nani? Kuna maulizo kumi ambayo tunataka kukuuliza juu ya Masiya.

**1) Kwanza, unafikili nini juu ya kuzaliwa kwake kwa ajabu?**

Hakuna mtu aliyezaliwa kama yeye. Yeye ni Yesu Mwana wa Maria. Unajua ya kwamba Yoane aliitwa mwana wa Zekaria, Solomono aliitwa mwana wa Daudi, Isimaeli aliitwa mwana wa Abrahamu. Kila mtu anakamata jina la baba yake kama jina lake mwenyewe au anaongeza jina la baba kwa jina lake. Lakini kwa maneno ya Yesu, kwa sababu gani jina la mama yake linaongezwa kwa jina lake? Ni kwa sababu hakuwa na baba duniani. Alizaliwa na mwanamke kijana aliyekuwa bikira. Alizaliwa kwa uwezo wa Mungu. Karibu miaka mia saba mbele ya kuzaliwa kwa Masiya, nabii Isaya alitabiri kama atazaliwa namna gani, wakati aliposema, *"**Bikira** atapata mimba naye atazaa mtoto mwanamume, na ataita jina lake Emanueli (maana yake, "Mungu pamoja nasi)!"* (Isaya 7:14; Matayo 1:23)

Mungu alifanya babu yetu toka vumbi la udongo. Sisi sote ni wazao wa Adamu, na manabii vilevile. Tuko wa dunia. Lakini Bwana Yesu alitoka mbinguni. Sisi sote ni kama udongo mchafu kwa sababu ya zambi zetu, lakini Yesu alikuwa kama mvua toka mbinguni. Alikuwa safi na mtakatifu, kama vile Mungu ni safi na mtakatifu. Habari Njema inatangaza: *"Yesu **alikuja kwa dunia** kuokoa wenye zambi."* (1 Timoteo 1:15) Mbele ya kufika kwa Yesu duniani, alikuwa pamoja na Mungu, kwa sababu yeye ni Neno la Mungu. Yeye mwenyewe alichagua kufika duniani na kukamata mwili wa mtu, kusudi aweze kutuokoa toka zambi zetu. Alikuja toka juu.

Everyday Publications Inc @ 2010

Kuna hadizi ya watu wawili walioanguka ndani ya kisima kilichokwenda chini sana. Mmoja alisema na mwenzake: "Eh wewe, uniponyeshe toka pahali hapa pabaya! Uniondoshe toka matope haya ya kuteleza!" Lakini mtu yule mwingine alisema naye, "Mpumbavu wewe, namna gani ninaweza kukuondosha wakati sisi wawili ni ndani ya shimo hili?" Wao wawili walikuwa ndani ya shimo, na hakuna mmoja wao aliyeweza kuondosha mwenzake toka shimo. Halafu walisikia sauti toka juu akisema nao kushika kamba iliyoshushwa shimoni. **Mmoja tu asiyeanguka ndani ya shimo yeye mwenyewe aliweza kuwasaidia.**

Hata manabii wazuri zaidi hawakuweza kutuokoa toka shimo linayokwenda chini kabisa la zambi, kwa sababu walikuwa wenye zambi wao wenyewe. Lakini Yesu hakuriti tabia ya zambi iliyo ndani ya watu. Alikuja **toka juu**. Alizaliwa na bikira. Tuliona vilevile ya kwamba Mungu alituma malaika zake, na ya kwamba aliweka nyota kubwa katika mbingu kutangaza kuzaliwa kwa Masiya mtakatifu, Mwokozi wa dunia! Maneno ya ajabu kabisa! Hakuna mtu aliyezali-

wa kamwe namna Mtu huyu alivyozaliwa. Hakuwa na kifani kwa namna alivyozaliwa. Lakini Yesu si mkubwa kwa sababu ya namna ya kuzaliwa kwake tu. Yeye hana kifani kwa namna ya **tabia** yake vilevile.

**2) Unafikili nini juu ya tabia yake takatifu?**

Yesu alikuwa mkamilifu. Hakufanya hata zambi moja kamwe. Hakuomba usamehe kamwe kwa sababu hakutendea mtu ye yote mabaya kamwe. Inapasa kila mtu anayeogopa Mungu kutubu zambi zake na kuomba kusamehewa. Manabii wote walifanya hivi. Lakini unaweza kutafuta ndani ya kitabu kizima cha Neno la Mungu, toka mwanzo hata mwisho, lakini hutaona hata shairi moja linalosema kwamba Bwana Yesu aliomba kusamehewa. Hakuhitaji usamehe kwa sababu **hakufanya zambi kamwe.** Rafiki na adui zake waliweza kumshuhudia ya kwamba hawakukuta hata kosa moja ndani yake. Rafiki, hakuna mwingine aliye bila zambi. Bwana Yesu anapita manabii. Alikuwa Neno la Mungu kabisa aliyetokea duniani kama mtu. Ndiyo, Yesu hakuwa na kifano kwa namna ya tabia yake! Lakini zaidi ya ile inatupasa kufahamu ya kwamba hakuwa na kifano kwa **masemo** yake.

Everyday Publications Inc @ 2010

**3) Unafikili nini juu ya masemo yake?**

Siku moja adui zake walituma askari kumfunga. Wakati walipofika pahali alipokuwa na kusikiliza mafundisho yake, walirudi karibu na wakubwa wao bila kumfunga. Walishangaa sana, wakasema, *"Mtu hajasema bado kama mtu huyu anavyosema!"* (Yoane 7:46)

Waza juu ya maneno aliyosema juu yake mwenyewe. *"**Mimi ni nuru ya dunia;** yeye ambaye ananifuata hatakwenda kwa giza kabisa, lakini atakuwa na nuru ya uzima."* (Yoane 8:12) Manabii ni kama mwezi na nyota zinazoleta nuru kidogo katika giza. Lakini Yesu ni kama jua. Nani anahitaji nuru ya mwezi na nyota wakati jua linapokwisha kupanda? Manabii waliita Masiya "Jua la Haki." (Malaki 4:2) Mwezi saa ya kupunguka kwake ni kama manabii. Lakini Yesu Kristo ni jua. Unakwisha kuona jua likipunguka? Sivyo, jua halizimiki kamwe. Linatoa nuru kwa dunia nzima, kwa Afrique na Europe, Asie na Amérique... Yesu Kristo ni kama jua. Hatapita kamwe. Yeye ni nuru kwa kila taifa la dunia.

Yesu alisema vilevile, ***"Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima."*** Yesu ni namna nyingine kabisa na viongozi wengine wanaotoa maagizo, wakisema, "Fanya hivi, fuata mafundisho haya. Hii ndiyo njia.

Shika amri hizi . . ." Bwana Yesu alisema, "**Mimi ni** njia. Uniamini, kuja kwangu, na utakuwa na ruhusa kukaa mbele ya Mungu kwa milele." **Yesu mwenyewe *ni* Njia**. Tujaribu kueleza maana ya kweli hii kubwa kwa njia ya mfano.

Kijana kidogo alipotea katika mji mkubwa. Mtoto aliuliza polisi kumwonyeshea njia ambayo itamrudisha kwa pahali jamaa yake walipopanga. Polisi alisema naye, "Kwenda mbele, geuka kwa kushoto kwa ndaki mbele ya duka, endelea kwa njia ile kufika wakati unapofika kwa nyumba kubwa ya serikali, shika njia inayokwenda kwa kuume, tambuka daraja (kilalo), fuata njia kubwa . . ." Mtoto alianza kutoa machozi. Polisi yule alikuwa ameeleza njia, lakini mtoto alitiwa wasiwasi na aliogopa kufuata maelezo ya polisi. Lakini saa ileile, mtu toka upande wa mji pahali mtoto alipopanga alikuja. Alishika mkono wa mtoto, akamwongoza. Wakati mtoto alipochoka na kutembea, mwanamume alimbeba kufika saa walipofika kwa nyumba ya jamaa ya mtoto. Polisi **alieleza njia**. Lakini, yule mtu mwingine **alikuwa njia**. Yesu alisema: **Mimi ni njia.** Mimi ni njia inayofikisha mbinguni, nyumba ya Mungu. *"Mimi ni njia na kweli na uzima; mtu hakuji kwa Baba, ila kwa mimi."* (Yoane 14:6) Hakuna mwingine aliyesema kama Bwana Yesu kamwe! Alikuwa namna nyingine kabisa. Lakini utukufu wa Yesu haukwishi na habari za kuzaliwa kwake, tabia yake na masemo yake. Tunaweza kuuona ndani ya **kazi** zake vilevile.

Everyday Publications Inc @ 2010

**4) Unafikili nini juu ya kazi za uwezo za Yesu?**

Anaweza kufanya kitu cho chote. Alipewa uwezo na amri yote. Kazi zo zote Mungu alizofanya, Bwana Yesu alifanya duniani, kuonyeshea watu pahali alipotoka na kama alikuwa nani. Nani anayeweza kutuliza upepo ila **Mungu**? **Yesu** alituliza upepo. Nani anayeweza kufufua wafu ila **Mungu**? **Yesu** alifufua wafu. Nani anayeweza kufungua macho ya vipofu ila **Mungu**? **Yesu** alifanya hivi vilevile. Aliponyesha kila namna ya ugonjwa. Alisema neno tu na pepo wachafu walikimbia. Aligeuza maisha ya watu wengi na kuwaokoa toka zambi. Mungu aliwapa wengine wa manabii uwezo kufanya maajabu fulani. Lakini Bwana Yesu alifanya maajabu kwa amri na uwezo wake mwenyewe. Aliweza kusimama karibu na mtu mwenye kupooza, kumkazia macho na kusema, *"Simama, unyanyue kitanda chako, ukaende kwa nyumba yako!"* (Luka 5:24) Mtu mwenyewe alisimama, akakwenda kwake akisifu Mungu! Yesu hakuponyesha watu na dawa au uchawi. Aliponyesha wagonjwa kwa uwezo na amri ya neno lake tu.

Mtu mmoja, jina lake Lazaro alikufa na kuzikwa. Wakati Yesu alipofika, siku ine zilikuwa zimepita tangu Lazaro alipozikwa. Yesu alifika karibu na kiburi, akasema, *"Lazaro, toka inje"* (Yoane 11:43). Maiti ilitoka kaburi. Yesu ana amri kufufua wafu, na kwa sababu hii aliweza kusema, *"Mimi ni **ufufuko** na **uzima**!"* (Yoane 11:25) Siku moja kwa wakati wa kuja watu wote walio ndani ya makaburi watasikia sauti yake na kusimama mbele yake. Wewe vilevile utatoka kaburini kama ulikufa. Hata sasa, Bwana Yesu anaweza kukupa uzima wa milele, na ruhusa kuishi katika paradiso kwa milele, kama ukimwamini kuwa Mwokozi na Bwana wako. Hata sasa Yesu anakaa kugeuza maisha ya watu wengi duniani. **Anaweza kugeuza maisha yako vilevile.** Unafikili nini juu ya Yesu? Unafikili nini juu ya kazi zake? Yeye ni pasipo kifani. Yeye ni Mwenyezi. Mbele ya kumaliza somo la leo, tunataka kukuuliza neno moja lingine juu ya Yesu:

**5) Unafikili nini juu ya majina yake na *majina* yake ya heshima (titres)?**

Kama tulivyoona ndani ya Maandiko ya Manabii, Yesu ana mia za majina na titres. Majina haya yanatusaidia kufahamu vizuri kama yeye ni nani. Kwa mfano, anaitwa: *Emanueli . . . Neno . . . Mwana wa Mungu . . . Mwana-Kondoo wa Mungu . . . Mkombozi . . . Mwokozi . . . Nuru ya Dunia . . . Bwana wa Utukufu . . . Ufufuko . . . Alfa na Omega, wa Kwanza na wa Mwisho . . . Mlango . . . Njia, Kweli na Uzima . . . na **Mwana wa Mungu**!*

Everyday Publications Inc
© 2010

Tuliona ya kwamba nabii wa Mungu, Musa, aliitwa *mtu wa Mungu*. Nabii Abrahamu aliitwa *rafiki ya Mungu*. Lakini Mmoja tu aliitwa ***Mwana wa Mungu.*** Utuambie kama nani ni karibu zaidi na mtu, rafiki yake au mwana wake? Sema kweli iliyo moyoni mwako. Ndiyo, Yesu aliitwa Mwana wa Mungu. Mungu aliita Yesu *Mwana wake* kumweka mbali na wote wengine. Tunasoma ndani ya Habari Njema ya kwamba Mungu alisema juu ya Yesu: *"Huyu ni Mwana wangu, mpendwa wangu; ambaye ninapendezwa naye. sikieni yeye."* (Matayo 17:5) Mungu alitaka kusema nini? Tunasema ya kwamba mwana ni kivuli cha baba yake. Mwana ni mfano wa baba. Yesu anatuonyeshea kama Mungu ni namna gani. Hii ndiyo maana ya masemo haya ya Mandiko: *"Hakuna mtu aliyeona Mungu wakati wo wote; Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye alimfunua."* (Yoane 1:18). Unataka kujua Mungu, na kuwa na ukaribu na upatano mtamu sana naye kwa milele? Basi kuja kwa Bwana Yesu, Yule ambaye Mungu aliita Mwana wake. Mwana anaweza kusema

kwa jina la baba yake. Yesu alifanya hivi wakati alipokuwa katikati ya watu. Kwa sababu hii jina lake linaitwa Emanueli, maana yake ***Mungu pamoja nasi.***

Wengine wanazania ya kwamba Mungu hawezi kuonekana duniani ndani ya mwili wa mwanadamu. Lakini mtu ye yote anayefikili hivi hajafahamu bado shauri la Mungu na njia aliyotayarisha kuokoa wenye zambi. Lilikuwa shauri lake kwa Mwana wa milele wa Mungu kutokea duniani yeye mwenyewe kwa mwili wa mtu, kujifunua kwa wana wa Adamu, na kuwakomboa toka mkono wa Shetani. Rafiki, **Mungu ni mkubwa** na anaweza kufanya neno lo lote, na anataka kila mtu kujuana naye. Kwa sababu hii aligeuka mtu na kuishi duniani.

Unafikili nini juu ya majina na titres za Yesu Masiya? Haiwezekani kumfananisha na mtu ye yote. Unafikili nini juu ya kuzaliwa kwake, tabia yake, masemo na kazi zake? Unafikili yeye ni nani? *"Munafikili nini juu ya Kristo? Yeye ni mwana wa nani?"* (Matayo 22:42)

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Everyday Publications Inc
@ 2010

Saa yetu ya leo inakwisha. Mungu akitaka, ndani ya somo la nyuma tutamaliza somo la leo na safari yetu katika Maandiko Matakatifu. . .

Mungu akubariki wakati unapowaza juu ya shairi hili toka Maandiko Matakatifu:

> ***"Katika yeye (Kristo) unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa mwili. Na ninyi (munaoamini) mumetimilika katika yeye (Kristo)."*** (Wakolosayi 2:9,10)
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

## Somo 100

# Unafikili nini juu ya Yesu?

## Sehemu 2

Salama iwe kwenu, rafiki, kwa jina la Mungu, Bwana wa salama, anayetaka watu wote kufahamu na kunyenyekea njia ya haki ambayo ametayarisha, na kukaa na salama ya kweli naye kwa milele.

Leo tutaendelea na maneno tuliyoanza ndani ya somo la mbele, lililoitwa **"Unafikili nini juu ya Yesu?"** Ni ulizo kubwa sana, kwa sababu jibu lako kwa ulizo hili litaonyesha nini unafikili juu ya Yesu Masiya na pahali gani utakaposhinda kwa milele. Ndani ya somo la mbele, tulikuuliza kama unafikili nini juu ya **ajabu la kuzaliwa kwake, tabia yake takatifu, masemo yake mazuri sana, uwezo wake mkubwa na majina (titres) yake ya heshima.** Leo tunataka kukuuliza maneno makubwa matano mengine juu ya Yesu.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Ulizo la kwanza ni:

**6) Unafikili nini juu ya mauti yake?**

Unajua **pahali** wewe utakapokufa? Au **namna gani** utakufa? Unajua **wakati gani** utakapokufa? Ndiyo, wewe na mimi hatujui maneno haya. Lakini Yesu hakuwa sawasawa nasi. Alijua **pahali** atakapokufa na alitangaza habari hizi wazi. Atakufa katika Yerusalema. Alionyesha vilevile kama atakufa **namna gani**. Aliwaambia wanafunzi wake,

> *"Tunapanda Yerusalema, na maneno yote yatatimizwa yaliyoandikwa na manabii juu ya Mwana wa watu. Kwa sababu atatiwa katika mikono ya Mataifa, atafanyizwa zihaka na kutendewa jeuri, na kutemewa mate; na watampiga fimbo, watamwua; na siku ya tatu atafufuka."* (Luka 18:31-33)

Aliwaambia wanafunzi wake vilevile **wakati gani** atakufa, ndiyo siku Wayuda watakapoua mwana-kondoo kushika siku kubwa ya Pasaka. Ni siku ile ile itakapompasa kufa kama Mwana-Kondoo ya

Mungu, kuwa sadaka kuondoa zambi za dunia.

Mauti ya Yesu ilikuwa namna nyingine na mauti zote nyingine, kwa sababu yeye mwenyewe **alichagua kufa.** Tulisikia Yesu akisema, *"Hakuna mtu anayeuondoa (uzima wangu) kwangu, lakini mimi mwenyewe ninautoa. Nina uwezo kuutoa, na nina uwezo kuutwaa tena."* (Yoane 10:18) Yesu hakufanya zambi kamwe; kwa sababu hii aliweza kuepuka zambi. Angaliweza kupanda mbingu tu pahali alipotoka, bila kufa. Lakini alichagua kufa kwa kutii mapenzi ya Baba yake na mapendo yake kwa wenye zambi. Alitoa uzima wake kwa sisi kwa njia ya kuruhusu watu kumfunga juu ya msalaba. Alikufa kutupatia usamehe kwa zambi, na zamana ya kwamba tutakuwa na pahali katika Paradiso. Karibu miaka mia saba mbele ya kuja kwa Masiya duniani, nabii la Mungu, Isaya alitangaza kwa sababu gani itapasa Mkombozi kufa:

> *"Lakini **aliumizwa kwa makosa yetu, alichubuka kwa maovu yetu.** Azabu ya salama yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea; tumegeuka kila mmoja kwa njia yake mwenyewe; na **Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote**."* (Isaya 53:5,6)

Everyday Publications Inc
@ 2010

Yesu Masiya alikufa kwa sababu yako na yangu. Yeye ni Mchungaji mwema aliyetoa uzima wake kwa kondoo kwa kutaka kwake mwenyewe. Hakuna mtu aliyekufa kamwe kama yeye. Yeye ni pasipo kifani katikati ya watu.

Ulizo lingine ambalo inakupasa kujibu ndilo hili:

**7) Unafikili nini juu ya kushinda kwake kwa mauti, maana ufufuko wake?**

Yesu alikufa na kuzikwa. Adui zake walifanya kila kitu walichoweza kulinda kaburi. Walifingirisha jiwe kubwa sana kufunga njia ya kuingia kaburi, kisha wakaweka muhuri juu yake. Waliweka askari pale kulinda kaburi. Lakini masumbuko yao hayakuweza kuzuiza Yesu asifufuke toka wafu. Ndiyo, Bwana Yesu alifufuliwa toka wafu siku ya tatu na alitokea kwa wanafunzi wake. Nyuma yake, alitokea kwa zaidi ya washuhuda mia tano kwa saa moja. Watu wale walimwona na macho, walimgusa, na walikuwa pamoja naye nyuma ya ufufuko wake. Aliwaonyesha vidonda ndani ya mikono yake, miguu yake na mbavu zake. Ndiyo, alifufuka toka wafu namna alivyotabiri! Mungu alifufua Yesu toka wafu kuhakikisha kwa dunia

nzima ya kwamba alikubali kazi ya Yesu juu ya msalaba kama Sadaka kamilifu na ya mwisho kulipa kwa zambi.

Mauti ni adui mkubwa. Wazazi wetu walikufa. Manabii walikufa vilevile, na maiti zao zinabaki ndani ya makaburi yao. Sisi tutakufa vilevile siku nyingine. Lakini Mungu asifiwe, **Yesu Kristo alishinda mauti!** Yeye ni Mwokozi hai na anaweza kuokoa wote wanaofika karibu na Mungu kwa njia yake, kwa sababu yeye ni hai na anaombea wote ambao wanamwamini. Kuna nabii mwingine aliye hai leo nyuma ya kufa kwake? Sivyo, hata mmoja. Yesu Kristo ni wa pekee aliyeshinda kaburi. Yeye ni hai leo, na kwa sababu hii sisi ambao tunamwamini hatuogopi kufa. Kufa ni kwenda juu tu karibu na Bwana wetu Yesu. Ndiyo, Yesu ni pasipo kifani. Hakuna mwingine sawasawa naye duniani au mbinguni. Unafikili nini juu ya kushinda kwake kwa mauti?

Ulizo lingine ni:

**8) Unafikili nini juu ya kupanda kwake mbinguni?**

Everyday Publications Inc
@ 2010

Nyuma ya kufufuka toka wafu, Bwana Yesu alionekana kwa wanafunzi wake kushinda pamoja nao kwa siku makumi ine. Kisha tulimwona akiagana nao, na kupanda mbinguni na kuketi kwa mkono wa kuume wa Mungu, pahali pa heshima zaidi. Kwa njia hii tunaona ya kwamba yeye ni mkubwa kupita malaika, manabii, na wanadamu wote! Hili ndilo neno Maandiko yanatangaza, yakisema,

> *"Mungu vilevile alim**tukuza sana**, na kumpa jina lililo **juu ya kila jina;** hata kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni na vya duniani, na chini ya dunia, na kila ulimi ukiri ya kuwa Yesu Kristo ni **Bwana**, kwa utukufu wa Mungu Baba."* (Wafilipi 2:9-11)

Ndiyo, Yesu ni pasipo kifani! Pamoja na ulizo 8 inakupasa kujibu ulizo hili vilevile:

**9) Unafikili nini juu ya kurudi kwake duniani?**

Yesu Kristo atarudi. Alisema hivi. Manabii walitangaza neno hili. Malaika walisema vivyo. Wanafunzi wote wa kweli wa Kristo wanangojea kurudi kwake. Atarudi kupeleka watu wake mbinguni. Atahukumu dunia na haki na kutawala juu ya dunia nzima. Atakuwa Mfalme wa dunia. Ni sharti kwake kutawala miaka elfu moja kufika wakati saa adui zake zote watakapoinama kwa miguu yake. Ndiyo, atarudi nyuma kidogo. Itapasa kila mtu kukiri ya

kwamba yeye ni Mfalme wa wafalme na Bwana wa wabwana. Atakuja na utasimama mbele yake, yule Mwamuzi mkubwa. Siku ile utakapomwona uso kwa uso, atakuuliza, **"Ulifikili nini juu yangu?"** Utajibu nini? Ukijibu, "Nilifikili ulikuwa mmoja wa manabii," atakuuliza kwa sababu gani hukumwamini na roho ya kweli—na utahukumiwa, kwa sababu hukuamini maneno aliyosema juu yake mwenyewe, na maneno manabii waliyoandika juu yake—ya kwamba yeye ni **Mwana wa Mungu toka mbinguni, Mwokozi wa pekee**. Nani atarudi kutawala? Abrahamu, Musa, Daudi au nabii mwingine atarudi kutawala? Sivyo. Bwana Yesu ndiye atakayerudi. Atakuwa **Mwamuzi**. Mungu alihakikisha neno hili kwa njia ya kumfufua toka wafu. Atarudi. Kila jicho litamwona. Kila goti litapigwa mbele yake. Kila ulimi utakiri ya kwamba *"Yesu Kristo ni Bwana!"*

Sasa tunafika kwa ulizo la mwisho:

**10) Unafikili Bwana anataka wewe kufanya nini?**

Bwana Yesu anasema, *"**Kujeni kwangu,** ninyi wote munaosumbuka na wenye mzigo mzito, **nami nitawapumzisha ninyi**. Tieni nira yangu juu yenu, na mufundishiwe nami, kwa sababu mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; na mutapaa raha kwa nafsi zenu."* (Matayo 11:28,29) Anakuita leo leo! Wakati alipoita wanafunzi wa kwanza kumfuata, waliacha vyote: nyumba zao, jamaa zao, na kazi yao. Anataka wewe kufanya vivyo. Si kusema ya kwamba inakupasa kujitenga na nyumba yako na kazi yako kufuata Yesu, lakini sharti umtolee maisha yako mazima na kumpa pahali pa kwanza ndani ya moyo wako. Anataka umtegemee, umwamini, na kumpokea kama Mwokozi na Bwana wako. **Anakutaka mzima**—nia yako, moyo wako, mwili na nafsi. Akiwa kweli Mwana wa Mungu kama anavyosema, anastahili vyote.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Kama tulivyoona, Yesu Kristo ni pasipo kifani na haiwezekani kumsawanisha na mwingine ye yote. Yeye ni pasipo kifano kwa maneno ya **kuzaliwa kwake, tabia yake, mafundisho yake, kazi zake, majina na titres zake, mateso na mauti yake, ufufuko wake, kupanda kwake mbinguni, kurudi tena**, na **namna anavyoweza kugeuza mioyo ya wana wa Adamu.** Yeye ni hai leo. Yeye ni pamoja na wale ambao wanamwamini. Nyuma kidogo atarudi. Hakuna mwingine kama yeye mbinguni au duniani. Kwa sababu hii ana amri kuwa Mfalme na Bwana wa maisha yako! Bwana Yesu Kristo anataka kuwa Mwokozi na Bwana wako. Kwa sababu hii alikufa msalabani na alifufuka tena! Ana uwezo kuondoa zambi zako na kukupa

ushirika wa ajabu sana na Mungu kwa milele. Anaweza kukupa uzima mpya, kusafisha moyo wako, na kukufanyiza mpya kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, lakini sharti umw**amini** na kumtegemea yeye na sadaka yake.

Ni huzuni kubwa kwa sababu watu wengi wanafikili Yesu Kristo ni nabii mkubwa, lakini hawakumpokea kamwe kuwa Bwana na Mwokozi wao. Haitoshi kuamini ya kwamba Yesu alikuwa nabii mkubwa tu! **Sharti upatane na Mungu ya kwamba Yesu ni Bwana juu ya *yote* na ya kwamba wakati alipokufa juu ya msalaba, alikufa kwa pahali *pako*.** Sisi sote wana wa Adamu tunasumbushwa na neno kubwa moja: **zambi.** Mungu, kwa rehema yake kubwa, ametayarisha njia kwa kutusaidia ndani ya neno hili, lakini **sharti tuipokee**. Nikiwa mgonjwa na ninafikia mganga, ataandika barua kwa mimi kuweza kupata dawa. Hivi ninakwenda na kununua dawa, kisha ninarudi kwetu, ninaweka dawa juu ya meza, ninaiangalia na dawa inaniangalia mimi. Kufanya hivi kutaniponyesha? Sivyo! Sharti nimeze dawa, **namna ninavyoagizwa.** Dawa ya Mungu ni Bwana Yesu Kristo na damu aliyomwanga juu ya msalaba.

Everyday Publications Inc
@ 2010

Labda mtu mmoja anauliza: "Namna gani ninaweza kukamata dawa ya Mungu kwa zambi yangu?" Kwa ufupi, inakupasa **kukiri mbele ya Mungu** ya kwamba wewe ni mwenye zambi, ya kwamba "kazi zako njema" ni kama vitambaa vichafu mbele yake, na ya kwamba huna njia kujiponyesha mwenyewe toka hukumu yake ya haki. Kisha inakupasa **kuamini moyoni mwako** ya kwamba Bwana Yesu Kristo alibeba azabu kwa zambi zako. Kama ukiamini ya kwamba Kristo alikufa na kufufuka tena kukuokoa, halafu Mungu atasamehe zambi zako, atakuvika na haki ya Kristo, atatuma Roho Mtakatifu yake ndani ya moyo wako, na kukupa ruhusa kuishi kwake kwa milele! Mungu atukuzwe kwani unaweza kufanywa haki leo leo—kama ukiamini!

Rafiki msomaji, umekamata "dawa ya Mungu" inayoweza kukuponyesha toka ugonjwa wa zambi na kukuokoa toka moto wa milele ya hadeze? Sharti mtu ye yote anayeona dawa ya Mungu bule, maana, **damu Yesu aliyomwanga**, ajue ya kwamba **hakuna njia nyingine** kumponyesha toka zambi. Hakuna hata moja! Mungu hana njia nyingine kusafisha wenye zambi na kuwafanya haki mbele yake. Hakuna **njia nyingine** kufikia Paradiso.

Waza maneno Maandiko Matakatifu yanayotangaza juu ya **njia**

**ya pekee ya haki** Mungu aliyotayarisha kwa wenye zambi kuwafanya haki mbele yake. Maandiko yanasema:

> (Waroma 3) *20 Kwa kazi ya kushika sheria* ***hapana mwenye mwili atakayehesabiwa haki*** *mbele yake . . . 21 Lakini sasa,* ***haki ya Mungu*** *imeonyeshwa pasipo sheria; imeshuhudiwa na sheria na manabii; 22* ***haki ya Mungu kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote, na juu ya wote wanaoamini;*** *maana hapana tofauti, 23 kwa sababu wote wamefanya zambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu; 24 wanahesabiwa haki bule kwa neema yake,* ***kwa njia ya ukombozi ulio katika Yesu Kristo*** *. . . 27 Basi wapi tena kujisifu? Kumefungwa inje. Kwa sheria gani? Kwa matendo? Hapana! lakini kwa njia ya sheria ya* ***imani.***
>
> *"Kwa maana mumeokolewa kwa neema kwa njia ya* ***imani,*** *wala neno hili halikutoka ndani yenu wenyewe, ni* ***zawadi ya Mungu, si kwa matendo,*** *asiwe mtu atakayejisifu."* (Waefeso 2:8,9) *"Kama ukikiri kwa kinywa chako ya kuwa Yesu ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua toka wafu,* ***utaokolewa*** *. . . kwa sababu kila mtu* ***anayeitia*** *jina la* ***Bwana ataokolewa!****"* (Waroma 10:9,13)

Everyday Publications Inc
@ 2010

Rafiki, umeitia jina la Bwana? Umepokea zawadi ya Mungu, ndiyo wokovu? Au unakaa kujaribu kujiponyesha kwa njia ya kazi zako mwenyewe, ndizo kazi njema? Tunakusihi usikatae njia haki ya wokovu ya Mungu. Mungu anajua roho yako. Kubali mbele yake ya kwamba wewe ni mwenye zambi, umevunja sheria zake takatifu. Umwambie ya kwamba unajua unastahili hukumu yake katika moto wa milele. Kisha umshukuru kwa sababu alituma Mwokozi asiyekuwa na zambi na aliyekubali kuteswa kwa pahali pako—akipokea azabu yako ya milele, kisha akifufuka tena na kushinda toka kaburi!

Rafiki, sharti uje kwa Mungu kwa **njia ya haki ambayo Yeye alisimamisha** — au huwezi kuja hata kidogo. Mungu, mwenye rehema na huruma, anakuita kuja leo. Kuja kwake leo na kuokolewa. *"Amini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokolewa – pamoja na nyumba yako."* (Matendo 16:31) Amina.

~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

Hili ni somo la mia moja la safari yetu katika Maandiko Matakatifu. Asante kwa kufungana nasi kwa masomo. Tunalagana nawe na ombi hili zuri sana ndani ya Neno la Mungu:
~~~~~~~~~~~~~~~~~~~~

***"Yeye anayeweza kuwalinda ninyi musijikwae, na kuwasimamisha ninyi mbele ya utukufu wake pasipo kilema katika furaha kubwa; yeye aliye Mungu pekee mwenye hekima, Mwokozi wetu, kwa Yesu Kristo Bwana wetu; utukufu ni wake, na ukubwa, na uwezo, na nguvu, tangu milele, na sasa, na hata milele. Amina."*** (Yuda 24,25)

Everyday Publications Inc
@ 2010